

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 23 Mei, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tunaomba tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tano, leo ni Kikao cha Thelathini na Nne.

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. ALMAS A. MAIGE - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Kuhusu Shauri linalomhusu Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE – K.n.y. MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Getere. Mheshimiwa Getere dada yako Mheshimiwa Catherine Ruge anapiga makofi sana, sijui kuna nini? Naomba nimuite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA – MSEMADI MKUU WA
KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MALIASILI NA
UTALII:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Juu ya Wizara ya Maliasili na Utalii Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

SPIKA: Ahsante sana.

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu. Waheshimiwa Wabunge nina orodha ndefu kidogo, leo tuanze na Zanzibar. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma uwe muulizaji wa kwanza, Mbunge wetu kwenye Bunge hili na Bunge la Afrika pia.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Spika, asante sana. Nashukuru sana kupata fursa hii ya kipekee na ya heshima kubwa sana kwangu na kwa Serikali yangu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, utendaji na utekelezaji wa Ilani ya chetu cha CCM kwa kiasi kikubwa umekuwa na mafanikio. Mheshimiwa Waziri Mkuu utekelezaji wa ilani katika sekta ya kilimo, nishati, elimu, afya, madini, n.k. kumekuwa na hatua ya kuridhisha sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa karibu kipindi chetu kinakwisha tunakaribia uchaguzi Mkuu wa 2020 naomba kuuliza Serikali, lakini kabla sijauliza niseme kwamba, mafanikio haya tuliyoyafikia leo yamefikiwa kupertia na juhud kubwa za Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na timu yake akiwemo Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia, Waziri Mkuu wewe mwenyewe Majaliwa na watendaji wote wa Serikali ambao wamefanya kazi nzuri kufikia maeneo hayo niliyoyataja hapo juu. Sasa hivi Serikali itakamilisha lini utaratibu wa kuwawezesha Watanzania wanaoishi nchi za nje kuweza kupata nafasi yao ya kidemokrasia kupiga kura?

SPIKA: Asante Mheshimiwa. Asante kwa swali lako. Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa anataka kujua Serikali inaandaa utaratibu upi wa kuwawezesha Watanzania walioko nje ya nchi kuja kupiga kura nchini wakati wa uchaguzi mkuu na chaguzi nyingine:-

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni la kisera na Serikali imeendelea kuona utaratibu huo kama unaweza kufaa kwa sababu, lazima kwanza tupate kujua nani wako nje ya nchi, idadi yao, wanafanya shughuli gani na kama je, bado ni Watanzania au waliomba uraia nchi za nje. Na pindi sera hiyo itakapokamilika pale ambapo itaonekana inafaa

tutakuja kulijulisha wote, Bunge na Tanzania nzima. Asante sana.

SPIKA: Ahsante sana; Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko uliza swali lako.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni wajibu wa Serikali kuyahudumia majeshi yetu kwa kuyapatia *uniform* ambazo ni viatu, soksi, suruali au sketi, shati, mkanda wa suruali, mkanda wa filimbi, nembo ya cheo, lakini na kofia. Imekuwa ni muda mrefu sasa majeshi haya hayapatiwi hizi *uniform* badala yake wanajinunulia wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mathalani Jeshi la Magereza tangu 2012 hawajawahi kupatiwa *uniform*, vivyohivyo kwa Jeshi la Polisi na hizi *uniform* wanajinunulia kwa belghali sana. Mathalani nguo ambazo za *jungle green* wanunua kwa 70,000/=, kofia 15,000/=, buti zile 70,000/= na hawa askari wetu wanafanya kazi kwa mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, ningetaka kujua sasa ukizingatia Askari Magereza kwa mfano mwenye *degree* analipwa sawa na Askari Magereza mwenye elimu ya kidato cha nne, shilingi 400,000 aweze kununua, ajigharamie nyumba na mambo mengine.

Ni nini sasa Kauli yako Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba, askari hawa wanapewa *uniform* zao, maana ni stahiki ambayo wanatakiwa kupewa, sanjari na kurudishiwa gharama zote ambazo wamekuwa wakijinunulia hizi *uniform* kwa kipindi chote ambacho Serikali ilishindwa kuwapa hizi *uniform*?

SPIKA: Mheshimiwa Esther inaelekea unajua mambo mengi kuhusu askari magereza, sijui umejuaje sijui?

Mheshimiwa Waziri Mkuu ufanuzi tafadhali.
(Kicheko)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi Serikali inao wajibu wa kutoa vifaa mbalimbali ikiwemo sare kwa majeshi yetu, ili waweze kufanya kazi yao kwa urahisi zaidi. Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo inasimamia Jeshi la Polisi, Magereza pamoja na Uhamiaji pamoja na Zimamoto ni Wizara ambayo inaendelea kuratibu namna nzuri ya kupata sare na vifaa mbalimbali, ili kuwawezesha watumishi wetu askari kwenye majeshi hayo waweze kufanya kazi yao. Na sera yetu ni kwamba, bado Serikali itaendelea kuwagharamia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ni shahidi mwaka jana tumekuwa tukijadili upande wa Jeshi la Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani ilipokuwa imeagiza, imetoa zabuni ya kununua sare na tukapata taarifa kwamba, kuna majora yako pale ambayo yameandaliwa kwa ajili ya kuwapa askari, hiyo ni dalili kwamba, Wizara ya Mambo ya Ndani bado inatoa huduma hizo kwa askari wake.

Mheshimiwa Spika, sasa kama kuna mahali ambako kwa Wizara upande huo wanunuwa hizo sare tutaweza kuwasilisna pia na Waziri mwenye dhamana, ili tuone kwa utaratibu huo ukoje na kwa nini sasa askari wanunue na kama ndio sera ya ndani ya Wizara tutaweza kujua na tunaweza tukafanya marekebisho kadiri ya mahitaji yalivyo, asante.

SPIKA: Mheshimiwa Esther, swalii fupi sana.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nakushukuru Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni ukweli kabisa kwamba, hawa askari hawapewi hizi sare na hata wakifanya *parade uniform* zao ziko tofauti-tofauti kwa *texture*, lakini hata kwa rangi.

Mheshimiwa Spika, nilitaka pia kujua, maana hujajibu swalii langu lile jingine, fidia ambazo watarudishiwa gharama ambazo wakati mnaendelea kujiratibu kuhakikisha

wanapewa hizi *uniform*. Je, wataweza kuridishiwa gharama ambazo wamekuwa wakizitumia kujinunulia *uniform* zao wenyewe?

SPIKA: Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhalii.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu umelieleza hilo na unaonesha unazungumza kama una uhakika wa kwamba, askari wetu wanawanua. Na ungependa kujua je, kama askari hao wanaweza kurudishiwa fedha zao kama sera ya kuwapa vifaa bure ipo?

Mheshimiwa Spika, basi naomba nilichukue hilo niwasiliane na Wizara husika, ili tuone msingi wa ununuzi wa vifaa hivyo, halafu tutaweza kuzungumza vizuri na Wizara ya Mambo ya Ndani na tutakupa taarifa Mheshimiwa Mbunge, asante. (*Makofii*)

SPIKA: Kamishna Mary Pius Chatanda uliza swalii lako tafadhalii.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kumuuliza Waziri Mkuu, Serikali imekuwa ikipeleka fedha nyngi katika Halmashauri zetu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na kukamilisha, lakini miradi hiyo imekuwa haitumiki kama ilivyokusudiwa kutokana na usanifu mbovu wa miradi na kutokamilika kwa miradi hiyo.

Je, Serikali ipo tayari kuchunguza na kuchukua hatua kwa wale wote watakaobainika kwamba, walisababishia hasara Serikali na kuwasabishia Wananchi kutopata huduma ambayo walikuwa wamekusudiwa kupewa na Serikali?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhalii.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba, miradi yetu mingi ya maji ambayo inatekelezwa kwenye maeneo mbalimbali iko mingine haitekelezwi kwa viwango na kwa hiyo, haina thamani ya fedha kama ambavyo tumekusudia iweze kutekelezwa. Lakini pia kama ambavyo Waziri mwenye dhamana alipokuwa ameleta bajeti yake mbele yetu Wabunge alieleza hatua mbalimbali zilizochukuliwa dhidi ya miradi yote ambayo imetangazwa na haina thamani kama iliyokusudiwa kwa fedha iliyotolewa. Na moja kati ya hatua ambazo amezifanya, alieleza hapa kwenye hotuba yake na ndio hasa kazi ambayo inafanywa, ameshaunda timu inayopita kukagua miradi yote nchini kwa kujiridhisha miradi hiyo kupitia *BOQ* zake kuona matengenezo yake na kama inakidhi thamani ya fedha kwa fedha zilizotolewa kwa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, na pale ambapo sasa hakuna thamani ya fedha hizo hatua ambazo Mheshimiwa Mbunge anataka kujua zinachukuliwa. Na ninataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tumewasikia ushauri wenu kwenye sekta ya maji ikiwemo na kuchukua hatua kali kwa watendaji wetu ambao wanasmamia miradi ya maji na maji hayapatikani, lakini mradi wenyewe haujatengenezwa kwa viwango kwamba, hatua kali zitachukuliwa. Na Wizara sasa imeanza kupitia, Wizara yenye pale Makao Makuu, na inashuka ngazi ya Mikoa mpaka Wilayani ili kujiridhisha kwamba, tunakuwa na watumishi wenyewe weledi wa kutekeleza miradi hii na kusimamia thamani ya fedha kwa manufaa ya Watanzania, ili huduma ziweze kutolewa kwa Wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaendelea na kazi hiyo na Wizara inaendelea kukagua miradi pamoja na ile tume, itakapokamilisha kazi itakuwa na majibu. Wale wote watakaothibitika hatua kali dhidi yao itachukuliwa. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, uliza swali lako, tafadhali.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu Swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu moja katika mikakati ya Serikali, ili kuinua sekta ya kilimo ni kuhakikisha kwamba, wakulima wadogo walioko vijijini wanapata pembejeo katika ubora na katika viwango vinavyokusudiwa. Na hilo litafanikiwa tu pale ambapo mfumo wa ufikishaji pembejeo kwa Wananchi ni mfumo endelevu ambao utahusisha kuwepo na maduka madogo-madogo vijijini ya pembejeo ambayo yataweza kuuza mbolea, mbegu bora pamoja na viuatilifu.

Mheshimiwa Spika, lakini imebainika kwamba, jitihada za wadau pamoja na Serikali za kuhakikisha kwamba, kunakuwa na maduka madogo-madogo ya pembejeo vijijini zinakwamishwa na gharama kubwa ya kufuzu kuwa na maduka hayo, ikiwemo gharama kubwa kwenye TOSKI zaidi ya laki moja na eneo la *TPRA* ambalo laki tatu na gharama nyingine ambazo zinamfanya mdau anayetaka kuwekeza kwenye sekta hiyo, lazima atumie zaidi ya 600,000 kabla hajanunua malighafi kwa ajili ya duka lake.

Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba, inapunguza au kuondoa gharama hizo, ili kufikia malengo tuliojiwekea ya kuhakikisha mkulima mdogo ananufaika kwa kupata pembejeo bora na salama kwa ajili ya uzalishaji?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhagama, Mbunge wa Madaba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali limekuwa na maelezo mengi, lakini msingi wake anataka kujua Serikali ina mpango gani

wa kutoa, kupunguza tozo za maduka yanayouza pembejeo, ili kumuwezesha mkulima kupata pembejeo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali imepokea ushauri na vilevile malalamiko kadhaa kutoka kwa wafanyabiashara mbalimbali wakiwemo hao wanaofungua maduka ya pembejeo juu ya tozo mbalimbali katika uendeshaji wa shughuli nzima za biashara. Nataka nikuhakikishie kazi kubwa inayofanywa na Serikali sasa ni kufanya mapitio ya tozo zote kuanzia kwa wakulima kwenye mazao yao, kwa wafanyabiashara wenyewe wanapofanya biashara, ili kutengeneza mazingira mazuri ya kufanya biashara nchini, ikiwemo maduka hayo yanayosambaza pembejeo, ili kufikisha pembejeo kwa urahisi kwa mkulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wenye dhamana ambao wana tozo mbalimbali kwenye Wizara zao zinazokwamisha kufanya biashara katika mazingira rahisi wameshakutana. Na hata juzi nilikuwa na Mawaziri hao kupata taarifa zao kwa pamoja kuona maeneo yote waliyyoyapitia na tozo zote ambazo zinataka kupitiwa upya na kazi hiyo inayoendelea sasa ikishakamiliaka sasa watakutana pia na Kamati ya Bajeti ya Bunge, watakutana pia na Wizara ya Fedha, ili kuona namna nzuri ya kuondoa tozo hizo, lakini badae itaenda kwenye mamlaka inayotoa ridhaa ya kuondoa kodi ikiwemo na hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jitihada za Serikali katika hiyo zimeshaanza na tutakapofikia hatua nzuri tutakagua pia na maeneo unayotaja ya maduka yanayouza pembejeo, ili kuwawezesha wafanyabiashara wa maduka hayo kupata pembejeo na kuzipeleka mpaka ngazi ya kijiji, ili wakulima waweze kupata pembejeo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mkakati wa Serikali unaendelea na niwape matumaini wafanyabiashara wote nchini kwamba, Serikali imewasikia vilio vyao na sasa tunafanya mapitio ya tozo hizo, tutakapofikia hatua nzuri tutawajulisha na tutawashirikisha katika kujua ni aina gani ya

tozo ambayo tunataka tuiondoe na au kuibadilisha kwa namna moja au nyngine, ili muendeleee kufanya biashara zenu katika mazingira rahisi.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, uliza swalii lako tafadhali.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa usikivu wake ilisikia kilio ambacho Wabunge pamoja na wananchi kuhusiana na migogoro ya ardhi ambayo imehusisha vijiji zaidi ya 360 katika muingiliano wa mipaka kati ya vijiji pamoja hifadhi za taifa au hifadhi za misitu au hifadhi za misitu au mapori tengefu n kupelekeea hivyo Mheshimiwa Rais aliunda kamati ya Mawaziri nane wakiongozwa na Mheshimiwa Lukuvi katika kuratibu na kumshauri namna bora ya kutatua changamoto hii ya vijiji hivi zaidi ya 360, vikiwemo Vijiji vya Mataweni na Stalike katika Jimbo la Nsimbo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua, je, Serikali ipo tayari kukaa kwa pamoja na Wabunge kupitia taarifa hiyo ikiwa ni namna ya kufanya *reconciliation* ili kusiwe na malalamikotena ya baadaye kwa sababu hili ni zoezi ambalo litakuwa linatatua kwa muda mrefu. Je, Serikali ipo tayari kukaa na Wabunge kupitia kabla ya kumkabidhi Mheshimiwa Rais ripoti hiyo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali, tunaomba majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mbogo, Mbunge wa Nsimbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kama ripoti ya ukaguzi wa ardhi ya Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Rais kama inaweza kuja kushirikisha Wabunge hapa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumekuwa tukipata taarifa mbalimbali za migogoro ya ardhi kwenye maeneo kadhaa. Wizara ya Ardhi imefanya kazi nzuri ya kupita maeneo yote yenye migogoro ya ardhi na mwisho Mheshimiwa Rais aliunda timu ya Mawaziri wanane kupita maeneo yote yenye migogoro kukagua na kusikiliza maoni ya wananchi kwenye maeneo hayo ili kuweza kuratibu vizuri na hatimaye tuweze kutoa utatuzi wa migogoro hiyo. Sasa timu ile ni ya Mheshimiwa Rais, matokeo ya ukaguzi wake yatawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais kwanza kabla ya kupelekwa mahali pengine, kiitifaki inatakiwa iwe hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia timu ile ilipokuwa inapita kwenye maeneo yale, tuliwaagiza Mawaziri watoe taarifa kwenye Mamlaka za Wilaya kule ili watu/wadau wote washirikishwe kule, tuna amini kama kulikuwa na Wabunge na wakati ule ullkuwa siyo wakati wa Bunge, miliweza kushiriki kwa namna moja au nyingine. Pia Mheshimiwa Rais ikimpendeza, baada ya kupata taarifa hiyo, anaweza kutujulisha lakini sasa kiitifaki kwanza aliyetaka tume iundwe ndiye ambaye ambaye tunaweza kumpelekea kwanza, hatuwezi kuileta Bungeni kwanza bila kumpelekea Mheshimiwa Rais mwenyewe kiitifaki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo litaangaliwa na kama Mheshimiwa Rais itampendeza anaweza akaamua kutushirikisha lakini tuna amini Wabunge kwa taarifa tulizopeleka kule kwenye hal mashauri zenu ili muweze kushiriki katika kutambua na kusaidia kueleza migogoro na kama ambavyo mmekuwa mkieleza hapa ndani, yale maoni yenu ya hapa ndani ndiyo yaliyochukuliwa na kwenda kuyafanya kazi, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Susan Lyimo, uliza swali lako.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi, nchi yetu takribani asilimia 70 ya wananchi wake wanategemea kilimo na Mheshimiwa Waziri Mkuu kilimo hiki kimekuwa na matatizo makubwa kuto kana na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo basi kilimo cha umwagililaji

kimeonekana ndiyo chenye tija na chenye uhakika wa chakula lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu utakubaliana nami kwamba kilimo hiki bado hakijapewa kipaumbele na hasa ukizingatia sasa hivi kuna maeneo mengi sana yana njaa hata Dodoma mazao yamekauka na maeneo mengine mengi.

Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba kilimo cha umwagiliaji sasa kinapewa kipaumbele ili tuwe na uhakika wa chakula lakini vilevile viwanda vyetu viweze kupata hiyo malighafi? Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhalii.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka nikiri kama ulivyosema kwamba hatujaona tija ya kilimo cha umwagiliaji nchini. Serikali hilo imeliona na mwenyewe nimechukua hatua wiki moja iliyopita, tumeivunja Tume ya Umwagiliaji yote, kwanini tumeivunja? Ni kwa sababu kilimo chetu nchini ambachohi kinategemea sana mvua na Serikali ilipopanga kuboresha kilimo na kuongeza uzalishaji kwa kuwa na Sekta ya Umwagiliaji, tumegundua kwamba mpaka leo hii Taifa haliwezi kuringia usalama wa chakula nchini kutegemea umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kwanza tumeiondoa Tume ya Umwagiliaji kutoka Wizara ya Maji ambayo Wizara ya Maji yenye we inashughulikia zaidi kwa Watanzania na kuihamishia Kilimo ili napo sasa iweze kusimamia vizuri Sekta ya Umwagiliaji kwa mipango walijonayo ya uzalishaji wa chakula nchini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mbili, tumegundua fedha yote tunayoipeleka pale kwa ajili ya kutengeneza miradi ya maji hajafanya kazi yake, miradi mingi ya umwagiliaji haijaleta tija, hiyo ndiyo imetusababisha tumevunja tume. Tumepitia

tumegundua tuna hasara, tayari tumepeleka timu ya kuchunguza; wakurugenzi sita tumewasimamisha, watendaji 25 tumewahamisha na sasa tunajenga upya tume ile ili iweze kuleta tija kwa maelekezo mapya kabisa ya Serikali chini ya usimamizi wa Wizara ya Kilimo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie Watanzia kwamba miradi yetu yote iliyopo huko ambayo inasuasua, itaratibiwa upya na timu mpya inayoundwa sasa na Waziri atakuja kutangaza tume na bodi muda mfupi ujao ili ianze kusimamia miradi yote iliyopo nchini. Na sasa ile *structure* ya utawala wa Tume ya Umwagiliaji ilikuwa wanaishia kwenye kanda, tumetoa utaratibu mpya waende mpaka wilayani. Tutakuwa na Afisa wa Umwagiliaji Mkoani, atakayekuwa anasimamia wilaya zote zenye miradi lakini tutakuwa na Afisa wa Umwagiliaji kila halmashauri asimamie mradi uliopo kwenye halmashauri badala ya kuishla kanda ambako walikuwa hawana uwezo wa kutembelea kwenye wilaya zetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, marekebisho haya, yanakuja kuleta tija sasa ya umwagiliaji nchini na tutasimamia kikamilifu kuhakikisha kwamba mabadiliko haya yanaleta tija kwa Watanzania, asante sana. (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Susan Lyimo, swali fupi la nyongeza.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pamoja na kuvunja tume hiyo sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa nini wakulima sasa wasipate wataalam bora kwa ajili ya kilimo hicho cha ili waendane sambamba na huu uvunjaji wa hii tume tupate kilimo chenye tija? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhalii.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu ambao sasa tunaufanya ni kwamba mbali ya kwamba kuna Tume ya Umwagiliaji, ina maafisa wake lakini tumewashirikisha pia Maafisa Kilimo wa Wilaya, Maafisa Ugani walio kwenye ngazi za vijiji, wote hawa wafanye kazi kama timu moja. kwa hiyo, usimamizi wa kilimo utakuwa ni wa pamoja na kila palipo mradi iwe mradi upo kijijini, tutakuwa na Afisa Ugani wa Kilimo pale kijijini lakini yupo Afisa Ugani kwenye ngazi ya kata, yupo afisa kilimo ngazi ya Wilaya na Afisa Umwagiliaji ngazi ya Wilaya; hawa wote wakifanya kazi kwa pamoja na kwa maelekezo tuliyowapa na kwa sababu pia tulishasambaza maafisa kilimo kwa kuwaamisha kwenye Halmashauri ya Wilaya kuwapeleka vijiji, tuna amini kwa maelekezo yetu chini ya usimamizi makini wa Waziri wetu wa Kilimo na timu yake, tunaweza kufikia hatua nzuri na tuwahakikishie kwamba tutasimamia vizuri Sekta ya Kilimo na hasa kwenye Sekta ya Umwagiliaji. (*Makof*)

SPIKA: Tunaendelea Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, uliza swali lako Mheshimiwa Rose.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni imani ya watanzania kuwa elimu bora ndiyo utakuwa msingi wa kuhakikisha vijana wa Taifa hili pale wanapohitimu wanakuwa na uwezo aidha wa kuajiriwa au kutumia *knowledge* na *skills* ambazo wamezipata shulenii kuweza kutambua fursa zilizopo ili waweze kujiajiri wenyewe. Sasa ni matumaini yangu Mheshimiwa Waziri Mkuu utakubaliana na mimi kuwa walimu bora ndiyo wenye uwezo wa *ku-transfer* au kuambukiza maarifa yaliyo bora kwa vijana wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilitaka kujua mkakati wa Serikali kuhakikisha tunatumia vijana ambao wana *division one* na *two* ili wawe walimu ambao tunategemea *wata-train* wanafunzi ambao watakuwa *competent either* kutumika kwenye nchi yetu au waweze kutoka nje ya nchi kujitafutia fursa kwa ajili ya maisha yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tweve, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba vijana wetu wakipata elimu bora wanaweza kuingia kwenye Sekta ya Ajira, ajira binafsi hata zile rasmi nje na ndani ya nchi. Na hii inatokana na uimara wa utoaji elimu tulionao nchini ambao pia tunaendelea kuboresha kila siku ili tuweze kufikia hatua hiyo ya kuwawezesha kuona fursa na kuweza kuzitumia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, utaratibu ambao tumeuweka Serikalini ni kubainisha kati ya Wizara ya Elimu na TAMISEMI kwa usimamizi imara kwenye maeneo haya. Wizara ya Elimu kama msimamizi wa sera, yeye ndiye mwenye uwezo na ndiyo tumempa dhamana ya kuhakikisha kwamba tunaandaa walimu bora wenye uwezo kwa madaraja uliyoyataja na vigezo vinavyotumika kupeleka walimu ni vile ambavyo vimeshafafanuliwa. Tunao walimu wa shule za msingi, walimu wa sekondari lakini pia tuna walimu wa vyuo, maeneo yote yana sifa zake na wote hawa wanakwenda kama sifa zao zinavyoeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, matokeo tunayoyapata sasa ni matokeo mazuri ya mipango ya Sera tuliyonayo lakini usimamizi wa utoaji elimu tumeipeleka TAMISEMI, wao ndiyo wanamiliki shule za msingi na sekondari kama elimu ya msingi kujihakikishia kwamba vijana wanaoandalialiwa kwenda mpaka elimu ya juu ni vijana ambao walishapewa msingi imara wa kielimu. Kwa hiyo, kazi hii inaendelea kwa kuwa na walimu imara, bora lakini pia kuimarisha miundombinu na wote Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote ni mashahidi, tumeipeleka fedha ya kutosha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, maabara na vyumba vingine pamoja na vifaa mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa mikakati hii yote inasababisha kuwa na elimu bora nchini na unapotoa elimu bora, unatoa

matokeo yaliyo bora na vijana wanaopata matokeo hayo, sasa wanaweza kuziona fursa zao na kuweza kuzitumia. Kwa hiyo, mkakati wa Serikali unaendelea na tutaendelea kupokea ushauri wenu kuona naona nzuri ya kuboresha Sekta ya Elimu ili tuweze kufikia hatua nzuri, asante. (*Makofii*)

SPIKA: Swali la mwisho la Mhesimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Babati Mjini uliza swali lako tafadhali.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mhesimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa niulize swali kwa Waziri Mkuu, ni azma ya Serikali yetu na ni Sera ya Serikali yetu kuwapatia wananchi maji safi na salama lakini kwa bei nafuu. Nafahamu pia mchakato wa Serikali kupandisha bili za maji kuititia mamlaka za maji kufanya *public hearing* na mwisho *EWURA* waweze kufanya maamuzi ya bili hizo.

Mhesimiwa Spika, *EWURA* wamemaliza mchakato bahati mbaya sana maoni ya wananchi hayajazingatiwa, bili hizi za maji kote nchini zimepanda kwa zaidi ya asilimia 80. Mfano, mtumiaji wa maji nyumbani alikuwa analipa *unit* 1 kwa shilingi 1,195 imepanda kuanzia hapo mpaka 1,800. Naomba nifahamu kauli ya Serikali juu ya ongezeko hili la zaidi ya asilimia 80 ya bili za maji nchini wakati wananchi waliomba kwamba bili hizi zisipande? (*Makofii*)

SPIKA: Mhesimiwa Waziri Mkuu majibu tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mhesimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mhesimiwa Gekul, Mbunge wa Babati Mjini kama ifuatavyo:-

Mhesimiwa Spika, azma ya Serikali katika kutoa huduma mbalimbali nchini bado ni njema na inawaangalia uwezo wa Watanzania mpaka yule mwananchi wa chini wanaweza kumudu kugharamia gharama hizo kwa uwezo wake wa kifedha. Umeeleza upo mchakato unaendelea na umeishia mahali ambapo gharama zimepanda kwa asilimia 80. Sisi Serikali tumetoa mamlaka kwenye hizi wakala ili kufanya mapitio na mapitio hayo lazima yaangalie uwezo

wa wananchi wenyewe nchini ili wawezeshe wananchi kupata huduma hiyo kwa urahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nimepata taarifa kwamba *EWURA* na Wizara ya Maji kuitia wakala wamekaa vikao vyao na sasa wameshatoa taarifa ya mwisho ya gharama hizo na zimefikia kwa kiwango ulichokitaja ambacho kimepanda kwa asilimia 80 lakini utaratibu Serikalini ni kwamba baada ya kuwa maazimio hayo yamefanywa, wanatoa taarifa Serikalini. Nashukuru kwamba umetuambia hilo na tumepata taarifa kwamba hata wadau hawakuweza kupata fursa ya kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni jukumu la Serikali sasa baada ya kupata matokeo yale, baada ya wao mjadala wao wataleta Serikalini tuone kwamba je, viwango walivyotoa vinawezesha Watanzania kupata huduma hiyo? Na tutakapogundua kwamba hawawezeshwi kupata huduma hiyo, basi Serikali itafanya maamuzi mengine dhidi ya hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikutake ufanye subira, *EWURA* walete matokeo ya vikao vyao na mapendelekezo yao, Serikali tutafanya maamuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Maji. Tukishawapa taarifa hiyo ya mwisho ndiyo itakuwa ndiyo bei ambazo zitakuwa zinatumika na mamlaka hiyo, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana, muda wetu wa nusu saa umeisha. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa heshima uliyotupatia kuweza kujibu maswali ya Waheshimiwa wabunge, ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaendelea na maswali ya kawaida, Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali ya kawaida TAMISEMI, Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini ndiyo atakuwa wa kwanza kuuliza swali na kwa niaba yake nimuite Mheshimiwa Zaynabu Vulu.

Na. 281

Shamba la Mitamba – Kibaha

MHE. ZAYNABU M. VULU (K.n.y. MHE. SILYVESTRY F. KOKA) aliuliza:-

Shamba la uzalishaji wa Mitamba Kibaha lipo katikati ya Mji wa Kibaha na limezungukwa na makazi ya watu:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya matumizi ya eneo hili kwa ufanisi zaidi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, tafadhali!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais –TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali uliopo ni kutumia shamba la mitamba lilioko katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha kwa ajili ya uzalishaji wa chanjo za mifugo na kuendelea kuimarisha kituo cha uhalishaji cha kanda ili kuendeleza Sekta ya Mifugo. Tayari Halmashauri imepima eneo la hekta 1,037 ambalo halijavamiwa na kupatiwa hati

yenye namba 395140 ya mwaka 2011. Kwa sasa eneo hilo linatumika kwa majaribio na *Tanzania Veterinary Laboratory Agency (TVLA)* kwa ajili ya kufanya majaribio ya kuzalisha chanjo za magonjwa ya mifugo na kuweka kituo cha kanda cha uhamilishaji na tayari mitambo ya kuzalisha kimiminika cha hewa baridi ya nitrojeni imesimikwa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Zaynab Vullu, nilikuona tafadhali.

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri na juhudzi za Serikali kuhakikisha kunakuwa na kituo maalum cha kuzalisha mitamba, nina maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo hilo ni kubwa, na kwa kuwa eneo hilo tayari limeshakuwa na wakazi zaidi ya 300 kwenye sehemu inayoitwa Vingunguti na wakazi hao wako kwa muda mrefu sana, na wanajie ndeleza na wamejiendeleza kwa muda mrefu. Je, haioni sasa ni wakati wa Serikali kulitoa eneo hilo na kuwapa wananchi hao ili waweze kuishi kwa usalama na amani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa suala hili linahusu mambo ya mifugo na ardhi, hii Tanzania ni nchi ya amani, upendo na ushikamano, na Tanzania yetu ina wakulima, wafugaji, wafanyakishara na wafanyakazi sehemu mbalimbali. Kumekuwa na tatizo la migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Je, Serikali haioni sasa ikatafuta mbinu mbalimbali mbadala za kuepukana na migogoro hiyo kwa kuwapatia maeneo wafugaji wakakaa wakaweka mifugo yao na wakulima na wananchi wengine wakaishi kwa amani na utulivu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba eneo hili lilikuwa na hekta zaidi ya 1,000 na baada ya Serikali kugundua kwamba wananchi

wameshaingia eneo hili, wamejenga, wamejiendeleza, tumefanya tathmini, tumewaachia wananchi zaidi ya hecta 2,900 ili waendelee kufanya shughuli zao za maendeleo.

Sasa naomba tupokee pia hoja ya Mheshimiwa Mbunge ya kwenda kufanya tathmini tuangalie kazi ya kuzalisha mitambo ambayo inafanyika eneo hili, faida yake, lakini pia na huduma za jamii za wananchi halafu tutaona busara tunafanye ili tuweze kuamua, ama tuwaachie au tuendelee kuweka mifugo pale ya kuzalisha mitambo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili anazungumzia migogoro ya ardhi; muda mfupi uliopita Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoka kuzungumza hapa namna ambavyo Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla wamepokea jambo hili la migogoro na kwamba halpaswi kuendelea. Mheshimiwa Waziri umefanya kazi hiyo, lakini pia wakuu wa mikoa na wilaya wamepewa maelekezo, lakini Wizara ya Ardhi inafanya pia mpango mahususi wa matumizi bora ya ardhi, sasa hili nalo kama kuna mgogoro pale unaendelea naomba tulipokee tuwasiliane na wenzetu mamlaka katika eneo lile tulifanyie kazi. Nia ya Serikali ni kwamba migogoro isiwepo, tunahitaji wakulima, tunahitaji wafugaji na wananchi na shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo biashara ili waendelee kufanya kwa amani na waweze kuchangia pato ikiwa ni pamoja na kulipa kodi. Ahsante.

SPIKA: Tunaendelea, na swalii la Wizara ya Maji la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke. Mheshimiwa Genzabuke tafadhalii.

Na. 282

Kutokamilika kwa Miradi ya Maji – Kakonko na Kibondo

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Mwezi Novemba, 2018, Waziri wa Maji alifanya ziara Wilayani Kakonko na Kibondo na kukagua miradi ya maji

iliyokwisha tumia zaidi ya shilingi bilioni moja lakini haifanyi kazi:-

Je, ni lini miradi hiyo itakamilika?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Kanyasu, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Miradi ya Maji ya Muhange, Kiduduye na Nyangwijima iliyopo Wilaya ya Kakonko baada ya kujengwa na kukamilika kulijitokeza changamoto zilizosababisha chanzo cha maji cha Mradi wa Muhange kujaa tope na kusababisha kazi ya kuondoa tope mara kwa mara. Aidha, katika Miradi ya Maji ya Kakonko, Nyabibuye na Gwanumpu sababu kubwa zilizosababisha miradi hiyo kutokamilika kwa wakati ni uwezo mdogo wa fedha kwa wakandarasi waliotekeleza ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto zilizojitokeza katika Miradi ya Maji ya Muhange, Kiduduye na Nyagwijima, Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko kwa kushirikiana na Mkoa wa Kigoma imefanya mapitio ya usanifu wa miradi na kupendekeza namna ya kuboresha miundombinu na kutatua changamoto zilizopo ambapo ghamama za kufanya marekebisho ya miundombinu ya vyanzo vya maji (*intake structures*) imekadiriwa kuwa shilingi milioni 373.99. Serikali itatoa fedha hizo ili kuhakikisha marekebisho hayo yanafanya kwa upande wa Miradi ya Maji ya Kakonko, Gwanumpu na Nyabibuye. Halmashauri imechukua hatua kwa wakandarasi wanaochelewesha miradi kwa kuwaandikia barua ya kusudio la kuvunja mikataba endapo watashindwa kukamilisha miradi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko, miradi iliyotekeliza kipindi cha miaka mitano, miradi hiyo imetekelezwa katika Vijiji vya Nyankwi, Nyabitaka, Kibingo, Kagezi na Minyima. Miradi ya Maji ya Nyankwi, Nyabitaka na Kibingo inafanya kazi na Jumuiya za Watumiaji Maji (*COWSO*) zimekabidhiwa kuendesha na kusimamia miradi hiyo. Serikali itaendelea na marekebisho yaliyojitekeza katika Miradi ya Kagensi na Minyinya ili iweze kutoa maji kwa wakati.

SPIKA: Mheshimiwa Genzabuke nimekuona tafadhalii.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda wa miradi hiyo kutokukamilika umekuwa mrefu sana, je, Serikali iko tayari kupeleka pesa ya kutosha ili miradi hiyo iweze kukamilika?

Mheshimiwa Spika, swalii langu la pili; kwa kuwa Makao Makuu ya Wilaya za Kibondo na Kakonko upatikanaji wa maji umekuwa ni wa kusuasua, na wilaya hizo zina watu wengi kutohana na ongezeko la watu wengi wakiwemo wakimbizi, na zipo taasisi nyngi ambazo ziko pale zikiwemo hospitali, shule pamoja na ofisi za mashirika ya wakimbizi. Ni lini sasa Serikali itapeleka pesa katika Wilaya za Kakonko na Kibondo kumaliza tatizo la maji katika miji hiyo mikuu ya wilaya hizo? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swalii hilo Naibu Waziri, Mheshimiwa Constantine Kanyasu, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kutumia nafasi hii kumpungeza Mheshimiwa Mbunge kwa juhudhi zake kubwa za kuhakikisha kwamba anapigania akinamama wa Wilaya za Kakonko na Kibondo waweze kupata maji safi na salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimesema kwamba Serikali itatoa pesa ili iweze kukamilisha mradi ambao ulikuwa umekwama na tayari kazi hiyo imekwishafanyika, na sasa hivi Wizara inakamilisha taratibu ili kazi ambayo ilikuwa inasababisaha miradi hiyo isikamilike iweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, katika swalı lake la pili, naomba kumfahamisha kwamba katika Wilaya ya Kibondo, tayari Serikali ilipeleka pesa shilingi milioni 500 kwa ajili ya mradi wa maji, na katika Wilaya ya Kakonko taratibu zinaendelea ili waweze kupatiwa pesa kwa ajili ya kukamilisha, tunafahamu kwamba eneo hili lina watu wengi, na hasa wakimbizi kama alivyosema.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, uliza swalı lako fupi tafadhali.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Hivi karibuni Mheshimiwa Rais alizindua mradi mkubwa sana wa maji kule Arumeru Magharibi, lakini wakati huohuo Arumeru Mashariki kuna shida kubwa ya maji kiasi kwamba wananchi wanaoga na kunywa maji ya *shallow wells*. Je, ni nini mkakati wa Serikali kutatua changamoto hii? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara nimekuona umesimama, tafadhali.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, ni kwamba baada ya uzindizi wa mradi ule ambao ni mradi mkubwa sana wa maji katika Jiji la Arusha na viunga vyake likiwemo eneo la Arumeru Mashariki. Mikakati ya Serikali ni kutekeleza mradi huo ambao umeanza kutekelezwa mwaka huu wa fedha ambao utakamilika mwaka 2022 na vilevile kuweka mkazo kwenye uchimbaji wa visima virefu vyta maji kwenye eneo la Uwanja wa Ndege na eneo la Magereza ambalo litatosheleza kabisa maji katika Jiji la Arusha na viunga vyake, likiwemo Jimbo la Arumeru Mashariki. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini.

Na. 283

Kurasimisha Bandari Bubu – Tanga

MHE. MUSSA B. MBAROUK aliuliza:-

Katika Vijiji vya Kigombe Wilayani Muheza na Kipumbwi Wilayani Pangani kuna bandari bubu zinazotumika kwa uvuvi na kusafirisha abiria na bidhaa:-

Je, ni lini Serikali itarasimisha bandari hizo kwa kujenga gati pamoja na kituo cha forodha?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Atashasta Justus Nditiye.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina taarifa ya uwepo wa bandari bubu yaani bandari zisizo rasmi katika Mwambao wa Pwani pamoja na changamoto za kiusalama, kiulinzi na kiuchumi zinazoletwa na bandari hizo.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti matumizi ya bandari hizo, mamlaka zinazohusika zimeelekezwa kushirikiana na kuweka mikakati ya pamoja ya kudhibiti matumizi ya bandari hizo. Miiongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kutambua bandari zenye umuhimu kwa wananchi kiuchumi na kijamii

ili kuzirasimisha kwa kuziweka chini ya uangalizi wa vijiji vilivyo kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maelekezo hayo, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*) ilikamilisha zoezi la kukusanya taarifa za bandari Tanzania Bara na kubaini kuwa kuna bandari zisizo rasmi 208 katika Mwambao wa Bahari ya Hindi. Baada ya zoezi hilo, *TPA* iliainisha bandari ambazo zinafaa kurasimishwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifa Bunge lako Tukufu kuwa Bandari za Kigombe na Kipumbwi Wilayani Muheza na Pangani ni miongini mwa bandari 24 zenye umuhimu kwa wananchi kiuchumi na kijamii na zimeorodheshwa kwa ajili ya kurasimishwa.

Mheshimiwa Spika, hatua inayoendelea hivi sasa kuhusu bandari hizo ni kuzipanga katika madaraja (*classification*) ili kubaini zile ambazo zitachukuliwa na *TPA* moja kwa moja kwa kuziendesha baada ya kuboreshwa na kuendelezwa kwa miundombinu yake ikiwemo kujenga gati pamoja na kuweka kituo cha forodha, zile ambazo zitaendeshwa kwa mkataba na zile ambazo zitawekwa chini uangalizi wa halmashauri kwa maeneo husika. Kazi hii inatarajiwa kukamilika kabla ya kumalizika kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, baada ya urasimishaji huo, usimamizi wa sheria na udhibiti wa maeneo hayo utafuata.

SPIKA: Mheshimiwa Mbarouk, swali fupi la nyongeza.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini imekuwa ni kawaida ya Serikali kutupa matumaini halafu masuala haya yanachukua muda mrefu sana. Na ni ukweli usiofichika kwamba bandari hizi zinatumika na bidhaa zinazotoka Zanzibar mara nyingi zinapitia katika bandari hizi. Sasa ninataka kujua, je, kwa nini bidhaa hizi zinapopita kutoka

Zanzibar zikipita katika bandari hizi zinatozwa ushuru mara ya pili?

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili, ni kusema kwamba kwa kutumia bandari hizi, kwa kuzirasimisha, tutakuwa tunaongeza mapato ya Serikali lakini pia ajira kwa watu wetu zitaongezeka lakini vilevile pia ajali zitapungua. Sasa ni lini ujenzi wa hiyo gati aliyosema Mheshimiwa Waziri na kujenga hivi vituo vya forodha utaanza rasmi?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer Nditiye*, Tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, kwenye majibu yangu ya msingi nimeeleza changamoto iliyopo kwenye bandari bubu na sisi kama Serikali tunaitambua changamoto iliyopo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna majahazi huwa yanachukua bidhaa kutoka upande wa pili wa Jamhuri yetu kuleta upande wa Tanzania Bara, na Serikali kupitia Jeshi la Polisi wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha kwamba biashara hiyo haifanyiki, na sina taarifa za moja kwa moja kwamba huwa wanatozwa ushuru kwa sababu wanatumia bandari bubu ambapo hatuna vituo vyetu vya forodha. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuzidhibiti hizo bandari bubu na tunaendelea kuzidhibiti kuhakikisha kwamba hazileti bidhaa ambazo si rasmi.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la pili; nimekwishaeleza kwamba kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha tutakuwa tumeshapanga mikakati yote na mwaka ujao wa fedha tutaanza sasa kutengeneza magati kwa sababu ni bajeti kubwa inayotumika katika kutengeneza magati ya kurasimisha hizo bandari bubu.

SPIKA: Tunaendelea na swali la Susanne Peter Massele, kwa niaba yake Mheshimiwa Tunza Malapo tafadhalii.

Na. 284

Kiwanja cha Ndege – Mwanza

MHE. TUNZA I. MALAPO (K.n.y. MHE. SUSANNE P. MASELLE) aliuliza:-

Kutokana na umuhimu wa kimkakati katika nyanja mbalimbali za maendeleo kwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa na nchi yetu kwa ujmla:-

Je, ni lini Jiji la Mwanza litakuwa na uwanja wa ndege unaoendana na hadhi na ukuaji wa kasi wa jiji hilo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika juhudzi za Serikali za kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege, Serikali iliingia mkataba wa ukarabati mkubwa wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza Oktoba, 2012 na Kampuni ya *Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd (BCEG)* wenye thamani ya shilingi 89,291,995,422. Mchanganuo wa fedha hizi ni kuwa Serikali ya Tanzania inachangia asilimia 82.5 na wabia wa maendeleo asilimia 17.5.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa zinazofanyika katika uboreshaji huu ni pamaja na kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege (*runway*) kutoka mita 3,300 kwa upana wa mita 45 hadi mita 3,800 kwa upana wa mita 45; kujenga majengo ya kuongozea ndege (*control tower*); kituo cha hali ya hewa; jengo la kupokea na kuhifadhi mizigo; kuboresha na kupanua maegesho ya ndege (*aprons*); kujenga barabara za viungio (*taxways*) na kituo cha umeme (*power station*).

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2019, ujenzi wa kazi hizi za mradi umefikia asilimia 87 na mkandarasi anaendelea vizuri na kazi ya ujenzi na anatarajia kumaliza kazi zote ifikapo Juni, 2019.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ipo kwenye mazungumzo na wabia wa maendeleo ambapo wameonyesha nia ya kufadhili jengo kubwa na la kisasa la abiria litakaloendana na maboresho haya makubwa ya kiwanja pamoja na hadhi ya Jiji la Mwanza. Tunategemea kufikia Mwezi Oktoba, 2019, kazi za ujenzi wa jengo hili zitakuwa zimeanza.

SPIKA: Mheshimiwa Tunza, swalii la nyongeza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Jiji la Mwanza unahuisha makazi ya watu katika Kata za Shibula na Kahama, na kwa kuwa Mwezi Januari mwaka huu timu ya Mawaziri wanane ilifika katika kata hizo na kuwaahidi kwamba watalipwa fidia zao. Sasa nataka kujua; Serikali inawaambia nini wananchi wa kata hizo kuhusu fidia hizo?

Mheshimiwa Spika, swalii langu la pilli; kumekuwa na kusuasua katika ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Mtwara, na taarifa zilizopo ni kwamba kwa sababu hakuna fedha za uhakika. Swalii langu; je, ni lini Serikali itapeleka fedha hizo ili uwanja ule uweze kukarabatiwa kwa kiwango kinachokubalika? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Majibu ya swalii lo Mheshimiwa Naibu Waziri nimikuona tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwenye eneo hili la Uwanja wa Ndege wa Mwanza wapo wananchi ambao wanadai fidia. Na ni kweli kuna timu ya Mawaziri ambao wanahusika na ulipaji wa fidia hii

walikuwa na jukumu la kushughulikia ili wananchi waweze kulipwa mapema. Ninawaambia nini wananchi wa maeneo haya; ninawaambia ule utaratibu unakamilishwa na ni mapema kadri itakavyowezekana watalipwa hizi fidia, kwa hiyo wasubiri tu mambo yanaendelea kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, na niseme na pia Mheshimiwa Mbunge Mabula yuko hapa, anafahamu kwa sababu karibu kila siku anafuatilia juu ya ulipaji wa fidia ya wananchi ambao wengi wako pia kwenye eneo lake. Kwa hiyo wananchi hawa wasiwe na wasiwasi, tunalifuatilia na kulishughulikia suala hili ili waweze kulipwa mapema iwezekanavyo. Lakini pia wakilipwa kuna kazi ambayo nimeitaja itafanyika ili iweze kufanyika, na utaratibu ulivyo ni wananchi walipwe kwanza fidia ili maboresho kadhaa yaweze kuendelea katika uwanja huu.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu Uwanja wa Ndege wa Mtwara, labda nimkumbushie tu Mheshimiwa Mbunge, atakuwa amesahau, ni hivi karibuni tu Mheshimiwa Rais alivyofanya ziara Mtwara alitoa maelekezo na sisi kama Wizara maelekezo yale kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, kuna fedha zilitolewa na kazi inaendelea vizuri katika ujenzi huu wa Uwanja wa Ndege wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, na nikwambie Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu tumejipanga kuhakikisha kila wakati tunaboresha uwanja huu na mwaka wa fedha huu unaokuja Bunge hili, Bunge lako limetupitishia fedha ambazo ni takribani bilioni 4.5, mmetuidhinishia ili sasa hii kazi isilale, kwamba kwa maana ya fedha zilizokuepo katika mwaka huu wa fedha na mwaka ujao tuna fedha za kutosha, hatutasinzia kwenye ujenzi wa uwanja, maboresho yatafanyika tuweze kukamilisha na wananchi waweze kupata huduma ya Uwanja wa Ndege huu wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana, Wizara ya Maliasili na Utalii swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge

wa Same Mashariki, uliza swali lako Mheshimiwa Mwenyekiti wa *PAC* sasa.

Na. 285

Serikali Kusaidia Uanzishwaji Misitu ya Vijiji – Same Mashariki

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Same Mashariki wako tayari kuanzisha misitu ya vijiji kwenye maeneo yenye ukame kama vile Kata za Bendera, Kihurio, Ndugu na Maore ili kuhifadhi mazingira.

Je, Serikali ipo tayari kuanzisha miradi ya utunzaji wa mazingira katika kata tajwa kwa kufundhisha wanavijiji uanzishwaji wa misitu ya vijiji?

SPIKA: Majibu ya swali hilo tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Same kiikoloji na kijiografia imegawanyika katika Kanda kuu mbili, yaani ukanda wa mlimani ambapo hali yake ya hewa ni nzuri ukilinganisha na ukanda wa tambarare ambapo hali ya hewa ni ukame. Kwa maana hiyo, kata zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge zipo katika ukanda wa tambarare na kwa bahati nzuri zina uoto wa misitu.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweka utaratibu wa kushirikiana na halmashari za wilaya na wananchi katika kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa maliasili. Mathalani, katika halmashauri ya Wilaya ya Same, utunzaji

wa mazingira umehusisha utoaji wa elimu kwa wananchi na kuanzisha Kamati za Maliasili na Misitu, kuandaa mipango ya usimamizi na kutunga sheria ndogo za usimamizi wa maliasili. Vilevile, kupitia utaratibu huu wananchi wanashirikiana na Wizara na halmashauri kupanda miti kwenye maeneo ya wazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kuendelea kutekeleza azma ya kuwasaidia wananchi wa Kata za Bendera, Kihurio, Ndungu na Maore kuhusu shabaha yao ya kutunza misitu hiyo ya asili. Hii inatokana na ukweli kwamba pamoja na kuwa vijiji hivi viko nyanda za ukame bado vina uoto mzuri wa asili ambao ukitunzwa vizuri utasaidia kuboresha hali ya hewa, uhifadhi wa baionuai na huduma za kijamii kama maji.

SPIKA: Mheshimiwa Naghenjwa nilikuona

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kweli jibu limekuwa la ujumla sana nipayende tu kusema kwamba Kata za Bendera, Ndungu, Kihurio zina ukame mkubwa sana na hata hivi tunavyoongea hakuna hata msitu mmoja ni Kata ya Maore tu ambayo ina kamsitu kadogo kaasili.

Swali langu la pili ni je, Serikali iko tayari kusaidiana na wanavijiji kutenga maeneo kisheria ambayo yatakuwa ni misitu ya vijiji badala ya kusema halmashauri inafanya wakati hatuoni kwamba sehemu hizi zinatendewa haki kwa kuotesha miti ambayo itapunguza ueneo wa jangwa katika eneo hili? Ahsante

SPIKA: Majibu ya maswali hayoMheshimiwaNaibu Waziri wa Maliasili na Utalii tafadhali

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba zoezi hili limekuwepo la uhamasishaji wa upandaji miti na Wizara yangu ina mkakati wa katika mwaka 2016 – 2021 kupanda miti milioni mia mbili na themanini katika maeneo

mbalimbali ya nchi. Tumechukua mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge kwenda katika eneo husika kwa kushirkiana na Serikali za vijiji ili vijiji vyenyewe vitoe ridhaa ya maeneo ambayo vinataka tuyatenge na kuyachukua na kuyaboresha kwa ajili ya misitu hiyo lakini uzoefu unaonesha sehemu nydingi ambazo tumekwenda baada ya kuyachukua maeneo haya na kuyaboresha wanavijiji tena wamerudi na kuyadai maeneo haya waweze kurejeshewa. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge yuko tayari kutoa ushirikiano Wizara yangu itakuwa tayari kutoa ushirikiano huo wa kwenda kuhamasisha upandaji miti katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini katika swali lake la pili tutatuma wataalam wetu katika Wizara yetu kwenda kuangalia uwezekano wa kuanzisha vitalu vya miti katika Kata hizo alizozitaja Mheshimiwa Mbunge.

SPIKA: Ahsante sana kwa majibu hayo kwa sababu ya muda Waheshimiwa mkiangalia saa mtaiona, tunakwenda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka. Mheshimiwa Kuchauka uliza swali lako tafadhali.

Na. 286

Ukiukwaji wa Haki za Binadamu unaofanywa na Polisi Nchini

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA aliuliza:-

Wakati Jeshi la Polisi likitekeleza majukumu yake kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na hata uvunjifu wa Katiba kwa kisingizio cha maagizo kutoka juu:-

(a) Je, ni mamlaka gani iko juu ya sheria?

(b) Je, maagizo hayo yanapopingwa na sheria za nchi na kukiuka haki za binadamu nini hukumu ya yule aliyetendewa kinyume cha sheria?

(c) Je, huyu anayekutwa na kadhia hii hana haki ya kumjua huyo mwenye mamlaka ya juu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Mambo ya Ndani ya Nchi, *Engineer Masauni*, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI (MHE. ENG. HAMAD Y. MASAUNI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zillizopo kwa msingi huo Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20 inampa mamlaka polisi kutumia nguvu ya wastani anapokuwa anatekeleza kazi yake kulingana na mazingira yaliyopo. Aidha, hakuna mamlaka ya juu katika Jeshi la Polisi iliyo juu ya sheria kiasi cha kuvunja sheria.

(b) Mheshimiwa Spika, nchi yetu inafuata misingi ya Demokrasia na Utawala Bora ambapo mtu yeoyote anao uwezo wa kwenda kutoa malalamiko yake kwenye chombo chochote cha kisheria na hauta stahiki zikachukuliwa.

(c) Mheshimiwa Spika, hakuna mamlaka inayomzuia mtu kumuona mtu ambaye anadhani atamsaidia kutatua tatizo Lake Linalomsibu.

SPIKA: Mheshimiwa *Engineer Chiza* nilikuona uliza swali la nyongeza.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Kuchauka ameuliza maswali ambayo yanahusiana na utendaji kazi wa Jeshi la Polisi, na kwa kuwa yamo masuala ya ukiukwaji wa haki za binadamu. Je, Mheshimiwa Waziri

uko tayari sasa ukutane na Mheshimiwa Kuchauka ili aweze kukupa maelezo kama yapo *specific* uweze kuyafanyia kazi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa swali lake zuri ameuliza suala kitaalam sana na nimuhidi kwamba huo ndiyo utaratibu mzuri kwa pale ambapo wawakilishi wa wananchi kama Wabunge wanapoona kuna tatizo *Specifically* limejitokeza kwa wananchi wao Serikali tupo kwa sababu hiyo. Kwa hiyo, wakati wowote Mheshimiwa Kuchauka atakapokuwa amerejea tutakuwa tayari kukaa naye tuweze kujua kama anakusudia kuna tatizo mahsusि ambalo analifahamu na uthibitisho wa tatizo hilo ili tuweze kusaidiana kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda sasa tuendelee na kutambulisha wageni.

Tunao wageni wengi kidogo, ninao wageni ambapo ni kutoka Ubalozi wa Usvis hapa Tanzania tunaye Mheshimiwa Balozi Tinguelly Mattli, Balozi wa Usvis nchi Tanzania, karibu sana Mheshimiwa Balozi ametupa ushirikiano mkubwa sana katika nchi yetu, naambiwa karibu anaagaaga hivi karibu kuondoka naomba tumpigie makofi kwa kazi yake nzuri ambayo amefanya nchini kwetu. Ahsante sana Mheshimiwa Balozi amefuatana na Afisa Balozi Moritz Burrichter, ahsante sana. (*Makofi*)

Wengine niwageni wa Mheshimiwa Dkt Hamis Kigwangala Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni watendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii ambao ni Katibu Mkuu Profesa Adolf Mkenda; Naibu Katibu Mkuu Dkt. Aloyce Nzuki; Mkurugenzi wa Idara ya Sera na Mipango Dkt. Iddi Mfundu; karibu sana, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TANAPA Jeneral George Waitara, karibu sana Jenerali; Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TTB Mheshimiwa Jaji Thomas Mihayo; Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Ngorongoro Profesa Abiudi Kaswamila; Mwenyekiti wa Bodi ya TAWA Meja Jenerali

Mstaafu Hamis Semfuko; Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya TFS Brigedia Jenerali Mbaraka Mkeremy, karibu; Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri NCTNdugu Imani Kajura; Mkurugenzi Idara ya Wanyamapori Ndg. Maurus Msuha, karibu sana.

Kamishna Mhifadhi Mamlaka ya Ngorongoro - Dkt. Freddy Manongi; Kamishna Mhifadhi Shirika la Taifa Uhifadhi - Ndugu Allan Kijazi; Mkurugenzi Idara ya Misitu na Nyuki - Dkt. Ezekiel Mwakalukwa; Mkurugenzi Idara ya Utalii - Ndugu Deogratius Mdamu; Mkurugenzi Idara ya Mambo ya Kale - Ndugu Digna Tillya; Mtendaji Mkuu Wakala wa Misitu Tanzania - Profesa Dosantos Silayo na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Bodi ya Utalii - Ndugu Devotha Mdachi. (*Makof*)

Waheshimia Wabunge, pia yuko mke wa Mheshimiwa Waziri shemeji yetu Dkt. Bayoum Awadh karibu sana, karibu sana mama na juzi alituandalia futari, tunashukuru. (*Makof*)

Lakini pia yuko mrembo wa dunia wa Utalii (*Miss Journalism World 2018*) kutoka Ukraine Miss Nina Yevtushenko, *can you stand up again, jamani huyo ndiyo mrembo 2018 nafikiri mnaona wenyewe ahsante sana thank you very much.* (*Makof*)

Wageni wengine 99 wa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangwala ambao ni Walimu Wakuu kutoka Wilaya ya Nzega Mkoa wa Tabora wakiongozwa na Ndugu Katunzi Kihembe, karibuni sana sana Wanyamwezi ninyi, mmependeza kweli kweli walimu. Wanatoka Katunzi safi sana. (*Makof*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wanne wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ni watoto wake wakiongozwa na Ndugu Jackline Kanyasu, watoto wa Mheshimiwa Waziri wale kule karibuni sana. (*Makof*)

Pia wapo wageni 20 wa Mheshimiwa Kanyasu ambao ni Wanakikundi Kazi cha Misitu cha Baraza la Biashara wakiongozwa na Ndugu Ben Sulus, ahsante sana. (*Makof*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Kanyasu ni Waheshimiwa Madiwani kumi kutoka Jimbo la Geita Mjini. Mkoa wa Geita wakiongozwa na Ndugu Leonard Bugomora, ahsante sana. (*Makofii*)

Pia wapo watumishi sita wa Rafiki Wildlife Foundation kutoka Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Mchungaji Clement Matwiga, karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni 15 wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni waratibu wa Shindano la *Miss World Journalism, 2018* wakiongozwa na Mratibu wa *Miss Journalism* Ndugu Samwel Malugu. (*Makofii*)

Pia kuna wageni 11 wa Mheshimiwa William Tate Ole Nasha kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu wakiongozwa na Mkurugenzi Idara ya Habari Utafiti na Mipango Dkt. Marcelina Baitilwake, wale kule na ahsanteni sana karibuni. (*Makofii*)

Wageni 15 wa Waheshimiwa Wabunge wenye mahitaji maalum ambao ni wanamichezo wa mpira wa miguu kwa watu wenye mahitaji maalum wakiongozwa na Ndugu Peter Sarungi, karibuni sana sana, naomba msimame tena hilo kundi naomba msimame tena endeleeni kusimama. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwasomee kidogo ujumbe wa kutoka kwa Mheshimiwa Riziki Lulida anasema; "Waheshimiwa Wabunge Tanzania imeteuliwa mwenyeji wa mashindano ya shirikisho la mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu Afrika Mashariki yanayotarajiwu kufanyika kuanzia tarehe 22 hadi tarehe 30 Juni, 2019. Mashindano hayo yatashirikisha Nchi tano Wanachama Tanzania Bara, Zanzibar, Uganda, Kenya na Rwanda na yatakuwa ya kwanza kufanyika katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, mashindano haya yameanzishwa kutokana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa haki za watu wenye ulemavu wa

mwaka 2005 kifungu namba 30 cha mkataba huo pamoja na kifungu namba 50 cha sheria Na. 9 ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2010 ambayo pia inatoa haki ya watu wenye ulemavu kushiriki katika michezo."

"Kutokana na uzito wa mashindano haya kufanyika hapa nchini Wabunge wenye mahitaji maalum pamoja na Wabunge wadau wa masuala ya watu wenye ulemavu Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Venance Mwamoto na Mheshimiwa Margaret Sitta kwa kushirikiana na Serikali kwa maana ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa Utamaduni na Michezo, wameandaa kamati ya pamoja ili kufanikisha jambo hili. Zaidi ya shilingi milioni 800 zinahitajika ili kufanikisha mashindano haya."

"Kwa heshima kubwa tunaomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie kuhamasisha ili tuchangie kwa kiasi fulani ili kufanikisha mashindano hayo na hiyo ni moja ya timu yetu ambayo itashiriki." (*Makof*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge shilingi 100,000?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

SPIKA: Wanaoafiki?

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja illiamuliwa na kuafikiwa kuchangia shilingi 100,000)

SPIKA: Ahsante sana nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge nawashukuruni sana sana, basi timu yetu Waheshimiwa Wabunge wanachangia tunawatarajia mtafanya vizuri katika mashindano haya na tutakuwa tunawafatilia kwa karibu sana vijana wetu. Ahsanteni mnaweza mkakaa. (*Makof*)

Tangazo la kawaida kutoka ofisini kwetu nawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba tumepokea

ombi kutoka *Commonwealth Parliamentary Association* Makao Makuu, London Uingereza kuhusu kuwasilisha jitihada na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Bunge letu katika kupambana na unyanyasaji wa Kimtandao kwa Wabunge hususan Wabunge wanawake. (*Makofii*)

Kwa kuzingatia kuwa Bunge la Tanzania ni Mwanachama wa Nchi za Jumuia ya Madola naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa ofisi ya Bunge imeandaa dodoso kwa ajili ya Wabunge wote kujaza na kutoa taarifa mbalimbali zinazohusiana na masuala mbalimbali ya unyanyasaji wa kimtandao kwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo la dodoso hili ni kupata taarifa za hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Bunge la Tanzania katika kupambana na unyanyasaji wa kimtandao unaofanywa dhidi ya Wabunge na hususan Wabunge wanawake katika kutekeleza majukumu yao.

Kwa hiyo, naomba dodoso hilo mliljaze Waheshimiwa Wabunge mkilionia liweze kutusaidia kuona namna gani ambavyo tunaweza tukakomesha tabia hii ya hovyo.

Mambo mawili madogo ya mwisho Waheshimiwa Wabunge wakati wa kukamata shilingi wakati tunapohitimisha hoja mbalimbali zinazokuwepo hapa baadhi ya wenzetu tunasimama na tunapenda jambo ambalo tunasemea lijadiliwe na wenzetu lakini hatujui kwamba au naomba niwakumbushe kwamba jambo hilo unalosimama kuli-raise na ukataka lijadiliwe na wengine nia yako ni kwamba mwisho wa siku Bunge lifanye maamuzi either or kwa hiyo, lazima anayekaa kwenye kiti mwisho ahoji Bunge linakubaliana na anayetoa hoja au linapingana naye.

Sasa wengi ambao tumekuwa hatukubali hoja zao ni kwa sababu inakuwa anachokisema anataka tu kijadiliwe lakini ikifika mahali pa maamuzi utashindwa kujua mnataka kuamua nini sasa? Kwa hiyo, naomba wale ambao wanapata fursa hiyo ujipange katika namna ambavyo hoja yako mwisho wa siku inaliongoza Bunge katika ama

kukubaliana na wewe, ama kutokukubaliana na wewe huo ni ushauri wa jumla tu. Ili kusaidia kazi yetu kuwa nyepesi zaidi hapa mbele.

Mwisho niwajulisse mnafahamu kwamba uchaguzi... naambia kuna mabondia kike, wapo wapi? Oooooh!

MBUNGE FULANI: Na wenyewe wachangiwe laki moja moja.

SPIKA: Ahsante sana eeeeeh! Hebu tuwaone tena kidogo hebu wekeni hivi tuone aaaah! Safi sana hawa ni wageni wa bondia mwenzao Mheshimiwa Sophia sasa sijui ni Sophia yupi. Aaah Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ahsante sana tunashukuru. Kwa hiyo, leo wale Wabunge mnajifanyaga ma-boxer leo chungeni sana nina wageni maalum mabondia hapa. (*Kicheko*)

Mnafahamu South Africa walikuwa na uchaguzi juzi, ambao umeisha hivi karibu sana. Sasa jana Bunge la Africa Kusini walifanya uchanguzi wa kumpata Spika wao na wamempata Spika mwana mama. Spika huyu anaitwa Thandi Modise ni Meja Jenerali Mstaafu wa Jeshi ni mpigania uhuru maarufu alikuwepo kuhu kwetu miaka hiyo, katika harakati za kutafuta uhuru na kadhalika tunamfahamu vizuri tumekuwa naye katika mikutano mingi hasa ya CPA. Ni mwenzetu ni *colleague* kwa hiyo tutamwandikia kumpongeza sana kwa nafasi hiyo aliyopata, *very challenging*. Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA KAMATI

KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE

SPIKA: Hoja za Kamati Waheshimiwa Wabunge ngoja niangalie hapa kidogo ni taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa kamati. Leo ni siku ya Maliasili na Utalii kwa

hiyo zoezi hili litachukua muda mfupi sana ili tuweze kuendelea na Wizara kama kawaida. Mheshimiwa Mwenyekiti tafadhalii.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

SPIKA: Ningependa kuokoa muda *unless* inahusiana na jambo hili?

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, ndio

SPIKA: Haya Mheshimiwa Mwambe.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mhehimiwa Spika, mbele yetu tuna hoja iliyotoka

SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukae kidogo tu.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mhehimiwa Spika, mbele yetu tuna hoja imetoka Kamati ya Maadili na historia ya jambo hili lilianzia ndani ya Bunge hili baada ya wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika kutuletea taarifa kwamba Mheshimiwa Masele kuna mambo ambayo ameyafanya ambayo ungependa kamati ya madili iyashughulikie. Sasa kadri ya utaratibu wa kawaida wa kibinadamu na masuala kiutawala bora isingependeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika uwe kiongozi wa jambo hili. Kwa hiyo, niombe meza yako labda ituambie kwa sababu kutakuwa na mijadala na mambo mengine ili kuweza kupata haki kusema *yes or no*.

SPIKA: Kwa sababu sio lengo letu kupoteza muda naomba ukae tu. Hakuna jambo ambalo litaenda kamati ya maadili ambalo Spika hajapeleka halipo. Labda unitajie kwamba lipo aina fulani ambalo Spika hawezi kupeleka. Hakuna jambo ambalo litaenda kwenye kamati yoyote mnayoshughulikia ambao Spika hajapeleka, na Spika kazi

yake hapa yeye hana kura hana nini kazi yake ni kuongoza kikao. Wenyewe kura wenye maamuzi ni Wabunge ninyi wenyewe. Kwa hiyo, kwa kuwa Mwambe maamuzi ni yako na sio yangu wala usiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti tafadhali tuendelee.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mhehimiwa Spika, naomba kuwasilisha taarifa ya haki maadili na madaraka ya Bunge kuhusu shauri linalomuhusu Mheshimiwa Stephen Julius Masele Mbunge la kudharau Bunge, Mamlaka ya Spika, kulifedhesha Bunge na kuchonganisha mihimili ya dola.

Mhehimiwa Spika, kwa mujibu Kanuni 4(3) ya Nyongozea ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu uchunguzi wa shauri uliotuletea la Mheshimiwa Stephen Julius Masele Mbunge kutokana na tuhuma za kudharau mamlaka ya Spika na kuchonganisha viongozi.

Mhehimiwa Spika, baada ya kamati kuchunguza vitendo alivyolalamikiwa ilijiridhisha kuwa vinakiuka maadili kutokana utoro Bungeni, kumdhara Spika hasa kwa kukaidi kurejea nyumbani hata baada kuandikiwa barua kadhaa ambazo alikiri kupokea. Mheshimiwa Masele ameabainika kumchonganisha Spika na viongozi wengine kwa maneno ya uwongo.

Mhehimiwa Spika, kamati ilimhoji Mheshimiwa Masele kuhusiana na tuhuma hizo ambapo alipewa muda wa kutosha wa kujieleza na aliwasilisha nyaraka mbalimbali za utetezi wake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa mashtaka na ushahidi na hatimaye ilimpata na hatia kwa makosa manne ambayo ni yafuatayo:-

- (i) Kuandika ujumbe MMS wa maneno ya uongo na kuutuma kwa viongozi.
- (ii) Kusafiri kwenda nje ya nchi bila kupata kibali cha Spika.
- (iii) Kutotii wito wa Spika uliomtaka kurejea Tanzania ili kuhojija na Kamati ya Maadili.
- (iv) Kuchonganisha viongozi kwa kutoa taarifa zisizokuwa na ukweli alipokuwa anahutubia Bunge la *African PAP*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ushaidi uliokuwa mbele ya kamati haukuweza kudhibitisha kosa la kugushi nyaraka kwa kuwa suala hili lilihitaji uchunguzi wa kitaalam ya kijinani yaa *forensic investigation*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumtia hatiani kamati ilijadili kuhusu adhabu ilizingatia ukubwa wa makosa na athari alizosabisha utetezi alioutoa, kuomba radhi kwake, umri alionao na uzoefu wake kisiasa pamoja na umuhimu wa nafasi anayoitumikia katika Bunge la PAP. Hivyo kamati iliona makosa yalifanywa yanatakiwa kupigwa vita na kukemewa vikali na Bunge letu ili yasijirudie na pia iwe somo kwa Wabunge na uma wote kwa ujumla.

Mhehimwi Spika, kwa ufupi huo ndio uchambuzi na mapendekeza ya kamati kuhusu shauri hili. Naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuadhimia mapendelezo ya kamati kwenye taarifa ya kamati. Aidha, naomba taarifa yote ya kamati ilivyo kwenye kitabu ambacho Wahehimwi Wabunge wamegaiwa iinginzwe katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, hili ni Azimio la Bunge kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya Mheshimiwa Stephen Julius Masele imetolewa chini yakifungu cha 54(1) na (3) na (6) na Kanuni ya 74(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016.

Kwa kuwa, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama moja ya Mhimili linaongozwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 sheria na kanuni za kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016 zilizotunga na Bunge kwa ajili ya kuliongoza katika kutekelea shughuli zake;

Na kwa kuwa, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa vyama mbalimbali vya kibunge duniani ikiwemo chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola yaani *Common Wealth Parliamentary Association*, Umoja wa Mabunge ya ulaya, yaani *Inter-parliamentary Union*. Bunge la Afrika yaani *Pan African Parliament* jukwaa la Mabunge ya nchi za Kusini mwa Afrika *SADC Parliament Forum* Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki *ELA* na umoja wa mabunge ya nchi za Maziwa Makuu;

Na kwa kuwa, Mheshimiwa Steven Julius aliachanguliwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuliwakilisha Bunge hili katika Bunge la *African PAP* baada ya kushinda kwenye uchaguzi;

Na kwa kuwa mnamo tarehe 13 Mei, 2019 Mheshimiwa Spika aliyasilisha shauri hili dhidi ya Mheshimiwa Stephen Masele Mbunge kuhusu tuhuma za kuchongaisha viongozi kugushi nyarakka, kutohudhuria vikao vya Bunge bila kupata kibali cha Spika, kudharau wito ulimtaka kurejea Tanzania ili afike mbele ya kamati ya Haki Maadili na Madaraka ya Bunge kwa mahojiano kuhusu tuhuma zilizokuwa zinamkabili;

Na kwa kuwa, Kamati ya Haki maadili ya Bunge ilichunguza suala la Mheshimiwa Stephen Julius Masele Mbunge na kubaini kuwa amekiuka masharti ya kifungu 26(e) cha sheria ya kinga, Haki na Madaraka ya Bunge kwa mamlaka ya Bunge kwa vitengo vyake vya kudharau mamlaka ya Spika kudharau Bunge na kuchonganisha viongozi, kutohudhulia baadhi ya mkutano wa Bunge la Bajeti kwa kusafiri nje ya nchi bila kupata kibali cha maandishi cha Spika;

Na kwa kuwa, vitendo hivyo vya Mheshimiwa Stephen Julius Masele vinalishushia Bunge na viongozi wa Bunge hadhi na hivyo kuleta taswira mbaya mbele ya umma na watanzania na mbele ya Jumuiya ya Kimataifa;

Na kwa kuwa, kamati ilimtia hatiania Mheshimiwa Stephen Julius Masele kwa kutenda kinyume cha kifungu cha 26(e) kinga madaraka na Haki za Bunge sura ya 296 na kanunu ya 146(4) ya Kanuni za Bunge toleo la Januari, 2016;

Na kwa kuwa, kanuni ya 74(4) (5) na (6) bunge linaweza kupendekeza adhabu yoyote kwa kadri itakavyooona inafaa. Kwa kosa la kudharau mamlaka ya Spika;

Na kwa kuwa, kamati ilitafakari sana juu uzito wa makosa ya shahidi yallyolifdhesha Bunge kugonganisha na kufarakanisha viongozi wa mihimili kuwa sio vitendo vyema na vilevile kamati ilizingatia kuwa hii ni mara ya kwanza kwa Mheshimiwa Stephen Masele kufanya makosa nakuletwa kwenye kamati aidha, ilizingatia kuwa ye ye ni Mbunge kijana mwakilishi wa nchi katika Bunge la Afrika yaani PAPambapo si rahisi kupata nafasi ya uongozi kama anayoitumikia sasa.

Mheshimiwa Spika, kamati ilifikiria pia kuhusu pia kuhusu kitendo chake kukiri kosa na kuomba kamati imuombee msamaha kwa Mheshimiwa Spika ingawa aliendelea kulalamika kwamba Mheshimiwa Spika hakumtendea haki;

Hivyo basi, Bunge lina adhimia kwamba Mheshimiwa Stephen Julius Masele asimamishwe kuhudhuria mikutano mitatu ya Bunge kuanzia tarehe ya Azimo hili katika Mkutano wa 15 wa Bunge la Bajeti;

Kwa hiyo basi, Bunge linaadhimia kwamba lina kubaliana na kuitisha mapendekezo ya adhabu hiyo kwa Mheshimiwa Stephen Julius Masele kama ilivyopendekezwa na Kamati Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Ahsante sana, tunakushukuru sana Mwenyezekiwa Kamati tulieni nawaomba mtululie sana katika jambo hili. *Details* za baadhi ya mambo zimo kwenye kitabu, ambacho sijui kama mmeshasambaziwa au bado lakini zipo kwenye kitabu lakini na hata kwenye kijitabu wamejitahi sana kutoweka *details* nydingi zaidi kwa ajili ya kulinda hadhi ya Bunge na masuala yanahusiana na nchi yenye. Isingwezekwa kwa makosa haya kuweka kila kitu vile kilivyo kwa hiyo wamejitahidi kuwa *very brief*.

Sasa jana nilipokea meseji kutoka kwa Mheshimiwa Masele ikitumia Mheshimiwa Spika kwa ridhaa yako naomba unipe nafasi hapa Bungeni niombe radhi kwako na kwa Wabunge wenzangu, natanguliza shukrani zangu za dhati kabisa kwa karatasi hili hapa. Huwa slo kawaida mtu anayetuhumiwa kupewa nafasi kuongea humu Bungeni yeye huwa anaongea kwenye kamati inapokuja huku huwa ni suala la Wabunge kusikiliza Kamati na yule aliyeitwa walikuwa wamezungumza nini.

Lakini kwa upekee wa jambo hili na uzito wa jambo hili nampa nafasi Mheshimiwa Masele dakika 10. (*Makofii*)

Naomba tusikilizane hili si jambo la ushabiki tusikilizane tunampa dakika 10 mwenzetu si jambo la ushabiki wala nini ili apate nafasi ya kuzungumza kwa sababu hapa kinachofanyika ni haki tupu wala hakuna mtu atakayeonewa chochote kile. Mheshimiwa Masele sijui anakaa upande gani, dakika 10 tafadhalii nakupatia, Katibu. (*Makofii*)

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyenzi Mungu na nimuombe anijalie hekima na utulivu mkubwa kwa nafasi hii niyopewa ndani ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwa unyenyekevu mkubwa kukuomba radhi wewe binafsi, wewe na familia yako kwa usumbufu wowote ambaao umeupata

kupitia sakata hili. Lakini nitumie nafasi kuwaomba radhi Wabunge wenzangu kwa usumbufu wowote ambao mmeupata. (*Makof*)

SPIKA: Ningewaomba sana Waheshimiwa Wabunge tumsikilize mwenzetu nawaomba tena usikivu wenu. Jambo hili si la ushabiki tumsikilize mwenzetu tumpe heshima ya kumsikiliza Mheshimiwa Masele ongea kwa uhuru kabisa karibu.

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwaomba radhi viongozi wangu wakuu nikiongozwa na Mwenyekiti wa Chama changu ambaye pia ni Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni Mwenyekiti wetu wa Wabunge wa CCM kwa usumbufu wowote ambao wameupata kutoka na jambo hilli.

Mheshimiwa Spika, kwa namna yoyote ile na nitapenda rekodi ikae sawasawa, makosa yalioorodheshwa katika shitaka langu, ningefurahi *hansard* ya kikao ingeletwa kwenye Bunge hili ili Wabunge na watanzania wajue ukweli.

Mheshimiwa Spika, barua hii nimeshika hapa ni barua imetoka *Pan Africa Parliament* ya maombi ya mwaliko wa Mheshimiwa Stephen Masele kama Makamu wa Kwanza wa Rais wa Bunge la Afrika kuudhuria kikao cha Bunge ambapo ninahushika na maandalizi ya Bunge hilo. Barua hii ni mawasiliano kati ya taasisi na taasisi. Taasisi ya Bunge la Afrika na taasisi ya Bunge letu. Na kwa utaratibu wa siku zote kwa kupitia *notification* hii ambayo ni *official/ambayo* inatumwa kwa Katibu wa Bunge sisi huwa taratibu zingine zote zinafuatwa na hii inasimama kama barua rasmi ya kuomba ruhusa ya kusafiri.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Bunge letu tunapokuja kwako kuomba kibali hatuombi ruhusa ya kusafiri tunatoa *notification* na Wabunge wenzangu watakubaliana na hilo. Unapewa photocopyna wewe unaondoka na *copy* yako. Kwa hiyo, nilileta *notification official/iliyoletwa* na Bunge

la Afrika kwenye ofisi ya Katibu wa Bunge. Hata hivyo tuhuma yangu inasema nimesafiri bila ruhusa yako kibali chako. Sisi tupo Wabunge wanne wa Bunge la Afrika kwa nini Masele peke yake achukuliewe hatua na Wabunge wenzangu wasichukuliwe hatua?

Mheshimiwa Spika, kwa barua hii nyingine ambayo uliindika siku ya tarehe 16 ikinisimamisha kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika ambayo niliipokea saa 11 jioni kule nchini Afrika Kusini nikiwa nasimamia vikao. Rais wa Bunge la Afrika alitumia hii barua yako kutaka kunivua madaraka ya uongozi wa Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia barua yako Spika wangu ninayekuheshimu, nilitafakari sana kwa haraka nifanye nini kwa maslahi ya Taifa langu, nifanye nini maslahi yangu mimi binafsi kama kijana ambaye ninakuwa katika uongozi. Nilifikiria haraka na busara yangu iliniongoza kama Spika wangu anaandika barua ya kunisimamisha bila hata kuniuliza, ana nihukumu, basi nikate rufaa kwenye chama changu.

Mheshimiwa Spika, ndio sababu yangu ya kuwasiliana na viongozi wangu wa chama kwa maana kwamba ya Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi pamoja na Mwenyekiti wa Wabunge wa CCM Bungeni ambaye ni Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye kiungo cha Bunge pamoja na Serikali. Niliwaandikia ujumbe na ku-forward barua hii, nikiomba ushauri wao na msaada, barua hii ilitumika kutaka kunichinja kukata kichwa changu, nisiwe Makamu wa Rais na nisiwe Mbunge wa PAP kama angekuwa mtu ye yote humu ndani ungefanya nini?

Mheshimiwa Spika, niliamua, mimi ni Kijana, wewe ni Mzee wetu, ni Kaka yangu, naamini mimi bado najifunza, na wewe ungekuwa na nafasi ya kunilea, kama ningekuwa nimekosea na umegundua nimekosea, ungenipigia simu na kuniuliza Mheshimiwa Masele kuna kitu gani kinachoendelea huko? Hukufanya hivyo uliamua kunihukumu kabla hata Kamati ya Maadili hajaketi.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima ninasikitika kwamba sikuchonganisha Mihimili bali nilikata rufaa kwa Chama changu kwa kuwa wewe ni Mkuu wa Mhimili huu, na nisingeweza kupeleka suala hili kwa Mheshimiwa Waziri, nisingeweza kupeleka suala hili kwa Mheshimiwa Katibu wa Wabunge wa CCM, kwamba muda ulikuwa hautoshi.

Waheshimiwa Wabunge kama mliona ile video ilikuwa ni suala la sekunde tu, yule Mheshimiwa *ame-move motion* ya kutaka kuniondoa kwenye madaraka, sikuwa na muda wa kutengeneza hotuba, lakini niliamini kwamba kwa kuwa anatumia iliyotoka kwa Spika wangu ambaye hakupata muda hata wa kuniuliza, hata kama angewauliza wenzangu ambao walikuwepo pale, niliamua nisimame kwa ujasiri na kusema kwamba *nina-support* ya Serikali yangu, kwa kutambua kwamba unapokuwa nje ya nchi mawasiliano ya nchi na nchi yanafanywa kupitia Serikali.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nilisimama kusema kwamba ninasapoti ya Serikali yangu na hii barua siitambui kwa sababu sikuwa na nafasi ya kuihakiki hii barua kama ni barua halali.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima nimekubali mimi ni kijana, ninabebea dhamana nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kukuomba radhi kama Mkuu wetu wa muhimili huu, na ieleweke kwa namna yoyote ile sikufanya mambo haya kwa makusudi ya kukuvunjia heshima, sikufanya haya yanayoitwa ni makosa kwa nia yoyote ya kukudharau, nilipokea mwaliko wako saa kumi na moja jioni saa za Afrika Kusini, ikinitaka kesho yake tarehe 15 niwe nimefika Dodoma saa nne Asubuhi.

Mheshimiwa Spika, unatambua, nimekwenda Afrika Kusini, bila kupewa *perdiem*, unatambua nimekwenda Afrika Kusini bila kupewa nauli, ningepata wapi hela ya kubadilisha tiketi kwa haraka niweze kurejea, na ukitambua sijapewa nauli, sijapewa *ticket*, ningepata wapi muda wa kulipa bili zangu za hotelini, ningepata saa ngapi muda wa kukabidhi

majukumu yangu kama Makamu wa Kwanza wa Rais, ambaye ninasimamia Utawala.

Mheshimiwa Spika, na wakati huo Bunge letu lilikuwa kwenye mgogoro mkubwa wa Rais yule kutuhumiwa kwa kashfa ya *Sexual harassment*. Viongozi wa AU kupitia *Chairperson* alinitumia watu wawili kutoka kwenye Ofisi yake, kuungana na mimi kusaidiana kuhakikisha haki inatendeka tulipounda Tume ya Bunge ya kumchunguza Rais wa Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Spika, ninatambua Rais wa Afrika anafanya mawasiliano na wewe kuhakikisha kwamba sirudi kule *PAP*, nasema haya kwa ujasiri kwa sababu nina uhakika, barua aliyokuandikia inayokanusha haki zangu kama Mbunge na Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika kwamba ilifojiwa ni barua aliyoandika Rais wa Bunge la Afrika ambayo ilikwenda kwenye nchi ya Mali, ambako kuna Makamu wa Pili wa Rais, ilikwenda nchi ya Algeria ambako kuna Makamu wa Tatu wa Rais kwenye *content* ya barua ile zote zinafanana.

Mheshimiwa Spika, iweje ya kwangu iwe imefojiwa na zile hazijafojiwa? Rais yule aliandika barua ya kuzikanusha barua zake za mwanzo tarehe 11 mwezi wa tano wakati yeye tulianza naye mgogoro tarehe 2 mwezi wa tano, na tukamuweka pembeni kwa uchunguzi lakini aliendelea kufanya makosa kwa kuendelea kufanya kazi ya kuwasiliana na nyumbani wakati yuko katikati ya uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuombe naamini umefanya ushauri wa kutosha ni Kijana wako, nimekubali makosa, kwa heshima ya Bunge langu, na kwa heshima ya Wabunge hawa, nimekubali makosa, nakuja mbele yako kuomba radhi kwa usumbufu uliouopata, lakini nashukuru kwa nafasi hii ya kueleza ukweli ili watanzania waweze kujua mazingira niliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, sikufanya hivyo, rekodi yangu ya nidhamu inafahamika, huu ni Ubunge wangu wa mwaka wa

tisa, sijawahi kuitwa kwenye Kamati yoyote ya nidhamu, sijawahi kufanya kosa lolote ninajitambua, ninajiheshimu na ninaaheshimu Viongozi wenzangu, nakuomba kwa kusema ukweli huu mbele ya Bunge lako Tukufu na kwa kutumia Kanuni ya 68(1) Kanuni inayovunjwa ya 63 kwa Mwenyekiti wa Kamati hii kuleta taarifa ambayo ina upungufu ninaomba Bunge lako nitoe hoja ya kukataa Kamati hii, na ripoti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Hatuendeshi mambo hivyo jamani. (*Kicheko*)

Hatuendeshi mambo hivyo. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, jambo hili ni jambo la kipekee sana katika Bunge letu, ndiyo maana nikasema ni vizuri tuwe na umakini mkubwa na usikilizaji mkubwa sana. Naomba tusikilizane sana, Waheshimiwa Wabunge mnaoongea wote naomba tusikilizane. (*Makofi*)

Bahati mbaya sana, Mheshimiwa Masele, haelewi hata hivi sasa ni nini kinachoendelea, bahati mbaya sana, Mheshimiwa Masele hakuitwa nyumbani kwa sababu ya jambo lolote la huko *PAP*, Tungemwitaje, kwa jambo la *PAP*, just imagine wewe ungekuwa mimi? Kuna mambo yanafanyika huko, wanaopaswa kutuarifu sisi kinachofanyika huko ni hawa Wabunge wetu Wawakilishi wetu. Sasa tungemwitaje nyumbani kwa mambo hayo ya huko, haya anayotueleza sisi haya.

Tulimwita nyumbani na nimerudia tena, na tena na kila nikirudia kwa makusudi anapotosha anapeleka mambo kwenye migogoro ambayo sisi hatuko nayo, tulimwita kwa mambo ya nyumbani, Mheshimiwa Masele ameandikia Mamlaka za juu kabisa jumbe za uchonganishi wa ajabu, akitunganisha muhimili huu na muhimili wa Serikali.

Katika maelezo yake yote amesema chochote kuhusu hilo, ndiyo sababu aliiwtwa hapa nyumbani, rudi kwa sababu ya tabia hiyo aliyofanya, mambo ya nyumbani, siyo

huko kwa hiyo tukapeleka barua ya kwanza Jumatatu, barua ile ilienda kwa ubalozi wetu, kuhakikisha kwamba anapata nakala, barua ile tulipeleka kwa Katibu wa Bunge la *PAP* ili kuhakikisha anapata.

Tukapeleka kwa *President* wa Bunge, kwa sababu Wabunge wanahusika na *President*, Wabunge mnahusika na Spika, mnaitika kwa Spika zaidi ya kuitika kwa Katibu. Kwa hiyo, tukapeleka kwa Rais wa *PAP* na tukapeleka meseji kwake *including WhatsApp* yake.

Hakurudi, kwa sababu wa unyeti wa hili tunalomwitia nyumbani, kesho yake tukampelekea taarifa tena, kesho kutwa yake tukampelekea taarifa tena, Jumatano sasa, Jumatatu, Jumanne, Jumatano.

Baada ya taarifa ya Jumatano ndiyo akasimama Bungeni akasema yake ambayo mliyasilika, kwamba Spika ameniita lakini Waziri Mkuu ameniambia nisi-*regard* analiambia Bunge la Afrika maneno ya aina hiyo, huyu kijana wetu, anaonyesha kwamba katika nchi ya Tanzania tuna migongano mikubwa kiasi hicho, *including* Spika na Waziri Mkuu.

Ameshagonganisha Spika na Rais, sasa anagonganisha Spika na Waziri Mkuu, na mengine mengi, Mheshimiwa Masele tumekuita kwa mambo ya tabia mbaya za hapa nyumbani. (*Makofi*)

Habari za huko mtajua wenyewe wawakilishi wa huko, hayatuhusu sisi hayo, hayo ni ya kwenu wenyewe, kuna mgogoro kuna nini? Japo tunasononeka pia tunasikitika lakini, hayo sitaki kuingia kwenye hayo, maana yake hata nikiingia kwenye hayo kwa vipengele ulivyokuwa unavishusha hapa, bado yaani, huwakilishi taswira ya Mtanzania katika chombo cha Kimataifa, lakini huko sitaki kwenda, wewe kila wakati unatupeleka huko.

Kila wakati nakurudisha, matatizo yako yako hapa, tatizo lako ni uwongo, kugonganisha viongozi, uwongo, fitina

na uchonganishi. Binafsi nimesononeka sana na ninaendelea kusononeka, kwamba hata sasa bado huelewi? Tunalalamika sisi mara nyingi kwamba wako watu wanamdaganya Rais, wanadanganya viongozi, hatusemagi hapa? Huyu kajipambanua katika hilo, ndiyo maana kapelekwa Kamati ya Maadili, na Kamati imekuja kusema kwamba walipomuhoji, amekiri tabia hiyo na akaomba hapa kwamba naomba Mheshimiwa Spika mbele ya Bunge lako niombe radhi.

Nimempa nafasi, anasema mengine ambayo ninyi na sisi ndiyo tunasikia mara ya kwanza, ooohh! Kwenye Bunge la *PAPsijui*, ahhah, hatukuita na hayo, tuseme mara ngapi utuelewe, hatukuita na hayo.

MBUNGE FULANI: Msamehe.

SPIKA: Tumekuita ya hapa nyumbani mdogo wangu, acha tabia hizo, acha, ujanja, ujanja wa kuzungusha maneno, uwongo, uwongo, kwa nini? Wamekuja Wazee, Wamekuja katika Bunge tuna watu wazima hapa wakanitajia pointi zake sina muda wa kurudia moja hadi jingine, kila moja walilolisema pale pale tuka-*prove* ni uwongo, linakuja la pili tuna-*prove* ni uwongo, hizo haki anazosema hizo, anasema Katibu Mkuu Kiongozi alikuja akaagiza akamwambia Katibu wa Bunge, atekelze, tunamwita Kagaigai, uwongo, anasema silipwagi hela, nadai, nikamuita *Chief Accountant* wa Bunge Mheshimiwa Masele anadai hata shilingi moja, hadai chochote, uongo.

Tunakuja sijui kitu, umeenda Afrika Kusini bila kulipwa ndiyo mnajua ninyi taratibu zetu, tunataratibu zetu, lazima tupate vibali vikamilike, ndiyo uweze kusafiri nje, ninyi Wabunge wote mnajua, tunapolipa lazima tuambatanishe kila kitu anasema *notification* ikija basi wewe Mbunge unasafiri tu, hata Mawaziri mpo hapa, yaani wewe ukialikwa na Chombo huko sijui *UNwameleta* barua au nani, basi wewe unasafiri tu.

Taratibu za ndani hufanyi ukakamilisha, ndiyo rafiki yetu anazungumza mambo hayo, kwa hiyo nilienda mwenyewe, si ulikata tiketi mwenyewe? Tiketi si unapaswa upewe na Bunge, Bunge halijakupa tiketi umesafiri mwenyewe, unavyojuia mwenyewe, sasa ukifika huko unamlamu nani?

Kwa sababu ya *notification*? Ndiyo utaratibu wetu? Masele umefanya na Bunge leo? Kwa hiyo, mtu akiongea hivi na kama mnamsikiliza hamna mtu anayejibu *uta-tend* kumuamini, lakini si kweli hata kidogo, tuache vitabia tabia vya namna hii.

MBUNGE FULANI: Msamehe bure Mheshimiwa, hajui alitendalo. (*Makofi*)

SPIKA: Nimalizie, Kwamba sijui barua tulioandika ilitaka kumtoa madarakani kivipi? Barua yetu inasema unaitwa nyumbani, acha unachofanya rudi nyumbani, unaitwa nyumbani, sasa hiyo inakutoaje madarakani? (*Kicheko*)

Ehhe! Waheshimiwa Wabunge mimi ni Spika wenu, ni mtu mzima, niseme kwa kifupi, tabia ambazo Mheshimiwa Masele aki-*display* za kusema uwongo hata kwenye Bunge hili amesema uwongo, kwenye Kamati kule uwongo na anathibitihiwa pale pale, kesho asubuhi akiamka uache mdogo wangu. (*Makofi*)

Tulienda kule Moshi, ndiyo tikisa kichwa, lakini kumbuka unaowadanganya ni hao hao viongozi wako, iwe ni hapa iwe ni kwenye Chama, unajua, ni viongozi wako wa Kamati Kuu, unaojaribu kuwaonyesha kwamba ni watu wa ajabu na nini, lakini tabia hiyo acha haikusaidii. (*Makofi*)

Hizi kampeni kampeni hazisaidii, lazima tuache tabia, na hii ni kwa wote jamani, tuache tabia za uwongo, tuache tabia za fitina fitina tuache, tuache kabisa. (*Makofi*)

Nasikitika sio kwako tu, hata kwa mwingine yeoyote anayefanya tabia kama hizi, tuache tabia hizi, Mheshimiwa Masele acha! (*Makofi*)

Acha kabisa! acha kabisa! acha kabisa! Kwa ajili hiyo, na kwa jambo hili ningeomba nichukue, unajua Wabunge katika, Bunge katika kuendeshwa kwake huwa unaangalia na Mabunge mengine, na mambo yaliyotokea huko nyuma sisi tumekaa hapa muda mrefu, yaliwahi kutokea mambo kama haya lakini katika namna tofauti kidogo alipokuwa Mzee Sitta ni Spika.

Katika mazingira kama haya, aliliomba Bunge limpuuze Mbunge fulani enzi hizo na kwa maana hiyo, na mimi nakuombeni sana, tumpuuze Mheshimiwa Masele na tumsamehe. (*Makofi*)

Muoneeni huruma Mheshimiwa Rais, anafanya kazi kubwa sana, achene kupeleka umbeya umbeya kwa Rais na uwongo na fitina, tunamyumbisha, tunamchanganya, tunamzeesha. (*Makofi*)

Msimgonganishe Waziri Mkuu na Spika hawana ugomvi, migongano ya nini? Nilipeleka hiki kwa Viongozi wangu, nilipeleka hivi, uchonganishi mtupu, hamna ukweli wowote. (*Makofi*)

Tuache hiyo tabia, una jambo njoo kwa Spika wewe ni Mbunge, chukua, wako Wabunge wenye heshima zao wengi tu wote hapa mna heshima zenu. Chukua wenzako watatu, wanne, watano njoo kwa Spika, kaa naye bwana, jamani Spika anifanyii mema. (*Makofi*)

Tunajadili tu, tutafika mahali tutaelewa tu. (*Makofi*)

Tutaelewana tu, hili la haki, haki, haki nina haki zangu, haki zipi? Haki ni za huko siyo hapa, naomba nimalize. (*Makofi*)

Hata huyo Rais, huyo unayemtuhumu huyo sijui mambo yenu huko, huko kwake, yaani ukipewa madaraka

huko, Ofisi ya huko ndiyo inayoshughulika na mambo yako, hivi unaponidai mimi nikupe walinzi wa Usalama wa Taifa, wakae hapo mgongoni kwako nawatoa wapi? Niambieni Wabunge? (*Kicheko/Makofi*)

Mimi nawatoa wapi? Acha masele, acha, nyumba kubwa, sijui magari Ma-V8 mi nayatoa wapi? Hivi vitu ni Rais ndiyo mwenye Mamlaka ya kutoa vitu hivyo kama hajaniambia siwezi kukupa nakujibu kila wakati hivi vitu siwezi, mpaka mwenye Mamlaka aseme, hunielewi Mheshimiwa Ndugai mbaya, mimi hayo nitayatoa wapi, majumba ya kukupa, magari, manini, walinzi mgongoni nitatoa wapi? (*Kicheko/Makofi*)

Ndiyo maana nikawaambia achene habari ya kupiga pigi makofi, ushabiki nini.

MBUNGE FULANI: Simba.

SPIKA: Kwa hiyo nawaombeni Waheshimiwa Wabunge jambo hili Mwenyekiti mtoa hoja liishie hapa tusamehe na kupuuza. (*Makofi/Vigelegele*)

Tuendelee na mambo ya maana zaidi, ahsanteni sana, nawashukuru sana Kamati ya Maadili mmefanya kazi kubwa, leo peke yake mmemaliza shughuli zenu saa nane usiku kwa jinsi ambavyo mmehangalka nawashukuruni sana na tuendelee kufanya kazi hii njema hatuna ubaya na mtu ye yote. (*Makofi*)

Ni tabia yako, nashukuru sana. (*Makofi*)

Baada ya hapo naomba tuendelee na ajenda za leo, naomba nimkaribishe Mwenyekiti.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia kitii

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Katibu!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Kaa chini. (*Kicheko/Makofi*)

Katibu!

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Maliasili na Utalii

MWENYEKITI: Waheshimiwa, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

Hoja imeshaapuuzwa na Mheshimiwa Spika, na limekwisha hili suala, nampongeza Mheshimiwa Spika kwa kutumia busara, ametumia uzoefu wake wa Kibunge na busara kubwa na hekima kulimaliza suala hili kama lilivyoletwa mbele ya Bunge lake.

Katibu!

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chenge!

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kusaidia Bunge lako kwa sababu tulikuwa na hoja mbele yetu ilitolewa na Mwenyekiti, ikaungwa mkono pamoja sasa na busara kubwa iliyotumika ya Mheshimiwa Spika ambayo na mimi nampongeza sana napendekeza...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chenge nakuomba radhi kwa heshima zote kaa chini,

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chenge kaa chini tafadhali.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tutumie kanuni ya 58(5) ili Mwenyekiti aiondoe...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chenge nafikiri wakati natumia hiyo kanuni ulikuwa hujanisikia nishafunga hoja zote. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili (*Kicheko*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, ninaomba Bunge lako tukufu lijadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka...

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba utulivu ndani ya Bunge mnaotoka tokeni kwa kufuata kanuni za Bunge, Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu ndani ya Bunge, Mheshimiwa endelea.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaomba Bunge lako tukufu lijadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha Mbele ya Bunge lako tukufu Hotuba ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Natumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo yao katika usimamizi

wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii. Maelekezo yao yameendelea kutoa dira ya uhifadhi, ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Japheti Ngailonga Hasunga Mbunge aliyekuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na sasa ni Waziri wetu wa Kilimo, Meja General Gaudence Milanzi Katibu Mkuu mstaafu, viongozi wengine, wananchi na madaktari kwa msaada na matibabu walionipa baada ya kupata ajali ya gari mwezi Agosti 4, 2018. Katika ajali hiyo wizara kwa masikitiko makubwa sana ilimpoteza Ndugu Hamza Temba Afisa Habari Daraja la I namuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahala pema peponi Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza wewe nampongeza Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu tukufu kwa weled mkubwa. Aidha, ninaishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushauri ambao umeendelea kuiwezesha wizara kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Vilvile nawapongeza Wabunge wote waliochaguliwa na kuteuliwa kasha kuapishwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Uadilifu wao, tabia ya kujituma, na kufanya kazi kwa bidii na weledi ndio sababu kubwa ya kuwa sehemu wa wawakilishi wa wananchi katika Bunge hili tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninawapongeza Wabunge walioteuliwa kuwa mawaziri na naibu mawazirii kuziongoza wizara mbalimbali katika kipindi hicho. Ninamshukuru Mheshimiwa Constantine John Kanyasu Mbunge Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda Katibu Mkuu na Dkt. Aloyce Nzuki, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, ninawashukuru wakurugenzi na wakuu wa vitengo, wakuu wa mashirika na taasisi, watumishi na wadau wote kwa ushirikiano wanaotupatia katika kutekeleza majukumu ya wizara yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Nzega Vijijiini kwa kuendelea kuniunga mkono kwa dhati katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii. Ninapenda kuwashimiza kuendelea kuimarisha uhifadhi wa maliasili, malikale na kuendeleza utalii kwa maendeleo endelevu. Aidha, namshukuru kwa dhati mke wangu mpenzi Dkt. Bayoum Kigwangalla na familia yangu kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kutoa pole kwa ndugu, marafiki na wananchi wa majimbo ya Buyungu na Korogwe Vijijiini kwa vifo vya Mheshimiwa Kasuku Bilago kilichotokea Mwezi Mei, 2018 na Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani kilichotokea Julai, 2018. Aidha, natoa pole za dhati kwa ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao na mali kuharibiwa kutokana na kushambuliwa na wanyamapor ajali na maafa mbalimbali yaliyotokea katika sehemu mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee natoa pole kwa ndugu, marafiki na watumishi wote wa wizara kutokana na watumishi waliopoteza maisha wakiwa wanatekeleza majukumu yao. Watumishi wawili walishambuliwa na wafugaji kwa kutumia mishale ya sumu, watumishi watano walishambuliwa na wanyapori na mtumishi mmoja alizama majini. Aidha, watumishi wanne walijeruhiwa na wananchi, mmoja na majangili, na mmoja na wanyapori. Kwa hakika hawa ni mashujaa na wamekufa wakitetea rasilimali za nchi yetu Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahala pema peponi Amina. Vilevile natoa pole kwa watumishi waliojeruhiwa na ninawaombea wapone haraka na kuendelea na majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo ninaomba kuwasilisha hotuba yangu ambayo imegawanyika katika sehemu kuu sita, sehemu ya kwanza ni utangulizi, ya pili ni dira , dhima na majukumu ya wizara ya tatu ni mchango wa maliasili malikale na utalii katika maendeleo endelevu

ya nne ni maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ya tano ni utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 na sehemu ya sita ni makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara imepewa dhamana ya kusimamia uhifadhi wa maliasili, malikale na maendeleo ya utalii kwa kushirikiana na wadau. Kutokana na dhamana hiyo dira ya wizara ni maliasili na malikale zilizohifadhiwa kwa manufaa ya watanzania wakati ikiongoza kuchangia ukuaji wa uchumi. Aidha, dhima ya wizara ni uhifadhi endelevu wa maliasili na malikale na kuendeleza utalii kwa manufaa ya Taifa. Vilvevile, wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuandaa na kupitia sera, mikakati na miongozo mbalimbali kuandaa kupitia na kusimamia sheria na kanuni, kufatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa sera, sheria, programu na miongozo. Kujenga uwezo wa kitaaluma na kitaasisi nakuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imejaliwa kuwa na maeneo ya hifadhi za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale yenye mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira ustawi wa wananchi na ukuaji wa uchumi. Maeneo ya maliasili yanatoa huduma za maji kwa matumizi mbalimbali makazi ya wanyamapori na viumbe wengine, uchavushaji, uhifadhi wa udongo, ufyonzaji wa kabooni na hivyo kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Uhusiano bora kati ya uhifadhi na maendeleo unachangia katika ustawi wa maliasili matumizi endelevu, ustawi wa wananchi, ukuaji wa uchumi na usalama wa Taifa letu. Hivyo naendelea kutoa rai kwa umma kuendelea kujenga mtazamo chanya na kushirikiana na wizara katika kuhifadhi maliasili malikale na kuendeleza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii imepitia taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 na kuchambua makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo

21 yanayolenga kuboresha utekelezaji wa majukumu ya wizara. Napenda kiliarifu Bunge lako tukufu kuwa ushauri wa kamati umezingatiwa katika mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara iliidhinishiwa kukusanya maduhuri ya shilingi 63,282,680,713. Hadi Machi 2019 shilingi 37,951,669,310 sawa na asilimia 60 ya makadirio zimekusanywa. Aidha, Mashirika ya TANAPA, NCAA, TAWA na TFS yaliidhinishiwa kukusanya shilingi 619,521,447,545. Hadi Machi 2019 shilingi 501,113,265,899.76 sawa na asilimia 80.9 ya makadirio zimekusanywa. Mashirika hayo yalitumia fedha hizo kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya uhifadhi, uendelezaji utalii na kuchangia katika mfuko mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliidhinishiwa bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya mendeleo ya shilingi 116,310,848,543.15. Bajeti hiyo inajumuisha shilingi bilioni 86,231,466,543 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 29,978,082,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi mwezi Machi, 2019 wizara imepokea jumla ya shilingi 49,842,260,769. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi 39,653,292,391 ni matumizi ya kawaida na shilingi 10,188,968,377 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara imekamilisha rasimu za sera za Taifa za misitu ya mwaka 2019 na sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 2019 na mikakati ya utekelezaji wake. Wadau wote wameshirikishwa kikamilifu katika kuandaa sera hizo hatua inayofuata ni kuwasilisha rasimu husika kwenye Baraza la Mawaziri kwa uidhinishajji. Aidha, wizara imekamilisha maandalizi ya rasimu ya mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Wanyapori sura ya 283 na inapitia sheria ya Mambo ya Kale na kuboresha sheria za kisekta kwa kupitia kanuni na kutayarisha miongozo mbalimbali. Serikali imepiga hatua na kupata mafanikio makubwa katika kutokomeza ujangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya sensa ya Tembo katika mfumo ikolojia wa Selous Mikumi iliyofanyika mwaka 2018 yanaonesha kuwa idadi ya tembo haipungui. Aidha,

sensa hiyo haikubaini mizoga mipyä ya tembo waliouwawa na majangili katika mfumo wa ikolojia huo. Sote tunashuhudia kuongezeka kwa idadi ya tembo na wanyamapori wengine waliokuwa wakiwindwa na majangili. Hali hiyo inasababisha wanyamapori kuanza kuonekana katika maeneo ambayo awali haikuwa rahisi kuwaona. Mfano hivi karibuni tembo wameonekana eneo la Chuo Kikuu cha Dodoma mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika kupambana na ujangili ni kutokana na uongozi shupavu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na viongozi wetu wote wa ngazi ya juu. Uongozi huu shupavu umefanya kazi ya kuratibu vyombo vya ulinzi na usalama kwenye kikosi kazi cha Taifa dhidi ya ujangili yaani *National Task Force Ant poaching* kuwa rahisi na yenye mafaniko makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudhi hizo tunashuhudia mapapa wa ujangili wakikamatwa kwa kasi kubwa zaidi kufikishwa mahakamani na kuhukumiwa vifungo vya miaka mingi. Mfano mhalifu sugu Bibi Yang Feng Lan kwa jina maarufu la *Queen of Ivory* yaani Malkia wa Tembo amehukumiwa kifungo cha miaka 17 jela na kulipa faini ya shilingi bilioni 26. Adhabu hiyo imetolewa kutokana na jangili huyo kujihusisha na kuratibu mtandao mkubwa wa biashara haramu ya nyara hususan meno ya tembo na pembe za faru. Aidha, watuhumiwa wengine wa ujangili wameendelea kukamatwa hususani wale wanaotuhumiwa kufanya biashara haramu ya meno ya tembo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za kupambana na ujangili zimetuwezesha kutambua mbini mbalimbali na mitandao ya ujangili. Hivi karibuni tumewanasa baadhi ya watumishi wa umma na hakimu mmoja kwa tuhuma za kushiriki kwenye mtandao wa kusaidia na kulinda majangili. Watuhumiwa wote wamefungiliwa mashtaka. Serikali itaendelea kuwasaka wote wanaofadhili na kuwezesha ujangili hadi kutokomeza kabisa uhalifu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kudhibiti ujangili Serikali imeanzisha jeshi Usu la kulinda maliasili zetu. Hatua hiyo inatoa msukumo wa kipekee katika kuimarisha nidhamu ya watumishi ikiwa ni pamoja na kukabiliana na changamoto za ujangili unaotumia mbinu za kisasa kama vile silaha za kivita. Mfumo huo ulizinduliwa rasmi mwezi Novemba 2018 na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hadi mwezi Machi, 2019 watumishi 2176 kutoka *TANAPA*, *NCAA*, *TAWA*, na *TFS* wamepatiwa mafunzo ya Jeshi Usu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara imeendelea kubadilisha hadhi maeneo ya hifadhi ili kuimarisha uhifadhi na ulinzi hususan katika maeneo ya mpakani na kuendeleza utalii. Katika utekelezaji wa azma hiyo wizara inakamilisha taratibu za kubadili hadhi, mapori ya akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika-Orugundu kuwa hifadhi za Taifa. Aidha, mchakato wa kubadili hadhi ya mapori ya akiba ya Kigosi, Moyowosi na Ugalla unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara imetayarisha mapendekezo ya kubadili mpaka wa hifadhi ya Taifa ya Serengeti ambao ni eneo la kilomita za mraba 14,763 kwa kujumuisha Pori Tengefu la Ghuba ya Speke lenye km 57 na sehemu ya ukanda wa Ziwa Victoria km 81. Hatua hiyo itahakikisha upatikanaji wa malisho na maji kwa wanyamapori muda wote. Pia kuimarisha usimamizi wa mazalia ya samaki kupunguza migogoro na kufungua fursa za maendeleo ya utalii kana ya ziwa na kuimariika kwa ustawi wa wananchi. Utekelezaji wa mapendekezo ya kubadili hadhi maeneo hayo unashirikisha wadau wote na fidia stahiki zitalipwa pale itakapolazimu kuhamishwa kwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara imepandisha hadhi misitu ya misitu ya hifadhi ya Mwambesi, Tunduru, Pindiro, Kilwa, Itulu Hill, Konge, Magmbera, Kilombero na Kalambo Falls Kalambo kuwa misitu ya hifadhi ya mazingira asilia. Aidha, wizara imezindua rasmi Mji wa Mikindani kuwa mji wa kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya watalii walioingia nchini imeongezeka kutoka 1,327,143 mwaka 2017 hadi kufikia watalii 1,505,702 mwaka 2018. Ongezeko hilo limechangia kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii kutoka dola za Marekani bilioni 2.2 mwaka 2017 hadi kufikia dola za Marekani bilioni 2.4 mwaka 2018. Mafanikio hayo yanatokana na jithada mbaimbali za kutangaza vivutio vya utalii kupitia maonesho ya WTM Uingereza, *ITB* Ujeruman, *Conservation and Tourism Fair Rwanda*, *Travel Market Top Resa* Ufaransa, *Magical Kenya Travel Expo Kenya*, *International Tourism Travel Expo Canada*, *China International Expo na Road show China*, *Dutch Expo Uhlanzi*, *Outbond Travel Market – OTM* na road show India, *Fitur Hispania*, *Holiday Fair* Ubelgiji na *International Mediterranean Tourism Market IMTM* Israel na Falme za Kiarabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jithada nydingine zilizofanyika ni kuendelea kutangaza vivutio vya utalii kupitia vyombo vya habari ndani na nje ya nchi kwa mfano, *TBC1*, *ITV*, *Clouds TV*, *BBC Swahili*, na *Doutche Welle* Ujeruman. Pia mitandao ya kijamii, kuandaa ziara za waandishi wa habari wa nje, *bloggers*, kutumia watu mashuhuri, na Ofisi za Balozi zetu nje ya nchi. Aidha, Wizara imekamilisha maandalizi ya utambulisho mpya wa utalii Tanzania ambao unajulikana kama *Tanzania Unforgettable*. Utambulisho huo umeanza kutumika kwenye maonesho mbalimbali yaliyofanyika nje ya nchi na ndani ya nchi. Vilevile, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imeanzisha Chaneli maalumu ya kutangaza vivutio vya utalii (*Tanzania Safari Channel*) ambayo itasaidia kuwavutia wageni wengi kutembelea nchini. Wizara imeendelea kuchangia katika kugharimia uanzishaji na uendeshaji wa chaneli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangazaji wa vivutio vya umeendelea kuonesha matokeo chanya ambapo mnamo tarehe 20 Aprili, 2019 Tanzania ilipokea kundi la watalii 1,000 kwa wakati mmoja kutoka nchini Israel. Kutokana na ujio huo, watalii wengi zaidi wanatarajiwa kuja kutoka nchi hiyo. Aidha, tarehe 12 Mei, 2019 kundi la watalii 336 wakiwemo waandishi wa habari kutoka nchini China lilipokelewa. Hili ni kundi la

kwanza kati ya watalii 10,000 wanaotarajiwa kuwasili nchini kutoka China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 01 Aprili, 2019 kundi la wafanya biashara ya utalii, Wakala wa Utalii na wahandishi wa habari za utalii kutoka nchi za Malaysia, Ufilipino, Thailand na Indonesia walifika nchini kutazama vivutio vya utalii vilivromo nchini na wameahidi kwenda kuvitangaza. Mafanikio haya yanatokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali kutangaza utalii katika masoko mapya ya Israel, China, India na Urusi. Aidha, mafanikio haya yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na juhud za Ofisi za Ubalozi zilizopo nje ya nchi yetu. Tunamshukuru kwa namna ya kipekee Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa kuongoza hafla mbalimbali za kupokea na kuyaaga makundi hayo ya awali ya watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza utalii, Wizara imeendelea na jitihada za kupanua wigo wa mazao ya utalii. Mazao hayo ni pamoja na utalii wa fukwe, utalii wa mikutano, utalii wa meli, utalii wa majini, utalii wa michezo, utalii wa utamaduni na kuanzisha shughuli mpya za utalii katika maeneo ya hifadhi. Shughuli hizo zinajumuisha safari za kutembea kwa miguu hifadhini, (*walking safaris*), safari za puto (*Hot Air Balloon*), utalii wa *Canopy walkway* na safari za mitumbwi kwenye hifadhi za maji kama vile Rubondo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Majiji ya Dar es salaam na Arusha imezindua safari za kitalii ndani ya miji hiyo (*city tours*). Vilevile, miongozo ya uwekezaji katika maeneo yanayosimamiwa na Wizara imeandaliiwa ili kutoa fursa za uwekezaji katika shughuli za utalii. Pia, ili kuweka mazingira wezeshi ya kukuza utalii wa meli, Wizara itajiunga tena na vyama vya waandaaji wa utalii wa meli duniani.

Wizara imeanza kutekeleza Mradi wa Kusimamia Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (*REGROW*). Mradi huo utafungua utalii Kanda ya Kusini na kwa kuanzia utaimarisha miundombinu ya ndani ya hifadhi za Taifa Ruaha, Mikumi, Milima ya Udzungwa na Pori la Akiba Selous Kanda

ya Kaskazini katika eneo la Matambwe kwa kujenga barabara, madaraja, viwanja vya ndege, malango ya kuingia, vituo vya utalii, kambi za watalii, na shughuli za kiuchumi za kijamii zinazozunguka hifadhi hizo. Aidha, ili kuhakikisha Mto Ruaha Mkuu unatiririsha maji yake mwaka mzima, mradi utaimarisha usimamizi wa matumizi ya maji katika Bonde la Usangu. Hadi sasa zabuni za usanifu wa ujenzi wa barabara, madaraja na majengo katika hifadhi tatu za taifa zipo katika hatua za mwisho za kupata wataalam washauri. Aidha, zabuni ya usanifu wa viwanja vya ndege ndani ya hifadhi ipo katika hatua ya kutangazwa na zabuni ya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji ya skimu ya umwagiliaji ya Madibira ipo katika hatua ya kupata mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imejenga ofisi sita na vituo 15 vya ulinzi katika hifadhi za mazingira asilia za Chome, Magamba, Mlima Rungwe, Mkingu, Minziro, na Uzungwa Scarp. Aidha, barabara zenye urefu wa kilometra 89.6 na njia za kutembea watalii zenye urefu wa kilometra 102.6 zimesafishwa katika misitu hiyo. Vilevile, ujenzi wa ngazi yenye mita 183 kuelekea kwenye maporomoko ya Kalambo umefanyika. Pia, kambi 11 za kupumzikia wageni zimesafishwa katika misitu saba ya hifadhi za asilia za Mlima ya Hanang, Rungwe, Uzungwa, Uluguru, Kimboza, Rondo na Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya hekta 1,734 zimepandwa miti katika mashamba mapya ya miti ya Wino (Songea), Iyondo Msimwa (Ileje), Biharamulo (Chato), Mpepo (Mbinga), Buhigwe (Kigoma) na Mtibwa/Pagale (Mvomero). Aidha, shamba jipya kwa ajili ya uzalishaji wa gundi inayotokana na miti ya migunga lenye ukubwa wa hekta 50,000 limeanzishwa katika Wilaya ya Iramba Mkoani Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeanza kuendeleza maeneo ya malikale kuititia mashirika ya TANAPA, NCAA, TAWA na TFSili kuhakikisha rasilimali hizo zinatumika kiatalii na kuongeza mchango katika Pato la Taifa. Mkakati huo unahusisha kuboresha miundombinu ya vituo hususan vituo vya kumbukumbu na taarifa, kuweka huduma muhimu kwa

watalii, ofisi na barabara ili viwe na muonekano unaovutia na kufikika kwa urahisi.

Katika kutekeleza azma hiyo, *TANAPA* imepewa vituo vya Caravan Serai kilichopo Bagamoyo, Makumbusho ya Mkwawa na Zana za Kale za Mawe Isimila vilivyopo Iringa, Dkt. Livingstone kilichopo Ujiji Kigoma na Nyumba ya Kumbukizi ya Mwalimu Nyerere iliyopo Magomeni Jijini Dar es Salaam. Aidha, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imepewa vituo vya Michoro ya Miambani ya Mumba, Nyayo za Engaraserero, Mfumo wa umwagiliaji Engaruka, Kituo cha Amboni na Kimondo cha Mbozi. Vilevile, *TAWA* imepewa vituo vya Magofu ya Kunduchi na Kilwa. Pia, *TFS* imepewa vituo vya magofu ya Tongoni iliyopo Tanga, Tembe la Kwhara na Old Afya Building yaliyopo Tabora, Magofu ya Kaole, Michoro ya Miambani iliyopo Kondoa na Ngome Kongwe iliyopo Bagamoyo. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mashirika yameanza kufanya tathmini ya namna ya kuviboresha na kuiviendeleza vituo hivyo. Ubreshaji huo utasimiwa na Idara ya Mambo ya Kale na Shirika la Makumbusho ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa kazi zilizofanyika ni ujenzi wa Makumbusho ya kisasa katika Bonde la Olduvai, Kituo cha Kumbukumbu na Taarifa katika eneo la Kimondo cha Mbozi, ukarabati wa Nyumba ya Kumbukizi ya Mwalimu Nyerere Magomeni, kuanzisha Siku ya Kimondo Duniani ambayo itakuwa inasherehekewa kila mwaka na kuanza maandalizi ya kusherekea miaka 60 (*Diamond Jubilee*) ya uvumbuzi wa fuvu la Zinjanthropus.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha utoaji wa huduma na ukusanyaji wa mapato ya Serikali, Wizara imekamilisha ujenzi wa mfumo fungamanishi wa kieletroniki wa kutoa leseni/vibali, kukusanya takwimu/taarifa na kukusanya mapato kutoka vyanzo mbalimbali ujulikanao kama *MNRT Portal*. Mfumo huo umeanza kutumika kukusanya maduhuli ya *TAWA*, *TFS*, *TAWIRI*, *TAFORI*, Makumbusho, vituo 16 vya malikale na kuuza vitalu vya uwindaji na mazao ya misitu kwa njia ya minada. Aidha, mfumo huo umefunganishwa na mifumo mingine ya *TEHAMA* ya Serikali

kama vile *TRA*, *GePG*, *eGA*, *BRELA*, *NIDA* na *TIRA* ili kuwezesha utoaji wa huduma mbalimbali kwa pamoja. Vilevile, uwekaji wa *internet (Wi-Fi)* na ufungaji *CCTV Camera* umefanyika kwenye malango ya kuingia na kutoka katika vituo vya *TANAPA* na *NCAA*. Mifumo hiyo imepunguza muda wa kuhudumia mteja; umerahisisha utoaji wa leseni, vibali na ada za mazao ya maliasili; lakini pia kuhakiki takwimu za wageni wanaoingia kwenye vivutio vya utalii na kuimarisha usalama wa wageni na watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango na Wadau wa Sekta ya Utalii imeendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara kama ilivyobainishwa katika mkakati ujulikanao kama *Blueprint*. Eneo mojawapo linalofanyiwa kazi ni kukusanya tozo mbalimbali zinazohusiana na biashara za utalii kupitia dirisha moja (*one payment stop center*) litakaloratibiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na kusimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Lengo la kutumia mfumo wa *MNRT Portal* ni kukusanya na kuonesha mgawanyo wa tozo mbalimbali kwa kila taasisi na mamlaka. Hatua hiyo itarahisisha ukusanyaji wa tozo, kumuhudumia mteja kwa muda mfupi na kuondoa uwezekano wa kutoza mteja kodi mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo Januari 15, 2019 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliwaagiza Mawaziri wa kisekta kuwasilisha mapendeleko ya ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo wanayoyasimamia. Wizara ya Maliasili na Utalii ni moja ya Wizara za kisekta zilizounda Kamati ya Mawaziri ya ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi. Kamati hiyo ambayo inaongozwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, imekamilisha kazi yake na kuwasilisha taarifa ya mapendeleko ya utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini. Wizara imejipanga vema kutekeleza maelekezo yote ambayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli atayatoa kuhusu utatuzi wa migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais, Wizara imeendelea kutatua migogoro kwa kushirikiana na Wizara nyingine na wananchi wa maeneo yenye migogoro. Baadhi ya jitihada zinazofanyika ni kutoa elimu ya uhifadhi, kuhakiki mipaka ya maeneo ya hifadhi, na kuweka alama za kudumu na mabango ya tahadhari ili mipaka ionekane kwa urahisi. Aidha, Wizara kwa kushirikisha na jamii imepima mipaka ya Kituo cha Makumbusho ya Mtwa Mkwawa - Kalenga chenye ukubwa wa ekari 7.6 na kituo cha Tembe la Dkt. Livingstone Kwihiara -Tabora na ipo katika hatua ya mwisho ya kupatiwa hati ya umiliki wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kudumisha na kuboresha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa kushiriki katika mikutano, semina na warsha mbalimbali. Kupitia Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Wizara imeshiriki katika kutayarisha Itifaki za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Usimamizi wa Mazingira na Maliasili, na Usimamizi wa Wanyamapori na Uendelezaji wa Utalii. Aidha, kupitia mradi wa Usimamizi wa Bioanuai na maeneo yaliyohifadhiwa (*BIOOPAMA I*), Wizara imeshiriki katika kutayarisha taarifa ya tathmini ya hali halisi ya maeneo yaliyohifadhiwa (*State of Protected Areas*). Kazi hiyo itawezesha utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa *BIOOPAMA*. Aidha, Wizara inashiriki katika kupitia vigezo vya madaraja ya hoteli na migahawa katika nchi wanachama wa Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilishiriki mkutano wa *SADC* uliofanyika nchini Afrika Kusini kwa ajili ya kujadili uendelezaji maeneo ya hifadhi yanayovuka mipaka (*Trans-frontier Conservation Areas*). Mkutano huo uliweka mkakati wa kukabiliana na changamoto za maeneo ya hifadhi yanayovuka mipaka. Aidha, Wizara ilishiriki Mkutano wa tatu wa *AFRI 100 Annual Partnership* uliofanyika nchini Kenya ukiwa na maudhui ya kurudishia maeneo ya uoto uliopotea Barani Afrika. Katika mkutano huo, Tanzania ilahidi kurudishia hekta milioni 5.2 za uoto wa asili uliopotea ili kuboresha uhifadhi wa mazingira na kuongeza malighafi za viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilishiriki Mkutano Mkuu wa 42 wa *UNESCO* wa Kamati ya Urithi wa Dunia uliofanyika nchini Bahrain ambao ulijadili taarifa ya uhifadhi wa Ngorongoro na Serengeti na mradi wa ujenzi wa Bwawa la kufua umeme kwenye Mto Rufiji katika Pori la Akiba Selous, na mkutano wa Shirika la Utalii Duniani (*UNWTO*) na *UNESCO* nchini Uturuki uliojadili Kanuni za Maadili ya Utalii na kujadili namna utalii wa utamaduni unavyochangia katika maendeleo ya uchumi. Kanuni hizo zinaandaliwa ili kuwezesha nchi kuwa na utalii utakaokidhi vigezo vya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa 24 wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi (*UNFCCC*) uliofanyika mjini Katowice, Poland, mwezi Disemba 2018. Mkutano huo ulihusu kujadilana na kukubaliana katika utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi, Itifaki ya Kyoto na Makubaliano ya Paris. Katika Mkutano huo, Wizara ilianzisha mazungumzo na Wizara ya Mazingira ya Poland kuhusu ushirikiano kati ya *TFS* na *State Forest Agency* ya nchini Poland.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo, kusimamia maslahi, maadili, ustawi na afya za watumishi; na kuboresha mazingira ya kufanyakazi. Mazingira ya kazi yameboreshwa kwa kuwajengea ofisi, kuwapatia vitendeakazi, vifaa vya mawasiliano na matumizi ya teknolojia ya kisasa; mfano kutumia *satellite collar* katika kufuatilia mienendo ya wanyamapori na matumizi ya maeneo yaliyohifadhiwa. Maboresho mengine yamehusisha matumizi ya ndege zisizo na rubani, kukamata wanyamapori kwa kutumia kemikali salama badala ya mitego, na kutumia *helicopter* katika maeneo hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake, Wizara imebadili mwelekeo kwa;

- 1) Kuendeleza vituo vya mambo ya kale kuititia *TANAPA*, *NCAA*, *TAWA*, na *TFS*;

- 2) Kuhamisha usimamizi wa vituo vya mambo ya kale kutoka Idara ya Mambo ya Kale kwenda Shirika la Makumbusho ya Taifa *yaani National Museum of Tanzania*;
- 3) Kuhamisha baadhi ya majukumu muhimu ya uendelezaji utalii kutoka Idara ya Utalii kwenda Bodi ya Utalii Tanzania (TTB)
- 4) Majukumu ya Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania (TTSA) yamehamishiwa TFS; na
- 5) Kuipa TAFORI jukumu la utafiti wa ufugaji nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hatua hiyo, Idara ya Mambo ya Kale na Idara ya Utalii zitaendelea kusimamia masuala ya kisera, sheria, na ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo ya Hifadhi ya Ngorongoro, Wizara imekubaliana na UNESCO kuhusu ujenzi wa barabara kutoka lango la Loduare hadi katika mpaka wake na Hifadhi ya Taifa Serengeti maarufu kama Golini, yenye urefu wa Kilomita 88 kwa kiwango cha lami ambayo ni rafiki kwa mazingira. Barabara hiyo itakapokamilika itarahisisha shughuli za uhifadhi, usafiri kwa watalii na utoaji huduma za kijamii kwa wenyeji. Aidha, hatua hiyo itapunguza gharama za matengenezo ya mara kwa mara ya barabara na uharibifu wa mazingira ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kufunga biashara ya wanyamaporl hai kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi. Serikali inakamilisha taratibu za kuwarudishia wafanyabiashara fedha walizotumia kulipia huduma mbalimbali. Aidha, kwa sasa Wizara inaandaa mkakati wa kitaifa wa biashara ya wanyamaporl hai kwa njia ya ufugaji wa wanyamaporl ili kuleta tija kwa wananchi na kwa taifa. Mkakati huo utatoa fursa ya ajira kwa Watanzania pamoja na upatikanaji wa nyara ghafi kwa ajili ya viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya uwindaji wa kitalii, inafanya mapitio ya

Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za Mwaka 2015. Mabadiliko yatakayofanyika katika Kanuni hizo yatahusisha kubadili mafungu (*packages*) ya siku za safari za uwindaji wa kitalii ili kupanua wigo na ufanisi katika biashara, kuongeza wigo wa idadi na *species* za wanyamapori wanaowindwa. Mabadiliko mengine ni pamoja na kupunguza madaraja ya vitalu kutoka matano hadi matatu. Aidha, muhula wa uwindaji wa kitalii utaongezwa kutoka miaka mitano ya awali kwenda miaka 10 kwa vitalu vya daraja la kwanza na pili na miaka 15 kwa daraja la tatu. Marekebisho hayo yanalenga kuongeza idadi ya watalii wawindaji na mapato kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeandaa Mwongozo wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii kwa njia ya mnada wa kielektroniki (*Guidelines for Allocation of Hunting Blocks through Auctioning*) pamoja na mfumo wa kielektroniki wa kugawa vitalu vya uwindaji wa kitalii. Utaratibu huo unatoa fursa kwa kampuni za uwindaji wa kitalii kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki kwenye ushindani wa kumiliki vitalu vya uwindaji wa kitalii, hivyo kuongeza uwazi na utawala bora katika tasnia ya uwindaji. Mnada wa kwanza umepangwa kufanyika tarehe 10 Juni 2019 na utahusisha vitalu 26. Tangazo la mnada limewekwa kwenye tovuti ya Wizara (www.mnrt.go.tz) na tovuti ya TAWA (www.tawa.go.tz).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilisitisha uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi mwaka 2015 kutokana na usimamizi hafifu, kutokuwepo vitalu vya uwindaji huo pamoja na ujangili. Wizara imefanya tathmini ya kina ya uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi na kuandaa mkakati wa kuboresha usimamizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilisitisha uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi mwaka 2015 kutokana na usimamizi hafifu, kutokuwepo vitalu vya uwindaji huo pamoja na ujangili. Wizara imefanya tathmini ya kina ya uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi na kuandaa mkakati wa kuboresha usimamizi wake. Kutokana na matokeo ya tathmini hiyo, Wizara sasa imefungua uwindaji huo katika maeneo matano kuanzia mwaka 2018. Maeneo hayo ni maeneo ya

wazi Kilwa, Kisarawe na Simbaguru na mapori tengefu ya Kitwai na Ugalla. Aidha, Wizara inatarajia kutenga maeneo mengine kwa ajili ya uwindaji wa wenyehi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara inakamilisha Kanuni za Uwindaji wa Wenyehi ambazo zitaruhusu uanzishwaji wa vituo na taratibu za kuuza nyamapori kwenye mabucha maalum. Narudia, vilevile, Wizara inakamilisha Kanuni za Uwindaji wa Wenyehi ambazo zitaruhusu uanzishwaji wa vituo na taratibu za kuuza nyamapori kwenye mabucha maalum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika ya *TAWA, TANAPA* na *NCAA* kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya na wadau wengine yameendelea kufanya doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, vituo vyta askari vimewekwa katika maeneo yenye changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile, mbinu na teknolojia mbalimbali zinazoendelea kutumika ni pamoja na kuweka uzio wa umeme na kuwalisha mikanda ya kielektroni (*satellite collar's*) tembo ili kufuatilia mienendo yao na kuwadhibiti wanapotoka ndani ya hifadhi kabla ya uhariibifu kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto ya mamba na viboko, sensa ya wanyamapori hao inaendelea katika maeneo ya Ziwa Rukwa na mito inayopita vijijiini. Matokeo ya sensa hiyo yataonesha idadi ya mamba wanaopaswa kupunguzwa katika maeneo yenye matukio ya wananchi kujeruhija na kuuawa na mamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi kufuatia uhariibifu wa mali na upotevu wa maisha uliotokana na wanyamapori wakali na waharibifu. Hadi Machi 2019, Sh.1,426,636,500 zimelipwa kwa wananchi 7,320 wa wilaya 57 kama kifuta jasho na kifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliyoundwa na Wizara mwezi Januari, 2018 imewasilisha taarifa yake ya namna bora

ya kusimamia eneo la Bonde la Kilombero. Taarifa hiyo imewasilisha mapendekezo ya kufuta au kurekebisha mipaka ya viji vili vyopimwa kinyume cha sheria ndani ya eneo la pori tengefu ambalo ni sehemu ya Bonde la Kilombero, kuendelea kuhifadhi maeneo nyeti ya ziada kwa uhai wa bonde, kuwaondoa wananchi waliovamia na kusitisha uingizaji mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo mengine yaliyowasilishwa ni kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi kwa kuendelea na zoezi la upimaji mipaka na uwekaji wa alama za kudumu, kubadili hadhi ya pori tengefu kuwa pori la akiba ili kuimarisha usimamizi na kuhimiza matumizi endelevu. Aidha, Kamati inasitisiza umuhimu wa kuendelea kuwaelimisha, kuwahamasisha na kuwashirikisha wananchi na wadau wengine katika usimamizi wa Bonde la Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mawaziri kuhusu ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi nchini ilipata fursa ya kutembelea Bonde la Mto Kilombero. Katika ziara hiyo, Kamati ilisitisiza umuhimu wa kuendelea kulinda na kuhifadhi maeneo ya hifadhi za misitu, wanyamapori na vyanzo vya maji. Wizara yangu itazingatia mapendekezo ya Kamati ya Mawaziri kuhusu ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi nchini, hususan katika kipindi hiki ambacho Serikali inatekeleza ujenzi wa Mradi mkubwa wa Kufua Umeme katika Bonde la Mto Rufiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya *WMA* yanasisimamia biashara ya uwindaji wa kitalii na yanahitaji kuwa na wajumbe wenye weledi na uelewa wa masuala ya uwekezaji, uongozaji na usimamizi katika tasnia ya utalii. Aidha, mabaraza ya *WMA* yanaingia mikataba na kampuni/watu wenye uelewa mkubwa katika matumizi endelevu ya wanyamapori. Kutokana na mahitaji hayo, Kanuni za *WMA's* za mwaka 2018 zimeweka masharti ya wajumbe wanaounda mabaraza hayo kuwa na elimu isiyopungua kidato cha nne. Hata hivyo, utekelezaji wa Kanuni hizo umekabiliwa na changamoto ya malalamiko kuwa baadhi ya watu ambaa hawana elimu tajwa wananyimwa haki ya kuwa wajumbe

wa mabaraza hayo. Katika kutatua changamoto hiyo, Wizara inafanya marekebisho Kanuni hizo ili kuweka uwiano kati ya wajumbe wa mabaraza wenye elimu ya kidato cha nne na wasio kuwa na sifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha ustawi wa wanyamapori na mazingira yao, Wizara imeandaa Kanuni za shoroba, maeneo ya mtawanyiko, maeneo ya kinga na mapito ya wanyamapori. Kanuni hizo zitawezesha kuongeza ukubwa wa maeneo ya wanyamapori, kupatikana kwa mazalia na malisho ya wanyamapori na kuendeleza tofauti za vinasaba kwa kuzuia kuzaliana kwa familia zenye uhusiano wa karibu. Aidha, shoroba na mapito ya wanyamapori 31 yamebainishwa baada ya kufanyiwa upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, maeneo na shoroba hizo yameendelea kutumika kwa shughuli za binadamu zikiwemo kilimo, ufugaji na makazi. Hali hiyo imesababisha kuzibwa kwa shoroba na kutokea kwa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi, Halmashauri, wananchi na wadau wengine kufungua shoroba husika na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza matumizi ya mkaa na kuhifadhi mazingira, Wizara imeendelea kuhimiza na kushauri wadau na taasisi binafsi kuongeza uzalishaji na matumizi ya nishati mbadala. Katika kutekeleza hilo, mikutano minne ya uhamasishaji imefanyika kwa vikundi vinne vya PORECO, TaTEDO, MBALAWALA na MAKAMBI kuhusu matumizi ya nishati ya makaa ya mawe kwa matumizi ya kupikia. Aidha, vikundi sita vinavyojihusisha na utengenezaji wa mkaa vilipatiwa mafunzo ya utaratibu wa sheria wa kusafirisha mazao ya misitu. Vilevile, vijiji vya Masungula, Igale na Kilimampimbi katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini vimewezeshwa kuanzisha mashamba ya miti yenye ekari 10 kwa ajili ya kuzalisha nishati ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeanza kuandaa Mradi wenye lengo la kupanua wigo na kuendeleza mazao ya utalii yenye matokeo ya haraka. Msukumo huo unatokana na tasnia ya utalii nchini kutegemea zaidi utalii wa wanyamapori. Upanuzi wa wigo wa mazao ya utalii kwa aina na jiografia utasaidia kuwa na utalii endelevu na kuongeza Pato la Taifa. Aidha, Tanzania ina fursa kubwa za kuendeleza utalii wa fukwe, meli na mikutano kutokana na kuwepo kwa ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi na maziwa makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuwepo kwa viwanja vikubwa vyta ndege vyta *Julius Nyerere International Airport*, *Kilimanjaro International Airport*, Mwanza na Songwe kunaweka mazingira wezeshi ya kuanzisha na kuendeleza utalii wa fukwe, meli na utalii wa mikutano. Kutokana na fursa hizo, mradi unaotayarishwa utaanza kutekelezwa katika maeneo ya Bandari ya Dar es Salaam na Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha utoaji wa elimu yenye weledi na kukidhi viwango katika Sekta ya Utalii na Ukarimu, Wizara imewezesha wakufunzi saba kupata mafunzo ya muda mrefu na 31 mafunzo ya muda mfupi. Aidha, watumishi 73 wa kada mbalimbali wamepatiwa mafunzo ili kuboresha utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Sekta Binafsi na wadau wengine imefanya maadhimisho ya Tamasha la Urithi wa Mtanzania (*Urithi festival*) kwa mara ya kwanza katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Arusha, Zanzibar na Wilaya ya Karatu. Lengo la tamasha hilo ni kuongeza wigo wa mazao ya utalii, uelewa wa wageni kuhusu Tanzania na idadi ya siku ambazo watalii watakaa nchini. Tamasha limejielekeza kwenye historia, utamaduni, malikale, lugha, chakula, mavazi, imani, mila na desturi zetu. Tamasha hilo litaendelea kufanyika Septemba kila mwaka katika mikoa yote Tanzania Bara ili kunadi urithi na utamaduni wa Mtanzania ndani na nje ya nchi kama zao la utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza miradi 11 ya maendeleo ambayo inalenga kuimarisha usimamizi wa maliasili na kuendeleza utalii Kanda ya Kusini, usimamizi endelevu wa ikolojia ya ardhioevu ya Bonde la Mto Kilombero na Mto Rufiji, kujenga uwezo wa maeneo ya hifadhi, mapori ya akiba na kikosi dhidi ya ujangili pia kupanda miti kibashara, kujenga uwezo wa jamii katika kusimamia misitu, kujenga uwezo wa taasisi na mafunzo ya misitu na ufugaji nyuki, kuwezesha wananchi kunufaika na misitu na uhifadhi wa misitu ya mazingira asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa kuzalisha umeme Rufiji unatekelezwa na Wizara ya Nishati, ambapo eneo la mradi liko katika Pori la Akiba Selous. Katika utekelezaji wa mradi huo, Wizara imefanya tathmini ya maliasili zinazopatikana katika eneo la mradi ili kutambua *species* za mimea na wanyamapori zinazoweza kuwa hatarini kutoweka na thamani ya mazao ya misitu yatakayovunwa na kuuzwa kibashara. Kutokana na tathmini hiyo, Wizara imeandaa mpango wa kuhifadhi *species* zilizo hatarini kutoweka na kukata miti katika eneo ambalo bwawa litajengwa. Aidha, Wizara imeimarisha ulinzi katika maeneo ya lindimaji na kutoa wataalam wa uhifadhi kwenye eneo la mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ni pamoja na upungufu wa vitendea kazini na miundombinu duni na ongezeko la migongano kati ya binadamu na wanyamapori. Aidha, matumizi yasiyo endelevu ya maliasili na uharibifu wa malikale, mabadiliko ya tabianchi, kuenea kwa hali ya jangwa na mmomonyoko wa ardhi, na uchomaji moto ovyo yameendelea kuathiri ubora wa maliasili na malikale. Changamoto nyingine ni maeneo ya shoroba kutumika kwa shughuli za binadamu ambazo zinazuia wanyamapori kupita kutoka eneo moja kwenda lingine na uchimbaji wa madini kwenye maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imejipanga kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. Hatua hizo ni pamoja na kuhimiza matumizi ya

teknolojia katika uvunaji na uchakataji wa mazao ya misitu na nyuki; na kuhamasisha na kutekeleza mikakati ya upandaji miti, kuhifadhi maeneo ya ardhoevu na misitu ya lindimaji. Aidha, Wizara itaendelea kuhimiza matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa misitu, kuongeza wigo wa mazao ya utalii na utangazaji wa vivutio vya utalii, kushirikisha wadau katika uhifadhi wa maliasili na malikale na kuendeleza utalii. Vilevile, Wizara itatekeleza mikakati ya kujenga uwezo wa kusimamia maliasili, malikale na maendeleo ya utalii, kufanya mapitio ya sera, sheria na kanuni zinazosimamia maliasili, malikale na utalii na kudumisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara inakadiria kukusanya Sh.71,538,430,944 kutoka katika vyanzo vya Idara, Mifuko na Taasisi zilizo chini yake. Kati ya fedha hizo, Idara zitakusanya Sh.22,671,945,992, Taasisi zinazopata ruzuku zitakusanya Sh.26,987,619,944.27 na Mifuko ya Uhifadhi ya *TWPF* na *TaFF* itakusanya Sh.21,878,865,008. Aidha, Sh.701,805,841,651 zinakadiria kukusanya; *TANAPA* (shilingi bilioni 314.1), *NCAA* (shilingi bilioni 169.1), *TAWA* (shilingi bilioni 65.1) na *TFS* (shilingi bilioni 153.5). Taasisi hizo hukusanya maduhuli kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali, Mifuko ya Uhifadhi na Maendeleo ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inakadiria kutumia shilingi bilioni 120.2. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 71.3 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 48.9 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Makadirio ya matumizi ya kawaida yanajumuisha makadirio ya mishahara ambayo ni shilingi bilioni 52.6 na makadirio ya matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 18.7. Aidha, shilingi bilioni 48.9 zitatumika kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 47.9 zitatoka kwa washirika wa maendeleo na shilingi bilioni moja zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itakamilisha nyaraka za Baraza la Mawaziri kuhusu Sera za Taifa za Misitu, 2019 na Utalii, 2019 na kukamilisha mapitio ya Sheria ya Mambo ya

Kale. Aidha, Wizara itafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki na Sheria ya Misitu, Sura 323. Vilevile, Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori, Sura 283, Sheria za Shirika la Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro zitaunganishwa na kuwa sheria moja ambayo itajumuisha Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania. Pia, Sheria Namba 5 ya mwaka 1980 iliyoanzisha *TAFORI* na Mpango wa Taifa wa II wa Utafiti wa Misitu (*NAFORM II* (2011 – 2020) utaendelea kufanyiwa mapitio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea na taratibu za kubadilisha hadhi maeneo ya hifadhi na yasiyohifadhiwa ili kukabiliana na changamoto za uharibifu wa maliasili na mazingira. Katika kutekeleza azma hiyo, Jumuiya ya Hifadhi ya Wami Mbiki na Mapori ya Litumbandyosi na Gesimazowa yatabadilishwa kuwa mapori ya akiba. Aidha, eneo la ardhloevu la Ziwa Natron litabdalishwa kuwa hifadhi ya ardhloevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara itakamilisha taratibu za kubadili hadhi ya Mapori ya Akiba Kigosi, Moyowosi na Ugalla kuwa hifadhi za Taifa. Pia, Wizara itabdalilisha hadhi misitu 12 kuwa misitu ya hifadhi ya mazingira asilia. Misitu hiyo ni Hassama *Hills* na Nou (Mbulu na Babati), Uzigua (Bagamoyo na Handeni), Pugu na Kazimzumbwi (Kisarawe); na misitu iliyopo katika vilima vya Mbarika ambako kuna misitu ya hifadhi ya Lugamba, Sali, Mahenge *Scarp*, Mselezi, Myowe, Nawenge (Mahenge) na Kimboza (Morogoro).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kupitia maonesho ya Sabasaba, Nanenane, Karibu Kusini, *East Africa Trade Fair*, Karibu Kili Fair, *SITE* na matamasha ya Urithi (Urithi Festival) na Utamaduni wa Mtanzania. Aidha, Wizara itashiriki katika maonesho ya uwindaji wa kitalii yanayofanyika nchini Marekani kila mwaka (*Safari Club International*na *Dallas Club International*). Vilevile, Wizara itatangaza vivutio vya utalii katika nchi za Ulaya, Amerika, Australia na Asia kwa kushirikiana na Ofisi za Balozi, Mawakala wa Utalii, Mabalozi

wa hiari wa utalii, vyombo nya habari ikiwemo *Tanzania Safari Channel*, watu mashuhuri na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendeleza mikakati ya kukuza utalii kanda ya kusini na maeneo ya hifadhi mpya za Bihamarulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika. Aidha, Wizara itaibua shughuli mpya za utalii ndani ya eneo la hifadhi ya Ngorongoro ikiwemo ujenzi wa *walking trails* katika kreta za Empakai na Olmoti, kutengeneza mtandao wa barabara katika eneo la Ndutu na barabara...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri umesoma vizuri sana, naomba uombe hela.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Taarifa yote iingie kwenye *Hansard* kama nillivyoilwasillsha na sasa naomba kuomba fedha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Sh.120,202,638,734 kwa matumizi ya Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii. Kati ya fedha hizo, Sh.71,312,649,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.48,889,988,734 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Sh.42,589,344,000 za mishahara na Sh.18,723,305,000 za matumizi mengineyo. Aidha, Fedha za Maendeleo zinajumuisha Sh.1,000,000,000 fedha za ndani na shilingi billioni 47.9 fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kwa kuzishukuru nchi, mashirika, taasisi mbalimbali na marafiki wa uhifadhi kwa ushirikiano waliooutoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Ninachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo:-

Serikali za Kanada, China, Ufini, Korea Kusini, Marekani, Norway, Ubelgiji, Ujeruman, Uswisi na Jumuiya ya nchi za

Ulaya. Mashirika na taasisi ni pamoja na *AWF, AWHF, ENABEL, FAO, FZS, GEF, GIZ, ILO, ICCROM, ICOM, ICOMOS, IUCN, KfW, NORAD, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninahitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na hotuba hii itapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii; mnrt.go.tz

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII MHESHIMIWA
DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA (MB), WAKATI AKIWASILISHA
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA
MWAKA WA FEDHA 2019/2020 – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, ninaomba Bunge lako tukufu lijadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

2. Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu, Hotuba ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Ninatumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu kwa maelekezo yao

katika usimamizi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii. Maelekezo yao yameendelea kutoa dira ya uhifadhi, ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi.

3. Kwa upekee, ninamshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Japhet N. Hasunga (Mb), aliyekuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na sasa Waziri wa Kilimo, Maj. Gen. Gaudence S. Milanzi (Katibu Mkuu Mstaafu), viongozi wengine, wananchi na madaktari kwa msaada na matibabu waliyonipa baada ya kupata ajali ya gari mwezi Agosti 4, 2018. Katika ajali hiyo, Wizara ilimpoteza ndugu Hamza Temba, Afisa Habari Daraja I. Ninamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahala pema peponi – Amina.

4. Mheshimiwa Spika, ninakupongeza wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kulingoza Bunge letu tukufu kwa weledi. Aidha, ninaishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushauri ambao umeendelea kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Vilevile, ninawapongeza wabunge wote waliochaguliwa na kuteuliwa kisha kuapishwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Uadilifu wao, tabia ya kujituma na kufanya kazi kwa bidii ndiyo sababu kubwa ya kuwa sehemu ya wawakilishi wa wananchi katika Bunge hili tukufu. Pia, ninawapongeza wabunge waliochaguliwa kuwa mawaziri na manaibu waziri kuziongoza wizara mbalimbali.

5. Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Mheshimiwa Constantine J. Kanyasu (Mb), Naibu Waziri; Profesa Adolf F. Mkenda, Katibu Mkuu; na Dkt. Aloyce K. Nzuki, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, ninawashukuru wakurugenzi na wakuu wa vitengo, wakuu wa mashirika na taasisi, watumishi na wadau kwa ushirikiano wanaotupatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

6. Mheshimiwa Spika, ninawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Nzega Vijijini kwa kuendelea kuniunga mkono kwa dhati katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge na

Waziri wa Maliasili na Utalii. Ninapenda kuwahimiza kuimarisha uhifadhi wa maliasili, malikale na kuendeleza utalii kwa maendeleo endelevu. Aidha, ninamshukuru kwa dhati mke wangu Dkt. Bayoum Kigwangalla na familia yangu kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekekeleza majukumu yangu.

7. Mheshimiwa Spika, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzango kutoa pole kwa ndugu, marafiki na wananchi wa majimbo ya Buyungu na Korogwe vijijiini kwa vifo vyta Mheshimiwa Kasuku Bilago kilichotokea Mei, 2018 na Mheshimiwa Stephen Hillay Ngonyani kilichotokea Julai, 2018. Aidha, ninatoa pole za dhati kwa ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao na mali kuharibiwa kutokana na kushambuliwa na wanyamapori, ajali na maafa yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini.

8. Mheshimiwa Spika, kwa upekee ninatoa pole kwa ndugu, marafiki na watumishi wote wa Wizara kutokana na watumishi waliopoteza maisha wakiwa wanatekeleza majukumu yao. Watumishi wawili walishambuliwa na wafugaji kwa kutumia mishale ya sumu, watumishi watano walishambuliwa na wanyamapori na mtumishi mmoja alizama majini. Aidha, watumishi wanne walijeruhiwa na wananchi, mmoja na majangili na mmoja na wanyamapori. Kwa hakika, hawa ni mashujaa na wamekuwa wakitetea rasilimali za nchi - Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahala pema peponi, Amina. Vilevile, ninatoa pole kwa watumishi waliojeruhiwa na ninawaombea wapone haraka na kuendelea na majukumu yao.

9. Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi, ninaomba kuwasilisha hotuba yangu ambayo imegawanyika katika sehemu kuu sita: **Kwanza**, Utangulizi; **Pili**, Dira, Dhima na Majukumu ya Wizara; **Tatu**, Mchangwa Maliasili, Malikale na Utalii katika Maendeleo Endelevu; **Nne**, Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii; **Tano**, Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019; na **Sita**, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA

10. Mheshimiwa Spika, Wizara imepewa dhamana ya kusimamia uhifadhi wa maliasili, malikale na maendeleo ya utalii kwa kushirikiana na wadau. Kutokana na dhamana hiyo, Dira ya Wizara ni "*Maliasili na malikale zilizohifadhiwa kwa manufaa ya Watanzania wakati ikiongoza kuchangia ukuaji wa uchumi*". Aidha, Dhima ya Wizara ni "*Uhifadhi endelevu wa maliasili na malikale na kuendeleza utalii kwa manufaa ya Taifa*". Vilevile, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuandaa na kupitia sera, mikakati na miongozo mbalimbali; kuandaa, kupitia na kusimamia sheria na kanuni; kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa sera, sheria, programu na miongozo; kujenga uwezo wa kitaaluma na kitaasisi na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

MCHANGO WA MALIASILI NA UTALII KATIKA MAENDELEO ENDELEVU

11. Mheshimiwa Spika, Tanzania imejaliwa kuwa na maeneo ya hifadhi za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale yenye mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, ustawi wa wananchi na ukuaji wa uchumi. Maeneo ya maliasili yanatoa huduma za maji kwa matumizi mbalimbali; makazi ya wanyamapori na viumbe wengine, uchavushaji, uhifadhi wa udongo, ufyonzaji wa kaboni na hivyo kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Uhusiano bora kati ya uhifadhi na maendeleo unachangia katika ustawi wa maliasili, matumizi endelevu, ustawi wa wananchi, ukuaji wa uchumi na usalama wa Taifa. Hivyo, ninaendelea kutoa rai kwa umma kuendelea kujenga mtazamo chanya na kushirikiana na Wizara katika kuhifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII

12. Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii imepitia taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha

2019/2020. Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo 21 yanayolenga kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Napenda kiliarifu Bunge lako tukufu kuwa ushauri wa Kamati umezingatiwa katika mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020.

UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Ukusanyaji Maduhuli

13. Mheshimiwa Spika, Wizara iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 63,282,680,713**. Hadi Machi 2019, **Shilingi 37,951,669,310** sawa na asilimia 60 ya makadirio zimekusanywa. Aidha, Mashirika ya TANAPA, NCAA, TAWA na TFS yaliidhinishiwa kukusanya **Shilingi 619,521,447,545**. Hadi Machi 2019, **Shilingi 501,113,265,899.76** sawa na asilimia 80.9 ya makadirio zimekusanywa. Mashirika hayo yalitumia fedha hizo kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya uhifadhi, uendelezaji utalii, na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

14. Mheshimiwa Spika, Wizara iliidhinishiwa bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo ya **Shilingi 116,310,848,543.15**. Bajeti hiyo inajumuisha **Shilingi 86,231,466,543** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 29,978,082,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi Machi 2019, Wizara imepokea **Shilingi 49,842,260,769**. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi 39,653,292,391** ni matumizi ya kawaida na **Shilingi 10,188,968,377** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni

15. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha rasimu za Sera za Taifa za Misitu (2019) na Utalii (2019) na mikakati ya utekelezaji wake. Wadau wote wameshirikishwa kikamilifu katika kuandaa sera hizo. Hatua inayofuata ni kuwasilisha rasimu husika kwenye Baraza la Mawaziri kwa uidhinishaji. Aidha,

Wizara imekamilisha maandalizi ya rasimu ya mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Wanyamapor Sura 283 na inapitia Sheria ya Mambo ya Kale na kuboresha sheria za kisekta kwa kupitia kanuni na kutayarisha miongozo mbalimbali.

Mafanikio

Kupungua kwa Ujangili

16. Mheshimiwa Spika, Serikali imepiga hatua na kupata mafanikio makubwa katika kutokomeza ujangili. Matokeo ya sensa ya tembo katika mfumo ikolojia wa Selous – Mikumi iliyofanyika mwaka 2018, yanaonesha kuwa idadi ya tembo haipungui. Aidha, sensa hiyo haikubaini mizoga mipya ya tembo waliouawa na majangili katika mfumo ikolojia huo. Sote tunashuhudia kuongezeka kwa idadi ya tembo na wanyamapor wengine waliokuwa wakiwindwa na majangili. Hali hiyo inasababisha wanyamapor kuanza kuonekana katika maeneo ambayo awali haikuwa rahisi kuwaona. Mfano, hivi karibuni tembo wameonekana eneo la Chuo Kikuu cha Dodoma mara mbili.

17. Mheshimiwa Spika, mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika kupambana na ujangili ni kutokana na uongozi shupavu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na viongozi wetu wote wa ngazi ya juu. Uongozi huu shupavu umefanya kazi ya kuratibu vyombo vyya ulinzi na usalama kwenye Kikosikazi cha Taifa Dhidi ya Ujangili (*National Task Force Antipoaching*) kuwa rahisi na yenye mafanikio. Kutokana na juhudhi hizo tunashuhudia mapapa wa ujangili wakikamatwa kwa kasi kubwa zaidi, kufikishwa mahakamani na kuhukumiwa vifungo vyya miaka mingi. Mfano, mhalifu sugu, Bibi Yang Feng Lan kwa jina maarufu la *Queen of Ivory*, amehukumiwa kifungo cha miaka 17 jela na kulipa faini ya shilingi bilioni 26. Adhabu hiyo imetolewa kutokana na jangili huyo kujihusisha na kuratibu mtandao mkubwa wa biashara haramu ya nyara hususan meno ya tembo na pembe za faru. Aidha, watuhumiwa wengine wa ujangili wameendelea kukamatwa hususan wale wanaotuhumiwa kufanya biashara haramu ya meno ya tembo kwa muda mrefu.

18. Mheshimiwa Spika, jitihada za kupambana na ujangili zimetuwezesha kutambua mbinu mbalimbali na mitandao ya ujangili. Hivi karibuni tumewanasa baadhi ya watumishi wa umma na hakimu mmoja kwa tuhuma za kushiriki kwenye mtandao wa kusaidia na kulinda majangili. Watuhumiwa wote wamefunguliwa mashtaka. Serikali itaendelea kuwasaka wote wanaofadhili na kuwezesha ujangili hadi kutokomeza kabisa uhalifu huo.

Uanzishwaji wa Jeshi Usu

19. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kudhibiti ujangili, Serikali imeanzisha Jeshi Usu la kulinda maliasili zetu. Hatua hiyo inatoa msukumo wa kipekee katika kuimarisha nidhamu ya watumishi ikiwa ni pamoja na kukabiliana na changamoto za ujangili unaotumia mbinu za kisasa kama vile silaha za kivita. Mfumo huo ulizinduliwa rasmi Novemba, 2018 na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais. Hadi Machi 2019, watumishi 2,176 kutoka TANAPA, NCAA, TAWA na TFS wamepatiwa mafunzo ya Jeshi Usu.

Kubadilisha Hadhi Maeneo ya Hifadhi

20. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kubadilisha hadhi maeneo ya hifadhi ili kuimarisha uhifadhi na ulinzi hususan katika maeneo ya mpakani na kuendeleza utalii. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara inakamiliشا taratibu za kubadili hadhi mapori ya akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda, na Rumanyika-Orugundu kuwa hifadhi za Taifa. Aidha, mchakato wa kubadili hadhi ya mapori ya akiba Kigosi, Moyowosi na Ugalla unaendelea.

21. Wizara imetayarisha mapendekezo ya kubadili mpaka wa Hifadhi ya Taifa Serengeti ($14,763 \text{ km}^2$) kwa kujumuisha Pori Tengefu Ghuba ya Speke (57 km^2) na sehemu ya ukanda wa maji Ziwa Victoria (81 km^2). Hatua hiyo itahakikisha upatikanaji wa malisho na maji kwa wanyamapori muda wote, kuimarisha usimamizi wa mazalia ya samaki, kupunguza migogoro na kufungua fursa za maendeleo ya utalii Kanda ya Ziwa na kuimarika kwa ustawi wa wananchi. Utekelezaji

wa mapendekezo ya kubadili hadhi maeneo hayo unashirikisha wadau wote na fidia stahiki zitalipwa pale itapolazimu kuhamisha wakazi.

22. Mheshimiwa Spika, Wizara imepandisha hadhi misitu ya hifadhi ya Mwambesi (Tunduru); Pindiro (Kilwa), Itulu Hills (Sikonge), Magombera (Kilombero) na Kalambo Falls (Kalambo) kuwa misitu ya hifadhi ya mazingira asilia. Aidha, Wizara imezindua rasmi mji wa Mikindani kuwa mji wa kihistoria.

Ongezeko la Idadi ya Watalii na Mapato

23. Mheshimiwa Spika, idadi ya watalii walioingia nchini imeongezeka kutoka 1,327,143 mwaka 2017 hadi kufikia watalii 1,505,702 mwaka 2018. Ongezeko hilo limechangia kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii kutoka Dola za Marekani bilioni 2.2 mwaka 2017 hadi kufika Dola za Marekani bilioni 2.4 mwaka 2018. Mafanikio hayo yanatokana na jitihada mbalimbali za kutangaza vivutio vya utalii kupitia maonesho ya WTM (Uingereza), ITB (Ujerumani), *Conservation and Tourism Fair (Rwanda)*, *Travel Market Top Resa (Ufaransa)*, *Magical Kenya Travel Expo (Kenya)*, *International Tourism Travel Expo (Kanada)*, *China International Expo na Road show (China)*, *Dutch Expo (Uholanzi)*, *Outbond Travel Market - OTM na road show (India)*, *FITUR (Hispania)*, *Holiday Fair (Ubeligiji)*, *na International Mediterranean Tourism Market - IIMTM (Israeli)* na Falme za Kiarabu.

24. Mheshimiwa Spika, jitihada nyingine zilizofanyika ni kuendelea kutangaza vivutio vya utalii kupitia vyombo vya habari ndani na nje ya nchi - kwa mfano, TBC1, ITV, Clouds TV, BBC Swahili, na Doutche Welle Ujerumani; mitando ya kijamii; kuandaa ziara za waandishi wa habari wa nje; *bloggers*; kutumia watu mashuhuri; na ofisi za Balozi zetu nje ya nchi. Aidha, Wizara imekamilisha maandalizi ya utambulisho mpya wa utalii Tanzania (*Tanzania Destination Brand*) ujulikanao kama "*Tanzania, Unforgettable*". Utambulisho huo umeanza kutumika kwenye maonesho mbalimbali yaliyofanyika nje ya nchi na ndani ya nchi. Vilevile,

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imeanzisha Chaneli maalumu ya kutangaza vivutio vya utalii "*Tanzania Safari Channel*" ambayo itasaidia kuwawutia wageni wengi kutembelea nchini. Wizara imeendelea kuchangia katika kugharimia uanzishaji na uendeshaji wa chaneli hiyo.

25. Mheshimiwa Spika, utangazaji wa vivutio vya utalii umeendelea kuonesha matokeo chanya ambapo mnamo tarehe 20 Aprili 2019, Tanzania ilipokea kundi la watalii 1,000 kwa wakati mmoja kutoka nchini Israel. Kutokana na ujio huo, watalii wengi zaidi wanatarajiwा kuja kutoka nchi hiyo. Aidha, tarehe 12 Mei 2019, kundi la watalii 336 wakiwemo waandishi wa habari kutoka nchini China lilipokelewa. Hili ni kundi la kwanza kati ya watalii 10,000 wanaotarajiwা kutoka China.

26. Mnamo tarehe 1 Aprili 2019, kundi la wafanyabiashara ya utalii, wakala wa utalii na waandishi wa habari za utalii kutoka nchi za Malaysia, Ufilipino, Thailand na Indonesia walifika nchini kutazama vivutio vya utalii vilivyomo nchini na wameahidi kwenda kuvitangaza. Mafanikio haya yanatokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali kutangaza utalii katika masoko mapya ya Israel, China, India na Urusi. Aidha, mafanikio haya yamechangiwa na juhudzi za ofisi za ubalozi zilizopo nje ya nchi. Tunamshukuru kwa namna ya pekee Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa kuongoza hafla za kupokea na kuyaaga makundi hayo ya awali ya watalii.

Kupanua Wigo wa Mazao ya Utalii

27. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza utalii, Wizara imeendelea na jithada za kupanua wigo wa mazao ya utalii. Mazao hayo ni pamoja na utalii wa fukwe, utalii wa mikutano, utalii wa meli, utalii wa majini, utalii wa michezo, utalii wa utamaduni na kuanzisha shughuli mpya za utalii katika maeneo ya hifadhi. Shughuli hizo zinajumuisha safari za kutembea kwa miguu hifadhini, safari za puto (*Hot Air Balloon*), utalii wa *Canopy walkway* na safari za mitumbwi kwenye hifadhi za maji kama vile Rubondo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Majiji ya Dar es salaam

na Arusha imezindua safari za kitalii ndani ya miji hiyo (*city tours*). Vilevile, miongozo ya uwekezaji katika maeneo yanayosimamiwa na Wizara imeandaliwa ili kutoa fursa za uwekezaji katika shughuli za utalii. Pia, ili kuweka mazingira wezeshi ya kukuza utalii wa meli, Wizara itajiunga tena na vyama vya waandaaji wa utalii wa meli duniani.

Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini kupitia Mradi wa REGROW

28. Mheshimiwa Spika, Wizara imeanza kutekeleza Mradi wa Kusimamia Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (REGROW). Mradi huo utafungua utalii Kanda ya Kusini na kwa kuanzia, utaimarisha miundombinu ya ndani ya hifadhi za Taifa Ruaha, Mikumi, Milima ya Udzungwa na Pori la Akiba Selous Kanda ya Kaskazini (Matambwe) kwa kujenga barabara, madaraja, viwanja vya ndege, malango ya kuingia, vituo vya utalii, kambi za watalii, na shughuli za kiuchumi za kijamii zinazozunguka hifadhi hizo. Aidha, ili kuhakikisha Mto Ruaha Mkuu unatiririsha maji mwaka mzima, mradi utaimarisha usimamizi wa matumizi ya maji katika Bonde la Usangu.

29. Hadi sasa, zabuni za usanifu wa ujenzi wa barabara, madaraja na majengo katika hifadhi tatu za Taifa zipo katika hatua za mwisho za kupata wataalam washauri. Aidha, zabuni ya usanifu wa viwanja vya ndege ndani ya hifadhi ipo katika hatua ya kutangazwa na zabuni ya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji ya skimu ya umwagiliaji ya Madibira ipo katika hatua ya kupata mkandarasi.

Kuboresha Miundombinu ya Utalii Ikolojia

30. Mheshimiwa Spika, Wizara imejenga ofisi sita na vituo 15 vya ulinzi katika hifadhi za mazingira asilia za Chome, Magamba, Mlima Rungwe, Mkingu, Minziro, na Uzungwa Scarp. Aidha, barabara zenye urefu wa kilometra 89.6 na njia za kutembea watalii zenye urefu wa kilometra 102.6 zimesafishwa katika misitu hiyo. Vilevile, ujenzi wa ngazi yenye mita 183 kuelekea kwenye maporomoko ya Kalambo

umefanyika. Pia, kambi 11 za kupumzikia wageni zimesafishwa katika misitu saba ya hifadhi za asilia za Mlima Hanang, Mlima Rungwe, Uzungwa, Uluguru, Kimboza, Rondo na Kilombero.

Kuanzisha na Kuendeleza Mashamba Mapya ya Miti

31. Mheshimiwa Spika, jumla ya hekta 1,734 zimepandwa miti katika mashamba mapya ya miti ya Wino (Songea), Iyondo Msimwa (Ileje), Biharamulo (Chato), Mpepo (Mbinga), Buhigwe (Kigoma) na Mtibwa/Pagale (Mvomero). Aidha, shamba jipya kwa ajili ya uzalishaji wa gundi inayotokana na miti ya migunga lenye ukubwa wa hekta 50,000 limeanzishwa katika Wilaya ya Iramba (Singida).

Kuendeleza Vituo vya Mambo ya Kale

32. Mheshimiwa Spika, Wizara imeanza kuendeleza maeneo ya malikale kuitia mashirika ya TANAPA, NCAA, TAWA, na TFS ili kuhakikisha rasilimali hizo zinatumika kiutalii na kuongeza mchango katika Pato la Taifa. Mkakati huo unahusisha kuboresha miundombinu ya vituo hususan vituo vya kumbukumbu na taarifa, kuweka huduma muhimu kwa watalii, ofisi na barabara ili viwe na muonekano unaovutia na kufikika kwa urahisi.

33. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hiyo, TANAPA imepewa vituo vya Caravan Serai (Bagamoyo), Makumbusho ya Mkwawa na Zana za Kale za Mawe Isimila (Iringa), Dkt. Livingstone Ujiji (Kigoma), na Nyumba ya Kumbukizi ya Mwalimu Nyerere Magomeni (Dar es Salaam). Aidha, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imepewa vituo vya Michoro ya Miambani Mumba, Nyayo za Engaraserero, Mfumo wa umwagililaji Engaruka, Kituo cha Amboni na Kimondo cha Mbozi. Vilevile, TAWA imepewa vituo vya Magofu ya Kunduchi na Kilwa. Pia, TFS imepewa vituo vya magofu ya Tongoni (Tanga), Tembe la Kwhara na *Old Afya Building* (Tabora), Magofu ya Kaole, Michoro ya Miambani (Kondoa) na Ngome Kongwe (Bagamoyo). Katika kutekeleza jukumu hilo, mashirika yameanza kufanya tathmini ya namna ya kuviboresha na kuiendezea vituo hivyo. Uboreshaji huo

utasimiwa na Idara ya Mambo ya Kale na Shirika la Makumbusho ya Taifa.

34. Hadi sasa kazi zilizofanyika ni ujenzi wa Makumbusho ya kisasa katika Bonde la Olduvai, Kituo cha kumbukumbu na taarifa katika eneo la Kimondo cha Mbozi, ukarabati wa nyumba ya Kumbukizi ya Mwalimu Nyerere Magomeni, kuanzisha Siku ya Kimondo duniani ambayo itakuwa inasherehekewa kila mwaka na kuanza maandalizi ya kusherekea miaka 60 (*Diamond Jubilee*) ya uvumbuzi fuvu la *Zinjanthropus*.

Kuimarika kwa Mifumo ya Ukusanyaji Maduhuli

35. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utoaji wa huduma na ukusanyaji wa mapato ya Serikali, Wizara imekamilisha ujenzi wa mfumo funganishi wa kieletroniki wa kutoa leseni/vibali, kukusanya takwimu/taarifa na kukusanya mapato kutoka vyanzo mbalimbali ujulikanao kama *MNRT Portal*. Mfumo huo umeanza kutumika kukusanya maduhuli ya TAWA, TFS, TAWIRI, TAFORI, NMT, vituo 16 vya malikale na kuuza vitalu vya uwindaji na mazao ya misitu kwa njia ya minada. Aidha, Mfumo huo umefunganishwa na mifumo mingine ya TEHAMA ya Serikali kama vile TRA, GePG, eGA, BRELA, NIDA na TIRA ili kuwezesha utoaji wa huduma mbalimbali kwa pamoja. Vilevile, uwekaji wa *internet* (Wi-Fi) na ufungaji *CCTV camera* umefanyika kwenye malango ya kuingia na kutoka katika vituo vya TANAPA na NCAA. Mifumo hiyo imepunguza muda wa kuhudumia mteja; umerahisisha utoaji wa leseni, vibali na ada za mazao ya maliasili; na kuhakiki takwimu za wageni wanaoingia kwenye vivutio vya utalii na kuimarisha usalama wa wageni na watumishi.

Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara

36. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango na wadau wa sekta ya utalii imeendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara kama ilivyobainishwa katika mkakati ujulikanao kama *Blueprint*. Eneo mojawapo linalofanyiwa kazi ni

kukusanya tozo mbalimbali zinazohusiana na biashara za utalii kupidia dirisha moja (*one payment stop center*) litakaloratibwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na kusimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Lengo la kutumia mfumo wa *MNRT Portal* ni kukusanya na kuonesha mgawanyo wa tozo mbalimbali kwa kila taasisi na mamlaka. Hatua hiyo itarahisisha ukusanyaji wa tozo, kumuhudumia mteja kwa muda mfupi na kuondoa uwezekano wa kutoza mteja kodi mara mbili.

Masuala Mtambuka

Utatuzi wa Migogoro

37. Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 15 Januari, 2019, Mheshimiwa Rais aliwaagiza mawaziri wa kisekta kuwasilisha mapendekezo ya ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo wanayoyasimamia. Wizara ya Maliasili na Utalii ni moja ya wizara za kisekta zilizounda Kamati ya Mawaziri ya ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi. Kamati hiyo ambayo inaongozwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekamilisha kazi yake na kuwasilisha taarifa ya mapendekezo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini. Wizara imejipanga vema kutekeleza maelekezo yote ambayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakayotoa kuhusu utatuzi wa migogoro hiyo.

38. Mheshimiwa Spika, sambamba na utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais, Wizara imeendelea kutatua migogoro kwa kushirikiana na wizara nyininge na wananchi wa maeneo yenye migogoro. Baadhi ya jitihada zinazofanyika ni kutoa elimu ya uhifadhi, kuhakiki mipaka ya maeneo ya hifadhi, na kuweka alama za kudumu na mabango ya tahadhari ili mipaka ionekane kwa urahisi. Aidha, Wizara kwa kushirikisha jamii imepima mipaka ya Kituo cha Makumbusho ya Mtwara Mkwawa - Kalenga chenye ukubwa wa ekari 7.6 na kituo cha Tembe la Dkt Livingstone Kwihiara -Tabora na ipo katika hatua ya mwisho ya kupatiwa hati ya umiliki wa ardhi.

Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

39. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kudumisha na kuboresha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa kushiriki katika mikutano, semina na warsha mbalimbali. Kupitia Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Wizara imeshiriki katika kutayarisha Itifaki za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Usimamizi wa Mazingira na Maliasili, na Usimamizi wa Wanyamapori na Uendelezaji wa Utalii. Aidha, kupitia mradi wa Usimamizi wa Bioanuai na maeneo yaliyohifadhiwa (BIOPAMA I), Wizara imeshiriki katika kutayarisha taarifa ya tathmini ya hali halisi ya maeneo yaliyohifadhiwa (*State of Protected Areas*). Kazi hiyo itawezesha utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa BIOPAMA. Aidha, Wizara inashiriki katika kupitia vigezo vya madaraja ya hoteli na migahawa katika nchi wanachama wa Jumuiya.

40. Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki mkutano wa SADC uliofanyika nchini Afrika Kusini kwa ajili ya kujadili uendelezaji maeneo ya hifadhi yanayovuka mipaka (*Trans-frontier Conservation Areas*). Mkutano huo uliweka mkakati wa kukabiliana na changamoto za maeneo ya hifadhi yanayovuka mipaka. Aidha, Wizara ilishiriki Mkutano wa tatu wa *AFRI 100 Annual Partnership* uliofanyika nchini Kenya ukiwa na maudhui ya kurudishia maeneo ya uoto uliopotea Barani Afrika. Katika mkutano huo, Tanzania illahidi kurudishia hekta milioni 5.2 za uoto wa asili uliopotea ili kuboresha uhifadhi wa mazingira na kuongeza malighafi za viwanda.

41. Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki Mkutano Mkuu wa 42 wa UNESCO wa Kamati ya Urithi wa Dunia uliofanyika nchini Bahrain ambao ulijadili taarifa ya uhifadhi wa Ngorongoro na Serengeti na mradi wa ujenzi wa Bwawa la kufua umeme kwenye Mto Rufiji katika Pori la Akiba Selous, na mkutano wa Shirika la Utalii Duniani (UNWTO) na UNESCO nchini Uturuki uliojadili Kanuni za Maadili ya utalii na kujadili namna utalii wa utamaduni unavyochangia katika maendeleo ya uchumi. Kanuni hizo zinaandaliwa ili kuwezesha nchi kuwa na utalii utakaokidhi vigezo vya kimataifa.

42. Wizara ilishiriki katika mukutano wa 24 wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mkataba wa Mabadiili ya Tabianchi (UNFCCC) uliofanyika mjini Katowice, Poland, mwezi Disemba 2018. Mukutano huo ulihusu kujadiliana na kukubaliana katika utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiili ya Tabianchi, Itifaki ya Kyoto na Makubaliano ya Paris. Katika Mukutano huo, Wizara ilianzisha mazungumzo na Wizara ya Mazingira ya Poland kuhusu ushirikiano kati ya TFS na *State Forest Agency* ya nchini Poland.

Utawala na Uendelezaji Rasilimaliwateru

43. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo; kusimamia maslahi, maadili, ustawi na afya za watumishi; na kuboresha mazingira ya kufanyakazi. Mazingira ya kazi yameboreshwa kwa kuwajengea ofisi, kuwapatia vitendeakazi, vifaa vyta mawasiliano na matumizi ya teknolojia ya kisasa – mfano, kutumia *satellite collar* katika kufuatilia mienendo ya wanyamapori na matumizi ya maeneo yaliyohifadhiwa. Maboresho mengine yamehusisha matumizi ya ndege zisizo na rubani, kukamata wanyamapori kwa kutumia kemikali salama badala ya mitego, na kutumia *helicopter* katika maeneo hatarishi.

44. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake, Wizara imebadili mwelekeo kwa: (i) kuendeleza vituo vya mambo ya kale kuititia TANAPA, NCAA, TAWA, na TFS (ii) kuhamisha usimamizi wa vituo vya mambo ya kale kutoka Idara ya Mambo ya Kale kwenda Shirika la Makumbusho ya Taifa (NMT) (iii) kuhamisha baadhi ya majukumu muhimu ya uendelezaji utalii kutoka Idara ya Utalii kwenda Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) (iv) majukumu ya Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania (TTSA) yamehamishiwa TFS na (v) kuipa TAFORI jukumu la utafiti wa ufugaji nyuki. Kufuatia hatua hiyo, Idara ya Mambo ya Kale na Idara ya Utalii zitaendelea kusimamia masuala ya kisera, sheria, na ufuatiliaji na tathmini.

Majukumu ya Wizara

Utekelezaji wa Masuala Mahsusi Sekta Ndogo ya Wanyamapori

Ujenzi wa Barabara kutoka Lango la Loduare hadi SENAPA (Golini)

45. Mheshimiwa Spika, katika eneo ya Hifadhi ya Ngorongoro, Wizara imekubaliana na UNESCO kuhusu ujenzi wa barabara kutoka lango la Loduare hadi katika mpaka wake na Hifadhi ya Taifa Serengeti (Golini), yenye urefu wa Kilomita 88 kwa kiwango cha lami rafiki kwa mazingira. Barabara hiyo itakapokamilika itarahisisha shughuli za uhifadhi, usafiri kwa watalii na utoaji huduma za kijamii kwa wenyeji. Aidha, hatua hiyo itapunguza gharama za matengenezo ya mara kwa mara ya barabara na uharibifu wa mazingira ndani ya hifadhi.

Usimamizi wa Biashara ya Wanyamapori Hai

46. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufunga biashara ya wanyamapori hai kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi. Serikali inakamilisha taratibu za kuwarudishia wafanyabiashara fedha walizotumia kulipia huduma mbalimbali. Aidha, kwa sasa Wizara inaandaa mkakati wa kitaifa wa biashara ya wanyamapori hai kwa njia ya ufugaji wa wanyamapori ili kuleta tija kwa wananchi na kwa taifa. Mkakati huo utatoa fursa ya ajira kwa Watanzania pamoja na upatikanaji wa nyaraghafi kwa ajili ya viwanda nya ndani.

Uwindaji wa Kitalii

47. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya uwindaji wa kitalii inafanya mapitio ya Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za mwaka 2015. Mabadiliko yatakayofanyika katika Kanuni hizo yatahusisha kubadili mafungu (*packages*) ya siku za safari za uwindaji wa kitalii ili kupanua wigo na ufanisi katika biashara, kuongeza wigo wa idadi na spishi za wanyamapori wanaowindwa. Mabadiliko

mengine ni kupunguza viwango vya ada za uwindaji wa wanyamapori na ada zinazolipwa kabla ya kuwinda kwa kuzingatia hali ya masoko, kupunguza madaraja ya vitalu kutoka matano hadi matatu. Aidha, muhula wa uwindaji wa kitalii utaongezwa kutoka miaka mitano ya awali kwenda miaka 10 kwa vitalu vya daraja la kwanza na pili na miaka 15 kwa daraja la tatu. Marekebisho hayo yanalenga kuongeza idadi ya watalii wawindaji na mapato.

48. Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa Mwongozo wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii kwa njia ya mnada wa kielektroniki (*Guidelines for Allocation of Hunting Blocks through Auctioning*) pamoja na mfumo wa kielektroniki wa kugawa vitalu vya uwindaji wa kitalii. Utaratibu huo unatoa fursa kwa kampuni za uwindaji wa kitalii kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki kwenye ushindani wa kumiliki vitalu vya uwindaji wa kitalii hivyo, kuongeza uwazi na utawala bora katika tasnia ya uwindaji. Mnada wa kwanza umepangwa kufanyika tarehe 10 Juni 2019 na utahusisha vitalu 26. Tangazo la mnada limewekwa kwenye tovuti ya Wizara (www.mnrt.go.tz) na TAWA (www.tawa.go.tz)

Uwindaji wa Wenyeji

49. Mheshimiwa Spika, Wizara ilisitisha uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi mwaka 2015 kutokana na usimamizi hafifu, kutokuwepo vitalu vya uwindaji huo pamoja na ujangili. Wizara imefanya tathmini ya uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi na kuandaa mkakati wa kuboresha usimamizi wake. Kutokana na matokeo ya tathmini hiyo, Wizara imefungua uwindaji huo katika maeneo matano kuanzia mwaka 2018. Maeneo hayo ni maeneo ya wazi Kilwa, Kisarawe na Simbaguru, na mapori tengefu ya Kitwai na Ugalla. Aidha, Wizara inatarajia kutenga maeneo mengine kwa ajili ya uwindaji wa wenyeji. Vilevile, Wizara inakamilisha Kanuni za Uwindaji wa Wenyeji ambazo zitaruhusu uanzishwaji wa vituo na taratibu za kuuza nyamapori kwenye mabucha maalum.

Ulinzi wa Wananchi na Mali zao Dhidi ya Wanyamaporì Wakali na Waharibifu

50. Mheshimiwa Spika, mashirika ya TAWA, TANAPA na NCAA kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya na wadau wengine yameendelea kufanya doria za kudhibiti wanyamaporì wakali na waharibifu. Aidha, vituo vya askari vimewekwa katika maeneo yenye changamoto kubwa ya wanyamaporì wakali na waharibifu. Vilevile, mbinu na teknolojia mbalimbali zinazoendelea kutumika ni pamoja na kuweka uzio wa umeme na kuwalisha mikanda ya kielektroni (*collar*) tembo ili kufuatilia mienendo yao na kuwadhibiti wanapotoka ndani ya hifadhi kabla ya uharibifu kutokea. Katika kukabiliana na changamoto ya mamba na viboko, sensa ya wanyamaporì hao inaendelea katika maeneo ya Ziwa Rukwa na mito inayopita vijiji. Matokeo ya sensa hiyo yataonesha idadi ya mamba wanaopaswa kupunguzwa katika maeneo yenye matukio ya wananchi kujeruhija na kuuawa na mamba.

51. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi kufuatia uharibifu wa mali na upotevu wa maisha uliotokana na wanyamaporì wakali na waharibifu. Hadi Machi 2019, **Shilingi 1,426,636,500** zimelipwa kwa wananchi 7,320 wa wilaya 57 kama kifuta jasho na kifuta machozi.

Usimamizi wa Eneo la Bonde la Kilombero

52. Mheshimiwa Spika, Kamati iliyoundwa na Wizara mwezi Januari, 2018 imewasilisha taarifa yake ya namna bora ya kusimamia eneo la Bonde la Kilombero. Taarifa hiyo imewasilisha mapendekezo ya kufuta au kurekebisha mipaka ya viji viliyopimwa kinyume cha sheria ndani ya eneo la pori tengefu ambalo ni sehemu ya Bonde la Kilombero, kuendelea kuhifadhi maeneo nyeti ya ziada kwa uhai wa Bonde, kuwaondoa wananchi waliovamia na kusitisha uingizaji mifugo. Mapendekezo mengine yaliyowasilishwa ni kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi kwa kuendelea na zoezi la upimaji mipaka na uwekaji wa alama za kudumu, kubadili hadhi ya Pori Tengefu kuwa pori la akiba ili kuimarisha

usimamizi, na kuhimiza matumizi endelevu. Aidha, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuendelea kuwaelimisha, kuwahamasisha na kuwashirikisha wananchi na wadau wengine katika usimamizi wa Bonde la Kilombero.

53. Mheshimiwa Spika, Kamati ya Mawaziri kuhusu ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi nchini ilipata fursa ya kutembelea Bonde la Mto Kilombero. Katika ziara hiyo, Kamati ilisisitiza umuhimu wa kuendelea kulinda na kuhifadhi maeneo ya hifadhi za misitu, wanyamapori na vyanzo vya maji. Wizara yangu itazingatia mapendelekezo ya Kamati ya Mawaziri kuhusu ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi nchini, hususan katika kipindi hiki ambacho Serikali inatekeleza ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme Rufiji.

Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapor (WMAs)

54. Mheshimiwa Spika, mabaraza ya WMA yanasmamia biashara ya uwindaji wa kitalii na yanahitaji kuwa na wajumbe wenye weledi na uelewa wa masuala ya uwekezaji, uongozi na usimamizi katika tasnia ya utalii. Aidha, mabaraza ya WMA yanaingia mikataba na kampuni/watu wenye uelewa mkubwa katika matumizi endelevu ya wanyamapor. Kutokana na mahitaji hayo, Kanuni za WMAs za mwaka 2018 zimeweka masharti ya wajumbe wanaounda mabaraza hayo kuwa na elimu isiyopungua kidato cha nne. Hata hivyo, utekelezaji wa Kanuni hizo umekabiliwa na changamoto ya malalamiko kuwa baadhi ya watu ambao hawana elimu tajwa wananyimwa haki ya kuwa wajumbe wa mabaraza. Katika kutatua changamoto hiyo, Wizara inafanya marekebisho Kanuni hizo ili kuweka uwiano kati ya wajumbe wa mabaraza wenye elimu ya kidato cha nne na wasio kuwa na sifa hiyo.

Shoroba na Maeneo ya Mapito ya Wanyamapor

55. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha ustawi wa wanyamapor na mazingira yao, Wizara imeandaa Kanuni za Shoroba, Maeneo ya Mtawanyiko, Maeneo ya Kinga na Mapito ya Wanyamapor. Kanuni hizo zitawezesha kuongeza

ukubwa wa maeneo ya wanyamapori, kapatikana kwa mazalia na malisho ya wanyamapori na kuendeleza tofauti za vinasaba kwa kuzuia kuzaliana kwa familia zenye uhusiano wa karibu. Aidha, shoroba na mapito ya wanyamapori 31 yamebainishwa baada ya kufanyiwa upembuzi yakinifu. Hata hivyo, maeneo na shoroba hizo yameendelea kutumika kwa shughuli za binadamu zikiwemo kilimo, ufugaji na makazi. Hali hiyo imesababisha kuzibwa kwa shoroba na kutokea kwa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara itaendelea kushirikiana na OR-TAMISEMI; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi; Halmashauri; wananchi na wadau wengine kufungua shoroba husika na kuandaa mijango wa matumizi bora ya ardhi.

Utekelezaji wa majukumu mengine ya Wizara katika sekta ndogo ya wanyamapori, umefafanuliwa kuanzia ukurasa 34 mpaka 42.

Masuala Mahsusni ya Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki

Nishati inayotokana na kuni na mkaa

56. Mheshimiwa Spika, ili kupunguza matumizi ya mkaa na kuhifadhi mazingira, Wizara imeendelea kuhimiza na kushauri wadau na taasisi binafsi kuongeza uzalishaji na matumizi ya nishati mbadala. Katika kutekeleza hilo, mikutano minne ya uhamasishaji imefanyika kwa vikundi vinne vya PORECO, TaTEDO, MBALAWALA na MAKAMBI kuhusu matumizi ya nishati ya mkaa ya mawe kwa matumizi ya kupikia. Aidha, vikundi sita vinavyojihusisha na utengenezaji wa mkaa vilipatiwa mafunzo ya utaratibu wa sheria wa kusafirisha mazao ya misitu. Vilevile, vijiji vya Masungula, Igale na Kilimampimbi katika kanda ya nyanda za juu kusini vimewezeshwa kuanzisha mashamba ya miti yenye ekari 10 kwa ajili ya kuzalisha nishati ya kuni na mkaa.

Kiwanda cha Kuzalisha Karatasi cha Mufindi (Mufindi Paper Mills)

57. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya utafiti wa bei za tetefya katika nchi jirani ili kuhakikisha kuwa ada na tozo za

miti katika Shamba la Miti Sao Hill zinaendana na ghamama za kukuza miti. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa ada ya tozo kwa miti inayotumika kutengeneza tetefya nchini zipo chini ikilinganishwa na nchi jirani. Kufuatia matokeo hayo, Wizara imefanya marekebisho ya ada na tozo kwa miti inayotumika kutengeza tetefya kutoka Shillingi 19,400 hadi Shillingi 21,450 kwa mita moja ya ujazo wa miti.

Utekelezaji wa majukumu mengine ya Wizara katika sekta ndogo ya misitu na ufugaji nyuki, umefafanuliwa kuanzia ukurasa 44 mpaka 51.

Masuala Mahsusni ya Sekta Ndogo ya Utalii

Mradi wa Kuendeleza Mazao ya Utalii yenyeye Matokeo ya Haraka

58. Mheshimiwa Spika, Wizara imeanza kuandaa Mradi wenyeye lengo la kupanua wigo na kuendeleza mazao ya utalii yenyeye matokeo ya haraka. Msukumo huo unatokana na tasnia ya utalii nchini kutegemea zaidi utalii wa wanyamapori. Upanuzi wa wigo wa mazao ya utalii kwa aina na jiografia utasaidia kuwa na utalii endelevu na kuongeza pato la Taifa. Aidha, Tanzania ina fursa kubwa za kuendeleza utalii wa fukwe, meli na mikutano kutokana na kuwepo kwa ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi na maziwa makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa). Vilevile, kuwepo kwa viwanja vikubwa vya ndege vya JNIA, KIA, Mwanza na Songwe kunaweka mazingira wezeshi ya kuanzisha na kuendeleza utalii wa fukwe, meli na mikutano. Kutokana na fursa hizo, mradi unaotayarishwa utaanza kutekelezwa katika maeneo ya bandari ya Dar es Salaam na Kigamboni.

Kuboresha Mafunzo Kuendana na Mahitaji ya Soko

59. Mheshimiwa Spika, ili kuboresha utoaji wa elimu yenyeye weledi na kukidhi viwango katika sekta ya utalii na ukarimu, Wizara imewezesha wakufunzi saba kupata mafunzo ya muda mrefu na 31 mafunzo ya muda mfupi. Aidha, watumishi 73 wa kada mbalimbali wamepatiwa mafunzo ili kuboresha utendaji kazi.

Utekelezaji wa majukumu mengine ya Wizara katika sekta ndogo ya utalii, umefafanuliwa kuanzia ukurasa 52 mpaka 55.

Masuala Mahsusni ya Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale

Tamasha la Urithi wa Taifa

60. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; sekta binafsi; na wadau wengine imefanya maadhimisho ya Tamasha la Urithi wa Tanzania (*Urithi festival*) kwa mara ya kwanzu katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Arusha; Zanzibar; na wilaya ya Karatu. Lengo la tamasha hilo ni kuongeza wigo wa mazao ya utalii, uelewa wa wageni kuhusu Tanzania, na idadi ya siku ambazo watalii watakanza nchini. Tamasha limejielekeza kwenye historia, utamaduni, malikale, lugha, chakula, mavazi, imani, mila na desturi. Tamasha hilo litaendelea kufanyika Septemba kila mwaka katika mikoa yote Tanzania Bara ili kunadi urithi na utamaduni wa mtanzania ndani na nje ya nchi kama zao la utalii.

Utekelezaji wa majukumu mengine ya Wizara katika sekta ndogo ya mambo ya kale, umefafanuliwa kuanzia ukurasa 56 mpaka 59.

Miradi ya Maendeleo

61. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza miradi 11 ya maendeleo ambayo inalenga kuimarisha usimamizi wa maliasili na kuendeleza utalii Kanda ya Kusini; usimamizi endelevu wa ikolojia ya ardhi oevu ya Bonde la Mto Kilombero na Mto Rufiji; kujenga uwezo wa maeneo ya hifadhi, mapori ya akiba na Kikosi Dhidi ya Ujangili; kupanda miti kibiashara; kujenga uwezo wa jamii katika kusimamia misitu; kujenga uwezo wa taasisi na mafunzo ya misitu na ufgajji nyuki; kuwezesha wananchi kunufaika na misitu na uhifadhi wa misitu ya mazingira asilia.

Utekelezaji wa Majukumu ya Kimkakati

62. Mheshimiwa Spika, Mradi wa kuzalisha umeme Rufiji unatekelezwa na Wizara ya Nishati, ambapo eneo la mradi

liko katika Pori la Akiba Selous. Katika utekelezaji wa mradi huo, Wizara imefanya tathmini ya maliasili zinazopatikana kwenye eneo la mradi ili kutambua spishi za mimea na wanyamapori zinazoweza kuwa hatarini kutoweka na thamani ya mazao ya misitu yatakayovunwa na kuuzwa kibashara. Kutokana na tathmini hiyo, Wizara imeandaa mpango wa kuhifadhi spishi zilizo hatarini kutoweka na kukata miti katika eneo ambalo bwawa litajengwa. Aidha, Wizara imeimarisha ulinzi katika maeneo ya lindimaji na kutoa wataalam wa uhifadhi kwenye eneo la Mradi.

Changamoto na Utatuзи Wake

63. Mheshimiwa Spika, baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ni pamoja na upungufu wa vitendea kazi na miundombinu duni, na ongezeko la migongano kati ya binadamu na wanyamapori. Aidha, matumizi yasiyo endelevu ya maliasili na uharibifu wa malikale, mabadiliko ya tabianchi, kuenea kwa hali ya jangwa na mmomonyoko wa ardhi, na uchomaji moto ovyo yameendelea kuathiri ubora wa maliasili na malikale. Changamoto nyingine ni maeneo ya shoroba kutumika kwa shughuli za binadamu ambazo zinazuia wanyamapori kupita kutoka eneo moja kwenda jingine, na uchimbaji wa madini kwenye maeneo ya hifadhi.

64. Mheshimiwa Spika, Wizara imejipanga kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. Hatua hizo ni pamoja na kuhimiza matumizi ya teknolojia katika uvunaji na uchakataji wa mazao ya misitu na nyuki; na kuhamasisha na kutekeleza mikakati ya upandaji miti, kuhifadhi maeneo ya ardhioevu na misitu ya lindimaji. Aidha, Wizara itaendelea kuhimiza matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa misitu, kuongeza wigo wa mazao ya utalii na utangazaji wa vivutio vya utalii, kushirikisha wadau katika uhifadhi wa maliasili na malikale, na kuendeleza utalii. Vilevile, Wizara itatekeleza mikakati ya kujenga uwezo wa kusimamia maliasili, malikale na maendeleo ya utalii, kufanya mapitio ya sera, sheria na kanuni zinazosimamia maliasili, malikale na utalii, na kudumisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Ukusanyaji Maduhuli na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

65. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara inakadiria kukusanya **Shilingi 71,538,430,944** kutoka katika vyanzo vya idara, mifuko na taasisi zilizo chini yake. Kati ya fedha hizo, idara zitakusanya **Shilingi 22,671,945,992**, Taasisi zinazopata ruzuku zitakusanya **Shilingi 26,987,619,944.27**, na Mifuko ya uhifadhi ya TWPF na TaFF itakusanya **Shilingi 21,878,865,008**. Aidha, **Shilingi 701,805,841,651** zinakadirwa kukusanya na TANAPA (**Shilingi 314,098,689,717**), NCAA (**Shilingi 169,141,823,000**), TAWA (**Shilingi 65,081,946,946**) na TFS (**Shilingi 153,483,381,988**). Taasisi hizo hukusanya maduhuli kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali, mifuko ya uhifadhi na maendeleo ya utalii.

66. Mheshimiwa Spika, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 120,202,638,734**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 71,312,649,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 48,889,988,734** miradi ya maendeleo. Makadirio ya matumizi ya kawaida yanajumuisha makadirio ya mishahara - **Shilingi 52,589,344,000** na makadirio ya matumizi mengineyo - **Shilingi 18,723,305,000**. Aidha, **Shilingi 48,889,988,734** zitatumika kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 47,889,988,734** zitatoka kwa washirika wa maendeleo na **Shilingi 1,000,000,000** zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Sera, Sheria na Kanuni

67. Mheshimiwa Spika, Wizara itakamilisha nyaraka za Baraza la Mawaziri kuhusu Sera za Taifa za Misitu (2019) na Utalii (2019) na kukamilisha mapitio ya Sheria ya Mambo ya Kale. Aidha, Wizara itafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki na Sheria ya Misitu Sura 323. Villevile, Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapor Sura 283, Sheria za Shirika la Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro zitaunganishwa na kuwa sheria moja ambayo itajumuisha Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapor Tanzania. Pia, Sheria Namba 5 ya mwaka 1980

iliyoanzisha TAFORI na Mpango wa Taifa wa II wa Utafiti wa Misitu (NAFORM II (2011 – 2020) utaendelea kufanyiwa mapitio.

Masuala Mtambuka

Kuimarisha Ulinzi na Maliasili na Malikale

68. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ulinzi na kudhibiti ujangili, Wizara itaendelea kufanya doria za ndani na nje ya maeneo ya hifadhi. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama. Vilevile, Wizara itakamilisha taratibu za uanzishwaji wa Jeshi Usu ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi na kununua vifaa mbalimbali.

Kubadili Hadhi Maeneo ya Hifadhi

69. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea na taratibu za kubadilisha hadhi maeneo ya hifadhi na yasiyohifadhiwa ili kukabiliana na changamoto za uharibifu wa maliasili na mazingira. Katika kutekeleza azma hiyo, Jumuiya ya Hifadhi ya Wami – Mbiki na mapori ya Litumbandyosi na Gesimazowa yatabadilishwa kuwa mapori ya akiba. Aidha, eneo la ardhioevu la Ziwa Natron litabadilishwa kuwa hifadhi ya ardhioevu. Vilevile, Wizara itakamilisha taratibu za kubadili hadhi ya mapori ya akiba Kigosi, Moyowosi na Ugalla kuwa hifadhi za Taifa. Pia, Wizara itabadiishi hadhi misitu 12 kuwa misitu ya hifadhi ya mazingira asilia. Misitu hiyo ni Hassama Hills na Nou (Mbulu na Babati), Uzigua (Bagamoyo na Handeni), Pugu na Kazimzumbwi (Kisarawe); na misitu iliyopo katika vilima vya Mbarika ambako kuna misitu ya hifadhi ya Lugamba, Sali, Mahenge Scarp, Mselezi, Myowe, Nawenge (Mahenge) na Kimboza (Morogoro).

Kutatua Migogoro

70. Mheshimiwa Spika, Wizara itashirikiana na wadau kuendelea kutatua migogoro katika maeneo ya hifadhi. Kazi zitakazotekelawa na TANAPA ni kutoa elimu kwa jamii na kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji 95 vinavyopakana na hifadhi za Taifa za Kilimanjaro,

Arusha, Mkomazi na Saadani. Kazi nyingine ni kusajili Matangazo ya Serikali yaliyoanzisha hifadhi za Taifa (Serengeti, Tarangire, Katavi, Mikumi, Udzungwa na Mahale) na kupata namba “*Plan Number*”; kusafisha mipaka yenye urefu wa kilomita 896; na kuweka alama 25 za kudumu za mipaka kwenye hifadhi za Taifa za Saadani, Burigi, Biharamulo, Kimisi na Ziwa Manyara. Aidha, mgogoro wa mipaka na vijiji saba vya wilaya ya Serengeti (Hifadhi ya Serengeti) utashughulikiwa; na kutoa fidia kwa wananchi wa vijiji 33 vya Usangu (Hifadhi ya Ruaha), Kalilani (Hifadhi ya Mahale), na Kimotorok (Hifadhi ya Tarangire).

71. Mheshimiwa Spika, TFS itaendelea kushirikiana na Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardh (NLUPC) kutayarisha mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 100 vinavyozunguka misitu ya hifadhi. Aidha, ulinzi wa misitu 106 ya hifadhi utaimarishwa kwa kupima upya na kuhakiki mipaka yenye urefu wa kilometra 759.4, kusafisha kilomita 408.2, kuweka vizingi 3,825, na mabango 1,016.

Kuendeleza na Kutangaza Vivutio vya Utalii

72. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kupitia maonesho ya Sabasaba, Nanenane, Karibu Kusini, *East Africa Trade Fair*, Karibu Kili *Fair*, SITE; na matamasha ya Urithi (*Urithi Festival*) na Utamaduni wa Mtanzania. Aidha, Wizara itashiriki katika maonesho ya uwindaji wa kitalii yanayofanyika nchini Marekani kila mwaka (*Safari Club International/na Dallas Club International*). Vilevile, Wizara itatangaza vivutio vya utalii katika nchi za Ulaya, Amerika, Australia na Asia kwa kushirikiana na ofisi za balozi, mawakala wa utalii, mabalozi wa hiari wa utalii, vyombo vya habari ikiwemo *Tanzania Safari Channel*, watu mashuhuri na mitandao ya kijamii. Pia, Wizara itashirikiana na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kutangaza utalii katika nchi ambazo ndege za Shirika zinafanya safari. Hii itatoa fursa kwa watalii kuweza kutumia ndege zetu na itasaidia katika kupunguza ghamama za safari za watalii.

73. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendeleza mikakati ya kukuza utalii kanda ya kusini na maeneo ya hifadhi mpya za Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika. Aidha, Wizara itaibua shughuli mpya za utalii ndani ya eneo la hifadhi ya NCAA ikiwemo ujenzi wa *walking trails* katika kreta za Empakai na Olmoti, kutengeneza mtandao wa barabara katika eneo la Ndutu na barabara za kushuka Kreta kuu. Vilevile, ukarabati wa miundombinu ya vivutio sita vya malikale ambayo ni Michoro ya Kolo (Kondoa), Magofu ya Kaole na Mji wa Zamani wa Bagamoyo, Tembe la Livingstone (Tabora), Jengo la Zamani la Afya (Tabora) na Magofu ya Tongoni (Tanga) utafanyika. Aidha, vituo vya malikale vya Caravan-Serai Bagamoyo, Kaburi (Mausoleum) la Mkwawa Kalenga, Eneo la zana za kale za mawe Isimila, Tembe la Dr. Livingstone Ujiji na nyumba ya Mwl. Nyerere Magomeni vitatangazwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

74. Mheshimiwa Spika, TAWA itaendelea kuboresha huduma za utalii katika mapori ya akiba ili kuongeza ushindani na kuvutia watalii zaidi. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kujenga hosteli za kisasa sita katika mapori ya akiba ya Swagaswaga (1) na Selous (5); na kambi 12 za kulala wageni katika mapori ya akiba Mpanga - Kipengere (1), Swagaswaga (4), eneo la Matambwe, Selous (4), na Kijereshi (3). Aidha, Mamlaka itajenga *picnic sites* sita katika mapori ya akiba ya Mpanga - Kipengere (1), Kijereshi (1), na eneo la Matambwe, Selous (4). Vilevile, Mamlaka itandaa mipango ya usimamizi wa mapori ya akiba ya Lukwati - Piti, Ikorongo - Grumeti na Pande. Pia, Mamlaka itafungua mtandao wa barabara za utalii zenye urefu wa Kilometra 300 katika mapori ya Mpanga - Kipengere, Swagaswaga, Selous, Maswa, Moyowosi - Kigosi na Rukwa - Lwafi na kukarabati viwanja viwili vya ndege vya Maswa na Mtemere, Selous.

75. Mheshimiwa Spika, TFS itaboresha miundombinu ya maeneo ya utalii ikolojia katika misitu ya hifadhi ya mazingira asilia kwa kujenga kilomita 41 za barabara mpya za misituni, kilomita 41 za njia za kutembea watalii, kambi 12 za kupumzikia wageni na minara mitatu ya kuona mandhari. Aidha, TFS itakarabati kilomita 214 za njia za kutembea watalii,

kilomita 95 za barabara za msituni, kambi 19 za kupumzikia wageni na minara minne ya kuona mandhari.

Kuboresha Mifumo ya Ukusanyaji Maduhuli

76. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji maduhuli kwa kutumia mfumo wa GePG na MNRT Portal. NCAA itaimarisha na kuboresha mifumo ya kieletroniki katika mageti yote ya kuingia na kutoka kwenye hifadhi. Aidha, TANAPA itaimarisha mifumo ya malipo kwa kutumia simu za mkononi; kuendelea kuboresha mifumo ya *online booking*; kuboresha mifumo ya teknolojia katika malango ya hifadhi za Kilimanjaro (5), Tarangire (4), Mikumi (2), Udzungwa, Rubondo, Gombe, Arusha (3), Ziwa Manyara (3), Kitulo (3), Ruaha (4), Serengeti (14), Mkomazi (2), Katavi na Mahale (3). Vilevile, TFS itanunua mashine 100 za kielektroniki za ukusanyaji maduhuli zitakazotumika kwenye maeneo yaliyo mbali na miji na yenye changamoto za mawasiliano ya intaneti.

Ushirikishaji wa Wadau, Elimu na Uhamasishaji

77. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi na washirika wa maendeleo, sekta binafsi na asasi zisizokuwa za kiserikali katika kutekeleza majukumu yake. TANAPA itatoa elimu ya uhifadhi kwa vikundi vya ulinzi shirikishi kwa viongozi 340 wa wilaya, kata, vijiji na Kamati za Maliasili za Vijiji vinavyozunguka hifadhi.

78. Mheshimiwa Spika, TFS itatoa mafunzo ya usimamizi wa misitu kwa Kamati za Maliasili za Vijiji 79; kuchangia shughuli za maendeleo kwa jamii zinazozunguka misitu kupitia miradi ya ufugaji wa nyuki, samaki na mbuzi wa maziwa; upandaji miti; na ujenzi wa madarasa katika shule 17. Aidha, wananchi na wadau wengine wa mazingira watashirikishwa kupanda miti milioni sita katika vyanzo vya maji na maeneo yaliyoharibika. Vilevile, miche milioni 1.5 itapandwa katika viunga vya Jiji la Dodoma katika kuendeleza programu ya kulifanya Jiji hilo kuwa kijani.

79. Elimu kwa umma juu ya uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki, itaendelea kutolewa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushiriki kwenye maonesho ya Saba Saba, Nane Nane, Siku ya Kupanda Miti Kitaifa, Siku ya Kutundika Mizinga Kitaifa, Siku ya Mazingira Duniani na Siku ya Utumishi wa Umma. Aidha, nakala 26,200 za machapisho mbalimbali zitasambazwa na kurusha vipindi 53 vya televisheni na 188 vya redio. Pia, NCAA itakamilisha uandaaji wa mpango mkakati wa elimu ya uhifadhi, itatoa elimu ya upandaji miti kwa kata 16 ndani na nje ya hifadhi na itapanda miti 400,000 ya asili.

Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

80. Mheshimiwa Spika Wizara itaendelea kutekeleza mikataba mbalimbali ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika nyanja za maliasili, malikale na utalii ambayo nchi imeridhia.

Miradi ya Maendeleo

81. Mheshimiwa Spika, Wizara itatekeleza miradi ya maendeleo ifuatayo:-

- (i) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi ya Ujangili;
- (ii) Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili;
- (iii) Mradi wa Kuzuia na Kupambana na Ujangili;
- (iv) Mradi wa Misitu ya Hifadhi ya Mazingira Asilia;
- (v) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki;
- (vi) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii katika Kusimamia Raslimali za Misitu kwa Tija na Misingi Endelevu;
- (vii) Mradi wa Kuongeza thamani kwa Mazao ya Misitu; na

(viii) Mradi wa Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (REGROW).

Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 umefafanuliwa kuanzia ukurasa 73 mpaka 83.

SHUKRANI

82. Mheshimiwa Spika, ninazishukuru nchi, mashirika, taasisi mbalimbali na marafiki wa uhifadhi kwa ushirikiano walioutoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Ninachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Kanada, China, Ufini, Korea Kusini, Marekani, Norway, Ubelgiji, Ujeruman, Uswisi na Jumuiya ya nchi za Ulaya. Mashirika na taasisi ni pamoja na AWF, AWHF, ENABEL, FAO, FZS, GEF, GIZ, ILO, ICCROM, ICOM, ICOMOS, IUCN, KFW, NORAD, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF.

MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

83. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, ninaomba Bunge lako tukufu liidhinishe **Shilingi 120,202,638,734** kwa matumizi ya Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 71,312,649,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 48,889,988,734** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

84. Mheshimiwa Spika, fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 52,589,344,000** za Mishahara na **Shilingi 18,723,305,000** za Matumizi Mengineyo. Aidha, Fedha za Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 1,000,000,000** fedha za ndani na **Shilingi 47,889,988,734** fedha za nje.

HITIMISHO

85. Mheshimiwa Spika, ninaomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii itapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: www.mnrt.go.tz

86. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Hoja hiyo imeungwa mkono, ahsante kwa kusoma vizuri. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Aridhi, Maliasili na Utalii. (*Makof*)

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha kwako, mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Aridhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yote iingie kwenye hansard. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ilitarajiwa kukusanya maduhuli ya kiasi cha Shillingi bilioni 63.1 kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato yatokanayo na sekta ya maliasili na utalii. Hadi kufikia Februari 2019 Wizara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 32.9 sawa na asilimia 52 ya kiwango kilichokadiriwa kukusanya kwa mwaka huu, hii ni pungufu kwa asilimia 17.4 ya makusanyo ikilinganishwa na kipindi kama hiki kwa Mwaka wa Fedha uliopita. Mwenendo wa makusanyo kwa ujumla hauridhishi, na kwa hali hiyo Wizara haitaweza kufikia malengo yake kikamilifu. Kamati inaona kuwa endapo sekta ya utalii itapewa kipaumbele na kuboreshwa hususan uwindaji wa kitalii, utalii wa picha, utalii wa fukwe, utalii wa malikale na utalii wa kitamaduni, Wizara itaweza kukusanya zaidi na kuchangia vizuri kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa utolewaji wa fedha kutoka Hazina umeonyeshwa katika jedwali namba moja la taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kwa ujumla mwenendo wa utolewaji wa

fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hauridhishi kwa kuwa kumekuwa na changamoto ya ucheleweshaji wa utolewaji wa fedha kwa wakati hususan fedha za ndani. Ukiangalia jedwali namba moja, hadi kufikia februari, 2019 hakuna fedha zozote za ndani zilizotolewa ikilinganishwa na asilimia 39.1 ya fedha za wafadhili zilizotolewa. Hali hii hairidhishi utekelezaji wa miradi na hivyo kuchangia malengo kutofikiwa ipasavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikagua mradi bamba 4631 ambao ni mradi wa Misitu Asilia (*Enhancing the Forest Nature Reserves Network for biodiversity Conservation in Tanzania*) uliotekelawa katika Misitu ya Hifadhi asilia ya Chome, Magamba, Mkingu, Minziro, Udzungwa na Rungwe. Kamati ilipata fursa ya kukagua utekelezaji wa mradi huu katika Misitu ya Hifadhi Asilia ya Chome na Magamba. Aidha Kamati ilitembelea Hifadhi ya Misitu Asilia wa Amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa mradi una lengo la kuziwesha Wizara, Idara, Halmashauri za Wilaya na Asasi za kiraia kuboresha usimamizi wa sheria za mazingira na kulinda mifumo ya ikolojia na baioanuai kwa ajili ya ustawi na usimamizi wa raslimali za misitu. Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2018/2019 shilingi bilioni 1.3 ziliidhinishwa kwa ajili ya kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi ili kunufaika na raslimali za misitu. Hadi kufikia Februari, 2019 shilingi milioni 100.1, zimetumika kutekeleza kazi mbali mbali ikiwemo kupandisha hadhi misitu mitano kuwa misitu ya hifadhi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa miradi ni wa kusuasua kwa kuwa hakuna fedha zozote za ndani zilizotengwa na badala yake unategemea zaidi fedha za wafadhili kutoka nje, hali itakayopelekea mradi kutokuwa endelevu. Aidha kamati iliarifiwa kuwepo kwa changamoto ya uharibifu mkubwa wa mazingira uliosababishwa na uvamizi na wachimbaji haramu wa madini

ya Dhahabu, hali inayotishia kuharibiwa kwa vyanzo nya maji. Aidha, shughuli za uchimbaji madini ndani ya misitu ya hifadhi asilia siyo tu inatishia kuharibu vyanzo nya maji bali pia uchafuzi wa maji kutokana na shughuli za uchenjuaji wa madini, hali inayotishia afya za wananchi wanaotumia maji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeelezwa kuwepo kwa fursa za kuzitumia hifadhi za misitu asilia kuwa vivutio nya utalii, na endapo Serikali itawekeza katika hifadhi hizi kwa kuweka miundombinu kama barabara, njia za miguu, sehemu za malazi na kadhalika, zinaweza kuwa chanzo kizuri cha mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwepo kwa miundombinu mibovu ya barabara, uchache na uchakavu wa magari ya kufanya doria pamoja na uhaba wa watumishi, hali inayofanya kazi ya kudhibiti uvamizi wa misitu kuwa ngumu. Aidha Kamati imebaini kuwa katika muundo wa utumishi katika hifadhi za misitu asilia hakuna kada ya maafisa utalii hivyo itakuwa vigumu kwa hifadhi hizi kutangaza vivutio hivi ipasavyo. Kamati inashauri Serikali iongeze kada ya maafisa utalii katika hifadhi za misitu asilia ili wasimamie shughuli za utalii katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo hauridhishi kutokana na kasi ndogo ya upatikanaji wa fedha. Hadi kufikia Februari, 2019 ni miradi miwili tu kati ya miradi 11 iliyopangwa kutekelezwa ndio iliopatiwa fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji. Hali hii imekuwa kama ndio utaratibu wa Serikali kwani tunapanga bajeti lakini fedha hazipelekwi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutopeleka fedha katika miradi hii kwa wakati kunaathiri mwenendo mzima wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Uchambuzi wa taarifa za miradi unaonyesha kuwa, hadi Februari 2019 Wizara

ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 10.5 fedha za nje sawa na asilimia 35 ya fedha zilizoidhinishwa, hali hii hairidhishi kabisa! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa yapo maoni yaliyofanyiwa kazi kikamilifu, yapo maoni yanayoendelea kufanyiwa kazi, lakini yapo maoni ambayo hayakufanyiwa kazi kabisa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dokta John Pombe Joseph Magufuli kwa kuyapandisha hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika kuwa hifadhi za taifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini ya Kamati kwamba Serikali itawekeza vya kutosha katika kuviendeleza vivutio vya utalii vya ukanda huu kwa kujenga na kuimarissha miundombinu ya barabara, maji, umeme pamoja na kuvutia wawekezaji kujenga mahoteli ili kuvutia watalii wengi zaidi kutembelea vivutio vyetu katika Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaridhishwa na hatua ya Serikali kutangaza vivutio vya utalii kwa kuanzisha televisheni ya kutangaza utalii wa Tanzania ijulikanayo kama *Tanzania Safari Channel*. Hii ni hatua muhimu sana katika kuvutia watalii wengi zaidi kuja nchini. Aidha, Televisheni hii pia inachangia kuwavutia watalii wa ndani kuvielewa vivutio tulivyonyavyo na hivyo kuamsha hamasa ya kutaka kwenda kuviona.

Aidha Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Tamasha la mwezi wa urithi wa utamaduni ambalo litaadhimishwa nchini kote. Tamasha hili si tu litapanua wigo wa vivutio vya utalii bali pia litachangia sana katika kutangaza na kuvutia watalii wengi zaidi wa ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hairidhishwi na namna Serikali inavyoshughulikia suala la kumaliza migogoro ya mipaka baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa maagizo aliyoyatoa hivi karibuni kwa baadhi ya Mawaziri wake kuhakikisha wanashughuilkia migogoro kati ya wananchi na hifadhi na kuimaliza katika muda aliowapangia. Ni matarajio ya kamati kwamba maagizo ya Rais yakitekelezwa kikamilifu, suala la migogoro katika hifadhi zetu litakuwa historia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hairidhishwi na namna Serikali inavyoshindwa kutumia fursa ya vivutio vya utalii kuongeza mapato yatokanayo na utalii. Tunaelezwa kwamba Tanzania ni nchi ya pili duniani kuwa na vivutio vingi vya asili vya utalii baada ya Brazil lakini inashikilia nafasi ya 140 kwa mapato yatokanayo na utalii ikilinganishwa na vivutio ilivyo navyo. Mathalani takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya watalii imeongezeka kutoka milioni 1.2 mwaka 2016 hadi kufikia milioni 1.3 mwaka 2017. Hii ni idadi ndogo sana, kuweza kujivunia ikilinganishwa na fursa zillizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hairidhishwi na kasi ya Serikali kushughulikia malalamiko ya wafanyabiashara wa wanyamaporai hai ambapo Serikali ilisitisha biashara hiyo mwezi Machi, 2016 na kusababisha hali ya taharuki kwa wafanyabiashara hao. Huu ni mwaka wa nne sasa tangu kusitishwa kwa biashara hiyo na kumekuwa na matamko mbalimbali ya Wizara lakini hakuna utekelezaji wowote. Kibaya zaidi tamko la kusitisha biashara ya viumbepori hai limeathiri hata vikundi vya akina mama katika hifadhi ya Msitu asilia wa Amani ambapo wao walikuwa wanazalisha vipepeo na kuwauza nje ya nchi. Jambo hili si tu limewaathiri wafanyabiashara na familia zao bali pia limeikosesha Serikali mapato. Takwimu zinaonesha kuwa Serikali ilikuwa inapata takriban shilingi billioni nne kutokana na tozo mbali mbali katika biashara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hajatekeleza ushauri wa Kamati wa kuipandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kuwa Mamlaka ya Misitu Tanzania, hali inayozidi kuchangia uharibifu wa misitu na vyanzo vya maji kwa kukosa udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii inahitaji uwekezaji mkubwa ili taifa liweze kunufaika. Inashangaza katika nchi yetu licha ya kuwa na fursa nyingi katika sekta hii, bado Serikali hajawekeza vya kutosha ili tupate matunda yanayotarajiwa. Taarifa mbalimbali zinaonesha ubovu wa miundombinu ya bara bara, uhaba wa sehemu za malazi, kutoendelezwa kwa vivutio vingine kama vile malikale, utamaduni, fukwe, hifadhi za misitu asilia na vingine vingi. Tumeelezwa pia kwamba watalii wengi wanaokuja nchini hutembelea vivutio vilivyoko katika ukanda wa kaskazini huku kanda zingine zikipata idadi ndogo ya watalii. Kamati inashauri Serikali kuharakisha utekelezaji wa mradi wa kuendeleza utalii kusini mwa Tanzania (*REGROW*) ili kuvutia watalii wengi kutembelea vivutio vilivyoko katika ukanda huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na vipaumbele na malengo ya kazi za Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Hata hivyo, vipaumbele, malengo na mipango hiyo itakamilika na kuinua Pato la Taifa kama makusanyo yatakusanya kama ilivyokusudiwa na mgao wa fedha za matumizi utakua ni wa kuridhisha kwa lengo la kuiwezesha wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 75 kutokana na vyanzo mbalimbali. Kiasi hiki ni nyongeza ya shilingi bilioni 11.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 63.2 zilizokadiriwa kukusanya katika mwaka wa fedha 2018/2019, sawa na ongezeko la asilimia 18.5. Ni mapendekezo ya Kamati kwamba Serikali ihakikishe inatafuta vyanzo vipyaa na mbinu bora zaidi za ukusanyaji wa mapato ili kuongeza mapato ya sekta ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Maliasili na Utalii inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi billioni 120.2. Kati ya fedha hizo shilingi billioni 71.3 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi billioni 48.8 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Bajeti ya maendeleo imeongezeka kutoka shilingi billioni 29.9 mwaka 2018/2019 hadi shilingi billioni 48.8 mwaka 2019/2020, sawa na ongezeko la asilimia 66. Pamoja na ongezeko hili changamoto itabakia kuwa ile ile ya kutenga fedha bila kuzipeleka jambo ambalo linadhoofisha miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na masuala mbalimbali yalijitokeza wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii. Masuala hayo ni pamoja na uchimbaji wa madini ndani ya hifadhi uliopelekea uharibifu wa vyanzo vya maji pamoja na kuongezeka kwa migogoro ya ardhi kati ya mamlaka za kutunza hifadhi na wananchi wanaozunguka hifadhi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya kamati kwamba, Kamati ya Mawaziri iliyoteuliwa na Mheshimiwa Rais itakuja na mapendekezo ya kumaliza migogoro ya ardhi katika maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto ya uhaba wa watumishi katika hifadhi zetu hususan askari wa kulinda hifadhi hizo. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaaajiri askari wa kutosha kwa ajili ya kulinda hifadhi zetu. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa vyuo vinavyotoa mafunzo ya misitu na wanyamapori viingize mafunzo ya jeshi usu ili vijana wetu wanaohitimu katika vyuo hivyo wawe wakakamavu na wazalendo wenye moyo wa kuzilinda raslimali za nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na m dororo katika sekta ya uwindaji wa kitalii kutokana na mabadiliko ambayo Serikali inakusudia kuyafanya ikiwemo utaratibu wa kugawa vitalu kwa njia ya Mnada. Jambo hili limechukua muda mrefu na utekelezaji wake umechelewa na hivyo kusababisha kuzorota kwa shughuli za uhifadhi na uwekezaji

katika vitalu hivyo kutokana na kukosa uhakika wa kuendelea kuvimiliki na hivyo kulikosesa taifa mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalli. Kamati inaishauri Serikali kurejesha utulivu katika tasnia hii kwa kuharakisha utekelezaji wa mabadiliko yanayokusudia kufanya vinginevyo taifa litaendelea kupoteza mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na uharibifu wa vyanzo vyta maji na uchafuzi wa maji katika hifadhi zetu hasa hifadhi za misitu asilia unaosababishwa na wachimbaji haramu wa madini ya dhahabu. Kamati inaishauri Serikali kuwaelimisha wananchi kuhusu athari zinazoweza kutokea kutokana na uchimbaji huo wa madini. Aidha Serikali iweke adhabu kali kwa wataokamatwa wanaharibu vyanzo vyta maji ili iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa misitu hasa misitu inayomilikiwa na vijiji na Serikali za mitaa ambayo inakadiriwa kuchukua zaidi ya asilimia 52 ya eneo lote la misitu hapa nchini. Uharibifu mkubwa wa misitu umeonekana sana katika misitu ya hifadhi ambayo imevamiwa na wananchi wanaoishi ndani ya hifadhi za misitu. Mfano mzuri ni Wilaya ya Kaliua ambako vijiji vingi vimo ndani ya hifadhi na vimesajiliwa kisheria. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka za kudhibiti ujangili wa misitu ili kuinusuru na kuiepusha nchi yetu na madhara yatokanayo na uharibifu wa misitu. Aidha Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania kuwa Mamlaka ili kuipa nguvu ya kisheria ya kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu yote hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeyapandisha hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika kuwa hifadhi za taifa hivyo kuliongezea Shirika la Hifadhi za Taifa mzigo wa kuzilea Hifadhi hizi mpaka hapo zitakapoweza kujitegemea. Hata kabla ya kupandishwa hadhi kwa Mapori haya kuwa hifadhi za taifa, ni hifadhi Tano tu kati ya 16 zilizokuwepo zilizokuwa na uwezo wa kuzalisha ziada iliyosaida kuendesha hifadhi nyingine 11. Sasa hifadhi

zimeongezeka na kufikia kumi na tisa, ni dhahiri kutakuwa na ongezeko la kibajeti kwa ajili ya kuhudumia hifadhi mpya zilizoanzishwa. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kulipunguzia Shirika la Hifadhi za Taifa kiwango cha gawio linachopeleka Serikalini ili kulipa nguvu ya kuhudumia hifadhi mpya.

Aidha, Serikali ifanye utaratibu wa kurekebisha mfumo wa utozaji Kodi ya Makampuni inavyotozwa kwa Shirika la Hifadhi za Taifa. Shirika linatoa asilimia 15 ya mapato ghafi ya Shirika kama gawio kwa Serikali, linatoa tatu ya mapato ghafi kwa Kodi ya kuendeleza utalii, linatoa michango kwa Taaiissi za uhifadhi, linatoa fedha kwa ajili ya miradi ya ujirani mwema lakini wanapotozwa kodi ya makampuni yaani (*Corporate Tax*) bado inatozwa katika mapato ghafi. Hali hii inadhoofisha uwezo wa Shirika kuhudumia hifadhi ambazo hazijaweza kuzalisha mapato ya kutosha kujlendesha zikiwemo hifadhi mpya tatu zilizoanzishwa hivi karibuni. Kamati inaishauri serikali kurejea upya sheria ya ukokotoaji wa kodi kwa shirika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na changamoto ya kuwepo kwa idadi ndogo ya watalii wanaofika kutembelea vivutio vyetu vya utalii inayochangiwa pamoja na sababu nyingine uhaba wa sehemu za malazi nje na ndani ya hifadhi. Moja ya sababu zinazosababisha uhaba wa malazi ni kutoendelezwa kwa *lodges* na *hotels* za Serikali zilizobinafsishwa na hivyo kuchangia uhaba wa malazi kwa watalii wetu. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya utendaji wa *lodges* na *hotels* za Serikali zilizobinafsishwa kuona kama zimezingatia mikataba ya mauziano na kuchukua hatua kwa zile zitakazobainika hazifanyi kazi kwa mujibu wa makubaliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mgongano wa kisheria unaosababisha utekelezaji wa Sheria ya Wanyamapor Na. 5 ya Mwaka 2009 kuwa mgumu. Mfano wa sheria zinazokinanza na sheria hii ni Sheria ya Ardhi ya Vijiiji Na. 4 ya Mwaka 1999, pamoja na Sheria ya Madini. Kamati inaishauri serikali kuunda timu ya wataalam ili kuzipitia

sheria hizi kwa lengo la kubaini vifungu vyenye mgongano na kuleta mapendekezo Bungeni kwa ajili ya kuzifanya marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu iliwahi kushauri Serikali ifanye Tathmini ya mfumo wa uhifadhi mseto (*Multiple Land Use*) katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuona kama umekuwa na tija au la. Huu ni mwaka wa nne sasa Serikali bado hajatekeleza. Idadi ya watu inaongezeka, mifugo inaongezeka na shughuli za binadamu ndani ya hifadhi zimeongezeka. Kamati kwa mara nyingine inaishauri serikali kufanya tathmini hiyo ili kuweza kujua kama iendelee na mfumo huo au ibadilishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maoni na ushauri wa Kamati kwa sekta mbalimbali zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya Utalii inazo fursa nyingi ambazo zikitumiwa kikamilifu zitaongeza mchango wake katika pato la Taifa. Kwa sasa sekta hii inachangia asilimia 17 tu ya Patola Taifa na asilimia 25 ya fedha za kigeni. Ili kuongeza Pato la Taifa kupitia sekta ya utalii, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

Kuvibaini vivutio vyote vyaa utalii vilivyoko nchini, kuiyendeleza na kuvitangaza ili vifahamike na hivyo kuvutia watalii wengi zaidi kuja nchini mwetu.

(a) Kuvibaini vivutio vyote vyaa utalii vilivyoko nchini;

(b) Kuiyendeleza na kuvitangaza ili vifahamike na hivyo kuvutia watalii wengi zaidi kuja nchini mwetu;

(c) Kuwekeza miundombinu kwenye vivutio vyaa utalii kwa kuimarisha au kujenga barabara, viwanja vyaa ndege, mahoteli, maji, vyoo na kadhalika ili kuvutia watalii kufika kwenye vivutio hivyo kwa kiurahisi;

(d) Kuhamasisha Halmashauri zetu kubaini vivutio vya utalii katika maeneo yao na kuvunganisha na utalii wa kitamaduni katika maeneo husika ili kukuza utalii na kuwaingizia wananchi kipato;

(e) Kutenga fedha za kutosha pamoja na kuhamasisha Bodi ya Utalii kupitia wizara hii kuongeza ubunifu katika kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi ili kuendana na ushindani uliopo katika sekta ya utalii;

(f) Kuutangaza mti unaosadikiwa kuwa mrefu kuliko yote Afrika ulioko katika hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ili utumike kama kivutio cha utalii. Mti huu unakadiriwa kuwa na urefu wa mita 84.7 na umepewa jina la Kamasuku na uligunduliwa na Mjerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ianze kuonyesha *Tanzania Safari Channel* katika ving'amuzi vya kimataifa ili kutangaza utalii wetu kuvutia watalii wengi kuja nchini.

Mheshimimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebarikiwa sana kuwa na hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Hifadhi za Jamii za Wanyamapori ambavyo ni vivutio vya utalii wa picha na pia uwindaji wa kitalii. Ili kuweza kuvitumia vivutio hivi kuongeza pato la Taifa, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha kwamba vyuo vyote vinavyotoa mafunzo ya usimamizi wa wanyamapori vinapatiwa mafunzo ya Jeshi Usu ili kupata Askari watakaoweza kukabiliana na changamoto za ujangili.

(b) Kuendeleza programu zinazolenga kuongeza idadi ya wanyama walio katika hatari ya kutoweka kama faru na Mbwa mwitu;

(c) Kushirikiana na Mamlaka husika kubaini mbinu za kupunguza vifo vya wanyamapori wanaokufa kwa kugongwa na magari katika barabara zinazokatiza katika

hifadhi zetu hasa katika hifadhi ya Taifa ya Mikumi ambako kwa wastani mnyama mmoja hugongwa kila siku; na

(d) Kusimamia mipaka ya maeneo ya mapori kwa lengo la kutatua migogoro iliyopo na inayoweza kujitokeza kwa lengo la kunusuru ikolojia, kulinda mazalia ya wanyama, mapitio ya wanyama pamoja na vyanzo vya maji kwa ajili ya kuendeleza hifadhi na utalii nchini.

(e) Serikali iangalie uwezekano wa kulipunguzia Kodi Shirika la Hifadhi za taifa ili kulipa nguvu ya kuhudumia hifadhi mpya na zile ambazo hazijaweza kujitegemea;

(f) Serikali iweke utaratibu wa kulinda shoroba za wanyamapori zisivamiwe. Aidha Serikali iendelee kuhamasisha kuanzishwa kwa Jumuiya za Hifadhi za wanyamapori (*WMA's*) hasa katika maeneo ya shoroba ili kuendeleza uhifadhi shirikishi;

(g) Serikali iangalie upya kanuni za kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori. Kanuni zilizopo sasa haziridhishi; malipo ni madogo na hayalipwi kwa wakati.

(h) Serikali iweke utaratibu wa kutumia njia za utambuzi za kielektroniki kwa watalii wanaoingia hifadhini badala ya kutumia mfumo wa *Single entry* ambao utawakosesha mapato wadau wengine wa utalii hususan WMA's na Utalii wa kitamaduni wanapotaka kutoka na kurudi ndani ya hifadhi ndani ya masaa 24;

(i) Serikali iwashirikishe wananchi katika zoezi la utambuzi wa mipaka kati ya hifadhi na vijiji kabla ya kuweka vivingi; na

(j) Serikali iharakishe mchakato wa kugawa vitalu kwa njia ya mnada kwani kuna vitalu vingi viko wazi na serikali inazidi kupoteza mapato.

Mheshimimiwa Mwenyekiti, Malikale ni rasilimali za urithi wa Taifa tangu enzi za wahenga wetu. Rasilimali hii ikiboresha ipasavyo itachochaea utalii na kuchangia ukuaji wa uchumi na kukuza Sekta ya Elimu hapa nchini. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuongeza mapato na kuinua Sekta ya Malikale:-

(a) Kuainisha vivutio vyatya malikale pamoja na kuiendezeza, sambamba na kuimarisha ulinzi, kukarabati na kutunza maeneo yenye majengo ya Malikale kwa lengo la kuuenzi utamaduni wetu na kuvutia watalii kutoka katika maeneo mbalimbali nchini; na

(b) Kuendelea kukuza utalii wa ndani kwa kuyatangaza maeneo ya Malikale ndani na nje ya nchi kama vivutio vyatya utalii na maeneo ya kujifunza historia ya nchi yetu.

Mheshimimiwa Mwenyekiti, Makumbusho ya Taifa ni moja ya Idara muhimu yenye kutunza kumbukumbu na historia ya Taifa kwa ujumla kabla na baada ya kupata uhuru. Ni kivutio cha utalii na ni kielelezo muhimu katika kuinua kiwango cha elimu nchini. Cha kusikitisha zaidi Serikali inaisahau idara hii muhimu hivyo Kamati inaikumbusha Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuinua Idara hii:-

(a) Kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya ukarabati wa maeneo ya makumbusho ya Taifa na kuanzisha mengine mapya;

(b) Kutangaza Makumbusho ya Taifa kama vivutio sambamba na vivutio vingine vyatya utalii;

(c) Kuhamasisha wananchi kuitambua, kuithamini na kuitembelea Makumbusho ya Taifa kama hatua ya kukuza utalii wa ndani pamoja na kuongeza uelewa wa historia ya nchi yetu;

(d) Kuendeleza Makumbusho ya Taifa kwa kujenga vivutio mbalimbali kama vile maduka, vyoo, migahawa kwa

lengo la kuinua utalii na kuwavutia watalii wengi kutembelea; na

(e) Kuitangaza Makumbusho ya Taifa hasa kituo cha Bonde la Olduvai ambacho ni chimbuko la historia ya binadamu wa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya misitu ni muhimu katika kuhifadhi mazingira, kurekebisha mfumo wa hali ya hewa, kupunguza mabadiliko ya tabia nchi, Kuhifadhi bioanuai, pamoja na kuhifadhi vyanzo vya maji. Pamoja na hayo, Idara hii ikitunzwa kikamilifu itachangia ongezeko la ajira na kupunguza umaskini. Kufuatia fursa hizi Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuinua Sekta ya Misitu na Nyuki:-

(a) Kuimarisha ulinzi katika misitu hapa nchini ili isivamiwe na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu kama uvunaji wa miti haramu, ufugaji, uchomaji mkaa usio endelevu na kilimo zinazopelekea hali ya rasilimali ya misitu kuwa duni;

(b) Kutangaza hifadhi za misitu asilia kama vivutio vya utalii ili kuongeza mapato yake;

(c) Kuharakisha mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania kuwa Mamlaka itakayokuwa na nguvu za kisheria ya kudhibiti matumizi ya rasilimali ya misitu nchini; na

(d) Kutoa mafunzo yanayohusu kuanzisha na kuendeleza misitu kwa wananchi wanaozunguka misitu ya hifadhi kwa lengo la kuimarisha ushiriki wa wananchi katika uhifadhi wa misitu na hifadhi za nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, nakupongeza wewe, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya

njema, hekima na busara katika kutekeleza majukumu na wajibu huu mkubwa mliokabidhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Waziri wa Maliasili na Utalii; Naibu waziri Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya maliasili na Utalii kwa ushirikiano waliotupa katika kutekeleza majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa usisome majina muda hautoshi.

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda upo.

MWENYEKITI: Hapana.

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII: Okay, nawashukuru sana Wajumbe wangu wa Kamati wote kutokana na muda sitaweza kusoma majina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu. Athuman Hussen, Makatibu wa Kamati Ndugu Gerald Magili na Elihaika Mtui, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao wa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii Fungu Namba 69 kama yalivyowasilishwa na mto hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kutoa kuwasilisha. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante kwa kusoma vizuri sana na leo umependa sana Mheshimiwa Kemilembe.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,
MALIASILI NA UTALII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA
2018/2019, PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO
KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Fasili ya 7 (1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 inataja majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na utalii kuwa ni :-

(a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii;

- (b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya wizara hii;
- (c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za wizara hii; na
- (d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu mengine yaliyoorodheshwa hapo juu, Kanuni ya 98(1), (2), ya kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo 2016 imeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa bajeti ya wizara inazozisimamia. Naomba kutoa taarifa kuwa tarehe 14 hadi 17 Machi, 2019 Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Aidha kati ya tarehe 26 hadi 28 Machi, 2019 Kamati ilichambua Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa- **fungu 69.**

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inatoa ufanuzi wa mambo manne yafuatayo:-

- (a) Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa maendeleo na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ikijumuisha;-
 - (i) Makusanyo ya Mapato 2018/19;
 - (ii) Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
 - (iii) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
 - (iv) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019
- (b) Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; ukijumuisha.

- (i) Makisio ya Makadirio ya Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;
 - (ii) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;
 - (iii) Mambo mengine muhimu yaliyokitokeza wakati wa kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020
- (c) Maoni na Ushauri wa Kamati;
- (d) Hitimisho

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MAJUKUMU YALIYOTEKELEZWA

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii ya Pili inajielekeza katika kutoa ufanuzi wa masuala mbalimbali kwa mtiririko ulioelezwa katika **kipengele 1.4** cha Sehemu ya Kwanza kama ifuatavyo;

2.1 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ulijikita zaidi katika makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo pamoja na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususan fedha za matumizi mengineyo (OC) na fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Njia zilizotumika ni pamoja na kuangalia hali halisi ya makusanyo ya maduhuli, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Februari na Machi 2019, na majadiliano yaliyofanyika yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

2.2 UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ilitarajiwa kukusanya maduhuli ya kiasi cha Shillingi **63,176,454,573.75** kutohana na vyanzo mbali mbali nya mapato yanayotokana na sekta ya Maliasili na Utalii. Hadi kufikia Februari 2019, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni **32,996,004,795** sawa na asilimia 52% ya kiwango kilichokadiriwa kukusanya kwa mwaka, hii ni pungufu ya asilimia 17.4% ya makusanyo ikilinganishwa na kipindi kama hiki kwa Mwaka wa Fedha uliopita. Mwenendo wa makusanyo kwa ujumla hauridhishi, na kwa hali hiyo Wizara haitaweza kufikia malengo yake kikamilifu. Kamati inaona kuwa endapo sekta ya utalii itapewa kipaumbele na kuboreshwa hususan uwindaji wa kitalii, utalii wa picha, utalii wa fukwe, utalii wa malikale na utalii wa kitamaduni, Wizara itaweza kukusanya zaidi na kuchangia vizuri kwenye pato la Taifa.

2.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii inabainisha utolewaji wa fedha kutoka hazina kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Uwiano na upatikanaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara, miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo hadi kufikia februari 2019 unaonyeshwa kwenye **jedwali Na.1**

Jedwali Na.1 Upatikanaji Fedha za Matumizi ya Kawaida, Miradi ya Maendeleo na Mishahara

NA	MAELEZO	FED HA ZILIZO IDHINISHWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019	FED HA ZILIZO TO LEWA HAD I FEBRUARI, 2019	A SILIM IA Y A FED HA ZILIZOTOLEWA
1	Mishahara & Matumizi Mengineyo	86,231,466,543.00	31,139,567,850.79	36%
2	Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo	3,000,000,000.00	0	0
3	Fedha za Nje za Miradi Maendeleo	26,978,082,000.00	10,551,289,825.00	39.1%

*Chanzo:Taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Maliasili na Utalii
2018/2019*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa kwa ujumla mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hauridhishi kwa kuwa kumekuwa na changamoto ya ucheleweshaji wa utolewaji wa fedha kwa wakati hususani fedha za ndani. Ukiangalia jedwali hapo juu hadi kufikia februari, 2019 hakuna fedha zozote za ndani zilizotolewa ikilinganishwa na asilimia 39.1% ya fedha za wafadhili zilizotolewa. Hali hii inaathiri utekelezaji wa miradi na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo ipasavyo. Jambo hili limekuwa kama utamaduni wa Serikali kutegemea zaidi Fedha za wafadhili kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Tusipochukua hatua za kutenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo tusitarajie muujiza wa kupata maendeleo hasa baada ya wafadhili kuondoka.

2.4 MATOKEO YA UKAGUZI WA BAADHI YA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Maliasili na utalii. Mradi uliokaguliwa ni mradi namba **4631 ambao ni** mradi wa Misitu Asilia (*Enhancing the Forest Nature Reserves Network for biodiversity Conservation in Tanzania*) uliotekelizwa katika Misitu ya Hifadhi asilia ya Chome, Magamba, Mkingu, Minziro, Udzungwa na Rungwe. Kamati ilipata fursa ya kukagua utekelezaji wa mradi huu katika Misitu ya Hifadhi asilia ya Chome na Magamba. Aidha Kamati ilitembelea Hifadhi ya Misitu Asilia wa Amani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa mradi una lengo la kuziwezesha Wizara, Idara, Halmashauri za Wilaya na Asasi za kiraia kuboresha usimamizi wa sheria za mazingira ili kulinda mifumo ya ikolojia na bioanuwai kwa ajili ya ustawi na usimamizi wa raslimali za misitu.

Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa. Katika mwaka wa Fedha 2018/19 shilingi **1,364,097,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya kuweka mazingira wezeshi kwa

wananchi ili kunufaika na raslimali za misitu. Hadi kufikia Februari, 2019 shilingi **100,100,000** zimetumika kutekeleza kazi mbali mbali ikiwemo kupandisha hadhi misitu mitano kuwa misitu ya hifadhi asilia. Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa mradi ni wa kusuasua kwa kuwa hakuna fedha zozote za ndani zilizotengwa na badala yake unategemea zaidi fedha za wafadhili kutoka nje hali itakayopelekea mradi kutokuwa endelevu. Aidha kamati iliarifiwa kuwepo kwa changamoto ya uharibifu mkubwa wa mazingira uliosababishwa na uvamizi wa wachimbaji haramu wa madini ya Dhahabu hali inayotishia kuharibiwa kwa vyanzo vya maji. Aidha shughuli za uchimbaji madini ndani ya misitu ya hifadhi asilia siyo tu inatishia kuharibu vyanzo vya maji bali pia uchafuzi wa maji kutokana na shughuli za uchenjuaji wa madini hali inayotishia afya za wananchi wanaotumia maji hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeelezwa kuwepo kwa fursa za kuzitumia hifadhi za misitu asilia kuwa vivutio vya utalii na endapo Serikali itawekeza katika hifadhi hizi kwa kuweka miundombinu kama barabara, njia za miguu (*Nature trails*) Sehemu za malazi n.k zinaweza kuwa chanzo kizuri cha mapato.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa miundombinu mibovu ya barabara, uchache na uchakavu wa magari ya kufanya doria pamoja na uhaba wa watumishi hali inayofanya kazi ya kudhibiti uvamizi wa misitu kuwa ngumu. Aidha Kamati imebaini kuwa katika muundo wa utumishi katika hifadhi za misitu asilia hakuna kada ya maafisa utalii hivyo itakuwa vigumu kwa hifadhi hizi kutangaza vivutio hivi ipasavyo. Kamati inashauri Serikali iongeze kada ya maafisa utalii katika hifadhi za misitu asilia ili wasimamie shughuli za utalii katika maeneo haya.

2.5 MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, lengo la kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ni kujiridhisha na uwepo wa miradi na matumizi ya fedha zilizoidhinishwa sawia na miradi husika ili

kuwa katika nafasi nzuri ya kuishauri Serikali ipasavyo. Kutokana na hali ilioonekana katika ukaguzi wa miradi na kutokana na taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilizowasilishwa, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(a) Utekelezaji wa miradi ya maendeleo hauridhishi kutokana na kasi ndogo ya upatikanaji wa fedha. Hadi kufikia Februari, 2019 ni miradi miwili tu kati ya miradi kumi na moja iliyopangwa kutekelezwa ndiyo iliyopatiwa fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji. Hali hii imekuwa kama ndiyo utaratibu wa Serikali kwani tunapanga bajeti lakini fedha hazipelekwi.

(b) Serikali kutopeleka fedha katika miradi kwa wakati kunaathiri mwenendo mzima wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, uchambuzi wa taarifa za miradi unaonyesha kuwa hata kwa miradi iliyotengewa fedha za ndani haikupelekewa fedha hizo kabisa. Aidha kwa ile iliopelekewa fedha hizo kiwango kilichotolewa ni kidogo sana, hadi februari 2019, Wizara ilipokea kiasi cha shilingi **10,551,289,825** fedha za nje sawa na asilimia 35% ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha hakuna fedha za ndani zilizotolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi. Hali hii hairidhishi kabisa.

Mheshimiwa Spika, Kwa utaratibu huu Serikali haina dhamira ya dharti ya kutekeleza miradi ya maendeleo na kwa vyovoyote vile haiwezi kufikia malengo yake kama ilivyokusudia.

2.6 UTEKELEZAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa yapo maoni yaliyofanyiwa kazi kikamilifu, yapo maoni yanayoendelea kufanyiwa kazi, lakini yapo maoni ambayo hayakufanyiwa kazi kabisa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt John Pombe Joseph Magufuli kwa kuyapandisha hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika kuwa Hifadhi za Taifa. Ni matumaini ya Kamati kwamba Serikali itawekeza vyta kutosha katika kuviendeleza vivutio vyta utalii vyta ukanda huu kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya barabara, maji, umeme pamoja na kuvutia wawekezaji kujenga mahotelili kuvutia watalii wengi zaidi kutembelea vivutio vyetu katika kanda ya ziwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhishwa na hatua ya Serikali kutangaza vivutio vyta utalii kwa kuanzisha Televisheni ya kutangaza utalii wa Tanzania ijulikanayo kama Tanzania Safari Chanel. Hii ni hatua muhimu sana katika kuvutia watalii wengi zaidi kuja nchini. Aidha Televisheni hii pia inachangia kuwavutia watalii wa ndani kuvielewa vivutio tulivyonavyo na hivyo kuamsha hamasa ya kutaka kwenda kuviona. Aidha Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Tamasha la mwezi wa urithi wa utamaduni ambalo litaadhimishwa nchini kote. Tamasha hili siyo litapanua wigo wa vivutio vyta utalii, bali pia litachangia sana katika kutangaza na kuvutia watalii wengi zaidi wa ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi na namna Serikali inavyoshughulikia suala la kumaliza migogoro ya mipaka baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa. Tangu wewe na watangulizi wako ukiwa Mwenyekiti wa Kamati hii kutoa maoni na ushauri kuhusu utatuzi wa migogoro ya mipaka bado migogoro imeendelea kuwepo. Kamati inaipongeza Mheshimiwa Rais Dr John Pombe Joseph Magufuli kwa maagizo aliyoyatoa hivi karibuni kwa baadhi ya Mawaziri wake kuhakikisha wanashughuulikia migogoro na kuimaliza katika muda aliowapangia. Ni matarajio ya kamati kwamba maagizo ya Rais yakitekelezwa kwa ukamilifu suala la migogoro litakuwa historia.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi na namna Serikali inavyoshindwa kutumia fursa ya vivutio vyta utalii kuongeza mapato yatokanayo na utalii. Tunaelezwa kwamba Tanzania

ni nchi ya pili duniani kuwa na vivutio vingi vya asili vya utalii baada ya Brazil lakini ni nchi inayopata mapato madogo yatokanayo na utalii ikilinganishwa na vivutio ilivyo navyo. Mathalani takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya watalii imeongezeka kutoka **1,284,279** mwaka 2016 hadi kufikia **1,327,143** mwaka 2017. Hii ni idadi ndogo sana kuweza kujivunia ikilinganishwa na fursa zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi na kasi ya Serikali kushughulikia malalamiko ya wafanyabiashara ya wanyamaporai hai ambapo Serikali ilisitisha biashara hiyo mwezi Machi, 2016 na kusababisha hali ya tataruki kwa wafanyabiashara hao. Huu ni mwaka wa nne sasa tangu kusitishwa kwa biashara hiyo na kumekuwa na matamko mbali mbali ya Wizara lakini hakuna utekelezaji wowote. Kibaya zaidi Tamko la kusitisha biashara ya viumbepori hai limeathiri hata vikundi vya akina mama katika hifadhi ya Misitu asilia wa Amani ambapo wao walikuwa wanazalisha vipepeo na kuwauza nje ya nchi. Jambo hili siyo tu limewaathiri wafanyabiashara na familia zao bali pia limekoshesha Serikali mapato. Takwimu zinaonesha kuwa Serikali ilikuwa inapata takriban shilingi billioni nne kutokana na tozo mbali mbali katika biashara hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali hajatekeleza ushauri wa Kamati wa kuipandisha hadhi Wakala wa Huduma za misitu Tanzania kuwa Mamlaka ya Misitu Tanzania hali inayozidi kuchangia uharibifu wa misitu na vyanzo vya maji kwa kukosa udhibiti.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya utalii inahitaji uwekezaji mkubwa ili Taifa liweze kunufaika. Inashangaza katika nchi yetu licha ya kuwa na fursa nyingi katika Sekta hii, bado Serikali hajawekeza vya kutosha ili tupate matunda yanayotarajiwa. Taarifa mbali mbali zinaonesha ubovu wa miundombinu ya bara bara, uhaba wa sehemu za malazi, kutoendelezwa kwa vivutio vingine kama vile Malikale, utamaduni, fukwe, Hifadhi za misitu Asilia na vingine vingi. Tumeelezwa pia kwamba watalii wengi wanaokuja nchini hutembelea vivutio vilivyo katika ukanda wa kaskazini huku kanda zingine zikipata idadi ndogo ya watalii. Kamati inashauri Serikali kuharakisha

utekelezaji wa mradi wa kuendeleza utalii kusini mwa Tanzania (REGROW) ili kuvutia watalii wengi kutembelea vivutio vilivyoko katika ukanda huo.

2.7 MPANGO WA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoa na:-

- a) Kutatua migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya hifadhi na wananchi
- b) Kuboresha vivutio na kutangaza utalii;
- c) Kupandisha hadhi Mapori Tengefu kuwa Mapori ya Akiba
- d) Kuhakikisha watumishi wote wa Sekta ya wanyamapori na Misitu wanapatiwa mafunzo ya Jeshi Usu
- e) Kupandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kuwa Mamlaka ya Misitu Tanzania

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na vipaumbele na malengo ya kazi za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Hata hivyo, vipaumbele, malengo na mipango hiyo itakamilika na kuinua pato la taifa kama makusanyo yatakusanya kama ilivyokusudiwa, na mgao wa fedha za matumizi utakua ni wa kuridhisha kwa lengo la kuiwezesha wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

2.8 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Makisio ya Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya shilingi **75, 012, 350,687/=** kutokana na vyanzo mbali mbali. Kiasi hiki ni

nyongeza ya shilingi **11,712,946,114/=** ikilinganishwa na shilingi **63,299,404,573=** zilizokadirwa kukusanya Mwaka wa Fedha 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia 18.5%. Ni mapendekezo ya Kamati kwamba Serikali ihakikishe inatafuta vyanzo vipyta na mbinu bora zaidi za ukusanyaji wa mapato ili kuongeza mapato ya Sekta ya Maliasili na Utalii.

2.9 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Maliasili na Utalii inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi **120,202,637,734**. Kati ya fedha hizo shilingi **71,312,649,000/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **48,889,989,734/=** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Bajeti ya maendeleo imeongezeka kutoka shilingi **bilion 29,978,082,000** mwaka 2018/2019 hadi shilingi **bilion 48,889,989,734** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 66%. Pamoja na ongezeko hili changamoto itabakia kuwa ile ile ya kutenga fedha bila kuzipeleka jambo ambalo linadhoofisha miradi ya maendeleo.

SEHEMU YA TATU

3.0 MASUALA MENGINE MUHIMU YALIYOJITOKESA WAKATI WA KUCHAMBUA NA KUPITISHA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HII KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, kulikua na maswala mbalimbali yaliyitokeza wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii, Maswala hayo ni pamoja na uchimbaji wa madini ndani ya hifadhi uliopelekeea uharibifu wa vyanzo vya maji pamoja na kuongezeka kwa migogoro ya ardhi kati ya Mamlaka za kutunza hifadhi na wananchi wanaozunguka hifadhi hizo. Ili kuondokana na migogoro hiyo **Kamati inaishauri Serikali kutafuta njia sahihi za kuweza kumaliza migogoro ya ardhi kati ya Mamlaka za hifadhi na wananchi wanaozunguka hifadhi**. Aidha uandaliwe mpango maalumu wa matumizi ya ardhi utakaoainisha maeneo ya hifadhi na mipaka yake na

maeneo kwa ajili ya malisho na shughuli nyingine za binadamu kwa lengo la kuwawezesha wafugaji kutumia maeneo hayo ipasavyo na sio kuvamia maeneo ya hifadhi. Kamati inashauri zoezi hili liwashirikishe wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto ya uhaba wa watumishi katika hifadhi zetu hususan Askari wa kulinda hifadhi hizo. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaajiri Askari wa kutosha kwa ajili ya kulinda hifadhi zetu. Aidha Serikali ihakikishe kuwa vyuo vinyavyotoa mafunzo ya misitu na wanyamapori viingize mafunzo ya Jeshi Usu ili vijana wetu wanaohitimu katika vyuo hivyo wawe wakakamavu na wazalendo wenye moyo wa kuzilinda raslimali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na m dororo katika sekta ya uwindaji wa kitalii kuto kana na mabadiliko ambayo Serikali inakusudia kuyafanya ikiwemo utaratibu wa kugawa vitalu kwa njia ya Mnada. Jambo hili limechukua muda mrefu na utekelezaji wake umechelewa na hivyo kusababisha kuzorota kwa shughuli za uhifadhi na uwekezaji katika vitalu hivyo kuto kana na kukosa uhakika wa kuendelea kuvimiliki na hivyo kulikos esha taifa mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii. Kamati inashauri Serikali kurejesha utulivu katika Tasnia hii kwa kuharakisha utekelezaji wa mabadiliko inayokusudia kufanya vinginevyo Taifa lita endelea kupoteza mapato.

Mheshimiwa Spika kumekuwepo na uharibifu wa vyanzo vya maji na uchafuzi wa maji katika hifadhi zetu hasa hifadhi za misitu Asilia unaosababishwa na wachimbaji haramu wa madini ya Dhahabu. Kamati inashauri Serikali kuwaelimisha wananchi kuhusu athari zinazoweza kuto kea kuto kana na uchimbaji huo wa madini. Aidha Serikali iweke adhabu kali kwa wataokamatwa wanaharibu vyanzo vya maji ili iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Spika kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa misitu hasa misitu inayomilikiwa na vijiji na Serikali za mitaa ambayo inakadiriwa kuchukua zaidi ya asilimia 52 ya eneo lote la misitu hapa nchini. Uharibifu mkubwa wa Misitu

umeonekana sana katika misitu ya hifadhi ambayo imevamiwa na wananchi wanaishi ndani ya hifadhi za misitu. Mfano mzuri ni Wilaya ya Kaliua ambako vijiji vingi vimo ndani ya hifadhi na vimesajiliwa kisheria. **Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kudhibiti ujangili wa misitu ili kuinusuru na kuiepusha nchi yetu na madhara yatokanayo na uharibifu wa misitu.** Aidha Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuiwandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania kuwa Mamlaka ili kuipa nguvu ya kisheria ya kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu yote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeyapandisha hadhi Mapori ya Akiba ya Bihamarulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika kuwa hifadhi za Taifa hivyo kuliongezea Shirika la Hifadhi za Taifa mzigo wa kuzilea Hifadhi hizi mpaka hapo zitakapoweza kujitegemea. Hata kabla ya kupandishwa hadhi kwa Mapori haya kuwa Hifadhi za Taifa, ni hifadhi Tano tu katika kumi na sita zilizokuwepo zilizokuwa na uwezo wa kuzalisha ziada iliyosaidia kuendesha hifadhi nyingine kumi na moja. Sasa hifadhi zimeongezeka na kufikia kumi na tisa. Ni dhahiri kutakuwa na ongezeko la kibajeti kwa ajili ya kuhudumia hifadhi mpya zilizoanzishwa. **Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kulipunguzia Shirika la Hifadhi za Taifa kiwango cha Gawio linachopeleka Serikalini ili kulipa nguvu ya kuhudumia hifadhi mpya.**

Aidha, Serikali ifanye utaratibu wa kurekebisha mfumo wa utozaji Kodi ya Makampuni inavyotozwa kwa Shirika la Hifadhi za Taifa. Shirika linatoa asilimia 15% ya mapato ghafi ya Shirika kama gawio kwa Serikali, linatoa 3% ya mapato ghafi kwa Kodi ya kuendeleza utalii, linatoa michango kwa Taaissi za uhifadhi, linatoa fedha kwa ajili ya miradi ya ujirani mwema lakini wanapotozwa kodi ya makampuni yaani Corporate Tax bado inatozwa katika mapato ghafi. Hali hili inadhoofisha uwezo wa Shirika kuhudumia Hifadhi ambazo hazijaweza kuzalisha mapato ya kutosha kujiendesha zikiwemo hifadhi mpya tatu zilizoanzishwa hivi karibuni. **Kamati inaishauri serikali kurejea upya sheria ya ukokotoaji wa kodi kwa Shirika hili.**

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo kwa changamoto ya kuwepo kwa idadi ndogo ya watalii wanaofika kutembelea vivutio vyetu nya utalii inayochangiwa pamoja na sababu nyingine uhaba wa sehemu za malazi nje na ndani ya hifadhi. Moja ya sababu zinazosababisha uhaba wa malazi ni kutoendelezwa kwa Loji na Hotel za Serikali zilizobinafsishwa na hivyo kuchangia uhaba wa malazi kwa watalii wetu. **Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya utendaji wa Loji na hotel za Serikali zilizobinafsishwa kuona kama zimezingatia mkataba wa mauziano na kuchukua hatua kwa zile zitakazobainika hazifanyi kazi kwa mujibu wa makubaliano.**

Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na mgongano wa kisheria unaosababisha utekelezaji wa Sheria ya wanyamapor Na 5 ya Mwaka 2009 kuwa mgumu. Mfano wa sheria zinazokinzana na sheria hili ni Sheria ya Ardhi ya vijiji Na 4 ya mwaka 1999, pamoja na sheria ya Madini. **Kamati inaishauri serikali kuunda timu ya wataalam ili kuzipitia sheria hizi kwa lengo la kubaini vifungu vyenye mgongano na kuleta mapendekezo Bungeni kwa ajili ya kuzifanyia marekebisho.**

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu iliwahi kushauri Serikali ifanye Tathmini ya mfumo wa uhifadhi mseto (multiple Land use) katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuona kama umekuwa na tija au la. Huu ni mwaka wa nne sasa Serikali bado haijatekeleza. Idadi ya watu imeongezeka, mifugo imeongezeka na shughuli za binadamu ndani ya hifadhi zimeongezeka. **Kamati kwa mara nyingine inaishauri serikali kufanya tathmini hiyo ili kuweza kujuua kama iendelee nao au ibadilishe.**

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Naomba nitoe maoni na ushauri wa Kamati kwa sekta mbalimbali zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo;-

4.1 SEKTA YA UTALII

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii inazo fursa nyingi ambazo zikitumiwa kikamilifu zitaongeza mchango wake katika pato la Taifa. Kwa sasa Sekta hii inachangia asilimia 17 tu ya pato la Taifa na Asilimia 25 ya fedha za kigeni. Ili kuongeza pato la Taifa kupitia Sekta ya Utalii, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

- a) Kuvibaini vivutio vyote vya utalii viliwyoko nchini, kuiendiyeleza na kuvitangaza ili vifahamike na hivyo kuvutia watalii wengi zaidi kuja nchini mwetu.
- b) Kuwekeza miundombinu kwenye vivutio vya utalii kwa kuimarisha au kujenga barabara, viwanja vya ndege, mahoteli, maji, vyoo n.k ili kuvutia watalii kufika kwenye vivutio hivyo kwa urahisi;
- c) Kuhamasisha Halmashauri zetu kubaini vivutio vya utalii katika maeneo yao na kuvunganisha na utalii wa kitamaduni katika maeneo husika ili kukuza utalii na kuwaingizia wananchi kipato
- d) Kutenga fedha za kutosha pamoja na kuhamasisha bodi ya utalii kupitia wizara hii kuongeza ubunifu katika kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi ili kuendana na ushindani uliopo katika sekta ya utalii;
- f) Kuutangaza mti unaosadikiwa kuwa mrefu kuliko yote Afrika ulioko katika hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ili utumike kama kivutio cha utalii. Mti huu unakadiriwa kuwa na urefu wa mita 84.7 na umepewaa jina la Kamasuka na uligunduliwa na mjerumani.
- g) Serikali ianze kuonyesha Tanzania safari Chanel katika ving'amuza vya kimataifa ili kutangaza utalii wetu na kuvutia watalii wengi kuja nchini

4.2 SEKTA YA WANYAMAPORI

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu imebarikiwa sana kuwa na hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Hifadhi za Jamii za wanyamapori ambavyo ni vivutio kwa utalii wa picha na pia uwindaji wa kitalii. Ili kuweza kuvitumia vivutio hivi kuongeza pato la Taifa, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

- a) Kuhakikisha kwamba vyuo vyote vinavyotoa mafunzo ya usimamizi wa wanyamapori vinapatiwa mafunzo ya Jeshi Usu ili kupata Askari watakaoweza kukabiliana na changamoto za ujangili.
- b) Kuendeleza programu zinazolenga kuongeza idadi ya wanyama walio katika hatari ya kutoweka kama faru na mbwa mwitu
- c) Kushirikiana na Mamlaka husika kubaini mbinu za kupunguza vifo vyta wanyamapori wanaokufa kwa kugongwa na magari katika barabara zinazokatiza katika hifadhi zetu hasa katika hifadhi ya Taifa ya Mikumi ambako kwa wastani mnyama mmoja hugongwa kila siku;
- d) Kusimamia mipaka na maeneo ya mapori kwa lengo la kutatua migogoro iliyopo na inayoweza kujitokeza kwa lengo la kunusuru ikolojia, kulinda mazalia ya wanyama, mapito ya wanyama pamoja na vyanzo vyta maji kwa ajili ya kuendeleza hifadhi na utalii nchini.
- e) Serikali iangalie uwezekano wa kulipunguzia Kodi Shirika la Hifadhi za taifa ili kulipa nguvu ya kuhudumia hifadhi mpya na zile ambazo hazijaweza kujitegemea
- f) Serikali iweke utaratibu wa kulinda shoroba za wanyamapori zisivamiwe. Aidha serikali iendelee kuhamasisha kuanzishwa kwa Jumuiya za Hifadhi za wanyamapori (WMA's) hasa katika maeneo ya shoroba ili kuendeleza uhifadhi shirikishi

- g) Serikali iangalie upya kanuni za kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori. Kanuni zilizopo sasa haziridhishi; malipo ni madogo na hayalipwi kwa wakati
- h) Serikali iweke utaratibu wa kutumia njia za utambuzi za kielektroniki kwa watalii wanaoingia hifadhini badala ya kutumia mfumo wa Single entry ambao unawakosesha mapato wadau wengine wa utalii hususan WMA's na Utalii wa kitamaduni wanapotaka kutoka na kurudi ndani ya hifadhi ndani ya masaa 24;
- i) Serikali iwashirikishe wananchi katika zoezi la utambuzi wa mipaka kati ya hifadhi na vijiji kabla ya kuweka vizingi; na
- j) Serikali iharakishe mchakato wa kugawa vitalu kwa njia ya mnada kwani kuna vitalu vingi viko wazi na serikali inazidi kupoteza mapato.

4.3 SEKTA YA MALIKALE

Mheshimiwa Spika, Malikale ni rasilimali za urithi wa Taifa tangu enzi za wahenga wetu. Rasilimali hii ikiboresha ipasavyo itachochea utalii na kuchangia ukuaji wa uchumi na kukuza sekta ya elimu hapa nchini. Hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuongeza mapato na kuinua sekta ya Malikale:-

- a) Kuainisha vivutio vya malikale pamoja na kuviendeleza, sambamba na kuimarisha ulinzi, kukarabati na kutunza maeneo yenye majengo ya Malikale kwa lengo la kuuenzi utamaduni wetu na kuvutia watalii kutoka katika maeneo mbalimbali nchini;
- b) Kuendelea kukuza utalii wa ndani kwa kuyatangaza maeneo ya Malikale ndani na nje ya nchi kama vivutio vya utalii na maeneo ya kujifunza historia ya nchi yetu;

4.4 MAKUMBUSHO YA TAIFA

Mheshimiwa Spika, Makumbusho ya Taifa ni moja ya idara muhimu yenye kutunza kumbukumbu na historia ya taifa kwa ujumla kabla na baada ya kupata uhuru. Ni kivutio cha utalii na ni kielelezo muhimu katika kuinua kiwango cha elimu nchini. Cha kusikitisha zaidi Serikali inaisahau idara hii muhimu hivyo Kamati inaikumbusha Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuinua idara hii:-

- a) Kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya ukarabati wa maeneo ya makumbusho ya Taifa na kuanzisha mengine mapya;
- b) Kutangaza Makumbusho ya Taifa kama kivutio sambamba na vivutio vingine vya utalii;
- c) Kuhamasisha wananchi kuitambua, kuithamini na kuitembelea makumbusho ya Taifa kama hatua ya kukuza utalii wa ndani pamoja na kuongeza uelewa wa historia ya nchi yetu;
- d) Kuendeleza Makumbusho ya Taifa kwa kujenga vivutio mbalimbali kama vile maduka, vyoo, migahawa kwa lengo la kuinua utalii na kuwavutia watalii wengi kutembelea; na
- e) Kuitangaza makumbusho ya Taifa hasa kituo cha Bonde la Olduvai ambacho ni chimbuko la historia ya binadamu wa leo.

4.5 SEKTA YA MISITU NA NYUKI

Mheshimiwa Spika, Idara ya misitu ni muhimu katika kuhifadhi mazingira, kurekebisha mfumo wa hali ya hewa, kupunguza mabadiliko ya tabia nchi, Kuhifadhi bioanuai, pamoja na kuhifadhi vyanzo vya maji. Pamoja na hayo, idara hii ikitunzwa kikamilifu itachangia ongezeko la ajira na kupunguza umaskini. Kufuatia fursa hizi Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuinua sekta ya misitu na nyuki;-

- (a) Kuimarisha ulinzi katika misitu hapa nchini ili isivamiwe na shughuli za kibinadamu zisizoendelevu kama uvunaji haramu, ufgaji, uchomaji mkaa usio endelevu na kilimo zinazopelekea hali ya rasilimali ya misitu kuwa duni;
- (b) Kutangaza hifadhi za misitu asilia kama vivutio vya utalii ili kuongeza mapato yake;
- (c) Kuharakisha mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania kuwa Mamlaka itakayokuwa na nguvu za kisheria ya kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu nchini
- (d) Kutoa mafunzo yanayohusu kuanzisha na kuendeleza misitu kwa wananchi wanaozunguka misitu ya hifadhi kwa lengo la kuimarisha ushiriki wa wananchi katika uhifadhi wa misitu na hifadhi za nyuki.
- (e) Kuweka mkakati wa kutunza vyanzo vya maji na kuepusha kukauka kwa baadhi ya mito mikubwa;Na
- (f) Kuhamasisha jamii kuanzisha mashamba ya miti (Woodlots) ndani ya maeneo yao ili kupunguza uvamizi ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa.

5.0 **HITIMISHO**

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa mliokabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt Hamisi Kigwangalla, Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu waziri Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya maliasili na Utalii kwa ushirikiano waliotupa katika kutekeleza majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

- | | | |
|---|---|--------------|
| 1. Mhe. Kemirembe Lwota, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Nape Mosses NNauye | - | Mjumbe |
| 3. Mhe. Mch Peter Simon Msigwa, Mb | - | Mjumbe |
| 4. Mhe. Boniface Mwita Getere , Mb | - | Mjumbe |
| 5. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb | - | Mjumbe |
| 6. Mhe. Lucy Mayenga, Mb | - | Mjumbe |
| 7. Mhe. Paulne Gekul, Mb | - | Mjumbe |
| 8. Mhe. Khalifa salim Suleiman, Mb | - | Mjumbe |
| 9. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb | - | Mjumbe |
| 10. Mhe. Magdalena Hamis sakaya, Mb | - | Mjumbe |
| 11. Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb | - | Mjumbe |
| 12. Mhe. Timotheo Mnzava, Mb | - | Mjumbe |
| 13. Mhe. Lucy Fidelis Owenya, Mb | - | Mumbe |
| 14. Mhe. Dkt Jasmin T.Bunga, Mb | - | Mjumbe |
| 15. Mhe. Risala Kabongo, Mb | - | Mjumbe |
| 16. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb | - | Mjumbe |
| 17. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb | - | Mjumbe |
| 18. Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb | - | Mjumbe |
| 19. Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb | - | Mjumbe |
| 20. Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mb | - | Mjumbe |
| 21. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb | - | Mjumbe |
| 22. Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb | - | Mjumbe |
| 23. Mhe. Dkt Stephen Lemomo Kiruswa, Mb | - | Mjumbe |
| 24. Mhe. Neema William Mgaya, Mb | - | Mjumbe |
| 25. Mheshimiwa Salim abdallah Turky | - | Mjumbe |

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussen, Makatibu wa Kamati Ndugu Gerald Magili na Elihaika Mtui, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii Fungu 69 kama yalivowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Kemirembe Julius Lwota, (Mb)

MAKAMU MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII

23 Mei, 2019

MWENYEKITI: Sasa namwita Msemaji Mkuu Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii na wewe umependeza vilevile. (*Makofi*)

MHE. CATHERINE N. RUGE - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Mheshimiwa Peter Msigwa napenda kuwasilisha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 na Mpango wa Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kabla sijaanza kusoma hotuba yangu naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na nguvu katika kipindi hiki kigumu sana katika ufanyaji wa siasa hasa kwa upande shindani na Chama Tawala na kuweza kusimama mbele ya hadhira hii ili kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu sekta nzima ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwapa pole viongozi wote wa Vyama vya Upinzani kwa madhira makubwa wanayokumbana nayo kutoka kwenye vyombo vya dola pamoja na matishio yaliyopo kutokana na sheria

mpya na mbaya sana ya kudhibiti vyama vya siasa hasa vile shindani na chama tawala. Pia kuwashukuru na kuwapongeza kwa mshikamano ambao unajengwa na hivyo kuhakikisha kuwa uchaguzi ujao tunaitoa Serikali hii ya Awamu Tano madarakani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msigwa anapenda kuwashukuru wapiga kura wake wa Jimbo la Iringa Mjini kwa kuendelea kumwamini na anawaahidi kwamba hatawaangusha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenendo na hali ya Maliasili Nchini; kwa muda mrefu zimejitokeza changamoto nyingi katika sekta hii ya uwindaji ikiwemo muda uliotolewa kwa uwindaji kupunguzwa kutoka miaka mitano mpaka miaka miwili na kuleta sintofahamu kwa wadau. Pamoja na jitihada nyingi zillizofanyika bado kuna changamoto nyingi ikiwemo vitalu vingi kukosa wamiliki na hivyo kupelekea vitalu hivyo kuvamiwa na wafugaji, wawindaji na majangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo Kambi Rasmi ya Upinzani inakemea tabia ya Serikali kuendelea kukandamiza Sekta Binafsi kwa kufanya maamuzi ya kukurupuka bila kuwasikiliza au kushauriana na wadau wa Sekta Binafsi ili kuleta ufanisi na ushirikiano wa kibiashara. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itambue mchango mkubwa wa sekta binafsi katika maendeleo yetu ikiwa ni pamoja na makusanyo ya kodi yanayotokana na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kukaa upya na wamiliki wa vitalu pamoja na wadau wengine wanaojihusisha na biashara ya utalii na uwindaji ili kufikia maamuzi ya pamoja kwa kuangalia namna bora ya kufanya kazi na kutatua changamoto kubwa na masononeko mionganoni mwa wawekezaji katika sekta hii, ili kulinda sifa ya Tanzania iliojijengea miaka ya nyuma katika soko la Kimataifa la Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya uwindaji imekuwa na changamoto nyingi sana zinazowakatisha tamaa wawekezaji. Ni biashara inayoelemewa na wingi wa kodi. Mfano, katika sekta hii ndogo ya uwindaji kuna takribani tozo 21 za kodi kubwa ukiachilia mbali zile za biashara ya utalii. Kodi zenyewe ni kama zinavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza Serikali kukaa na wadau hawa ili kujaribu kutatua changamoto hizo ambazo bado zinaikabili sekta hii ndogo ya uwindaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Biashara ya Usafirishaji Viumbe Hai Nje ya Nchi; tunakumbuka kwamba Machi, 2016 Serikali ilipiga marufuku usafirishaji wa viumbe hai nje ya nchi, ikitoa sababu kuwa inatengeneza mfumo ambaao utaisaldla kudhibiti na kufuatilia kwa karibu biashara hiyo ya viumbe hai. Hata hivyo, katika upigaji marufuku huu Serikali haikutoa suluhu kwa wafanyabiashara ambaao tayari walikuwa wameshakuwa na bidhaa hiyo tayari kwa usafirishaji na gharama za kuwatunza zitalipwa na nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa ahadi kwa wadau hao kwamba itarejesha tozo na gharama za wafanyabiashara wa viumbe hai ambaao tayari walikwishalipa ambazo hakutaja kiasi chake lakini ni mamilioni ya fedha, baada ya kumaliza zoezi la uhakiki. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupata majibu ni kwa nini hasa maamuzi ambayo mara nyingi yanapochukuliwa na Serikali ndio inapata hasara zaidi na pale wahusika wanaposhindwa kurejeshewa fedha zao kwa wakati ili waweze kuwekeza katika mambo mengine ya kuwaingizia kipato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akiongea na wadau wa biashara hiyo, alisema, Serikali imepoteza kiasi cha shilingi trillioni 2.5 kama mapato yatokanayo na biashara ya usafirishaji wa viumbe hai kwa kipindi cha miaka miwili. Kambi

Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuta agizo lake la kuzuia biashara ya viumbi hai nje ya nchi na iwalipe fidia wafanyabiashara kwa hasara na usumbufu iliowasababishia wafanyabiashara hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka za Hifadhi, Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*); Taasisi za uhifadhi duniani hupatiwa ruzuku kutoka Serikali Kuu ili kujenga miundombinu ya maendeleo mengine ya maeneo ya hifadhi, lakini kwetu sisi, *TANAPA* inajijendesha bila ya kutegemea ruzuku na pia inalazimika kulipa kodi Serikalini. Kutohana na mfumo wetu wa kodi ambao badala ya kuipa *TANAPA* unafuu wa kutekeleza majukumu yake ya kimsingi inaifanya ishindwe kutimiza majukumu yake. Changamoto hizo za kikodi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna asilimia 30 Kodi ya makampuni, asilimia 18 Kodi ya ongezeko la thamani kwa maana ya VAT, asilimia 15, gawio la Serikali; asilimia tatu Kodi ya maendeleo ya ufundi, kodi ya *stamp*, kodi ya forodha kwa maana ya (*Import and excise duties*), Kodi kwa maendeleo ya jamii-*CSR*, Kodi inayotozwa kwenye michango mbalimbali (*Taxation on contribution*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa ni muda muafaka sasa kuondoa au kupunguza viwango vya kodi za kisheria zinazopelekwa Serikalini, Bodi ya Utalii na Taasisi za Hifadhi na kodi inayokatwa kwenye michango inayogharamia miradi ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Mkaguzi, TANAPA ilitoa kandarasi za miradi miwili mnamo tarehe 6 Mei, 2017 kwa mkandarasi *JECCS Construction Supplies Limited* na tarehe 9 Februari, mwaka 2017 kwa Mkandarasi *Secao Builder Limited*. Gharama ya mikataba yote miwili ilikuwa ni shilingi milioni 961. Kipindi cha mikataba yote hii miwili kilimalizika tarehe 17 Februari, 2018 na tarehe 10 Oktoba, 2017, mtawalia. Hata hivyo, hadi kufikia Februari mwaka 2019 mwaka mmoja (1) kutoka tarehe iliyopangwa

kukamilika, miradi hiyo haikuwa imekamilika. Ujenzi wa miradi yote miwili bado hadi sasa haujakamilika. Kadhalika, muda wa nyongeza pia ulikuwa umekwisha tangu tarehe 5 Novemba, mwaka 2018. Hakukuwa na juhudhi zozote zilizofanywa na *TANAPA* ili kuhakikisha miradi hii inakamilika. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutupa taarifa ya utekelezaji wa miradi yote hiyo miwili na hatua ambazo zimechukuliwa kwa Mkandarasi huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *KfW-Serengeti*, Tarehe 16 Desemba, 2013, (*TANAPA*), iliingia makubaliano ya kifedha na *KfW* na *Frankfurt Zoology Society* kwa ajili ya kuendeleza mazingira ya mbuga ya Serengeti na Ngorongoro. Gharama za mradi zilikadiriwa kuwa *EUR* za Ulaya milioni 24.12. *KfW*likubali kufadhili *EUR* za Ulaya milioni 20.5, wakati *Frankfurt Zoological Society*likubali kufadhili *EUR* za Ulaya milioni moja na zillzobaki *EUR* za Ulaya milioni 2.62 zifadhiliwe na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa Tanzania kwa maana *TANAPA*. Muda wa mradi ulikadiriwa kuwa mitano kuanzia tarehe 11 Julai, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilitarajia kujenga nyumba za watumishi, vituo vya watalii, mifereji ya maji, kuanzisha mpango wa matumizi matumizi bora ya ardhi vijijiini, kurasimisha matumizi ya ardhi, kuanzisha mpango wa matumizi bora ya mali kwenye Kanda na kuanzisha Jamii ya Wanyamapor na Usimamizi Bora wa Misitu. Pia, fedha hizo zilitarajia kujenga barabara za kimkakati Vijiji vya Serengeti na Ngorongoro, kusaidia mbuga ya Serengeti, programu ya kugawana faida na kusaidiwa jamii za vijijiini na kujenga miundombinu ya kiuchumi na kijamii. Walikubaliana kuwa kodi zote za Serikali na tozo zingine zitagharamiwa na Serikali au Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa Tanzania na *KfW* ina haki ya kukataa kutoa fedha baada ya 30 Juni, 2018 kama ilivyoonyeshwa kwenye mkataba wa makubaliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpaka kufikia Januari, 2019, miaka minne baadaye toka kuanza kwa mkataba huo hakuna kilichofanyika. Sababu za kuchelewa ni kwamba vitu vya ujenzi vilitakiwa visamehewe kodi wakati wa kuvilingiza

nchini kutoka nje. Hata hivyo, mpaka wakati wa ukaguzi Januari, 2019, msamaha wa kodi ulikuwa haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa Tanzania tunapoteza fursa nydingi kutokana na kuwapa uongozi watendaji wasiokuwa na uwezo wa kibashara na matokeo yake wao wanaangalia kidogo kilichopo, lakini hawaoni kikubwa tunachotegemea kupata kesho au keshokutwa. Hili ni tatizo kubwa la watendaji wetu wa Taasisi zinazohusika na utoaji wa vibali na ukusanyaji wa mapato. Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuzingatia weledi na uwezo wa watendaji wanaopewa majukumu ya kaliba hii ili kutuvusha kutoka kwenye dimbwi la umaskini linalotukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro ni moja ya kivutio kikubwa cha kimataifa katika utalii kutokana na binadamu kuishi pamoja na wanyama, hata hivyo kivutio hiki kiko kwenye hatari ya uharibifu wa mazingira kama hatua stahiki hazitachukuliwa kunusuru bonde hilo. Kwa mfano kuongezeka kwa makazi ya binadamu ndani ya bonde hilo, kuongezeka kwa idadi ya mifugo, uvamizi na ukataji wa miti, kuzuwa kwa njia za asili za wanyama, kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu na mahusiano mabaya kati ya jamii na watumishi wa hifadhi ya Ngorongoro. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuchukua hatua stahiki kunusuru hifadhi hii ya Bonde la Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kumekuwa na matumizi mabaya ya pesa katika Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro. Bodi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro ilifanya jumla ya vikao 20 na semina sita kwa mwaka wa fedha 2017/18, ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.10 zilitumika kama ilivyoainishwa hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya namna hii ya kuwakirimu wajumbe wa bodi inaweza ikaleta tafsiri kuwa lengo la menejimenti ni kuwaghiribu wajumbe wa bodi ili ishindwe kufanya au kutekeleza jukumu lake la msingi la

kuisimamia menejimenti hiyo. Kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona litakuwa ni jambo la busara Mheshimiwa Waziri kuilekeza Bodi ya Bonde la Ngorongoro kujitathmini na kuona kama bado ina uhalali wa kuendelea kuisimamia menejimenti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utalii katika Fukwe za Bahari. Utalii wa fukwe ni mojawapo ya kivutio kikubwa sana kwa watalii ambao wengi wao wanatoka katika mataifa ambayo hayakupata bahati kuwa na fukwe, au kutokana na kubadilika sana kwa misimu ya majira ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili kuna visiwa ambavyo vinakodishwa na kumilikiwa na watu binafsi. Miiongoni mwa visiwa hivyo ni kisiwa cha Shungumbili ambacho kwa sasa kinaitwa *Thanda Island* ambacho ni sehemu ya kisiwa kilicho ndani ya kisiwa kinachoitwa Nyororo, vyote vikiwa katika Wilaya ya Mafia au Kisiwa cha Mafia. Kwa bahati mbaya sana kisiwa hiki cha Shungumbili au *Thanda Island* ambacho ni *Private Island* kina hoteli ambayo ni ghali kuliko hoteli yoyote ile Duniani, kwani kulala kwa siku ni dola za kimarekani 25,000. Mtu kukaa hapo ni lazima uanze kukaa kuanzia siku saba, jaribu kufikiria kwa mwaka kisiwa hicho au vingine kama vile visiwa vingine kama viliviyotajwa hapo chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kusema kuwa Wizara imeshindwa kupata taarifa za kisiwa hiki cha Shungumbili, na badala yake taarifa zake zinapatikana kutoka *The US Military Intelligence*. Maana yake ni kwamba, chochote kinachoendelea kwenye visiwa hivyo vya binafsi Serikali haina taarifa. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuleta taarifa rasmi za visiwa hivyo vinavyomilikiwa na watu binafsi ili kuwa na taarifa sahihi kuhusu watalii wanaoingia katika nchi hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *Theme Park Jijini Dar es Salaam*. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi 250,000,000 kwa ajili ya upembuzi yakinifu ili kuufanya Mji wa Dar es Salaam kuwa Mji wa kitalii. Katika hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa mwaka wa fedha

2016/2017 iliishauri Serikali kutenga eneo la Msitu wa Pande kuwa ehemu ya Bustani ya Wanyamapori ili kupunguza gharama za kujenga eneo lingine litakaloweza kushabihiana na mazingira ya kuishi wanyama ikiwa ni pamoja na eneo la mazalia ya wanyamapori ndani ya Jiji la Dar es Slaam. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 mradi huu ultengewa jumla ya shilingi milioni 500. Lakini hadi mwezi Februari 2019 hakuna hata senti moja iliyotolewa, na kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hakuna hata shilingi iliyotengwa kwa ajili ya mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha inatoa fedha zilizotengwa, badala ya mfumo wa sasa unaotumiwa na baadhi ya wanasiisa kwa kufanya matumizi ambayo hayajatengwa wala kuidhinishwa na Bunge, jambo ambalo ni kinyume cha Sheria ya Bajeti. Pamoja na hilo Kambi Rasmi inataka kujua uwepo wa taarifa ya mabasi yaliyonunuliwa kwa ajili ya kutoa huduma za kutembeza watalii katika vivutio mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam? Je, mabasi hayo yaliyonunuliwa, je, ni sehemu ya mradi huu? Je, gharama yake ni shilingi ngapi? Na Je, mabasi hayo ni mangapi?

Mheshimiwa mwenyekiti, Mwenendo wa Sekta ya Utalii Nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini utalii ni hatua ya kujenga uchumi wa Tanzania kutokana na nchi kuwa na vivutio vya asili, utamaduni na kuwa kwenye jiografia ya kimkakati na hivyo kuwa na manufaa makubwa hata katika sekta nyingine za uchumi. Utalii unapanua fursa za ajira zenyet kipato cha moja kwa moja au kwa shughuli nyingine zinazofungamana na utalii. Ili kufikia sekta ya utalii kuwa ya manufaa kwa nchi, ushirikishwaji wa sekta binafsi kutasaidia sana katika ujenzi wa miundombinu ya utalii wa kimataifa kwenye maeneo ya bahari, maziwa na misitu. Hivyo utalii utaboresha soko la bidhaa zinazozalishwa nchini. Rejea kitabu cha sera cha CHADEMA uk. 24 na 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idadi ya Watalii Tanzania Bara na Zanzibar. Kumekuwa na sintofahamu juu ya takwimu zinazotolewa juu ya idadi ya watalii wanaoingia nchini. Sintofahamu hii inatokana na idadi ya watalii ambayo

imekuwa ikiripotiwa kwenye hotuba mbalimbali ikiwemo Randama ya Wizara Fungu 69. Katika Randama inaonesha kuwa kwa mwaka 2016 watalii walioingia nchini walikuwa 1,284,279 na kwa mwaka 2017 walikuwa ni takribani watalii 1,327,143 na kwa mwaka 2018 kufikia 1,494,596. Ripoti hizi zimebainisha kuwa watalii hao walikuja kutembelea Hifadhi za Taifa, Mamlaka za Hifadhi za Ngorongoro na Zanzibar. Hii ina maana kwamba watalii walioingia kutoa Zanzibar nao wamejumuishwa katika idadi ya watalii wote walioingia nchini kwa mujibu wa maelezo ya randama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunatambua kuwa masuala ya sekta ya utalii si masuala ya Muungano. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ituambie ni lini hasa imeamua mambo ya utalii kuwa sehemu ya Muungano? Pia tunaitaka Serikali itupe takwimu sahilii za watalii wanaoingia nchini kwa maana ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mujibu wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano, katika kuhakikisha sekta ya utalii inakuwa endelevu na yenye tija kwa Taifa, ikiwa ni pamoja na kuongeza namba ya watalii wanaoingia Tanzania kutoka 1,200,000 mwaka 2016/2017 hadi 2,000,000 ifikapo mwaka 2020. Kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ya Utalii na Wanyama Pori ya Kenya, juu ya utendaji wa sekta ya utalii iliyotolewa mwaka 2018 ni kuwa nchi hiyo kwa mwaka 2017 iliingiza watalii 1,474,671 na mwaka 2018 iliingiza watalii 2,025,206. Wakati huo huo vitanda kwa ajili ya watalii viliongezeka kufikia milioni 4.05 kulinganisha mwaka 2018 ambapo ilikuwa vitanda 6,000,000. Nasikitika kusema kwamba Tanzania tuna vitanda 35,000 plus.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali badala ya kutafuta mchawi itafakari takwimu hizi za washindani wetu na tuje na mkakati wa kuboresha sekta ya utalii katika karne ya 21 ili tuweze kushindana na jirani zetu kwa kuongeza idadi ya watalii na fedha za kigeni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Demokrasia na Ukuaji wa Sekta ya Utalii. Katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ya mwaka 2016/2017 ilitolea mfano wa nchi ya Sri Lanka. Katika gazeti la *New York Times*, nchi kama Sri Lanka iliwhi kupata hadhi ya kujulikana kama nchi ya kwanza duniani kwa vivutio vyaa watalii. Hata hivyo kukandamizwa kwa demokrasia na misukosuko ya kisiasa nchini Sri Lanka kama inavyotokea Tanzania leo ilipelekeea utalii wa nchi hiyo kushuka kwa kasi ya asilimia 43 ndani ya kipindi cha mwaka mmoja na hivyo kuanguka kabisa kwa uchumi wa nchi hiyo. Hivyo, kuanza kusuasua kwa sekta hii ya utalii kwa uminywaji wa demokrasia ni dalili mbaya na isipoangaliwa inaweza kutupeleka katika kile kilichotokea Sri Lanka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardh, Maliasili na Utalii ambayo imetolea mfano wa nchi kama Botswana ambayo imekuwa na tozo la VAT katika huduma za kitalii kwa sasa wameongeza VAT kutoka asilimia 14 kwenda asilimia 15 kama mfano wa nchi Barani Afrika zenye mfumo wa VAT. Ni vyema Serikali hii ikatambua kuwa pamoja na tozo ya VAT kwenye utalii nchini Botswana bado kiwango hicho haijafikia ukubwa wa tozo kama tozo ya asilimia 18 iliyoko Tanzania kwa sasa. Vilevile, ikumbukwe kuwa nchi ya Botswana imepunguza mrundikano wa kodi tofauti na Tanzania yenye takribani kodi 36 kwenye sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Zinazoendesha Sekta ya Maliasili na Utalii. Sera haiwezi kusimama peke yake wakati inatungwa, ni lazima iangalie sera zingine zinasemaje ili kuondoa mwingiliano wa kiutendaji katika kufikia malengo ya sera; vivyo hivyo pia katika utunzi wa sharia. Sheria nzuri inayotoa matunda bora ni lazima vitu vyote vimalizikie kwenye ofisi moja (*one stop center*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya maliasili na utalii inaongozwa na sheria na kanuni zipatazo 13, na vyote hivi vinafanyakazi kwa wakati mmoja na mdau wa utalii ni lazima aendane na matakwa ya sheria hizo na kanuni zake. Uwepo wa sheria na kanuni zipatazo 13 umepelekeea ukiritimba

uliopitiliza. Mbali ya ukiritimba pia vifungu nya sheria hizo vinakinzana na kusababisha wadau wa utalii kushindwa kufikia malengo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa sheria hizo ambazo vifungu vyake vinakinzana sana na kuleta sintofahamu ni Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009; Kanuni na Sheria ya Wanyamapori na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999; Kanuni na Sheria ya Wanyamapori za Mwaka 2018 na Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009; Sheria ya Nyanda za Malisho ya Mwaka 2010 na Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia sheria na kanuni zote zinazokinzana ili kuleta utengamano mzuri wa kisheria kwa manufaa na maendeleo ya sekta nzima ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Migogoro Sugu Bainya Serikali na Wananchi Wanaoishi Kando ya Hifadhi. Tumekuwa na tatizo sugu la migogoro baina ya Serikali na wananchi wanaoishi kando kando ya hifadhi kwa muda mrefu. Mfano ilioletwa ni pamoja na maeneo ya Wilaya ya Bunda yanayopakana na pori la Akiba la Grumeti, Vijiji nya Kegonga na Masanga, pia maeneo ya Ulanga Vijiji nya Iputi na Lupiro yakiwa ni baadhi tu ya maeneo ambayo migogoro imesababishwa na Mamlaka za Wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiwakumbatia baadhi ya wawekezaji ambao wamekuwa chanzo au sehemu ya migogoro sugu ya wanavijiji wanaoishi maeneo ya hifadhi. Mfano ni mgogoro wa Loliondo uliyodumu zaidi ya miaka 26. Mgogoro huu uliwahi kuundiwa kamati mbalimbali ili kutafuta suluhu lakini mpaka leo Serikali imegoma kurudisha mrejesho kwa wananchi kujua kinagaubaga na hatua mahususi zilizopendekezwa. Ni wazi kuwa migogoro hii imeendelea kuwepo kutokana na ripoti nyingi kuwa za siri na wananchi kutoshirikishwa ipasavyo katika maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti hufanywa siri au mali ya watu wachache badala ya mali ya umma. Mfano katika ripoti mbalimbali za Serikali, mashirika na taasisi binafsi pamoja na hotuba mbalimbali za Kambi Rasmi ya Upinzani zimezungumzia kwa kina watuhumiwa wakubwa wa mgogoro wa Loliondo ambapo Kampuni ya *Otterlo Business Corporation* ambayo imetuhumiwa kwa muda mrefu kuwa sehemu kubwa ya chanzo cha mgogoro katika Bonde Tengefu la Loliondo. Kampuni ya *Greenmile* imekuwa na kashfa nydingi na kuwa sehemu ya migogoro, Kampuni ya Thomson Safaris imekuwa ikituhumiwa kama sehemu kuu ya migogoro katika vijiji vilivyopo katika Hifadhi ya Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza, bado Serikali hajaweza kuziwajibisha kampuni hizi. Hii ni mifano midogo tu kati ya migogoro mingi inayoendelea nchini ambapo Serikali imeshindwa kuja na majibu na mikakati ya kudumu jambo ambalo linazua shaka kubwa na ari ya kutaka kujua ni nani hasa mnufaika wa migogoro ya namna hii? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaitaka Serikali kuhakikisha inaweka wazi ripoti zote za Kamati Maalum zilizowahi kushughulikia migogoro hii ili kutoa fursa kwa wawakilishi wa wananchi kujadili kwa uwazi ripoti hizo na hata kutoa mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba aya ya 46 pamoja na 47 iingie kwenye *hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa ekolojia ya Bonde la Kilombero na Mto Rufiji ni muhimu sana kwa sasa kutokana na ukweli kwamba utekelezwaji wa mradi wa ufuaji wa umeme ni kuwa utaleta hasara kwa mazingira kwa kusababisha uharibifu mkubwa wa misitu na hivyo kuondoa mazalia ya wanyama na ndege wengi ambao walikuwa wanaleta utofauti mkubwa na wa kipekee wa mbuga ya Selous.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha na fedheha kubwa kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano kuwa mstari wa mbele katika kuyafuta yale mazuri tuliyoyaridhia

kama taifa ili kulinda mazingira ya sasa na ya vizazi vijavyo. Nayasema haya kwa kuwa Serikali hii ya awamu ya tano mapema mwaka jana ilifanya upembuzi katika kile walichokisema ni mpango wa Serikali wa kuanzisha mradi mkubwa wa kuzalisha nishati ya umeme (*Stiegler's Gorge*) katika pori la akiba la Selous kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu yoyote mwenye akili timamu asiyejua umuhimu wa Pori la Akiba la Selous na umuhimu wa kuilinda kwa wivu mkubwa ikolojia ya eneo hilo ambalo kwa kupitia Mto Rufiji imekuwa ni chanzo kikubwa cha maji yanayotegemewa na binadamu, mimea, wanyamapori, samaki na mifugo. Pamoja na Serikali kusema imefanya upembuzi yakinifu, ni vyema ikaamua kufanya mkakati wa tathimini ya mazingira kwa miaka minge ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambl Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya mikakati ya kimazingira ya muda mrefu kabla ya kuanza kwa mradi huu. Serikali ikumbuke makosa makubwa iliyofanya katika kujenga mradi wa stesheni ya mabasi yaendayo kwa kasi (*DART*) ambao kwa sasa inaigharimu Serikali kutokana tu na kufanya miradi ya namna hii bila kuangalia athari za muda mrefu za kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya ufugaji wa nyuki imekuwa halfanyi vizuri kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo kutokupewa kipaumbele ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* mwaka 2016/2017 Serikali ilitoa kiasi cha shilingi milioni 104 kwa wafugaji saba kwa kipindi cha miaka miwili lakini cha kushangaza mizinga minge haina nyuki na miradi hiyo imesimama. Kwa mfano katika mizinga 150 iliyowekwa Manispaa ya Dodoma ni mizinga saba tu yenye nyuki, katika Halmashauri ya Kishapu mizinga 150 imewekwa mahali ambapo sio mazingira sahihi kwa mazalia ya nyuki na hivyo hakuna nyuki. Mradi huu wa Kishapu umegharimu takribani milioni 40. Katika Halmashauri ya Misungwi kati ya mizinga 150 ni mizinga 14 tu ndiyo ilikuwa na nyuki kwa kipindi cha

miaka miwili hivyo mizinga 136 haikuwa na nyuki huku. Hii ni baadhi tu ya mifano mingine mingi ambapo fedha nyingi hutumika huku matokeo yakikosa tija kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni hatua gani stahiki zimechukuliwa kwa uzembe huu mkubwa wa upotevu wa fedha za umma katika miradi inayogharimu mamilioni bila kuwa na faida yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji Wa Bajeti 2018/2019 na Mpango wa Maendeleo 2019/2020. Kwa mujibu wa ripoti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 sekta ya utalii ilichangia asilimia 17 ya Pato la Taifa na takribani asilimia 25 ya fedha za kigeni (*foreign currency*). Hii ikiwa ni kati ya sekta tano muhimu zinazichangia zaidi katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuona umuhimu huu wa sekta ya utalii na mifano ya nchi mbalimbali wanavyonufaika katika utalii wa aina tofauti tofauti bado hapa nchini kwenye sekta hii imekuwa ikisuasua na kutegemea wahisani katika miradi mbalimbali ya maendeleo, kama tulivyomsikia Mheshimiwa Waziri alivyokuwa anawashukuru wahisani ambao wamechangia Sekta hii, tunaona jinsi gani tumeweka sekta yetu ya utalii rehani kwa wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Randama ya Wizara Fungu 69 ya mwaka 2016/2017 fedha za miradi ya maendeleo zilijumuisha shilingi 15.7 ambapo fedha za ndani zilikuwa shilingi 2,000,000,000. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 fedha za ndani zilizotolewa zilikuwa shilingi 11.4 na fedha za nje ni shilingi 16.6, hii ikiwa na maana fedha za ndani zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zinaendelea kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 zilitengwa shilingi bilioni 29.9. Kati ya fedha hizo za ndani ni shilingi 3,000,000,000 na fedha za nje ni shilingi bilioni 26.9 ambazo ni sawa na asilimia 89.9 ya

fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Februari 2019 fedha zilizopokelewa ni shilingi 10.5 fedha za nje na sawa na asilimia 35 ya fedha zote za Wizara. Kwa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hakuna hata shilingi moja ya fedha za ndani zilizotolewa kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2019/2020...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzunguaji)

MWENYEKITI: Malizia.

MHE. CATHERINE N. RUGE - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia, mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 48.9 ili kutekeleza miradi minane ya maendeleo, kati ya fedha hizo fedha za ndani ni shilingi bilioni moja tu na fedha za nje ni shilingi bilioni 47.9

MWENYEKITI: Ahsante, saa saba ilishaingia, ulishasema zote zilishaingia kwenye hansard ulishasema tangu mwanzo.

MHE. CATHERINE N. RUGE - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay, naomba kuwasilisha.* (*Makofi*)

HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

I. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na nguvu katika kipindi hiki kigumu sana katika ufanyaji wa siasa hasa kwa upande shindani na Chama Tawala na kuweza kusimama mbele ya hadhira hii ili

kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu sekta nzima ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

2. Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwapa pole viongozi wote wa vyama vyaya Upinzani kwa madhira makubwa wanayokumbana nayo kutoka kwenye vyombo vyaya dola pamoja na matishio yaliyopo kutokana na sheria mpya na mbaya sana ya kudhibiti vyama vyaya siasa hasa vile shindani na chama tawala, pia kuwashukuru na kuwapongeza kwa mshikamano ambao unajengwa na hivyo kuhakikisha kuwa uchaguzi ujao tunaitoa Serikali hii ya awamu tano madarakani.

3. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wangu wa Iringa Mjini kwa kuendelea kuniamini, na imani kubwa waliyo nayo kwangu. Naendelea kuwaahidi kuwa sitawaangusha.

II. MWENENDO NA HALI YA MALIASILI NCHINI

a) Sekta ya Uwindaji

4. Mheshimiwa Spika, sekta ya Uwindaji ni sekta muhimu katika Utalii. Kuanzia Mwaka 2009-2016 sekta hii ilichangia takribani dola za kimarekani milioni 163,465,077.01 sawa na takribani shilingi bilioni 3.5 za Kitanzania ndani ya sekta. Mwenendo wa biashara ya Uwindaji, inaonekana kuperomoka kuanzia mwaka 2014/15 mpaka mwaka 2017 ambapo makadirio yanaonyesha kuendelea kuperomoka zaidi. Mwaka 2010/11 mapato yalifkia dola 26,399,634 ikilinganishwa na mwaka 2015/16 ambapo mapato yalifkia kiasi 17,406,860 na mwaka 2016/2017 kiasi cha shilingi 18,787,976 tu¹. Hii ikiwa na maana kwamba miaka ya nyuma sekta hii ilifanya vizuri tofauti na ilivyo sasa.

5. Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu zimejitokeza changamoto nyingi katika sekta hii ya uwindaji ikiwemo muda

¹ Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhii Maliasili na utalii

uliotolewa kwa uwindaji kupunguzwa kutoka miaka mitano mpaka miaka miwili na kuleta sintofahamu kwa wadau, pamoja na jitihada nyingi zilizofanyika bado kuna changamoto nyingi ikiwemo vitalu vingi kukosa wamiliki na hivyo kupelekea vitalu hivyo kuvamiwa na wafugaji, wawindaji na majangili.

6. Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo Kambi Rasmi ya Upinzani inakemea tabia ya serikali kuendelea kukandamiza sekta binafsi kwa kufanya maamuzi ya kukurupuka bila kuwasikiliza au kushauriana na wadau wa sekta binafsi ili kuleta ufanisi na ushirikiano wa kibashara. Kambi Rasmi ya Upinzania inaitaka serikali itambue mchango mkubwa wa sekta binafsi katika maendeleo ya nchi yetu ikiwa ni pamoja na makusanyo ya kodi yanayotokana na sekta binafsi.

7. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kukaa upya na wamiliki wa vitalu pamoja na wadau wengine wanaojihusisha na biashara ya utalii na uwindaji ili kufikia maamuzi ya pamoja kwa kuangalia namna bora ya kufanya kazi na kutatua changamoto kubwa na masononeko mionganoni mwa wawekezaji katika sekta hii, ili kulinda sifa ya Tanzania iliyojijengea miaka ya nyuma katika soko la Kimataifa la Utalii.

8. Mheshimiwa Spika, biashara ya uwindaji imekuwa na changamoto nyingi sana zinazowakatisha tamaa wawekezaji. Ni biashara inayoelemewa na wingi wa kodi. Mfano, katika sekta hii ndogo ya Uwindaji kuna takribani tozo 21 za kodi kubwa kuachilia mbali zile za biashara ya utalii. Kodi zenyewe ni kama zifuatazo:

Jedwali 1: Mgao wa leseni, ada, kodi na tozo sekta ya uwindaji nchini

<i>Aina ya Kodi</i>	<i>Kiwango (USD)</i>	<i>Kiwango (TZS)</i>	<i>Muda</i>
Tala A	5,000	11,000,000	Kwa mwaka
Tala B	1,000	2,200,000	Mwindaji Mtaalamu (Professional Hunter-PH)kwa Mwaka
Leseni ya Biashara	3,000	6,600,000	Kwa mwaka
Leseni ya PH	3,000	6,600,000	Kwa Mwaka
Kibali cha kazi	1,000	2,200,000	Kwa Mwaka
Kibali cha Ukazi A	2,050	4,510,000	Kwa kichwa kwa mwaka
Kibali cha Ukazi B	3,050	6,710,000	Kwa kichwa kwa Mwaka
Leseni ya Kuwinda	4,600	10,120,000	Kwa leseni ya mteja kwa kichwa
Category 1	60,000	132,000,000	Kwa mwaka
Category 11	30,000	66,000,000	Kwa Mwaka
Category 111	18,000	39,000,000	Kwa Mwaka
Category 1V	10,000	22,000,000	Kwa Mwaka
Category V	5,000	11,000,000	Kwa Mwaka
Observer Tax	100	220,000	Kwa siku
Hunter Conservation Tax	150	330,000	Kwa siku
Rifle Import permits	120	264,000	Per firearm on application
Trophy handling fee	500	1,100,000	On application
Mchangwa kijamii	5,000	11,000,000	Kwa kitalu kwa mwaka (N lazima)
Maombi ya kitalu ya mara nyngine (renewal)	5,000	11,000,000	Kwa kitalu (Non- refundable)
Ada ya kuhamisha kitalu	50,000	110,000,000	Kwa kitalu
Maombi ya kuhamisha kitalu	5,000	11,000,000	Kwa kitalu

9. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuendelea kukaa na wadau hawa ili kujaribu kutatua changamoto hizo ambazo bado zinaikabili sekta hii ndogo ya uwindaji.

b) Biashara ya Usafirishaji Viumbe Hai Nje ya Nchi

10. Mheshimiwa Spika, tunakumbuka kwamba Machi, 2016 Serikali ilipiga marufuku usafirishaji wa viumbe hai nje ya nchi, ikitoa sababu kuwa inatengeneza mfumo ambao utaisaidia kudhibiti na kufuatilia kwa karibu biashara hiyo ya viumbe hai. Lakini katika upigaji marufuku huo Serikali haikutoa suluhu kwa wafanyabiashara ambao tayari walikuwa wameshakuwa na bidhaa hiyo tayari kwa usafirishaji na gharama za kuwatunza zitalipwa na nani.

11. Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa ahadi kwa wadau hao kwamba itarejesha tozo na gharama za wafanyabiashara wa viumbe hai ambao tayari walikwisha lipa ambazo hakutaja kiasi chake lakini ni mamilioni ya fedha, baada ya kumaliza zoezi la uhakiki. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata majibu ni kwa nini hasa maamuzi ambayo mara nyngi yanapochukuliwa Serikali ndiyo inapata hasara zaidi na pale wahusika wanashindwa kurejeshewa fedha zao kwa wakati ili waweze kuwekeza katika mambo mengine ya kuwaingizia kipato?

12. Mheshimiwa Spika, kwa taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akiongea na wadau wa biashara hiyo kwamba, Serikali imepoteza kiasi cha shilingi trilioni 2.5 kama mapato yatokanayo na biashara ya usafirishaji wa viumbe hai kwa kipindi cha miaka miwili.

13. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuta agizo lake la kuzuia biashara ya viumbe hai nje ya nchi na iwalipe fidia wafanyabiashara kwa hasara na usumbufu waliowasababishia wafanyabiashara hao.

III. MAMLAKA ZA HIFADHI

a) Shirika la Hifadhi za Taifa-TANAPA

14. Mheshimiwa Spika, taasisi za uhifadhi duniani hupatiwa ruzuku kutoka Serikali Kuu ili kujenga miundombinu na maendeleo mengine ya maeneo ya hifadhi, lakini kwetu sisi, TANAPA inajientesha bila ya kutegemea ruzuku na pia inalazimika kulipa kodi serikalini. Kutohana na mfumo wetu wa kodi ambao badala ya kuipa unaifuu TANAPA kutekeleza majukumu yake ya kimsingi unaifanya ishindwe kutimiza majukumu yake. Changamoto hizo za kikodi ni kama ifuatavyo:

Na.	%	Aina ya kodi inayodipwa
1.	30	Kod ya makampuni-Corporate tax
2	18	Kod ya Ongezekola thamani-Vat
3.	15	Gawila Serikali- Hitaji la kisheria
4.	3	Kod yamaendeleo ya ufundi-SDL
5.		Kod ya Stampkodi ya frodha (Import and excise duties)
6.		Kod kwamaendeleo ya jamii-CSR
7.		Kod inayotowa kwenye michango mbalimbali-Taxation on contribution

15. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa ni muda mwafaka sasa kuondoa au kupunguza viwango vya kodi za kisheria zinazopelekwa Serikalini, Bodii ya Utalii na taasisi za hifadhi na kodi inayokatwa kwenye michango inayogharamia miradi ya kijamii.

16. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Mkaguzi, TANAPA ilitoa kandarasi za miradi miwili mnamo tarehe 06 Mei, 2017 kwa mkandarasi JECCS Construction & Supplies Ltd na tarehe 09 Februari, 2017 na Mkandarasi Secao Builder Co Ltd. Gharama ya mikataba yote miwili ilikuwa ni shilingi milioni 961. Kipindi cha mikataba kwa miradi hii miwili kilimalizika tarehe 17 Februari, 2018 na 10 Oktoba 2017, mtawalia. Hata hivyo, hadi Februari 2019 yapata mwaka mmoja (1) kutoka tarehe iliyopangwa kukamilika, miradi hiyo haikuwa imekamilika. Ujenzi miradi yote miwili bado hadi sasa hajakamilika. Kadhalika, muda wa nyongeza pia ulikuwa umekwisha tangu tarehe 05 Novemba, 2018. Hakukuwa

na juhudzi zozote zilizofanywa na TANAPA ili kuhakikisha miradi hii inakamilika.

17. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kutupa utekelezaji wa miradi hiyo na hatua ambazo zimeshachukuliwa kwa Mkandarasi huyo.

b) **Mradi wa KFW - Serengeti**

18. Mheshimiwa Spika, Tarehe 16 Desemba, 2013, Tanzania kupitia Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), iliingia makubaliano ya kifedha na *KFW* na *Frankfurt Zoology Society* kwa ajili ya kuendeleza mazingira katika mbuga ya Serengeti na Ngorongoro. Gharama za mradi zilikadiriwa kuwa *EUR* za Ulaya milioni 24.12. *KFW* ilikubali kufadhili *EUR* za Ulaya milioni 20.5, wakati *Frankfurt Zoological Society* (FZS) ilikubali kufadhili *EUR* za Ulaya milioni 1, na zillizobaki *EUR* za Ulaya milioni 2.62 zifadhiliwe na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania. Muda wa mradi ulikadiriwa kuwa miaka mitano kutoka tarehe 11 Julai 2014.

19. Mheshimiwa Spika, Fedha hizi zilitarajia kujenga nyumba za watumishi, vituo vya watalii, mifereji ya maji, kuanzisha mpango wa matumizi ya ardhi vijijiini, kurasimisha matumizi ya ardhi, kuanzisha mpango wa matumizi bora ya mali kwenye kanda, na kuanzisha jamii ya Wanyama pori na usimamizi bora wa misitu.

20. Mheshimiwa Spika, Pia, fedha hizo zilitarajia kujenga barabara za kimkakati za vijiji vya wilaya ya Serengeti na Ngorongoro, kusaidia mbuga ya Serengeti, programu ya kugawana faida na kusaidiwa jamii za vijijiini na kujenga miundombinu ya kiuchumi na kijamii. Walikubaliana kuwa kodi zote za serikali na tozo zingine zitagharamiwa na Serikali au Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania, na KFW ina haki ya kukataa kutoa fedha baada ya 30 Juni, 2018 kama ilivyoonyeshwa kwenye mkataba wa makubaliano.

21. Mheshimiwa Spika, Mpaka kufikia Januari, 2019, miaka minne baadaye toka kuanza kwa mkataba tarehe 11 Julai,

2014 hamna kilichofanyika. Sababu za kuchelewa ni kwamba vitu vyatya ujenzi vilitakiwa visamehewe kodi wakati wa kuviingiza nchini kutoka nje. Hata hivyo, mpaka wakati wa ukaguzi Januari 2019, msamaha wa kodi ulikuwa haujakamilika.

22. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa Tanzania tunapoteza fursa nyngi kutoptana na kuwapa uongozi/madaraka watendaji wasiokuwa na uwezo wa kibashara na matokeo yake wao wanaangalia kidogo kilichopo lakini hawaoni kikubwa zaidi kinachokuja kesho au keshokutwa. Hili ni tatizo kubwa la watendaji wetu wa taasisi zinazohusika na utoaji wa vibali na ukusanyaji wa mapato. Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuzingatia uweledi na uwezo wa watendaji/wataalam wanaopewa majukumu ya kaliba hii ili kutuvusha dimbwi la umaskini linalotukabili.

c) Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro

23. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro ni moja ya kivutio cha kimataifa katika utalii kutoptana na binadamu kuishi pamoja na wanyama, hata hivyo kivutio hiki kiko kwenye hatari ya uharibifu wa mazingira kama hatua stahiki hazitachukuliwa kunusuru bonde mfano:-

- Kuongezeka kwa makazi ya binadamu ndani ya bonde hilo
- Kuongezeka kwa idadi ya mifugo
- Uvamizi na ukataji wa miti
- Kuzuiwa kwa njia za asili za wanyama
- Kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu
- Mahusiano mabaya kati ya jamii na watumishi wa hifadhi ya Ngorongoro.

24. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka serikali kuchukua hatua stahiki katika kunusuru hifadhi hii ya Bonde la Ngorongoro. Matumizi mabaya ya pesa katika Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro. Bodi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro ilifanya jumla ya vikao 20 na semina 6 kwa mwaka wa fedha 2017/18, ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.10 (1,102, 907,602) zilitumika kama ilivyoainishwa hapa chini:

Mchanganuo wa gharama za vikao ulikuwa ni kama ifuatavyo:

- Posho ya kujikimu shilingi 799,906,220.00
- Hela kwa ajili ya mafuta shilingi 81,225,678.00
- Gharama za ukumbi shilingi 29,320,800.00
- Chakula na viburudisho shilingi 34,449,834.00
- Malazi shilingi 57,459,684 .00
- Gharama nyingine za usafiri shilingi 100,545,386.00

25. Mheshimiwa Spika, matumizi ya namna hii ya kuwakirimu wajumbe wa bodi, inaweza ikaleta tafsiri kuwa lengo la menejimenti ni kuwaghiribu wajumbe wa bodi ili ishindwe kufanya/kutekeleza jukumu lake la msingi la kuisimamia menejimenti hiyo. Kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona litakuwa ni jambo la busara Waziri kuilekeza Bodi ya Bonde la Ngorongoro kujitathmini na kuona kama bado inao uhalali wa kuendelea kuisimamia menejimenti.

d) Utalii katika Fukwe za Bahari

26. Mheshimiwa Spika, utalii wa fukwe ni mojawapo ya kivutio kikubwa sana kwa watalii ambao wengi wao wanatoka katika mataifa ambayo hayakupata bahati kuwa na fukwe, au kutokana na kubadilika sana kwa misimu ya majira ya mwaka.

27. Mheshimiwa Spika, katika hilo kuna visiwa ambavyo vinakodishwa na kumilikiwa na watu binafsi, moja ya visiwa hivyo ni kisiwa cha Shungumbili ambacho kwa sasa kinaitwa Thanda Island ambacho ni sehemu ya kisiwa kilicho ndani ya kisiwa kinachoitwa Nyororo, vyote vikiwa katika Wilaya ya Mafia/Kisiwa cha Mafia. Kwa bahati mbaya sana kisiwa hiki cha Shungumbili au Thanda Island ambacho ni Private Island kina hotel ambayo ni ghali kuliko hotel yoyote ile Duniani, kwani kulala kwa siku ni dola za kimarekani 25,000. Mtu kukaa hapo ni lazima ucae kuanzia siku saba, jaribu kufikiria kwa mwaka kisiwa hicho au vingine kama vile visiwa vya;

- i. Lupita (kilichopo Ziwa Tanganyika)
- ii. Shungumbili/Thanda (Mafia)

- iii. Mnemba (Zanzibar)*
- iv. Funjove*
- v. Bawe (Zanzibar)*
- vi. Changuu (Zanzibar)*
- vii. Chumbe Island (Zanzibar)*

28. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kusema kuwa katika records za Wizara imeshindwa kupata taarifa za kisiwa hiki cha Shungumbili, na badala yake taarifa zake zinapatikana kutoka “*the US military intelligence*”, maana yake ni kwamba chochote kinachoendelea kwenye visiwa hivyo vya binafsi Serikali haina taarifa. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuleta taarifa rasmi za visiwa hivyo vinavyomilikiwa na watu binafsi ili kuwa na taarifa kuhusu watalii wanaoingia katika nchi hii.

e) **Mradi wa Theme Park Jijini Dar es Salaam**

29. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 serikali ilitenga kiasi cha shilingi 250,000,000 (mil 250) kwa ajili ya upembusi yakinifu ili kufanya Mji wa Dar es Salaam kuwa Mji wa kitalii. Katika hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa mwaka wa fedha 2016/2017 iliishauri serikali kutenga eneo la Msitu wa Pande kuwa sehemu ya Bustani ya Wanyamapori ili kupunguza gharama za kujenga eneo jingine litakaloweza kushabihiana na mazingira ya kuishi wanyama ikiwa ni pamoja na eneo la mazalia ya wanyamapori ndani ya Jiji la Dar es Salaam. Kwa mwaka wa fedha 2018/19 mradi huu ilitengewa jumla ya shilingi milioni 500. Lakini hadi mwezi Februari 2019 hakuna hata senti iliyotolewa, na kwa mwaka wa fedha 2019/20 hakuna hata shilingi iliyotengwa kwa ajili ya mradi huu.

30. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuhakikisha inatoa fedha zilizotengwa, badala ya mfumo wa sasa unaotumiwa na baadhi ya wanasiwa wa kufanya matumizi ambayo hayajatengwa wala kuidhinishwa na Bunge jambo ambalo ni kinyume cha Sheria ya Bajeti. Pamoja na hilo Kambi Rasmi inataka kujua uwepo wa taarifa ya mabasi yaliyonunuliwa kwa ajili ya kutoa

huduma za kutembeza watalii katika vivutio mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam? Je, mabasi hayo yaliyonunuliwa ni sehemu ya mradi huu? Je, gharama yake ni shilingi ngapi? Na Je, mabasi hayo ni mangapi?

IV. MWENENDO WA SEKTA YA UTALII NCHINI

31. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa utalii ni hatua ya kujenga uchumi wa Tanzania kutokana na nchi kuwa na vivutio vya asili, utamaduni na kuwa kwenye jiografia ya kimkakati na hivyo kuwa na manufaa makubwa hata katika sekta nyingine za uchumi. Utalii unapanua fursa za ajira zenye kipato cha moja kwa moja au kwa shughuli nyingine zinazofungamana na utalii. Ili kufikia sekta ya utalii kuwa ya manufaa kwa nchi, ushirikishwaji wa sekta binafsi kutasaidia sana katika ujenzi wa miundombinu ya utalii wa klimataifa kwenye maeneo ya bahari, maziwa na misitu. Hivyo utalii utaboresha soko la bidhaa zinazozalishwa nchini, *rejea kitabu cha sera cha Chadema uk. 24 na 25.*

a) Idadi ya Watalii Tanzania Bara na Zanzibar

32. Mheshimiwa Spika, kumekuwa na sintofahamu juu ya takwimu zinazotolewa juu ya idadi ya watalii wanaoingia nchini. Sintofahamu hii inatokana na idadi ya watalii ambayo imekuwa ikiripotiwa kwenye hotuba mbalimbali ikiwemo Randama ya Wizara Fungu 69. Katika Randama inazoonyesha kuwa kwa mwaka 2016 watalii walioingia nchini walikuwa 1,284,279 na kwa mwaka 2017 walikuwa ni takribani watalii 1,327,143 na kwa mwaka 2018 kufikia 1,494,596. Ripoti hizi zimebainisha kuwa watalii hao waliokuja kutembelea Hifadhi za Taifa, Mamlaka za Hifadhi za Ngorongoro na Zanzibar. Hii ina maana kwamba watalii walioingia kutoa Zanzibar nao wamejumuishwa katika idadi ya watalii wote walioingia nchini kwa mujibu wa maelezo ya Randama.

33. Mheshimiwa Spika sote tunatambua kuwa masuala ya sekta ya utalii sio masuala ya Muungano. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ituambie ni lini hasa imeamua mambo ya utalii kuwa sehemu ya Muungano pia tunaitaka

serikali itupe takwimu sahihi za watalii wanaoingia nchini kwa maana ya Tanzania Bara.

34. Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano, katika kuhakikisha sekta ya utalii inakuwa endelevu na yenye tija kwa taifa, ikiwa ni pamoja na kuongeza namba ya watalii wanaoingia Tanzania kutoka 1,200,000 mwaka 2016/17 hadi 2,000,000 ifikapo mwaka 2020. Kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ya Utalii na Wanyama Pori ya Kenya, juu ya utendaji wa sekta ya Utalii iliyotolewa mwaka 2018 ni kuwa nchi hiyo kwa mwaka 2017 iliingiza watalii 1,474,671 na mwaka 2018 iliingiza watalii 2,025,206. Wakati huo huo vitanda kwa ajili ya watalii vikiongezeka kufikia milioni 4.05 mwaka 2018 kulinganisha na milioni 3.5 mwaka 2016.

35. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka serikali badala ya kutafuta mchawi itafakari takwimu hizi za washindani wetu na tuje na mkakati wa kuboresha sekta ya utalii katika karne ya 21 ili tuweze kushindana na jirani zetu kwa kuongeza idadi ya watalii na fedha za kigeni.

b) Demokrasia na Ukuaji wa Sekta ya Utalii

36. Mheshimiwa Spika, Katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ya mwaka 2016/2017 ilitolea mfano wa nchi ya Sri Lanka. Katika gazeti la New York Times, nchi kama Sri Lanka iliwahi kupata hadhi ya kujulikana kama nchi ya kwanza duniani kwa kivutio cha watalii. Lakini kukandamizwa kwa demokrasia na misukosuko ya kisiasa nchini Sri Lanka kama inavyotokea Tanzania leo ilipelekeea utalii wa nchi hiyo kushuka kwa kasi ya asilimia 43 ndani ya kipindi cha mwaka mmoja na hivyo kuanguka kabisa kwa uchumi wa nchi hiyo. Hivyo, kuanza kususua kwa sekta hii ya utalii ni dalili mbaya na isipoangaliwa inaweza kutupeleka katika kile kilichotokea Sri Lanka.

37. Mheshimiwa Spika, katika taarifa za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambayo imetolea mfano wa nchi kama Botswana ambayo imekuwa na tozo la VAT

katika huduma za kitalii kwa sasa wameongeza VAT kutoka 14% kwenda 15% kama mfano wa nchi Barani Afrika zenyе mfumo wa VAT, ni vyema serikali hii ikatambua kuwa pamoja na tozo ya VAT kwenye utalii nchini Botswana bado kiwango hicho haijafikia ukubwa wa tozo kama tozo ya 18% kama ilivyo kwa Tanzania kwa sasa. Vilevile, ikumbukwe kuwa nchi ya Botswana imepunguza mrundikano wa kodi tofauti na Tanzania yenye takribani kodi 36 kwenye sekta ya utalii pekee. Ikiwa ndio nchi inayoongoza kwa wingi wa kodi katika biashara ya utalii Afrika ya Mashariki. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kurejea tozo hii ya VAT kwenye huduma za utalii

c) Sheria Zinazoendesha Sekta ya Maliasili na Utalii

38. Mheshimiwa Spika, Sera haiwezi kusimama peke yake wakati inatungwa, ni lazima langalle sera zingine zinasemaje ili kuondoa mwingiliano wa kiutendaji katika kufikia malengo ya sera. Vivo hivyo pia katika utunzi wa sheria, na sheria nzuri inayotoa matunda bora ni lazima vitu vyote vimalizikie kwenye ofisi moja, *“one stop center”*.

39. Mheshimiwa Spika, katika sekta ya maliasili na utalii inaongozwa na sheria na kanuni zipatazo 13, na vyote hivi vinafanyakazi kwa wakati mmoja na mdau wa utalii ni lazima aendane na matakwa ya sheria hizo na kanuni zake. Uwepo wa sheria na kanuni zipatazo 13 umepelekea ukiritimba uliopitiliza. Mbali ya ukiritimba pia vifungu vyya sheria hizo vinakinzana na hivyo kusababisha wadau wa utalii kushindwa kufikia malengo yao.

40. Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa sheria hizo ambazo vifungu vyake vinakinzana sana na kuleta sintofahamu ni sheria ya ardhi ya vijiji namba 5 ya mwaka 1999 na Sheria ya Wanyamapor namba 5 ya mwaka 2009; kanuni na sheria ya wanyamapor (Wildlife Corridors, Dispersal Area, Buffer Zones and Migratory Routes Regulations 2018) na sheria ya ardhi ya vijiji namba 5 ya mwaka 1999); Kanuni na sheria ya wanyamapor za mwaka 2018 na sheria ya wanyamapor namba 5 ya mwaka 2009; Sheria ya Nyanda za Malisho ya

mwaka 2010 na Sheria ya Wanyamapor ya mwaka 2009. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kwamba, sheria na kanuni zote zinazokinzana ili kuleta utengamano mzuri wa kisheria kwa manufaa na maendeleo ya sekta nzima ya maliasili na utalii.

V. MIGOGORO SUGU BAINA YA SERIKALI NA WANANCHI WANAOISHI KANDO YA HIFADHI

41. Mheshimiwa Spika, tumekuwa na tatizo sugu la migogoro baina ya serikali na wananchi wanaoishi kando kando ya hifadhi kwa muda mrefu sasa. Pamoja na jitihada mbalimbali za kuizungumzia na kushauri hatua stahiki za kuitatua bado hali inaonyesha migogoro hii imekuwa na nguvu kubwa kuliko uwezo wa serikali kuitatua.

42. Mheshimiwa Spika, migogoro hii imedumu muda mrefu ambapo imegharimu maisha ya wananchi wengi, tumeopoteza wanyama ambao ndio fahari yetu na chanzo cha mapato, migogoro hii imesababisha kuenea kwa magonjwa yanayosababishwa na wanyamapor, mifugo na hivyo kuathiri afya za binadamu na wanyama wa kufugwa na wale wa porini. **Mheshimiwa Spika**, Mifano iliyotolewa ni pamoja na maeneo ya Wilaya ya Bunda yanayopanaka na Pori la Akiba la Grumeti, Vijiji vya Kegonga na Masanga, pia maeneo ya Ulanga Vijiji vya Iputi na Lupiro yakiwa ni baadhi tu ya maeneo ambayo migogoro imesababishwa na Mamlaka za Wanyamapor.

43. Mheshimiwa Spika, serikali imekuwa ikiwakumbatia baadhi ya wawekezaji ambao wamekuwa chanzo au sehemu ya migogoro sugu ya wanavijiji wanaoishi maeneo ya hifadhi. Mfano, katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilizungumzia kwa kina sana historia ya mgogoro wa Loliondo uliyodumu kwa takribani miaka 26. Mgogoro huu uliwahi kuundiwa kamati mbalimbali ili kutafuta suluhu lakinii mpaka leo serikali imegoma kurudisha mrejesho kwa wananchi kujua kinagaubaga na hatua mahususi zilizopendekezwa. Ni wazi kuwa migogoro mingi imeendelea kuwepo kutokana na ripoti nyingi kuwa za siri

na wananchi kutoshirikishwa ipasavyo katika maamuzi. Jamii pia inapaswa kujua mambo yaliyo katika ripoti hizo na hatua stahiki zitakazochukuliwa. Mara nyingi tumeshuhudia ripoti nyingi zikiwa zimeghubikwa na usiri mkubwa na hivyo kuwanyima wananchi fursa ya kujua yale yaliyo ndani ya ripoti hizo za kamati huku fedha nyingi zikitumika katika uchunguzi.

44. Mheshimiwa Spika ripoti hufanywa kuwa mali ya watu wachache badala ya mali ya umma. Mfano, katika ripoti mbalimbali za serikali, mashirika na taasisi binafsi pamoja na hotuba mbalimbali za Kambi Rasmi ya Upinzani zimezungumzia kwa kina watuhumiwa wakubwa wa mgogoro wa Loliondo ambapo Kampuni ya Otterlo Business Corporation (OBC) ambayo imetuhumiwa kwa muda mrefu kuwa sehemu kubwa ya chanzo cha mgogoro katika Bonde Tengefu la Loliondo mpaka sasa haijatataliwa kutohana na wananchi wa maeneo hayo kutoridhishwa. Kampuni ya Greenmile Co.Ltd imekuwa na kashfa nyingi na kuwa sehemu ya migogoro, kampuni ya Thomson Safaris imekuwa ikituhumiwa kama sehemu kuu ya mgogoro katika vijiji vilivyo ndani ya hifadhi ya Serengeti n.k.

45. Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza bado serikali hajjaweza kuziwajibisha kampuni hizi. Hii ni mifano midogo tu kati ya migogoro mingi inayoendelea nchini ambapo serikali imeshindwa kuja na majibu na mikakati ya kudumu jambo ambalo linazua shaka kubwa na ari ya kutaka kujua ni nani hasa mnufaika wa migogoro ya namna hii? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuhakikisha inaweka wazi ripoti zote za Kamati Maalum za zilizowahi kushughulikia migogoro hii, ili kutoa fursa kwa wawakilishi wa wananchi kujadili kwa uwazi ripoti hizo na hata kutoa mapendekezo.

VI. UHARIBIFU WA MAZINGIRA KATIKA HIFADHI

46. Mheshimiwa Spika, suala la utunzaji wa mazingira ni muhimu sana kwa ikolojia ya misitu, bahari, mbuga zetu kwani uwepo wa maji, hali nzuri ya hewa na udongo vinapelekea mimea na wanyama kuzaliana na kuwa katika hali bora zaidi.

47. Mheshimiwa Spika, Kilombero and *Lower Rufiji Wetlands Ecosystem Management* mradi namba 4809 ambao ni mradi wa kuendeleza ekolojia ya ardhi oevu ya bonde la Kilombero na Mto Rufiji, ambao unaendelezwa kwa pamoja kati ya Tanzania na Ubelgiji. Kwa mwaka wa fedha 2018/19 ulitengewa jumla ya shilingi 1,494,193,471. Lakini hadi mwezi Februari 2019 hakuna hata shilingi moja ambayo ilikuwa imekwenda katika mradi huo.

48. Mheshimiwa Spika, umuhimu wa ekolojia ya Bonde la Kilombero na Mto Rufiji ni muhimu sana kwa sasa kutokana na ukweli kwamba utekelezwaji wa mradi wa ufuaji wa umeme ni kuwa utaleta hasara kwa mazingira kwa kusababisha uharibifu mkubwa wa misitu na hivyo kuondoa mazalia ya wanyama na ndege wengi ambao walikuwa wanaleta utofauti mkubwa na wa kipekee wa mbuga ya Selous.

49. Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha na fedheha kubwa kwa serikali hii ya awamu ya tano kuwa mstari wa mbele katika kuyafuta yale mazuri tuliyoyaridhia kama taifa ili kulinda mazingira ya sasa na ya vizazi vijavyo. Nayasema haya kwa kuwa serikali hii ya awamu ya tano mapema mwaka jana ilifanya upembuzi katika kile walichokisema ni mpango wa serikali wa kuanzisha mradi mkubwa wa kuzalisha nishati ya umeme yaani Stiegler's Gorge katika pori la akiba la Selous kwa bei nafuu.

50. Mheshimiwa Spika, hakuna mtu yoyote mwenye akili timamu asijejuwa umuhimu wa Pori la Akiba la Selous na umuhimu wa kuilinda kwa vivu mkubwa ikolojia ya eneo hilo ambalo kwa kupitia Mto Rufiji imekuwa ni chanzo kikubwa cha maji yanayotegemewa na binadamu, mimea, wanyamapor, samaki na mifugo. Pamoja na serikali kusema imefanya upembuzi yakinifu, ni vyema ikaamua kufanya mkakati wa tathimini ya mazingira kwa miaka mingi ijayo.

51. Mheshimiwa Spika, endapo chanzo hiki cha maji kitaharibiwa basi tujue hata umeme unaotaka kuzalishwa hautakuwa endelevu kwa miaka mingi ijayo. Tunatambua

umuhimu mkubwa wa upatikaji wa nishati ya umeme nchini, lakini serikali hii ya awamu ya tano itambue umuhimu mkubwa wa kuhifadhi vyanzo vya maji hususani chanzo hiki muhimu kwani bila maji hakuna uhai, bila maji hakuna umeme, bila maji hakuna chakula.

52. Mheshimiwa Spika, bado nchi yetu ina namna nyingi ya kuzalisha umeme katika maeneo mengi ambayo athari zake za kimazingira sio makubwa kama itakavyotokea kwenye chanzo hiki cha mto Rufiji. Pori la Akiba la Selous limekuwa chanzo kikubwa cha mapato ya wananchi na ajira kutokana na utalii wa Southern Circuit. Mpaka sasa Pori hili limeorodheshwa katika maliasili zilizo hatarini kupotea kwa mujibu wa Mkataba wa Urithi wa Dunia kutokana na kuongezeka kwa mauaji ya tembo na kuharibika kwa mapitio ya wanyama. Na endapo mradi huu utalazimishwa kufanyaika basi tutambue athari kubwa ya kimazingira huko mbeleni na pengine kutoweka kabisa kwa pori hili kwani uendeshaji wa mitambo hiyo ya umeme unaotumia maji husababisha joto la maji jambo ambalo ni hatari kwa baionuai.

53. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuangalia upya mikakati ya kimazingira ya muda mrefu kabla ya kuanza kwa mradi huu. Serikali ikumbuke makosa makubwa iliyofanya katika kujenga mradi wa stesheni ya mabasi yaendayo kwa kasi (DART) ambao kwa sasa inaigharimu serikali kutokana tu na kufanya miradi ya namna hii bila kuangalia athari za muda mrefu za kimazingira.

54. Mheshimiwa Spika, kauli ya Mheshimiwa Rais kuhusu kuwaacha wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi kama walikuwa wanafanya shughuli zao za kutafuta riziki kuendelea kufanya hivyo na wasisumbuliwe, je, kauli hiyo ya Mheshimiwa Rais hadi sasa Wizara imeishaiwekea utaratibu gani wa kuitekeleza ili iwe ya kisheria badala ya kuwa kauli ya kisiasa kama kauli zingine zinazoongewa katika harakati za kutafuta kuungwa mkono na kundi fulani katika jamii?

VII. MISITU NA NYUKI

55. Mheshimiwa Spika, sekta ya ufugaji wa nyuki imekuwa haifanyi vizuri kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo kutokupewa kipaumbele ipasavyo. Miradi mingi inayoanzishwa na serikali imekuwa haifanyi vizuri na mingi imeshindwa kuendelea kutokana na utunzaji mbovu na kutofuatilia mara kwa mara.

56. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya CAG 2016/2017 serikali ilitoa kiasi cha shilingi 104,072,000 (mil. 104) kwa wafugaji 7 kwa kipindi cha miaka miwili lakini cha kushangaza mizinga mingi haina nyuki na miradi hiyo imesimama. Mfano, katika mizinga 150 iliyowekwa Manispaa ya Dodoma ni mizinga 7 tu yenyе nyuki, katika Halmashauri ya Kishapu mizinga 150 imewekwa mahali ambapo sio mazingira sahihi kwa mazalia ya nyuki na hivyo hakuna nyuki. Mradi huu wa Kishapu umegharimu takribani milioni 40. Katika Halmashauri ya Misungwi kati ya mizinga 150 ni mizinga 14 tu ndio ilikuwa na nyuki kwa kipindi cha miaka miwili hivyo mizinga 136 haikuwa na nyuki huku mradi ukigharimu takribani shilingi milioni 20. Hii ni baadhi tu ya mifano mingine mingi ambapo fedha nyingi hutumika huku matokeo yakikosa tija kabisa.

57. Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inataka kujuu ni hatua gani stahiki zimechukuliwa kwa uzembe huu mkubwa wa upotevu wa fedha za umma katika miradi inayogharimu mamilioni bila kuwa na faida yoyote.

58. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/19 idara iliomba fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi minne na mwaka wa fedha 2019/20 miradi hiyo hiyo inaombewa fedha, ambayo ni; *i. mradi wa misitu asili* uliomba kutekelezwa kwa shilingi 1,364,097,000.00 lakini hadi mwezi februari, 2019 shilingi 100,100,000.00 ndizo zilizokuwa zimetolewa. Kwa mwaka wa fedha 2019/20 mradi unaombewa jumla ya shilingi 3,136,480,000.00 fedha za nje. *ii. Mradi kuendeleza misitu* na ufugaji wa nyuki unaombewa shilingi 200,000,000.00 fedha za ndani. *iii. mradi wa kuongeza thamani* kwa mazao ya misitu 2019/20 unaombewa shilingi 4,742,850,000.00. kwa mwaka

2018/19 ziliidhinishwa shilingi 5,950,860,993.00 lakini hadi mwezi februari, 2019 zilipokelewa shilingi 868,341,377.00 tu sawa na asilimia 14.59 na hizi zote ni fedha za nje.

VIII. UTEKELEZAJI WA BAJET 2018/19 NA MPANGO WA MAENDELEO 2019/2020

59. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 sekta ya utalii ilichangia 17.5% ya Pato la Taifa (GDP) na takribani 25% ya fedha za kigeni (foreign currency). Hii ikiwa ni katи ya sekta tano muhimu zinazichangia zaidi katika pato la taifa.

60. Mheshimiwa Spika, takwimu za serikali zinaonyesha sekta hii ya utalii hutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 500,000 na zisizo za moja kwa moja 1,000,000². Pamoja na hilo, sekta hii ya utalii imekuwa ikichangia katika kukuza kipato cha wananchi mmoja mmoja kutokana na manunuzi ya bidhaa katika hoteli zikiwemo vyakula, huduma za samani, vifaa vya ujenzi na malazi.

61. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuona umuhimu huu wa sekta ya utalii na mifano ya nchi mbalimbali wanavyonufaika katika utalii wa aina tofauti tofauti bado hapa nchini kwenye sekta hii imekuwa ikisuasua na kutegemea wahisani katika miradi mbalimbali ya maendeleo hususani World Bank, WWF, Belgium, German, Norway na Finland.

62. Mheshimiwa Spika, katika kuonesha kuwa Serikali haipo makini katika kuinua uchumi wa nchi, kwa kutumia sekta hii ya utalii ili kuingizia fedha nyngi za kigeni na kuzalisha ajira nyngi. Mwaka wa fedha 2018/19 zilitengwa jumla ya shilingi 7,330,006,404 kwa ajili ya matumizi ya idara, bodi ya utalii na wakala wa chuo cha Taifa cha utalii lakini hadi mwezi Februari 2019 zilitolewa jumla ya shilingi 3,615,157,217.01 ambazo ni sawa na asilimia 50.68

² Rejea Randama ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2017/2018

63. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Randama ya Wizara Fungu 69 ya mwaka 2016/2017 fedha za miradi ya Maendeleo zilijumuisha shilingi 15,746,682,000 fedha za ndani na shilingi 2,000,000,000 fedha za nje. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 fedha za ndani zilizotolewa zilikuwa shilingi 11,353,250,489 na fedha za nje ni shilingi 16,593,530,813 hii ikiwa na maana fedha za ndani zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zinapungua.

64. Mheshimiwa Spika, makadirio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 zilitengwa shilingi 29,978,082,000 kati ya fedha hizo za ndani ni shilingi 3,000,000,000 na fedha za nje ni shilingi 26,978,082,000 ambazo ni sawa na asilimia 89.99 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo. Hadi kufika mwezi Februari 2019 fedha zilizopokelewa ni shilingi 10,551,289,825 fedha za nje na sawa na asilimia 35 ya fedha zote za wizara, kwa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Hakuna hata shilingi moja ya fedha za ndani zilizotolewa kwa ajili ya kuendeleza sekta ya utalii hadi mwezi februari.

65. Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2019/20 Wizara imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 48.9 ili kutekeleza miradi minane ya maendeleo, kati ya fedha hizo fedha za ndani ni shilingi bilioni moja tu na fedha za nje ni shilingi bilioni 47.9

66. Mheshimiwa Spika, hili ni tishio kubwa kwa Wizara kwani kuzidi kutegemea misaada kutoka kwa wahisani hakuwezi kamwe kunyanya sekta hii. Hii inaonesha kuwa bado serikali hajakubali kuwekeza ipasavyo kaika sekta hii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali ione umuhimu wa kuwekeza katika sekta hii nyeti ambayo inauwezo wa kutoa ajira zaidi, kuongeza pato la Taifa na fedha kuongeza fedha za kigeni.

IX. HITIMISHO

67. Mheshimiwa Spika, nashauri sote tutafute makala ilioandikwa na Yende Nsizwazonke kutoka Afrika Kusini inayosema "*Natural resources: Are we blessed with a curse*

or cursed with a blessings?" Maneno haya mazito yanaonyesha dhahiri tunahitaji taasisi imara (*strong institutions*) ambapo mifumo ya utendaji kazi ndani ya Wizara inakuwa imara katika utendaji na sio kila wakati anapopewa nafasi kiongozi fulani hubadili sera na taratibu kwa kufuata matakwa yake binafsi. Kujenga taasisi zenyе mifumo imara itasaidia kuvutia wawekezaji wengi zaidi, itapanua soko la utalii ndani na nje ya nchi, mapato ya ndani yataongezeka na hivyo tutakuwa tumepanua wigo wa fedha nyngi zaidi katika miradi ya maendeleo nchini.

68. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani naomba kuwasilisha.

.....
Mch. Peter Simon Msigwa (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

23/05/2019

MWENYEKITI: Ahsante waheshimiwa muda wetu umekwisha hatutakuwa na mchangiaji yejote asubuhi hii tutaanza kuchangia jioni ya leo na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mchungaji Peter Msigwa, wa pili Lucy Owenya, na watatu Benadetha Mshashi. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10:00 jioni.

(Saa 7:00 mchana Bunge lilitishwa hadi saa 10:00 jioni!)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilitrudia)

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka
wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Tukae. Asubuhi nilimtaja Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Owenya na Mheshimiwa Mushashu. Tunaanza na Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Mbele yetu ni Wizara nyeti katika Taifa letu na hasa katika shughuli nzima za kluchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni kama kufanya *business*. Na ili ku-*operate business* kubwa lazima uwe na *investiment* kubwa, kuwe na *brain* kubwa ambayo unaiweka katika *business* unayotaka kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sana nimekuwa Mbunge sasa wa miaka tisa, lakini katika Wizara hii imekuwa ni kutatua migogoro ya Loliondo na wafugaji, kutatua migogoro ya watu wa Ngorongoro na wafugaji, kutatua migogoro ya TANAPA na wananchi, mipaka ni tatizo. Imekuwa ni kutatua migogoro ya maeneo chepechepe, kwa mfano kule Kilombero, Ihefu na wananchi. Kwa hiyo, badala ya kufanya *business* tunajikuta kama Taifa tuko *busy* kutatua migogoro badala ya kusonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni wakati muafaka kama Serikali tufike mahali tuseme *enough is enough*, tufanye biashara inayotokana na Wizara hii, kwa sababu, migogoro imekuwa mingi hatutoi suluhisho la kudumu katika masuala ya mipaka, kwenye maeneo oevu, kwenye maeneo ya hifadhi, hatujatoa suluhisho la kudumu. Hatuwezi kuendelea kama tunaendelea kukaa chini na kutatua migogoro badala ya kufanya *business* na kushindana kimataifa namna gani tuweze kufanya hii biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo napenda nizungumze kwa upana sana eneo moja. Kumekuwa na biashara ya viumbe hai, wanyama hai ambao wamekuwa wakisafirishwa. Biashara hii imekuwa ikifanywa toka wakati wa mkoloni na wakati wa mkoloni ni wazungu tu walikuwa wanasafrisha, mpaka mwaka 1974 ikabadilishwa wakawa wanafanya wazawa peke yao. Sasa kwa bahati mbaya sana hawa watu wamefanya biashara na wamefanya kwa mujibu wa sheria, lakini kama hotuba yetu ilivyosema ghafla wakati wa Mheshimiwa Maghembe biashara hii ilisitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilisitishwa wakati watu hawa wameshafanya maandalizi, wamekamata wanyama wamewaweka kwenye *holding grounds*, wamekopa mikopo, wamefanya *contact* na wateja wao duniani kote, ikaja hii biashara ghafla ikasitishwa. Watu hawa hii biashara hawafanyi wanyama ambao wako kwenye *National Parks*, kwenye *Game Reserves*, wanafanya biashara ya huku porini ambako kuna nyani, kuna ngedere, kuna *spiders*, kuna konokono na nyoka na mijusi, vitu ambavyo havitumiki kwa biashara nyingine katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa watu baada ya Serikali kusitisha wameingia katika umasikini mkubwa sana, wengine mpaka juzi nimesikia wamekufa. Ningombala Mheshimiwa Waziri hebu tutoe jibu kwa hawa watu ni kwa namna gani tutawalipa fidia, hawa ni Watanzania. Ukiangalia biashara hii illikuwa inaongeza pato la Taifa, fedha yake inayotumika asilimia 100 Serikali haiingii hasara na tunapata fedha ya kigeni, hawa watu wamefanya kazi kubwa sana kulikuwa na wakamataji, kulikuwa na mahotelii, ikasitishwa na wengine mpaka walikuufa, wale watu waliopelekwa Mahakamani mpaka leo walishinda kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wameendelea kuwatesa, tumewa-*cripple*, ningombala Serikali itoe jibu lake; wametoa malalamiko kwako Waziri, Waziri aliyepita, wametoa kwa Rais, naomba hawa watu Mheshimiw Waziri awaangalie kwa jicho la huruma. Muda mwingi tumezungumza watu wengine sana, hawa ni wafanyabiashara wadogo wadogo na ni Watanzania wazawa ambao walikuwa wanajitahidi kujitokeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi Serikali huwa inatumia pesa nyingi kuangamiza ndege kama kwelea kwelea. Kwa mfano kuna wakati waliuwa ndege karibu milioni 70, sasa unapoua wale ndege dawa zile wanaposhusha kuwaua wale ndege, dawa zile zinua na mijusi na hao nyoka ambao wale watu wangewasafirisha tukapata hela. Sasa haya ni mambo ambayo hebu tuangalie namna gani tunaweza tukafanya biashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza hapo mwanzoni hii biashara ni *business* na namshukuru Waziri ni mfanyakia biashara, lazima ana *business mind*. Wizara hii tukiichukulia kama Wizara nyingine bila kuwa na upeo wa kibashara hatuwezi kusonga mbele, hatuwezi kuingia kwenye ushindani, lazima kuwe na fikra za kibashara. Katika maeneo mengine Mheshimiwa Waziri amefanya vizuri, siwezi kumkandamiza katika kila eneo; alitoa kwa mfano ile *Tanzania Unforgetable*, nilitamani sana ingetumika hata wakati wa Timu yetu ya Taifa, *Tanzania Unforgetable*, kuliko ile tuliyotumia "Sasa hivi ni Zamu Yetu", tukienda nchi sasa hivi ni zamu yetu haiwezi kutusaidia, ingetusaidia kutangaza utalii, lakini tungelitumia hilo neno ni neno zuri ambalo linaitangaza nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo wamefanya vizuri ni kwenye masuala ya ujangili. Wizara imefanya vizuri, hatuwezi kuwalaumu, nimekuweko kwenye Wizara hii ujangili kweli umeporomoka, lazima tuwapongeze katika hilo; lakini ninachosema kwenye eneo hili la hawa watu amba wana shida, tumewatesa kiasi cha kutosha naomba Waziri atakaporudi atoe tamko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la sheria zinazokinzana; kuna sheria nyingi zinakinzana, Sheria za Ardh, Sheria za Mazingira, Sheria za Maliasili, zinakinzana maeneo mengi kiasi kwamba, hazitekelezeki, Sheria za Madini, kuna maeneo mengi ambayo hizi sheria zinakinzana kila eneo. Ningeomba hili suala limalizwe ili tuache kukaa muda wote tunagombana na kutatua migogoro, tuwe tunafanya biashara tunashindana na watu wengine duniani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *success is attracted, you don't pursue success*, ni lazima tutengeneze mazingira ambayo *yata-attract* mafanikio katika nchi yetu, lakini hatuwezi kutengeneza mazingira kama tuna watu wa aina ileile. Ili *tu-attract success* katika nchi yetu lazima tuwe na watu amba wanavutia hayo mafanikio. Ni sawa na mbegu ya mahindi, mbegu ya mahindi ukiweka kwenye simenti

haiwezi kuota mpaka uitengenezee mazingira uweke maji, uweke udongo mzuri, uweke mwanga na *oxygen*, hewa, maana ndio itaota. Sasa tukiwa na watu ambao hawafikiri kibashara, tukiwa na watu ambao hawafikiri Kitaifa, *we have to think globaly and act local*, lazima tubadili namna ya kufikiri katika namna nzima ya kuiendeleza Wizara hii ya Maliasili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Waziri, najua wamefanya kazi kwa sehemu ambayo wanaenda mbele, kwa mfano wamefungua *Television* ambayo inatangaza nchi yetu, tutakuwa hatufanyi vizuri kama tusiposema mambo haya, hayo ni mambo mazuri ambayo lazima tuyapongeze kwa sababu tunataka *attractwatalii* zaidi. Hata hivyo, bado tunahitaji urithi tulionao na *resources* tulizonazo, *it is highly time* kwamba, tuchague, ni kwa kiasi gani Ngorongoro inatusaidia na tuna falda nayo. Tuchukue maamuzi ambayo yatatufanya Ngorongoro itusaidie, ni kwa namna gani maeneo oevu kama Kilombero yanatusaidia kama Taifa? Tufike mahali tuamue tunataka watu wachunge ng'ombe au tuache maeneo oevu ambayo yanatasaidia mpaka kule *Selou*? Ni wakati muafaka tuangalie mipaka tulioipanga katika nchi yetu, tutaendelea kuwa na migogoro mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kupata vitu ambavyo ni *standard* kama tuna fikra ambazo ni *sub-standard*. Kuna watu wako *under average* wanataka wapate mshahara ambao ni *above average*, haiwezekani. Kwa hiyo, tunashindana na Mataifa mengine kama Botswana, tunashindana na Mataifa mengine kama *South Africa*, hatuangalii ni *brain* kiasi gani *wame-invest* katika tasnia hizo, ili wapate *return* kubwa. Huwezi ku-*invest brain* ndogo ukategemea upate *return* kubwa *in terms of money, in terms of* mipango, mambo mengi hayo *yana-involve* mipango mizuri, tumezungumza sana kuhusiana na masuala ya migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mambo matatu ambayo nimeyazungumza Mheshimiwa Waziri ni suala la

viucombe hai wanaosafirisha ambalo kwa kweli wamewa-*cripple*, jambo ambalo sio sawasawa, lakini bado suala la pili nimezungumza kuhusiana na sheria ambazo zinakinzana ziko nyingi na kanuni ambazo ziko kwenye uwezo wao. Afadhalii sheria labda zitachukua muda, lakini kanuni nyingi ziko kwenye uwezo wao wanaweza wakazileta hapa tukazirekebisha kuondokana na migogoro ili tufanye *business*.

Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, Wizara hii ni Wizara ambayo inategemewa kuleta mapato mengi katika nchi yetu, tufike mahali waache *legacy* katika Wizara hii, imekuwa ni Wizara ya kufukuza watu wengi, ya kubadilisha watu wengi, hapo nyuma tumegombanagombana, lakini kwa namna moja au nyingine sasa hivi kuna mwanga unaonekana, kuna kazi inafanyika. Wanasema mara nyingi hatusifu, leo Mheshimiwa Dkt. Kigwangala nisifu kidogo kuna sehemu ya kazi inafanyika, mambo madogo madogo yarekebishwe. (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lucy Owanya, Mheshimiwa Mushashu na Mheshimiwa James Millya wajiandae.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi. Nipende kuipongeza Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri pamoja na ile ya Kamati. Nategemea Mheshimiwa Waziri atachukua maoni yale na kuyafanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita zaidi katika Sekta ya Utalii. Kwenye *report* nyingi tumeona kwamba, sekta hii ni kati ya sekta inayochangia katika pato la Taifa kwa asilimia 17.5 na asilimia 25 kwa fedha za kigeni, lakini naona Serikali bado haijaichukulia *seriously* hii sekta ya utalii. Kwa mfano kwenye fedha za maendeleo ziliidhinishwa shilingi bilioni 26.8, lakini zilitoka bilioni 10.5 tu. Sasa kwa mtindo huu na fedha hizi zilizotoka ni kutoka kwa wafadhili, hata Kambi

ya Upinzani imeelezea hilo. Sasa ningependa kujuu Serikali wamejipangaje ili tuweze kuwa na fedha zetu wenyewe, ili tuweze kuendeleza maeneo ambayo yanahitajika kuendelezwa? Mfano, kama tunataka kuendeleza Katavi, tunataka kuendeleza kule *Southern Circuit*, lakini kwa mtindo huu sioni kama wafadhili wakijitoa ina maana hatutaendeleza zile *parks* nyingine zilizokuwa zinatakiwa kuendelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sekta ya utalii ni moja ya sekta ambayo inazalisha ajira nyingi sana. Mfano, Mlima Kilimanjaro kwa mwaka 2017 zilipatikana ajira takriban elfu 20 kwa wapagazi. Hii achilia mbali bado wafanyakazi wa mahotelini, wafanyakazi ambao wanapeleka watu mbugani na kadhalika. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali kwa kweli, ihakikishe kwamba, inaichukulia hii sekta *very serious*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine cha kusikitisha ni hizi kodi. Tumekuwa tukizungumzia kila siku, unakuta mtu analetewa kodi ya *OSHA 1.5 million*, kodi ya *NEMC 1.5 million*, kodi ya *COSATA 1.5 million*, bado kodi nyingine nyingi tu zaidi ya 36; sasa unajuliza *COSATA* wanakuja wanakutoza kwa sababu umeweka *television* ndani ya hoteli, lakini tukumbuke kwamba, huyu mwenye hoteli bado analipa mfano kwa *DStv*, *Azam Tv* na kadhalika. Sasa ningependa kujuu *OSHA* wanakuja wanatoza labda 1.5, wanawasaidiaje hawa wafanyakishara, hawatoi elimu wanakuja kuangalia kama mmeweka waya vizuri za umeme na kadhalika, lakini *return on investment*, wanawasaidia nini wale wafanyakishara ambao wanakuja kuwatoza hizo hela? Hizo hela zinaenda kufanya nini maana hazirudi kwa wale wafanyakishara kuja kufanya ile biashara? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linalofanya *destination* ya Tanzania inakuwa *expensive* ni hizi *hidden cost*. Unakuta mfano, mtalii akitoka *let say* Amsterdam kwa *package* ya siku nane, kutokea kule Amsterdam atalipa dola 4,698 kwa mtu, lakini akija Tanzania analipa dola 5,797 kwa mtu. Kwa hiyo, *destination* ya Tanzania inaonekana ni *expensive* sana nami naamini kabisa ni kwa sababu ya hizi

tozo ambazo tunaziongeza kwa hiyo, mfanyabiashara kazi yake ni kufanya biashara kwa hiyo, kila chochote anachokipata anakiongezea kwa yule mteja kwa hiyo, *destination* inakuwa ni *very expensive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningetaka Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara ya Fedha labda watusaidie, *high season* inakuja mwezi wa Sita na *bureau de change* wamezifunga. Kwa huu muda mchache walivyozifunga zimeleta bughudha kubwa sana, watalii au wageni wanaokuja kwenye hizi sehemu za wageni unakuta benki zinafungwa saa 10.00 *hazi-operate* kwa *24 Hours* na wakati wa *holidays* pia zinafungwa na Jumapili zinafungwa, sasa hii inakuwa ni bughudha kwa wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nagependa kujua, sidhani kama ni *bureau de change* zote ambazo zilikuwa zina matatizo, pengine zile zilizokuwa hazina matatizo zingefunguliwa. Kama haiwezekani basi ningombaa Serikali labda walete *mobile bureau de change*, wawashauri benki wawe na yale magari waweze kutoa hii *service* kwa sababu hoteli nyngi hawawezi kuweka fedha nyngi ndani ya hoteli kwa sababu ya ujambazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tukiendelea kwa mtindo huu ina maana tunarudi kwenye miaka ya 70 ya *black market* na watalii au wageni wataanza kutuuzia fedha *fake* na Tanzania tutakuwa kwenye *bad records*. Kwa hiyo, naomba twende na wakati, tuko kwenye karne ya 21 jamani, tusirudi tena kwenye miaka 30 iliyopita. Wakati ule tulikuwa tunaficha fedha kwenye vitanda na nini, sasa hivi na sisi twende kwa wakati, sijui hao wanaomshauri Mheshimiwa Rais au walioishauri *BOT* kufunga zile *bureau de change* walikuwa wana maana, pengine walikuwa na maana nzuri, lakini sidhani kama kila mtu alikuwa na kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kulizungumzia ni kuhusu utalii wa utamaduni. Nchi zilizoendelea wana-*keep* historia zao, unatumia majengo kama Ulaya unakuta *museam* watu wakienda kwenye

museam wanalipa fedha, lakini hapa kwetu unakuta kama Dar-es-Salaam tulibomoa majengo yale ya kale na kujenga maghorofa, lakini kuna vivutio vingi sana katika kila wilaya. Mfano mzuri ni kule Moshi Vijijini, *Old Moshi*, wakati wa Vita ya Kwanza na ya Pili ya Dunia Wajerumani pale Kikarara walijenga mapango kule chini, lakini mapango yale yamekaa tu *idle*, sasa sijui kama Wizara wanalitambua hill? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawalitambui basi ni vizuri kwenda kufungua yale mapango iwe kama moja ya vivutio vya utalii ili wale Wajerumani wanavyokuja au tunavyoenda kuuza utalii kule Ujerumani na nini iwe ni mojawapo ya kivutio cha utalii. Kwa ushauri tu, pengine Wizara ingeangalia ni jinsi gani inaweza kutembelea katika kila wilaya wa-*identify* vitu gani ambavyo vinaweza vikawa ni vivutio na kudumisha utamaduni wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ningependa kuzungumzia kuhusu kuutangaza utalii. Utalii tumekuwa kweli tukiutangaza, lakini mara nyingi wafanyabiashara wamekuwa wakitangaza zaidi na inakuwa ni ghali sana kwao. Sasa nimekuwa nikishauri mara nyingi *TTB*ivezeshe ili wafanyabiashara sasa waweze kupunguziwa bei waweze kuitangaza Tanzania zaidi; Mheshimiwa Waziri hapa amesema kuna watalii kutoka Israel walikuja 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjulishe Mheshimiwa Waziri kwamba, hawa watalii waliokuja mwaka huu 1,000 wamekuwa wakija kila mwaka wakati wa *low season*. Kwa hiyo, asije aka-*add up* ufikiri labda ni tangazo limefanywa mwaka jana ndio tukapata watalii 1,000. Hawa watalii kutoka Israel 1,000 *they have been coming here all these years for the past five years* wamekuwa wakija hapa kwa hiyo, sio watu wageni. Inabidi sasa tuangalie ni jinsi gani tunaenda kwenye *new destinations* huko nchi za Russia, Zchesklovakia na nini, maana sasa hivi ndio utalii mpya umekuja wawawezeshe *TTB* waweze kwenda kule twende tukaingie kwenye hizi *new market* sio tung'ang'anie tu hizi *market* za Ujerumani sijui, Uingereza na Ulaya, lakini twende kwenye hizi nchi ndogondogo nina hakika kabisa tukienda

huko tutapata watalii wengi zaidi na tutaongeza pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mushashu, atafuatia Mheshimiwa Milly na Mheshimiwa Catherine Magige ajiandae.

MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi. Kwanza kabisa naanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa hotuba nzuri, lakini vilevile kwa kazi nzuri wanayofanya ndani ya Wizara yao. Kwa kweli, kazi wanayofanya ni nzuri na inaonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Utalii ina jukumu la kutangaza utalii na kutangaza vivutio vilivyo ndani ya Tanzania ili kuweza ku-*attract* watalii wengi waje. Wamefanya kazi nzuri sana, tumeona matangazo kwenye magazeti, kwenye majorida mbalimbali yaliyo ndani na nje ya nchi, tumeona kwenye mikutano wanatangaza, kwenye michezo wanatangaza, kwenye matamasha wanatangaza kwa kweli, wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangazaji huu umeanza kuzaa matunda ndio maana tunaona sasa makundi mbalimbali ya watalii wanaingia kwa makundi kwa maelfu, kwa mamia, ndani ya Tanzania kuja kuangalia vivutio vilivyo kwetu, lakini vilevile imechangia kwenye pato la Taifa kwa sababu, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ametwambia kwamba, imechangia kwenye pato la Taifa takribani dola bilioni 2.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo kuitia *TBC* kwa kuweza kuanzisha chaneli ya utalii ambayo inaitwa *Safari Chanel*, kwa kweli hii ndiyo chaneli yetu ila sasa naomba tuiwezeshe iweze kuonekana hata nje kwa sababu

tukiendelea kuiangalia sisi wenyewe, haitatusaidia. Nilikuwa nafikiri tuendelee vilevile kuboresha maudhui ya *Safari Chanel* ili iweze kuvutia watalii wengi zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tunaonyesha wanyama, mimea, maua na samaki wanaopatikana Tanzania lakini vilevile tuoneshe na hoteli nzuri za kitalii yaliyo ndani ya Tanzania kusudi yule mtalii sasa aone kwamba loh! Kumbe nikienda Tanzania naenda kulala kwenye hoteli nzuri kama hii, tunazo. Vilevile sisi wenyewe tuna utamaduni, ngoma za kitamaduni za kila mahali, tuiweke kwenye ile chaneli kuongeza ule mvuto wa ile chaneli kusudi watu wapende kuiangalia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tuonyeshe ndege kubwa zinazotua ndani Tanzania; tuonyeshe *KLM*, *Qatar Airways*, *Emirates*, *British Airways* bila kusahau ndege yetu wenyewe ya *ATCL* kwamba inaweza kwenda ikabeba watalii na kuwaleta hapa, kwa kufanya hivyo basi tutaweza kupanua wigo na watalii watakuja wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kupandisha yaliyokuwa mapori ya akiba ya Bihamulo, Burigi na Kimisi ambayo sasa hivi imekuwa hifadhi inayoitwa BBR na kupandisha Ibanda, Rumanyika na sasa hivi inaitwa Hifadhi ya IR kuwa Hifadhi za Taifa. Kwa sasa mmekaza mzizi wa fitina, kwa sababu tulikuwa tunakaa humu Wabunge tunachangia tunasema kwanini inaonekana utalii unakuwa *promoted* kwenye sehemu moja ya Tanzania ambayo ni kaskazini ilhali vivutio viro katika sehemu zote? Sasa tunaloona mnaenda kutambua hivi vivutio kuvendeleza na kuendeleza utalii katika Kanda ya Ziwa, tunasema asanteni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi hizi za BBK na IR zinasambaa kutoka Chato ambayo iko katika Mkoa wa Geita kuja Muleba, Bihamulo, Ngara, Karagwe ambazo zipo katika Mkoa wa Kagera. Je, hifadhi hizi zitaendelea kuitwa kwa majina haya BBK na IR au mna mpango wa kuyapa majina mengine yanayovutia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujio wa hifadhi una manufaa makubwa sana. Kwanza zipo karibu na mipaka, kule kwetu tunapakana na nchi ya Rwanda na zenyewe hifadhi zinapakana na Rwanda. Mnapoongeza ulinzi ndani ya hifadhi hizi ina maana kwamba masuala ya ulinzi na usalama katika hayo maeneo utakuwa umeimarika, watu wataweza kupita kirahisi bila kuogopa kutekwa. Vilevile uoto wa asili utakapoongezeka, uta-attract mvua kubwa itanyesha, ile milima iliyo ndani ya hifadhi ndiyo itakuwa inatiririsha maji kuititia Mto wa Kagera, Mto Mwisa, Msega kuingia kwenye Ziwa Victoria, kitakuwa ni chanzo kizuri cha maji kuingia ndani ya Ziwa Victoria halafu tunavuta tunapeleka Shinyanga, Tabora mpaka Singida kwa hiyo ni manufaa makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutakuwa na mimea mbalimbali, samaki wapo mpaka sasa hivi kwenye maziwa mbalimbali yaliyo ndani ya hifadhi; Burigi, Ngoma, Nyarwamba, Kasinga, Nyamarambe na Victoria yenye ambao ni wa aina yake, ni adimu. Kwa hiyo, hii itavutia watu ambao wanaotaka kufanya masomo na utafiti watakuja Mkoa wa Kagera, watakwenda Mkoa wa Geita kwenda kujifunza. Ujio huu wa Hifadhi za Taifa utawapa vijana wetu ajira mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maombi kwa Serikali. Kuna vikundi vya vijana; kwa mfano pale Muleba kuna kikundi cha vijana wanatengeneza vinyago, pale Ngara kuna kikundi cha wakina mama wanatengeneza *table mats* na vitunga mbalimbali, kuna watu Karagwe kule wanatengeneza vitunga, mikeka pamoja na Misenyi; tunaomba wawezeshwe, wapewe mitaji, wafundishwe ujasiriamali kusudi watengeneze vitu vizuri zaidi vitakavyokuja kuwapendeza hao wajasi amali na waweze kuvinunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuboreshe miundombini ya barabara zinazozunguka zile hifadhi pamoja na ndani. Kiwanja cha Ndege cha Chato pale, Kiwanja cha ndege cha Bukoba Mjini viendelee kuboreshwa, viwekewe taa kusudi sasa watalii wanaoingia kuititia Uganda, Rwanda na

Burundi waweze kutua wakati wowote usiku na mchana na kufanya utalii ndani ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuendelee kuwavutia wawekezaji; hii ni fursa kwa watu wa Mkoa wa Kagera na Mkoa wa Geita, tuone sasa hapa kuna fursa ya uwekezaji, twende tujenge hoteli, tutengeneze zile fukwe zipendeze, tuandae hoteli na mahali pa kulala watalii hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Kagera na Geita ina urithi mkubwa wa historia ya Machifu Abakama, Ebikale; tunachoomba ni kwamba sasa twende tuyatambue maeneo haya yaendelezwé, inaweza ikawa kivutio kimoja wapo cha utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi kubwa ninaloomba, kwenye vijiji hivi na kata zilizokuwa zinazozunguka, hizi sasa ambazo zitakuwa hifadhi, watu hawa wamezoea kuingia kwenye hifadhi kukata miti kwa ajili ya kuni, kutengeneza mkaa na kuwinda, kuna haja ya kwenda kufanya mafunzo na ushawishi wa kutosha ili watu hawa waweze kuelewa umuhimu wa uhifadhi na hifadhi hizi. Mkishafanya hivi ina maana kwamba hawa watu wenyewe sasa ndiyo watakuja kuwa walini namba moja ya hifadhi hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Wizara, *TANAPA, Ngorongoro Conservation Authority, TAWA, TFC* na wadau wengine kwa kudhibiti ujangili. Wanyamapori walikuwa wanatoroshwa lakini sasa hivi hali imetulia, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo ni rasilimali ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu, inabidi tuitunze kwa ajili ya vizazi vijavyo lakini na kwa ajili ya dunia nzima. Mnamo mwaka 2009 inasemekana ndani ya Tanzania kulikuwa na tembo takriban 110,000 lakini wakaendelea kuuwawa kikatili na ujangiri na nini na kutoroshwa, ilipofika mwaka 2014 tulikuwa na tembo 43,000 tu kwa hiyo asilimia 60 yote walishauwawa. Lakini nawapongeza sana Wizara, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri mmeefanya kazi nzuri, mikakati

mliyoweka na ulinzi mlioweka, sasa hivi tembo wameanza kuongezeka na tunaona data zinasema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo linalojitokeza sasa hivi, tembo hawa wanahama kutoka kwenye makazi yao, wanakwenda kwenye makazi ya binadamu, wanafanya uharibifu kubwa, wanaharibu mazao ya wananchi lakini wakati mwininge wanaua hao wananchi. Nilikuwa napenda kujua je, Serikali imefanya utafiti kujua kwa nini hili tatizo ndiyo linajitokeza? Kwa nini tembo wameamua kuhama kutoka kwenye maeneo yao wanakwenda kwenye maeneo ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, mtu akiharibiwa mazao yake au akauwawa na tembo, fidia inasemaje? Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba ukija kuhitimisha utueleze. Vilevile Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba haya mambo sasa hayajitokezi tena, tembo wakae hukohuko kwenye mbuga/mapori kusudi wasiwaingilie binadamu, binadamu waendelee kufanya kazi zao? Sasa hivi ukiona sehemu mbalimbali wanaonesha kwamba hata watoto wanaogopa kwenda shule kwa sababu ya hawa tembo wanaohama na kuwafuata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nasema Wizara hii ina majukumu makubwa sana, inabidi iongezewe bajeti ili waweze kuboresha utalii na utalii utaweza kutuletea Pato kubwa la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Millya, ajiandae Mheshimiwa Catherine Magige.

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kuwapongeza watumishi wa Wizara wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri wetu Dkt. Kigwangala kwa kazi kubwa wanayofanya kufufua na kuendeleza sekta hii ya utalii nchini mwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikia kidogo hoja za wenzetu, mtu anasema kwa kawaida miaka yote tumekuwa tukipokea watalii kutoka nchi ya Israel kila msimu, unapata shida kidogo kwa sababu mtu hataki kusifia yale mazuri yanayofanya kwa wakati huu. Kama hivyo ndivyo, kwa nini mtu asigusie watalii takriban 340 waliofika juzi wa kutoka China? Hili ni eneo jipya ambalo hatukuwa nalo, Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wamefanya vizuri na uongozi wa nchi hii. Tungeona watu waungwana wataje na hayo. Kwamba siyo lazima utaje ya Russia au utaje mahali pengine kama Ukraine, taja na China kwamba hili ni soko kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri kwa kuboresha kidogo hilo, ningeomba ushirikishe balozi zetu nchini. Balozi zote zilizopo mataifa mengine ya nje watuandalie illi watu wetu wanaofanya utalii hapa ndani kama Arusha au maeneo mengine tuwapeleke na wafanyabiashara wakakutane na wale ambao wanauza biashara ya utalii duniani kote wakutane na watu kama ambavyo nchi ya Kenya inafanya mara nyngi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niongelee hoja kubwa aliyofanya Mheshimiwa Rais. Vijiji vyetu vya wafugaji kwa miaka mingi sana baada ya uhuru na hata wakati wa uhuru na Mheshimiwa Waziri umegusia kwenye hotuba yako. Tumeumia muda mrefu kwa miaka mingi, Mheshimiwa Rais baada ya kusikia kilio cha vijiji takriban 350 nchi hii, akaamua kuelekeza Wizara karibu nane zikae pamoja na akawatuma Mawaziri kila mahali, walifika Kimotoro Mawaziri nane. Nia ya Mheshimiwa Rais ni kutatua hii hali iliyokuwepo ya muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona wenzetu wakiendelea kuuliza hivi itawezekana kufanyika kweli? Nia ya Mheshimiwa Rais ni njema, niombe sasa Wizara yako Mheshimiwa Waziri msukume jambo hili ili lisijelikawa ni jambo ambalo halitatekelezeka, wananchi wanesubiri kwa hamu Kimotoro, Simanjiro na nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma vizuri hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ukurasa wa 18 na 19; wenzetu bado hawaweki imani kwamba Serikali hii ni Serikali ambayo haiongei tu bali inatenda na hizi zote ni sifa za Mheshimiwa Rais. Ukiona kwenye hotuba yao wanagusia suala la *Stiegler's Gorge*; Serikali inataka umeme wa kutosha. Wanaongelea pia suala la hizi hifadhi, kwamba kwa nini tumege eneo fulani la hifadhi halafu tuwape wananchi; wenzetu mmeuliza tayari *SGR*tunafanya nini? Mnauliza bado masuala ya ndege. Mimi niseme kitu kimoja, nimepata bahati ya kupanda ndege hizi mpya za Serikali, ni ndege za kisasa zitatuongezea utalii na nimeambiwa kuanzia mwezi ujao mtaanza kwenda India na Afrika ya Kusini, huu ni mwanzo mzuri sana. Na crewyetu mimi nilivyoisikiliza kwa uzoefu wangu wa masuala ya ndege, ni crew nzuri, tutaongeza utalii kwenye nchi hii na Mungu aendeleee kuwabariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusema kitu kimoja, nchini Ghana baada ya kupata uhuru, Kwame Nkurumah alianzisha miradi mikubwa sana. Tulipata wasaliti waliompinga Kwame Nkurumah wakati ule. Lakini mnakumbuka pia katika ukombozi wa Congo, wakati Congo inakombolewa kulikuwa na mtu anaitwa Patrice Lumumba akatokea msaliti mmoja anaitwa Moise Tshombe wakati wa kugawa Jimbo la Katanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasaliti duniani hawakosekani wala Mheshimiwa Rais asiache kufanya miradi mikubwa ya kusaidia nchi kwa sababu ya kusikiliza kelele za wale ambao hawatakii mema nchi hii, aendeleee kupambana na sisi wengine ambao tupo upande huu, tunajua anafanya mema kwa ajili ya nchi hii, tupo tayari kusaidia Taifa hili na tutamuunga mkono Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, na Mheshimiwa Dkt. Kigwangala usitishwe na maneno yoyote ya watu wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nigosie suala la Makumbusho ya Taifa letu. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, bajeti tunayotenga ni ndogo sana, Makumbusho ya Taifa yanaisaidia Serikali na sisi Watanzania kuhifadhi kumbukumbu

ya leo, kesho na miaka ijayo. Inawezekana mambo mengine yanafanyika kwa sababu ya kutaka kutufurahisha tulioko duniani sasa, tuna watoto na wajukuu wanaokuja keshokutwa wanataka kujua Tanzania imetoka wapi, inaenda wapi na miaka mingine inaenda wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri, bajeti ya makumbusho iongezwe, ni ndogo kweli. Hii ni taasisi muhimu ambayo haipigiwi kelele mara nyingi. Mimi nimepata bahati ya kuzunguka kwenye makumbusho mbalimbali, kuna makumbusho mazuri sana duniani, naomba usaidie ya kwetu, ya kwetu ipo hoi bin taaban. Ninaomba Mheshimiwa Waziri unapokuja kuhitimisha hoja yako ugusie hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lingine ni Kuhusu Ujangili. Nimeona umesifiwa kuhusu ujangili. Mimi Simanjiro nimepata ujumbe jana, wafugaji wanalamika kuhusu ujangili, ujangili umeongezeka Simanjiro eneo la Terat, Sukro mpaka Kimotoro, ninaomba usaidie. Lakini nimesikia kwenye hotuba yako umeongea mambo mazuri, umesema unaanzisha *hunting blocks* tena na unagawa vibali vipyta, hilo litasaidia kwa sababu kwa kugawa *hunting blocks*, wale ambao umewapa *hunting block* watasaidia kushirikiana na Serikali kulinda wanyamaporis wasiuwawe. Wachungaji wetu wa Simanjiro wanashindwa kuchunga kwa sababu wanahisi wanawenza kupigwa risasi na majangili, ninaomba muongeze *taskforce* ile *National Taskforce* ya *Anti-poaching* ipelekwe Simanjiro sasa hivi wanyama wanauwawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la fidia. Hatuwezi kumfidia binadamu, juzi Simanjiro kijana mmoja mtoto wa shule ya sekondari alienda machungani aka uwawa na tembo. Ninaomba msaidie mfikirie kuleta sheria hapa Bungeni tubadilishe *at least* tuplicate kidogo kifuta machozi kizuri. Mngechukua mila zetu za kifugaji za Kimasai, mtu akiuwawa kwa namna yoyote bahati mbaya, sisi tulikuwa tunatoa fidia mpaka ng'ombe 49.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mfikirie ni namna gani basi, kwa sababu katika mila za Kiafrika, mimi ninavyofahamu kama wafugaji wa Kimasai, mtoto ni kama kiiunua mgongo cha mzazi, akishaondoka binadamu mtu unamtegemea ni mtoto wako. Ninaomba msaidie hili suala la fidia mlirekebishe kidogo, halijaka sawasawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kuna lingine, kuna mfugaji wa Morogoro, *Game Reserve* ya Matambwe aliuwawa ng'ombe wake 200 kwa kupigwa risasi na watumishi wa Wizara yako mwaka 2015, ametozwa faini lakini bado maaskari wale wakapiga risasi; ninao ushahidi hapa maaskari wa wanyamapor wakipiga ng'ombe 200 risasi; mpaka leo mfugaji yule hajapewa fidia yoyote, hajaangaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri nitakuletea ushahidi huu wote uwasadie, nina majina ya hawa walioamuru ng'ombe hawa wapigwe risasi. Jina la huyu aliyepiga risasi na mtu aliyechukua video lakini naomba kwa muktadha wa hoja hii nisitaje majina yake lakini nitakuletea ili wewe kama kiongozi wetu wa kisiasa katika Wizara usaidie hilo lipatikane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya ujirani mwema. Asilimia 70 ya wanyamapor wako nje ya hifadhi, tunawatunza sisi lakini hatuoni faida gani mnatupa kama kuchimba maji, hospitali, kuhudumia shule mnatoa kidogo sana. Mheshimiwa Waziri naombeni mfikirie kwenye Wizara yako ili hili tupate na lenyewe kwa sababu mkitushirikisha tukapata faida ya wanyama hawa, tutawatunza kwa sababu tunaona faida yao, ninaomba Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niunge mkono hoja, kwamba unafanya kazi nzuri kwa kweli Wizara haipo kama ilivyokuwa mara ya kwanza, hizi sifa tukupe na Serikali imejitahidi sana. Baada ya kusema hayo nawatakia heri katika utekelezaji wa majukumu yenu, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Catherine Magige, jiandae Mheshimiwa Cosato Chumi.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kufanikiwa kudhibiti ujangili katika nchi yetu. Tumeshuhudia Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala akizunguka nchi nzima, siku 48 pori kwa pori. Nilifuatilia katika Gazeti la Mwananchi, walifanya tathmini, walisema Mheshimiwa Kigwangala amezunguka kilometra 28,000. Mimi mwenyewe nilikuwa nikiangalia najiuliza huyu mtu ni wa namna gani? Kwa kweli Mheshimiwa Kigwangala anastahili pongezi, amefanya kazi kubwa sana; anamsaidia Mhehsimiwa Rais na vilevile hata Watanzania na sisi wenyewe tunamuona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tembo wanaongezeka kwa wingi, wanaendelea kuzaliana, ujangili umepungua. Zamani ilikuwa hata tembo akifa bahati mbaya, unakuta majangili wameshachukua meno ya tembo lakini sasa hivi tembo akifa tunakuta meno kama yalivyo, ina maana ni Wizara imejitahidi sana kupunguza ujangili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuanzisha Jeshi Usu kwa ajili ya misitu na wanyamapori. Sasa hivi wanyama na misitu yetu ipo salama. Vilevile nawapongeza kwa kuanzisha kikosi kazi kwa ajili ya kudhibiti ujangili na ndiyo maana siku hizi hatusikii tena habari za ujangili kama ilivyokuwa hapo nyuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya watalii inaendelea kuongezeka kila siku, yaani watalii wanaendelea kumwagika katika nchi yetu; zote hizi ni jitihada za Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Waziri, watendaji wake na taasisi zake mbalimbali. Hivi karibuni hapa tumeshuhudia meli ya watalii 2,500, ndege ya Waisraeli 1,000 na Wachina 343, wote hawa wanapokuja katika nchi yetu wanaondoka wanarudi huko, wakisharudi fikiria kila mmoja aliyekuja huku akifika katika nchi yake anawaambia watu wangapi na wanatangaza

Tanzania kwa namna ama nyingine; wanatangaza vivutio vyetu kwa namna moja ama nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze katika Mkoa wangu wa Arusha kwa wafanyabiashara wa hoteli za kitalii. Wafanyabiashara hawa wamekuwa wanatozwa *bed night levy* kwa siku ambapo wanalipa dola moja na nusu. Nayo haijalishi kwa hoteli ambayo labda inachaji dola 150 au 200 kwa siku, au hata ile hoteli ndogo ambayo inachaji kwa siku 40,000, wote wanalipa sawa. Kitu hiki kimekuwa kikiwaumiza sana wafanyabiashara wa mahotelii, kwa sababu inawezekanaje mtu ambaye anachaji mtu kulala kwa siku dola 250 na mwininge 40,000 wakalipa sawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alikuja Arusha, alikutana na wadau wa utalii walimwambia, lakini kipindi kile nadhani alishindwa kuamua labda kwa sababu tulikuwa hatujaenda kwenye bajeti. Sasa Mheshimiwa Waziri ndiyo wakati muafaka, wafanyabiashara wa utalii wanamwamini sana na wamesema nimfikishie hili na wana imani kubwa na ye ye na atalitekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iendelee kuangalia mazingira ya Ziwa Manyara; kina kinapungua na tunajua kuwa Ziwa Manyara lina ndege wazuri sana amba ni kivutio cha watalii wengi, ndege aina ya *flamingo*. Kwa hiyo kina hiki kinapungua ndege watapotea na tutakosa watalii. Naomba sana Serikali iangalie kwa karibu ili tusije tukapata hasara ya kupoteza ndege aina ya *flamingo*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali iangalie mazingira ya Ngorongoro kwa sababu Ngorongoro magugu yanaharibu mazingira, wanyama wadogowadogo wanakosa chakula, wanakufa. Serikali ifanye utafiti namna ya kukabiliana na changamoto ya mmea vamizi kwenye Hifadhi ya Ngorongoro amba ni urithi wetu wa dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkao wangu wa Arusha, eneo la Ngorongoro kuna shule moja ya wasichana ilitakiwa kujengwa katika Kata ya Alaitole, eneo la Isere. Shule hii wananchi wamejitahidi wamekusanya mawe, wamekusanya mchanga, halmashauri imetupa milioni 288, lakini mpaka sasa hivi Ngorongoro hawajatoa kibali cha kujenga shule hii. Akinamama wamekuwa wakilalamika, hata wiki iliyopita waliandamana, akinamama wanataka watoto wao waende shule, lakini hatujajua ni kwa nini wanazuiwa kujenga, mpaka sasa hivi hawajapata kibali kutoka hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mashaka na Mheshimiwa Waziri, vilevile na watu wa Ngorongoro. Naomba ikiwezekana tukutane twende tukasikilize hasa kuna changamoto gani ili tuangalie ni jinsi gani akina mama hawa watasaidiwa watoto wao waende shule. Tunajua Mheshimiwa Rais anasisitiza watoto wasome na akinamama hawa wanataka watoto wao waende shule na ndiyo maana juzi waliandamana kwa uchungu mkubwa sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri alichukue hili na alifanyie kazi ili shule hii iweze kujengwa na watoto wetu waweze kwenda shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na watendaji wa Wizara yake kwa kazi nzuri sana wanayofanya ya kuhakikisha nchi yetu inanufaika na vivutio vyta utalii tulivyonyavyo. Nawapongeza sana kwa mkakati wa *krebrand* nchi yetu kupitia kaulimbiu ya *Tanzania Unforgettable*. Hili ni jambo zuri na muhimu katika kutangaza nchi yetu na kuingia katika ushindani wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, lazima kufanya kazi ya ziada ili kweli kauli hii iwe ya maana na iwe kauli endelevu. Hii ni kuhakikisha kwamba tunapokwenda kila mahali Watanzania wanaitangaza *Tanzania Unforgettable*; timu zetu za Tanzania zinabeba *Tanzania Unforgettable*; wasanii wetu wanabeba, hata Mawaziri wetu wanapokwenda kwenye mikutano ya Kimataifa wanaibebe hii *Tanzania Unforgettable*. Vilevile hii siyo kazi ya Wizara ya Maliasili tu, ila Wizara ya Maliasili ni kama wenywewe wana-coordinate, lakini tunatakiwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema hivi inawezekana hata Wabunge wengi hawaelewi maana yake, hata Mawaziri, inawezekana asilimia 90 hawaelewi, wanahitaji kueleweshwa na kufahamishwa ili tunapoongea *Tanzania Unforgettable* kila mahali iwe ni kwa ajili ya Watanzania wote, siyo Wizara tu, tuitangaze kila mahali. *Tanzania Unforgettable* ni *experience itakayopata watalii au mgeni kutoka kutangaza*. Mfano, mgeni anapofika tunaangalia ni jinsi gani mazingira ya *immigration* wamempokea mgeni, wamemkaribishaje. Hiyo nayo ni *Tanzania Unforgettable*, akitoka anakwenda kuitangaza Tanzania. Tunaangalia amepokelewaje kwenye hoteli, amepataje usafiri, usalama wa mgeni, akitoka katika njia salama anakwenda kuiongelea vizuri nchi yetu, tunaangalia mambo mengi kuhusiana na hii. Au njia rahisi za mtu hata kufanya biashara Tanzania, vilevile akitoka anakwenda kuiongelea Tanzania vizuri. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kukupongeza, unajitahidi sana pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara. Naomba atakapokuja kujibu anijibu kuhusiana na hii shule, maana akinamama kule wanapata shida, wanafuatilia kuhusiana na hii shule. Vilevile na wafanyabishara wa *middle class hotels* wa Arusha; naomba anijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chumi, atafuta Mheshimiwa Nchemba na Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Niseme wazi na pengine naweza nisieleweke lakini ndiyo ukweli; kama kuna Wizara zilikuwa pasua kichwa, basi Maliasili na Utalii, Nishati na Madini siku za nyuma, lakini mnyonge mnyongenii, haki yake mpeni; toka Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ameingia hapo kwa kweli,

tuwe wakweli wa nafsi za ukweli; Wizara imetulia, Wizara imekuwa ina mwelekeo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ana timu nzuri. Nikiona Katibu Mkuu Profesa, Naibu Katibu Mkuu Dokta, *TFS* yuko Profesa, lakini pia hata Wenyeviti wake wa Bodi wengi ni Mabrigedia, ni Majenerali. Kwa hiyo bila shaka kazi hii, pamoja na msaidizi wake, Mheshimiwa Kanyasu, wataendelea kuifanya ili Watanzania waweze kupata neema na pato linalotokana na utalii liweze kuongezeka. Napongeza hili kwa dharti ya moyo wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, nipende kupongeza pia uongozi wa *TFS*, lakini pia na uongozi wa Shamba la *Sao Hill* pale Mafinga na Wilaya ya Mufindi kwa jinsi ambavyo tunashirikiana. Zamani kulikuwa na shida sana ya mambo ya vibali, ujanja ujanja ulikuwa mwingi, lakini taratibu tumekuwa na vikao vya pamoja, tumekuwa na vikao vya wadau na mambo kiasi fulani yamekwenda katika mstari ambaao unastahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, katika Sekta ya Misitu na mimi niseme mambo makubwa mawili; kwanza, sisi tunaotoka ambako misitu inatuongozea maisha kwa asilimia siyo chini ya 50 mpaka 70, tulikuwa tumependekeza na kuishauri Serikali iweze kuondoa lile zio la kusafirisha mazao ya misitu saa 24. Nilitarajia Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo namwamini, toka tukiwa *DARUSO*, mimi niko Mlimani ye ye yuko Muhimbili, tukiendesha gurudumu la kuhakikisha kwamba mambo ya *cost sharing* yanakaa vizuri, namwamini katika hili na naamini atalitekeleza na wananchi wa Mafinga na maeneo mengine watalisikia katika hotuba yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu gani? Nime-peruse kitabu hiki kutoka ukurasa wa kwanza mpaka ukurasa wa 97, nilitarajia nitaikuta kauli inayohusiana na jambo la kuruhusu mazao ya misitu kusafiri saa 24, kwa hiyo natarajia Mheshimiwa Waziri atakapokuja katika kujumuisha atatueleza lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kama nilivyosema, sisi wananchi wa Mufindi, Mafinga, Iringa, Njombe na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini tunaendesha maisha yetu kwa kutegemea mazao ya misitu. Sasa kuna watu ambao wanavuna katika Misitu wa *Sao Hill*. Nimwomba Mheshimiwa Waziri, wakati umefika sasa, kama ambavyo walifanya katika Sekta ya Madini ambapo kuna mikopo kwa wale wachimbaji wadogowadogo, hebu sasa tuwe na utaratibu wa kuwapa mikataba hata ya miaka mitatu mitatu wavunaji wetu ili waweze kukopesheka katika mabenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya kutoa kibali ni utaratibu mzuri, lakini tunawomba Mheshimiwa Waziri tunakoelekea sasa watu hawa wapate mikataba ili kwa mikataba ile kwanza, watakuwa na uhakika wa kuajiri watu, lakini pia watakuwa na uhakika wa kupata mikopo na mwisho watakuwa na uhakika wa kuchangia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende pia kusema katika suala zima la Chuo cha Misitu Olmotonyi; Mheshimiwa Waziri, tumekuwa tukiomba na hiki ni kilio chetu watu wa Mafinga na maeneo yale, kwamba walau tungekuwa hata na *campus* kwa ajili ya chuo cha misitu katika Nyanda za Juu Kusini na bahati nzuri pale *Sao hill* majengo yapo. Jambo hili ni mwaka wa tatu sasa nalisema. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi ambavyo anajituma katika kufanya kazi na wasaidizi wake; hebu waone kwamba sasa ni wakati wa Chuo cha Misitu kuwepo Nyanda za Juu Kusini na pale Mafinga, *Sao Hill*, tayari majengo yapo. Hii yote itakuja kuleta tija katika uvunaji wa misitu, lakini katika kuchakata mazao yanayotokana na misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie utalii; sisi hapa Tanzania tunasema ni wa pili baada ya Brazil, hii hapa tunaita ni *comparative advantage*, lakini Mheshimiwa Waziri ili tunufaikie na utalii lazima tufanye kitu kinaitwa *competitive advantage*. Kwa sababu kama ni wa pili tayari ni wa pili, sasa kuwa kwetu wa pili tunanufaika vipi? Kweli nimeona hapa katika takwimu za Mheshimiwa Waziri ameonesha ambavyo ongezeko la watalii kwa mwaka huu tunapoelekea

ni watalii milioni 1.5. Kwa ongezeko hili tumejapata fedha za kigeni dola billioni 2.5 mwaka 2017 na sasa imeongezeka mpaka Dola za Kimarekani bilioni 2.4. Sasa tukisema dola pengine mwingine haelewi, hizi fedha kwa Kitanzania ni zaidi ya trilioni 5.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipunguza vikwazo katika Sekta ya Utalii tunaweza sisi tukahakikisha ndani ya miaka michache tuna watalii wasiopungua milioni tano. Tukipata watalii milioni tano maana yake ni nini; ikiwa sasa kwa watalii milioni moja na laki tano tunapata walau trillioni 5.2 kwa mwaka, maana yake ni kwamba tutakuwa tunakadiria kupata mapato yasiyopungua trillioni 15, hiyo ni nusu ya bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tufike huko tusibaki tu kusema kwamba sisii ni wa pili, sasa sisii kuwa kwetu wa pili tufanye nini? Tumeona kuna vikwazo mbalimbali katika kuhakikisha kwamba biashara ya utalii inakua. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, kama walivyofanya wenzetu wa madini, aitishe kongamano, nampongeza, alipoingia tu katika Wizara hii aliita mkutano wa wadau, lakini ulikuwa ni wa wadau wa Sekta nzima ya Maliasili na Utalii, namwomba waitishe mkutano maalum tu kwa ajili ya mambo ya utalii. Ikiwa hii ni sekta inayotupa fedha za kigeni zaidi ya asilimia 20, kwa nini tusiilee ili tuweze kuongezea pesa za kigeni na hivyo kuendelea kujenga uchumi wetu imara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende pia kuzungumza kuhusu maeneo mahususi, *historical sites*; Mheshimiwa Waziri amesema ambavyo wameongeza maeneo na mazao mapya ya utalii, lakini nitatoa tu mfano, pale Kilolo kwa kaka yangu, Mheshimiwa Mwamoto, kuna Gereza la Mgagao, gereza hili walikuwa wanakaa, Walter Sisulu amekaa pale, Mandela amekaa pale na watu wa *South Africa* wangependa kuja kutembelea pale kama sehemu ya makumbusho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi alipofika pale na kukuta tumefanya gereza akasikitika kwamba ninyi

mnatukumbusha enzi za *apartheid*. Namwomba Mheshimiwa Waziri akae katika Serikali waangalie mambo ya *historical sites*, kule Iringa kuna maeneo ya Isimila, kule Kalenga kuna kaburi la Bismarck; haya yote kwa pamoja yanaweza kutuungezea sisi kuleta idadi kubwa ya watalii, lakini tukiendana pia na kuondoa vikwazo ambavyo kwa namna moja au nyingine vinarudisha sekta nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, wakati Simba inacheza, Klabu Bingwa Afrika, Haji Manara anasifika kwa kuhamasisha na watu kujaa Uwanja wa Taifa, zaidi ya 60,00; *Taifa Stars* ilipocheza na Uganda, zaidi ya watu 60,000 wameingia pale Uwanja wa Taifa. Mheshimiwa Waziri, aje na mkakati wa kuhakikisha tunahamasisha pia utalii wa ndani... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Hebu rudia tena, klabu gani hiyo?

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la michezo, kuna msemaji anaitwa Haji Manara wa *Simba Sports Club*...

MBUNGE FULANI: Bodaboda!

MHE. COSATO D. CHUMI: ...kuna msemaji anaitwa Thobias Kifaru, kuna msemaji anaitwa Masau Bwire; hawa watu wanaleta hamasa watu wanaenda viwanjani. Je, sisi kama Taifa kwa nini tusihamasishe watu wetu waweze kwenda kwenye mbuga ili tuwe na...

MBUNGE FULANI: Bodaboda!

MHE. COSATO D. CHUMI: ...tupate fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, Mheshimiwa Rais juzi amesema Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, wawe na laini za *ITCL*. Nami nitoe wito; familia zetu sisi viongozi ziwe za kwanza kwenda kufanya utalii wa ndani ili kuhamasisha na hivyo kujipatia fedha kwa sababu utalii wa

ndani unaingiza fedha, mama anauza bagia, mama anauza sambusa, fedha inakwenda moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno haya, naunga mkono hoja na Mungu atubariki sote. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nchemba, ajiandae Mheshimiwa Lulida.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nichangie hoja hii iliyopo mbele yetu. Nianze na pongezi; kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayofanya ya kuutambua utalii.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Order ndani ya Bunge, order!

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, shida kubwa iliyopo sasa hivi ni jinsi gani Rais alivyojipanga na kuhakikisha kwamba sasa utalii unakuwa katika nchi yetu, ndani ya miaka mitano amefanya kazi kubwa sana. La kwanza, amenunua ndege, hizi ndege kununuliwa kwake maana yake zinaporuka nje ya nchi zinatangaza tayari Tanzania ni kitu gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Dkt. Hamisi Kigwangalla kwa kazi nzuri anayoifanya, wakati huo huo nimpe pole kubwa sana kwa sababu kipindi kile baada ya kumaliza bajeti ya mwaka jana, 2018, alipata ajali mbaya sana. Hatukutegemea tena kwamba leo atasimama na kuisoma tena hotuba yake ya bajeti; yote hayo ni kwa sababu ya uwezo wa Mwenyezi Mungu, leo kamrejesha tena ndani ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hiyo inatokana na jinsi anavyojituma kwa Watanzania. Amesema Mheshimiwa Catherine Magige, amezunguka Tanzania nzima kuona kero ambazo zilikuwepo kwa muda mrefu na miaka mingi ambazo

zilikuwa zinawagusa Watanzania; nimpongeze sana na nimpe pole sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Kanyasu, kwa kazi nzuri anayofanya, akimsaidia Waziri. Hata alipokuwa anaumwa alifanya kazi nzuri, lakini pia ushirikiano wake ni mzuri. Vile vile nimpongeze Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya na ushirikiano wanaompa Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Bodi ya Utalii; bodi hii kwa sasa inafanya kazi, sasa imesimama. Niwapongeze sana kwa sababu Mheshimiwa Jaji na timu yake yote wanafanya kazi nzuri sana ya kuutangaza na kuusimamia utalii kwa ujumla. Hivi karibuni tumeona watalii ambao walifika kutoka China, lakini tumeona mambo makubwa waliyoyafanya. Kwa hiyo, niendelee kuwapongeza kwamba Tanzania sasa inapaa kwa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, ninze sasa kuchangia Mkoa wangu wa Tabora. Wakati nachangia Wizara ya Viwanda na Biashara nilitoa tahadhari na leo natoa tahadhari kwa sababu haya ninayoyachangia nachangia kwa Waziri, sichangii kama Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, nachangia kama Waziri wa Maliasili na Utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora kuna vivutio vingi sana vya utalii ambavyo nchi hii ya Tanzania ikitaka kufuatilia vivutio vya Tabora na sababu yake, ni kubwa sana. Tabora kuna njia kubwa ya utumwa ambayo ilikuwa inatoka Tabora kwenda Kigoma, watumwa wale walikuwa wanapita njia ile, nimeomba katika miaka yote hii kwamba hii njia ifanyiwe utafiti ili iweze kuboreshwa na watalii wapite waone jinsi gani watumwa walivyokuwa wanasafirishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Tabora kuna njia ya watumwa ambayo ilikuwa inapita chini kwa chini kuititia boma kubwa inakwenda *railway station* ili wasiwatoroke.

Kwa hiyo bado vivutio vikubwa sana viko pale. Wabunge wote wa Tabora kila mtu anayesimama ni lazima azungumzie habari ya utalii wa Tabora. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna boma kubwa la Ujerumani ambalo liko pale, kwa hiyo hakuna sababu ya kutokuwaleta Wajerumani Tabora ili waone vizazi vyao karne zilizopita walifanya nini, kwa hiyo ni *history* ambayo itatembea. Hata hivyo, pia kuna maboma makubwa ambayo yaliachwa na Machifu. Tabora ilikuwa inaongoza kwa Machifu, Tabora ndiyo kazi ambayo walikuwa wanafanya na mpaka wakasaidia kusitisha suala zima la utumwa. Kwa hiyo historia ambayo iko pale, nimwombe Waziri alone. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mimi nikuombe lakini si hilo tu, pia tuna *Ugala Reserve* ambayo iko pale inasaldla pia, ukiwatoa watalii kwenye mambo ya historia unawapeleka sasa kwenye utalii ambapo wanaenda kupumzika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati napitia vitabu hivi, nimeangalia kwenye ukurasa 69 na 70; nishukuru kwamba Wizara imetambua kwamba kweli kuna vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nina ombi, hakuna barabara zinazo unganisha kutoka pale Kwihaala kwenda kwenye maboma ambayo yapo, njia za watemi, hakuna. Kwahiylo niombe basi Wizara yako itusaidie kuhakikisha kwamba kuna barabara za lami zinajengwa kutoka Urambo kwenda Ugala, lakini pia ijengwe barabara hata kama kwa changarawe kutoka pale kwihaala kwenda kwenye maboma yale ambayo watumwa waliweza kufikia pale, lakini pia Warabu, Stanley na Livingston walikutana pale. Kwahiylo kuna historia kubwa sana kama wataboresha; lakini pia hata katika ukarabati nimeona pale haipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna historia ya uhuru. Wakati nauliza swali langu namba mia ngapi huko wiki iliyopita walisema kwamba hii historia ya uhuru inakwenda

Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo. Hata hivyo ni vizuri pia hata Wizara ya Maliasili na Utalii ikaeleza historia ya Baba wa Taifa, ikaeleza tarata tatu zilipatikanaje, ikaeleza uhuru, kwasababu kuna utalii wa ndani. Watu wengine wanasoma tu kwenye vitabu lakini Tabora bado ipo, kuna watu ambao wamesoma Tabora, Tabora Waingereza waliitambua na ikawa ina shule nzuri, Kuna watu waliosoma Tabora Boys na Tabora Girls. Kwahiylo historia yake bado ikipangwa vizuri utalii unaweza ukafanikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hilo tu kuna suala zima ambalo nilitaka niliongelee, la TAWA. Wakati nimeuliza swalii langu hapa nilimuuliza Naibu Waziri kuhusu Bodi ya TAWA, hajakabidhiwa mpaka hivi leo, tangu ya Naibu Waziri alivyotoa kauli, kwamba sasa mkoa iwakabidhi. Sasa hivi TAWA ina mipango mizuri lakini haiwezi kufanya kazi, haina meno. Siku ile nillomba sana kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba kwanini utaratibu huu haufuatwi? Kama Wizara imetoe amri, maelekezo au waraka, kwamba sasa Bodi ile ianze kufanya kazi; hakuna kazi inayofanyika kwenye *game reserve*, hakuna kazi inayofanyika kwenye Zoo ya Tabora Manispaa; hakuna chochote kinachofanyika kwa sasa kwasababu hawana meno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nipate majibu vinginevyo hapa tena ndiyo itakuwa tabu. Nipate majibu kwanini mpaka sasa Bodi hiyo haijapewa nafasi ya kufanya kazi, na kwanini hawajahamisha kuwapa madaraka kutoka Mkoani kwenda kwenye Bodi hiyo ambayo ni ya TAWA? Mpaka sasa hawajapewa kitu chochote na bado makabidhiano hayajafanyika, hii figisufigisu inatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine nililotaka kuchangia ni kuhusu Chuo cha Nyuki; hapa sasa leo napongeza. Niipongeze sana Wizara hii na hasa niwapongeze kwa kazi nzuri wanayofanya kwasababu sasa kuna mabadiliko ya Chuo cha Nyuki. Yale mahitaji ambayo yalikuwa yanahitajika kwa kweli angalau Serikali imefanya kazi nzuri na imetambua. Sasa kwa kuwa kitakuwa chuo rasmi

sasa cha kufuga malkia wa nyuki ni vyema sasa niiombe Serikali iongeze fedha na fedha zipelekwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ombi langu kwa Chuo cha Nyuki, kuna uzio ambao walitoa ahadi kwamba utajengwa; niombe sasa fedha ziende kwa wakati ili ule uzio ujengwe kwasababu wananchi wanasogea na wakisogea wananchi kuwatoa ni gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyio mimi niiombe Wizara ya Maliasili na Utalii, nikuombe sana Mheshimiwa Kigwangala, hebu iangalie hii mipaka, kwa sababu kuna Chuo cha Ardh ambacho kiko pembeni na kuna shule ya Msingi. Kwahiyio tusipoziba uzio na tusipoweka mipaka ya uhakika tutakuja kuwaondoa wale kwa gharama kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyio mimi msisitizo wangu ni huo, kwamba Bodi ipewe meno ya kufanyakazi, kwasababu hata kama ina mipango ya kufanya kazi haitafanyika kwasababu tunakwenda kwa utaratibu na tunakwenda kwa sheria. Sasa kama ni sheria basi utakapokuja hapa kumalizia kutoa majibu nipate jibu sahihi lini Bodi ya TAWA itapewa meno ya kufanya kazi au itakabidhiwa rasmi ili waweze kufanya kazi hiyo lakini...

(Hapa kengele illila kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri Mheshimiwa Lulida

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono asilimia 100.

MWENYEKITI: ...jiandae Richard Mbogo

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia katika hoja

iliyokuwepo mezani; nitachangia michezo pamoja na walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeridhia haki za walemavu ndani ya Umoja wa Mataifa, na katika eneo ambalo inabidi lifanyiwe kazi ni utalii ndani ya Umoja wa Mataifa. Katika takwimu tulizonazo za dunia walemavu tuko asilimia 15, na katika kuwa asilimia 15 walemavu wale wanahaki ya kufanya utalii katika nchi yetu ya Tanzania. Ndiyo maana leo mmewaona *Tembo Warriors* wamekuja hapa kuja kuwawakilisha walemavu na kumtangaza Tembo katika nchi yetu ya Tanzania. Kila Mtanzania anatakiwa kusema *say no to poaching*; ujangili basi, imetosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini nazungumza hivi kila mwaka Kenya wakiwa katika mukutano wa UN wanasesma *come and visit Kenya and visit Serengeti, and visit Ngorongoro and Zanzibar*. Kwanini, wenzetu wako wanajitangaza. Mimi leo nasema nimejitolea ninataka kusimama kwa hili nikishirikiana na mashirika yote ya utalii ya TANAPA na Ngorongoro watushirikishe na kumpa bendera Mheshimiwa Ikupa aende UN akatangaze utalii ndani ya UN. Naomba Wizara tatu za kushirikiana nazo zimpe ushirikiano Ikupa. Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri Mkuu impe ushirikiano Ikupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina sababu za msingi; kule ndani ya Mkutano wa UN kuna *event* inafanyika katika kila nchi, *state parties*. Si kila siku Ikupa atakwenda Marekani anakwenda kufanya nini; tunataka akapeleke ujumbe kama Tanzania yenye utalii na walemavu inawezekana. Na walemavu waliokuwa kule ni maprofessor, wafanyabiashara; ina maana hii *17 percent* ambayo ni *point two* mnaitegemea, tunauwezo wa kuiongezea na iwe hela nyngi zaidi katika suala la utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninaona katika Bunge hili walemavu tunazidi kuongezeka Mheshimiwa Kigwangwala sasa hivi ni mlemavu wa matatizo ya mikono, tunakukaribisha katika kundi la walemavu, karibu sana

unakaribishwa, Mheshimiwa Kanyasu ukiwa mrefu sana na ukiwa mfupi sana vile vile nalo lina matatizo kidogo ya kulemavu ulemavu ulemavu; na wewe vile vile katika kundi letu la walemavu na mtuunge mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile *desk linafurahisha*, ina maana tutawaunganisha walemavu ambao watahudhuria katika mkuutano ule na kuwaambia Tanzania kuna utalii. Juzi ilikuja meli na watalii 2500 wameshindwa kushuka Dar es Salaam kwa vile hakuna mazingira ya walemavu wale kuingia Dar es Salaam. Kurudia makosa ni kosa lakini sisi tunataka kusema kwamba kuanzia leo Jiji la Dar es Salaam lianzishe mradi wa *city tour* ili walemavu waweze kupata uwezo wa kutembelea Jiji la Dar es Salaam. Nina imani Mkurugenzi wa Dar es Salaam Mama Spolar Liana amelianzisha hili, mpeni ushirikiano Spolar aanzishe utalii Dar es Salaam ili watalii wa kawaida na walemavu waanze kuingia Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe pongezi zangu za dhati. Kwanza nimpongeze Allan Kijazi, nimpongeze Manongi kwa kweli mimi sina cha kusema; hawa watu wameweza kusimamia mifumo mizuri ndani ya Mashirika haya. TANAPA sasa hivi inaweza kutoa milioni 37 ndani ya Serikali kama ruzuku, na bilioni 20 kusaidia miradi mbalimbali kwa Tanzania hii. Pia Ngorongoro ni hivyo hivyo, wameweza kupeleka Serikalini; wamevuka malengo wamepeleka bilioni 22. Mashirika mengi yanachukua ruzuku ya Serikali lakini hawa wameweza kutengeneza mifumo mizuri ambayo Serikali badala ya kuwalipa wao, wao wanaipelekea pesa za ruzuku ili kuuendesha utalii na uweze kuwa endelevu na nchi kupata uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa nchi nyingine hawa watu wangepewa *nobel*, na mimi bila kusema chochote nasema ninawapongeza. Kwa niaba ya walemavu wenzangu na baadhi ya walemavu wenzangu na baadhi ya wapenda maendeleo ya utalii nasema Ngorongoro kwa kupitia Manongi na Mr. Kijazi, Mungu awabariki. Wanakaribia kustaafu, na kama wanastaafu wawaandae vijana ambao watashika ule mfumo usiharibike. Ule mfumo ulioko kule

umeifanya sasa hivi Serikali inapata mapato yake bila kuwa na matatizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizokuwepo; kuna changamoto ambayo ng'ombe ukimkamua sana huyu ng'ombe ataharibikiwa. Wakiondoka Kijazi na Manongi tunaweza tukaiona *TANAPA* na Ngorongoro zinakufa. Serikali naomba isimame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Wizara ya Fedha kuna tozo zinatozwa ambazo zinazifanya taasisi hizi zisijiendeshe. Wanahitaji barabara wanahitaji mifumo ya maji, wanahitaji mifumo ya mawasiliano wanahitaji kupata mishahara kwa wafanyakazi. Sasa Serikali inayotusikiliza, wanasema Serikali sikuvi na mimi nasema ndiyo; naomba wawaangalie na hizi tozo zilizopo mziangalie kwa makini msije kuiue *TANAPA* na Ngorongoro ili baadaye mashirika haya yapewe ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja kwenye hoja ya pili. Kuna uchonganishi; unazungumzia mikoa ya kusini ni Lindi, Mtwara Ruvuma, ukizungumzia Nyanda za Juu Kusini ni Iringa, Mbeya Katavi na Sumbawanga; na hii imekuwa ni mazoea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umekuja mradi wa *SAGCOT* (*Southern Agricultural Corridor of Tanzania*) Lindi, Mtwara Ruvuma hatumo. Mradi huu umepita, watu wamenufaika, mikoa imenufaika sisi hatukunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umekuja mradi wa *World Bank* kuna haja gani kusema mikoa ya Kusini? *Definition* ya Mikoa ya Kusini iko wapi ilhali Lindi na Mtwara hatumo? Ina maana mmetuweka sisi kikaangoni tukingojea mikoa mingine ikipata maendeleo sisi tukiendelea kuswaga kuwa masikini na ilhali tunaongoza kwa utalii mkubwa kuliko mikoa mingine yoyote? Nataka niorodheshe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pesa ya Kilwa ya mwaka 1000 leo imeonekana Australia nchi ilipokuwa inajitegemea. Katika urithi wa dunia Kilwa iko namba 21, lakini katika urithi

wa dunia huu utashangaa katika mradi wa kusini Lindi, Kilwa, Mtwara Ruvuma mpaka Namtumbo hazimo. Sasa tunafika mahali tunajiliza hawa wataalam nafikiri wanatufanya sisi tuwe na chuki na mazingira haya. Haiwezekani leo utalii mkubwa wa Selou, maana Selou kutokea Kingupila kwenda Lindi tunachukua *two third*; Matambwe iko Morogoro na Morogoro iko Mashariki hivyo usichanganye na Kusini. Hivyo kama unaipeleka Matango, Udzungwa na Mikumi haiko Kusini kabisa. Leo tutajivunia nini Kusini na utalii wa Kusini? Hatumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivutio vikubwa vilivyokuwa kusini, kwanza *corridor* ya *Selous Niassa*, Mozambique, ile *corridor* ni ya tembo, mbwa mwitu, samba nyati. Nimepiga kelele mpaka leo sioni kama kuna majibu ya kueleweka. Lakini nilikwenda mimi; niishukuru taasisi ya GIZ ilinipa nafasi ya kutembelea na baadhi ya waandishi wa habari; zile corridor wanazopita tembo tayari wafugaji ambao wametolewa lhefu wamevamia; na baada ya kuvamia mnataka kuhalalisha ili viwe vijiji vya asili; maeneo wanapita tembo unahalalisha kuna nini hapo? Tunaji-*contradict*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninaomba ujumbe huu ninaotoa sasa hivi umfikie Mheshimiwa wangu Rais kwa vile jamaa zake ndio wanafujo ya kupeleka mifugo katika maeneo hayo na wanaingia na magobole. Hivyo tutakapowamaliza hawa tembo na simba utalii utakwisha. Simba anatoka Mozambique anaingia Selou anaingia Tunduru, anaingia Masasi, anaingia Masasi Liwale, anaingia Matambwe, anaingia Mikumi anaingia Kilosa, anaingia Mkungunero, anateremka Ngorongoro, anakwenda Serengeti anakwenda Maasai Mara. Njia hizi mkiziharibu hawa wanyama watapita wapi? Binadamu wamevamia haya maeneo na katika kuvamia maeneo haya ilikuwa *only 20 percent* ya hifadhi katika Tanzania inakwenda kwa wanyama. Sasa hivi tumezunguza na tuko chini ya *15 percent*. Tukizidi kupunguza tunaisaidia nchi au tunaiharibu nchi. (*Makof!*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako mzuri, Mheshimiwa Mbogo jiandae Malocha.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa hii nafasi na nashukuru Mungu ametuwezesha tuko salama mpaka muda huu. Kwanza nianze kupongeza watendaji ndani ya hii Wizara wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangwala, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Constantine Kanyasu; na nipongeze watendaji wote na taasisi zilizoko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni leo tu Mkurugenzi wa TFS ametatua kero ambayo iko kwenye Jimbo langu naomba nimpongeze sana Professor Dos Santos Silayo kwa kuitikia kilio hicho kwa haraka, na kazi ambazo unazifanya ndani ya ndani ya muda huu uko kwenye hii taasisi unaleta mambo mazuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia kuhusiana na Hifadhi ya msitu wa Msaginia wenyewe rramani JB 215 ulotokana na *GN 447* ya tarehe 24 Disemba, 1954, maana yake ni kabla ya Uhuru wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto katika msitu huu kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika mawasilisho ambayo tumewasilisha kwenye ile kamati ambayo iliundwa na Mheshimiwa Rais; na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kusikiliza kilio cha sisi Wabunge na wananchi kuhusiana na maeneo haya na kuunda kamati hii ambayo inamshauri namna ya utatuizi; kuna vijiji ambavyo vilipimwa ndani ya msitu huu, kijiji cha Igongwe na Matandarani, na rramani namba 48870 ilitoka. Vilevile katika rramani hii ya msitu wa Msaginia kuna vijiji ambavyo kwenye rramani vimekatwa lakini *GN* hii 447 bado hajabadiishwa, na vijiji hivi kisheria bado vinasoma viko ndani ya hifadhi. Vijiji hivyo ni Msaginya, Mwenge, Songambele, Mtakuja, Kapalala, Magamba, Makongoro, Isanjandugu pamoja na kijiji cha Namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Msitu huu wa Msaginia nikienda sambamba na Hifadhi ya Wanyama ya Katavi, chini ya hifadhi hiyo, inapakana na Kijiji cha Stalike; sasa kuna eneo la Kitongoji cha Stubwike ambapo kuna sehemu Serikali iliwatoa wananchi kwasababu mbalimbali tu za kiusalama dhidi ya wanyama wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maombi Yangu. niombe sasa Serikali tuone namna ya kubadilishana sehemu ya kitongoji cha Stubwike na hifadhi ya msitu ambao uko chini ya TFS. Yaani Stubwike tuwamegee Katavi *National Park*, lakini kwa ukubwa huo hata mkitoa na *bonus mmege* sehemu ya msitu wa TFS ili sasa mwingiliano kati ya wananchi na Katavi *National Park* tuupunguze, na mpaka itakuwa ni barabara ambayo inayoelekea Mpimbwe kwenye Jimbo la Kavuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo llingine ni kwenye Msitu wa *North East Mpanda*. Msitu wa *North East Mpanda* tulivyokaribisha wakimbizi kutoka nchi ya Burundi mwaka 1972, tuliweka makazi pale ya wakimbizi, ambayo ni ya Katumba. Niiombe Serikali iendelee kushughulikia eneo hili kwasababu ni ndani ya hifadhi ya msitu uolimegwa. Wananchi wanaishi mule kwa miaka hii mingi zaidi ya miaka 40, na shughuli na ujenzi na sasa TAMISEMI imeingia, tunaboresha miundombinu tunapeleka umeme na tunapeleka maji. Niiombe Serikali, muone namna bora ya kutatua jambo hili kwa haraka. Kama tuwe na mpango wa matumizi bora ya ardhi na kupima mipango mji basi lifanyike kwa haraka ili tuondoe hali ya sintofahamu kwasababu wananchi hawa wamekuwa sasa hawawezi kufanya maendeleo kwasababu bado mamlaka ziko zinasimamia maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ndani ya makazi hayo hayo kwa ufadhili ya UNHCR ilijengwa shule ya msingi ambapo ina vyumba vya madarasa sita nzuri kabisa matundu ya vyoo na nyumba za walimu ziko mbili. Thamani yake ni si chini ya milioni 150. Sasa niombe Wizara tumesha iachia ile shule baada ya kufanyika ile *eviction*; lakini hebu tuombe muichukue ndiyo iwe moja ya makambi ya mafunzo

ya vijana wenu, kwa aidha mtupe fedha au mtujengee shule kama hiyo hiyo katika maeneo ambayo tunauhitaji wa vyumba nya madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika msitu huo wa *North East Mpanda* tunaomba Serikali tunaomba Serikali ingalie namna gani huenda kwenye msitu *North East Mpanda* au Msitu wa Msaginia kuna maeneo ambayo yamekuwa na uvamizi wa miaka mingei. Wananchi wanalima pembezoni mwa Msitu huu wa Msaginia na *eviction* zilifanyika na niseme kwa bahati mbaya iliokea tarehe 24 Disemba, mwaka jana kuna wananchi watano walijeruhiwa baada ya kuonesha kuwa walitaka kupambana na askari wa Usu na wakafyatua risasi ziliwajeruhi watu watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kuondoa adha hii ya wananchi wetu kuumizwa kutokana na uvamizi hebu tuombe sehemu ya Msitu wa Msaginia kwa kipande cha kutoka Sitalike mpaka unakuja Maili Kumi watumegee maeneo ambayo tayari sasa hivi yanalinwa zaidi ya miaka 20, katika mpango huu ambaao Rais anauruhusu ili wananchi hawa wapate maeneo ya kulima. Maana kwa upande mwiningine kwa mfano Kijiji cha Mtisi katika Kata ya Sitalike ni shughuli za madini ambazo maeneo yale huweze kufanya shughuli za kilimo kutokana na ardhi ilivyo. Kwa hiyo tuombe sana Serikali tuondoe mgogoro huo wa wananchi basi kwa kumega hiyo sehemu wapate sehemu za kulima, itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika mpaka wa Kijiji cha Sitalike na hifadhi ya Katavi *National Park* kuna Mto wa Katuma. Sasa niombe serikali hebu tumege sehemu ya mto hata kama kilometra moja tuwape wananchi kwa ajili ya uvuvi wa samaki aina ya kambare. Hii itakuwa ni moja ya ujirani mwema ambayo inawasaidia sana wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie juu ya suala utalii, tumeona Serikali inafanya juhudhi kubwa sana, watalii wanatoka 1.3 milioni mpaka 1.5. Sasa tuiamshe mbuga yetu ya Katavi tuna uwanja mzuri wa ndege wanaleta watalii

kutoka nchi mbalimbali basi wapate wadau wa kuboresha, kujenga hoteli na mbuga yetu ni nzuri wanyama *very natural* na tembo wakubwa katika nchi hii wanatoka Katavi na kuna yule twiga chotara ambaye tupo kwenye Mbunga ya Katavi. Hebu tuletewe watalii ili tukuze uchumi na vijana wetu wapate ajira za kubeba na kuongoza watalii katika Mkoa wetu wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho lakini si dogo, niombe sasa kwa Wizara hii pia halmashauri zetu zinahitaji kuongeza mapato ya ndani basi tuone kwa Sheria ya Misitu ya mwaka 2002, watumegee sehemu kwa ajili ya kuweka malisho na tuweke *block* za malisho sehemu ya msitu kwa ajili ya halmashauri yetu kuongeza mapato ya ndani kwa kuweza kuweka wafugaji na kuweka sehemu za malisho. Kwa hiyo, wakitumegea na sheria inaruhusu, tuombe Waziri awasilishe kwa mujibu wa Sheria ya Misitu, 2002, Na.14, halmashauri yenyewe ipate sehemu ya msitu, hii ikiwa ni sehemu ya kuongeza mapato ya ndani tukizingatia kwamba vyanzo vingi sasa hivi vimeshuka vya kimapato kwenye halmashuri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niseme tu napongeza Serikali, nampongeza Rais wetu kwa kusikiliza kilio na kuunda ile Kamati, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, alifika Stubuiko yote, Makutano alitembelea na pia Mheshimiwa Kanyasu ameenda amefunga mafunzo, ameona jinsi gani Katavi ilivyo, sasa waende wakainyanyue na iweze kunyanyua mkoa wetu kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa ni Mheshimiwa Malocho, wajiandae Mheshimiwa Marwa Ryoba na Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya Maliasili na Utalii. Kwanza kabisa

nimpungeze Mheshimiwa Waziri Dkt. Kigwangalla, Naibu wake na watendaji wote wa ofisi yake. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana, unaweza kusema sasa Wizara imepata viongozi na sio viongozi wamepata Wizara. Hongereni sana kwa kazi nzuri. Tumeona kuna mabadiliko mengi ongezeko la watalii na mambo mbalimbali. Kwa kweli hongereni sana tunawaombea kwa mwenyenzi Mungu aweze kuwazidishia afaya muweze kuitendae haki nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo ambayo yanaweza wakati mwininge yakafanywa na watu chini yake na si yeye ni vyema kabisa tukamweleza japo kuwa nimeeleza kwa njia moja au nyininge, nimeona leo hii nirudie. Upo mgogoro mkubwa sana kati ya wavuvi wa Ziwa Rukwa na watu wa Maliasili wa Uwanda wa *Game Reserve*. Hii uwanda wa *Game Reserve* miaka ya 60 ilikuwa na *squire kilometre* 5,000, lakini baada ziwa kupanuka limemeza uwanda mkubwa wa game reserve limemeza karibu kilomita 4,100. Kwa hiyo nchi kavu ya *Uwanda Game Reserve* ishabakia na kilomita 490, kwa hiyo, sehemu yote ni ziwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wapo wavuvi kutoka maeneo mbalimbali au kutoka mikoa mbalimbali ambao wanaenda kutafuta riziki katika maeneo yale na wanapoingia wanakata leseni za biashara, wanakata leseni za mitumbwi, wanakata leseni za uvuvi, wanakata leseni za mazao ya samaki. Wanaingia kwa njia halali, lakini hawa watu wanasurubishwa, wanakamatwa, wanaharibiwa vyombo vyao utadhani sio Watanzania, utadhani hawalipi kodi. Mgogoro huu ninaozungumza ni mkubwa sana umefika mahali ambapo kama Wizara haitachukua hatua utaleta mgongano mkubwa sana kwa sababu, watu wanaohusika na uvuvi ni watu wa uvuvi. Lakini maliasili wameingilia katika kuwa-*harass* wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule wanaenda akinamama wajane, vijana wanaotoka vyuoni wanakwenda kujipatia riziki, lakini wanakamatwa. Mpaka saa hivi kuna *engine* kama tisa zimenyang'anywa, boti 30, *engine* 17 zimepasuliwa, na *engine* mbili zimechomwa katika Forodha ya Nankanga na

llanga. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri alifuatie jambo hili. Niliongea na Mheshimiwa Kanyasu, sikuongea na Mheshimiwa Waziri, akanimbia atakwenda kuongea na wavuvi aone kulikoni na vilevile katibu Mkuu nimeongea naye, nashangaa mpaka sasa hivi sijaona hatua zozote. Kwa hiyo naomba sana najua amekuja kwangu mara ya kwanza, alifanya kazi nzuri sana na alisharejesha nidhamu, lakini katika hili namwomba tena atafute namna ya kwenda kuumaliza mgogoro huu, wavuvi wanapata tabu sana. wananyanyaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie wakati fulani wale watendaji wadogo wanachukua rushwa, kama huna hela unaonekana sio mtu, ukitoa hela wanakuachia tu, wanakuachia uendelee kufanya shughuli zako. Ndugu zangu wapo akinamama wajane wanaenda kujitafutia riziki, lazima ifikie mahali tuwe na ublinadamu. Kama Mheshimiwa Rais anaweza kuwa na huruma ya kusema tuangalie mapori yale ya akiba, tuwasaidie wafugaji na wakulima, sasa itakuwa eneo ambalo lipo ndani ya maji ambalo ni kwa ajili ya wavuvi. Tufike mahali wakati mwingine tuangalie mwelekeo na huruma ya Rais wetu na tumuunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka hili nilisisitize sana sana hasa kule llanga, llanga ipo karibu na *reserve* ya Lukwati. Sasa watu wanaingia kuvua wanakamatwa, wananyang'anywa vifaa, wanapelekwa Mpanda, wanaambiwa kung'oka hapa ni mpaka milioni mbili. Kwa kweli wanawa-*harras* vibaya sana. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri na jambo hili alifuatilie, naona kama hanisikilizi vizuri anashika makaratas. Jambo hili litaleta matatizo makubwa sana, naomba anisikilize na alifuatilie, wakati anatoa majumuisho alitolee uamuzi. Hizi *engine* ambazo zimekatwa wazirejeshe, wameziweka tu boti, *engine* za watu, wamerundika kwenye stoo zao zinafanya kazi gani? Tunaomba Waziri atoe tamko la kurejesha vifaa hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, alipokuja kule kwenye

jimbo langu aliahidi kusaidia ile Zahanati ya Maleza ili iweze kumalizika na aliwaahidi kuwachimbia kisima cha maji. Pia wakati Mheshimiwa Profesa Maghembe akiwa Waziri, naye aliwaahidi Kijiji cha Kilangawana kuwapatia mabati 100. Hii ni ahadi ya Wizara, hata kama hayupo tunaamini kwamba Wizara ipo na Waziri yupo, tunaomba atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni wingi wa mamba katika Ziwa Rukwa. Ziwa hili lina mamba wengi sana hakuna mwaka ambao mambo hawajala watu zaidi wawili watatu. Wanakula watu na wengine wanajeruhiwa, wengine wanakatika miguu, wengine mikono, ni kigugumizi gani kinafanya wasipunguzwe mamba katika hili Ziwa Rukwa? Mamba wapunguzwe, si ni biashara, wanaweza wakafanyiwa biashara ya ngozi, kuliko waendelee kula binadamu, kuwapunguza binadamu na kupunguza nguvu kazl. Ningombaa sana katika suala hili Mheshimiwa Waziri aweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nirudie kumpongeza Mheshimiwa Waziri, anafanya kazi vizuri na Manaibu wake isipokuwa hawa watu wa chini ndio wanaweka doa katika Wizara hii. Tunaomba sana sana ufuatilie wavuvi hawa warudishiwe haki zao na ikiwezekana Wizara ya Maliasili na Wizara ya Uvubi wakutane wajadili namna ya watu, wanaoenda kuvua ziwani kwa nini wanakamatwa? lle ni ajira, wasione vijana tu, hata wa chuo kikuu wanakimbilia ziwani na lile ziwa linachukua mikoa mingi. Ukienda watu wa Mbeya, Songwe wapo kule hata watu wake wa Tabora akija atawakuta, hata watu wa Katavi wapo kule wanajitafuta riziki, tuwasaidie vijana hawa na wananchi hawa waweze kupata riziki na bahati nzuri wanalipa kodi, hawana matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ryoba, jiandae Mheshimiwa Kapufi.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya katika Wizara hii. Anafanya kazi kubwa sana Mungu ambariki sana. Niseme Mheshimiwa Waziri kuna jambo atakumbukwa sana ni jambo la ujenzi wa barabara ya kuanzia lango la Loduare kule Ngorongoro mpaka pale Golini Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ya Ngorongoro ni barabara ambayo Waziri anafahamu udongo wake ni *volcanic*, katika matengenezo ya kawaida ilikuwa imeshindikana. Kwa hiyo niseme, Mungu ambariki sijui nimpe nini? Wamefanya kitu kikubwa ambacho watakumbukwa milele na milele, kujenga barabara ya lami katika eneo hili na tena kizuri zaidi wameruhusiwa na *UNESCO*. Niseme Mheshimiwa Waziri Mungu ambariki yeye pamoja na Ndugu Kijazi. Maana ilikuwa sio kazi rahisi kuruhusiwa na *UNESCO* kujenga barabara hii, lakini niseme Mungu ambariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kidogo, kwenye eneo hili la barabara kilomita 88, ni bora waka-*extend* ikafika lkoma *gate* kwenye ile *gate* la Serengeti ili ikae vizuri. Hata hapa niseme wamefanya jambo kubwa na Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni mapendekezo nimesoma kwenye kitabu cha Waziri ukurasa wa 33, ile namba 75 kuhusu masharti ya wajumbe wanaounda *WMA*, nimeisoma vizuri kwamba kwenye kanuni ambazo zilikuwa zimetengenezwa, kwamba wale wajumbe ambaao ni darasa la saba walikuwa hawaruhusiwi kugombea na kwenye maelezo ya kitabu cha Waziri amesema imeleta mgongano, sintofahamu kidogo na nimeona Wizara wapo tayari kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri alisimamie, wafanye marekebisho kwa sababu kanuni hii kimsingi inapingana na katiba ya nchi. Katiba ya nchi inasema mtu ajue kusoma na kuandika ndio achaguliwe sasa tukiweka kwa wale Wenyeviti wa *WMA*, bahati nzuri tuna kina

Musukuma hapa ni Mbunge, lakini si darasa la saba? Kwa hiyo, nadhani ni vizuri kanuni ile irekebishwe ili darasa la saba na wao wapate fursa ya kugombea kuwa Wajumbe wa WMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mgogoro wa mipaka kati ya vijiji ambavyo viro Serengeti na Serengeti *National Park*, tunafahamu, tumeongea mara nyingi mimi na yeze na ameonesha *positive response* na aliahidi kwamba tutaenda na yeze Serengeti. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, nimwombe sana rafiki yangu akipata nafasi hebu twende kwenye Vijiji vya Merenga, Machochwe, Mbalibali, Tamkeri, Bisarara, Bonchugu angalau aone uhalisi wa kile kinachozungumzwa, kwa sababu kuna maeneo vizingi vimewekwa kwenye maeneo ya vijiji kabisa katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi kuna siku moja nimekwenda kwa Mheshimiwa Waziri, akikamatwa na ng'ombe kwenye maeneo hayo anaflisiwa ng'ombe na anafungwa. Kwa mfano kuna mama mmoja alikamatwa ni mjamzito, ngo'mbe walitaifishwa wameunzwa wote, amefungwa, amepigwa faini na sasa hivi amejifungulia yupo magereza. Nimwombe Mheshimiwa Waziri yeze anatokea maeneo ya wafugaji na bahati nzuri mwenyewe ni mfugaji anafahamu ninachokiongea, sio vyema kuwafanya watu wetu kuwa maskini, ni vema tuwasaidie watu wetu kujali Hifadhi ya Serengeti, kwa sababu kama una jirani ni lazima uishi naye vizuri, sio kwa kugombana. Kwa hiyo nimwombe twende Serengeti akaone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambao nataka niongee ni jambo la utafiti umefanyika, inaonekana kama Serengeti hoteli kama zinakuwa nyingi vile. Huku nje hakuna hoteli, nimwombe pamoja na tatizo la *single entry*, ni bora tusaidie watu wajenge hoteli nyingi nje ya hifadhi, kukiwa na utitiri wa hoteli ndani ya hifadhi kutakwamisha *migration* ya wanyama kwenda kule Masai Mara. Kwa sababu kutakuwa na utitiri wa hoteli, tuweke nje hoteli zitasaidia wananchi wanaozunguka hayo maeneo kukua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuangalia kwenye kitabu cha hotuba ya Kambi la Upinzani, ukurasa wa tano ile namba 13; wanasema Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuta agizo lake la kuzuia biashara ya viumbe hai nje ya nchi na iwalipe fidia wafanyabiasha kwa hasara na usumbufu waliowasababishia wafanyabiashara hao. Maana yake kambi ya Upinzani inasema Serikali iruhusu wanyama wauzwe nje ya nchi. Sasa nakumbuka mwaka fulani tukiwa nje ya Bunge waliokuwa wanapiga kelele wanyama kuuzwa nje ya nchi walikuwa ni Kambi ya Upinzani au nasema uongo jamani?

WABUNGE FULANI: Kweli.

MHE. MARWA R. CHACHA: Walikuwa wanapiga kelele twiga amepandishwa kwenye ndege, walikuwa ni akina nani, si ni akina Msigwa hawa?

WABUNGE FULANI: Kweli.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Msigwa anakuja na maoni hapa kwamba wanyama wauzwe, maana yake leo Upinzani wangepewa nchi hili wangeuza wanyama wote wakaisha. Mheshimiwa Waziri asiingie kwenye huo mkenge, akatae hiyo biashara, azuie wanyama wasiuze, kwa ajili ya manufaa ya vizazi...

TAARIFA

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Marwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia mchangiaji nilikuwa nadhani angechukua muda kidogo kujielimisha. Wanyama tunaozungumza warudishwa hawa wananchi wanaouza ni tofauti kabisa na hao wanyama anaosema twiga, tembo. Wanaozungumziwa ni mijusi, konono, vipepeo ambavyo havihuiani kabisa na wanyama anaosema.

MWENYEKITI: Ahsante. Taarifa hiyo Mheshimiwa Ryoba.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu Mchungaji nini asichoelewa, wewe si unasoma maandiko unalewa vizuri. Mmesema inataka kufuta agizo lake kuzuia biashara ya viumbe hai, viumbe hai ni wapi? Sasa ungekuwa unamaanisha konono, ungekuwa unamaanisha mijusi ungetaja lakini hujataja. Kwa hiyo hapo usijifiche hapa, nilikuwa najaribu kushangaa nimwombe Mheshimiwa Waziri, wasamehe maana hawajui walitendalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni jambo la *Kfw*, Mheshimiwa Waziri na hususan Mheshimiwa wa Fedha naomba anisikilize, tumepata msaada kutoka Ujeruman, kwa ajili ya kusaidia Ngorongoro na Serengeti kwenye barabara kwenye afya na maji. Leo kuondoa *exemption* miradi hii ifanyike imekuwa ngumu, mpaka leo tunaongelea mwaka wa tano miradi hajafanyika. Nimwombe Mheshimiwa Waziri bado asichoke, nimwombe Waziri wa Fedha jamani wakae waangalie hili jambo, hivi mtu anakuletea msaada wewe unaukata eti alipe kodi, hiyo ya wapi jamani, hiyo haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sikuwa na mambo mengi. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kapufi, ajiandae Mheshimiwa Julius Kalanga.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi, awali ya yote, nami nimpongeze Mheshimiwa Waziri Dkt. Kigwangalla na timu yake, lakini niwapongeeze watendaji wote kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha nyuma nilibahatika kutembelea Ngorongoro kama ambavyo sifa zimekwenda kwa ndugu yetu Manongi na naomba niendelee kusema uimara wa mhifadhi huyu unaendelea kutusaidia kulihifadhi eneo lile, najua hayupo peke yake

pamoja na timu nzima. Vivyo hivyo kwa mzee Kijazi wa TANAPA na wengine wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu, eneo la utalii kwa ujumla wake ni tofauti na maeneo mengine. Tofauti yake inakuja hapa; unatakiwa utengeneze mazingira rafiki, mazingira ya kuweza kumshawishi mtalii ili kesho aweze kurejea nyumbani kwako. Utengeneze mazingira, kwa sababu fedha ni ya kwake yaani, huyo mtalii fedha ni ya kwake, yeye ndio ana hiyari aitumieje, kwa hiyo usipotii kiu yake haji, mazingira yasipokuwa mazuri hutomwona mtalii, huduma zikiwa za hovyo hovyo hutomwona mtalii. Kwa hiyo ninachoomba sana, pamoja na kujisifu kwamba tuko vizuri eneo la utalii, lakini tusipotii kiu, mahitaji ya Watalii itabaki kuwa historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yasipokuwa mazuri hutomuona mtalii, huduma zikiwa za hovyo hovyo hutomuona mtalii. Kwa hiyo ninachoomba sana, pamoja na kujisifu kwamba tuko vizuri eneo la utalii, lakini tusipotii kiu, mahitaji ya watalii itabaki kuwa historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri wa Sekta hii unaweza ukampata mtalii mmoja makini akakusaidia hata katika maeneo mengine. Sasa unakusudia kuwa na aina gani ya watalii hilo nalo ni jambo jingine. Kwenye fani kuna mpaka watalii wanaitwa watalii vishuka; mtalii ambaye mnaenda kugombania wote muhindi wa kuchoma na vitu vingine vya namna hiyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sehemu ya utalii, sikatai, lakini kuna mtalii ambaye akifika hapa kwanza anajuliza je, mna huduma ya hoteli za kueleweka? Mna huduma ya tiba? Kwamba hata ikitokea afya yake imekorofisha atapata tiba kabla ya kurudi nyumbani kwake? Je, huduma za Viwanja vya Ndege zinaeleweka? Kwa hiyo ninapoenda kuzungumzia utalii kwa ujumla wake tuyaa ngalie maeneo yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru nchi kwa ujenzi ule mzuri wa Uwanja wa Ndege Terminal III, ni mlango wa

kuingilia kwenye suala la utalii. Hata hivyo, ni aina gani ya watu wapo hapo? Kwa sababu kuwa na hoteli nzuri, kuwa na uwanja mzuri ni sawa lakini je, watendaji kazi wanaeleweka? Hilo nalo ni jambo linguine. Kwa hiyo naomba pia Wizara isiache kufikisha weledi kuwa na *trained personnel* hata katika masuala ya hoteli na maeneo mengine hayo. Kwa sababu *a trained personnel* yeye ni balozi wetu pia, anaanza kutuwakilisha pale, kuiuza nchi na Kuzungumzia masuala ya nchi. Pia tusiache masuala ya amani na utulivu, ni vigezo muhimu sana kwenye kuhakikisha masuala ya utalii yanachukua nafasi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mimi natoka Mkoa wa Katavi, nakuomba Mheshimiwa Waziri; nakubali viboko, mamba ni muhimu. Hata hivyo tunalo bwawa la milala, huko wamejaa viboko, wamekuwa ni tishio kwa uhai wa watu wetu, ni hatari hata kwa wanafunzi, wanakula mazao ya wananchi wetu, naomba Mheshimiwa Waziri kwa kuwa dhamana hii iko mikononi mwako katusaidie kuokoa tatizo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wote kuhusu suala la *Tanzania Safari Chanel*, ni jambo jema. Hata hivyo Mheshimiwa Waziri muda wote biashara ni matangazo. Haya mambo yote mazuri ya Ngorongoro, sijui wapi; bila kujikita kwenye matangazo, bila Bodi ya Utalii kuwezeshwa; na hapa narudi kwenye raslimali fedha; nimesikitika kidogo kwa kupitia taarifa ukizungumzia habari ya miradi yote ya maendeleo fedha hakuna, wakati hawa watu wanazalisha kwa kiwango kikubwa; tusipowarejeshea fedha tutakuwa tumewakata miguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha nyuma niliwahi kusema hapa, tusipowarejeshea fedha, tutawakata miguu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na la mwisho, Mheshimiwa Waziri, mimi nilikuwa naendelea kuomba, nchi hii labda tunachanganyikiwa kwa sababu tuna vitu vingi; tuna fukwe nzuri, tuna mbuga nzuri; sasa tukishaona kila kitu tunacho,

lakini tusipokuwa na vipaumbele, *at the end of the day* tutakuwa hatuna hata kimoja tulichokifanya kwa ufasaha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa naomba sana, Mheshimiwa Waziri tuamue, kama ni fukwe basi tuzifanye kwa ufasaha, kama ni Ngorongoro yetu iendelee kulindwa. Na mafanikio bila kuyajengea wigo, bila kyalinda hatima yake itabaki kuwa historia pia, na tukumbuke tuko kwenye dunia ya ushindani. Mtalii kama hana kitu kipy Cha Kuona, anaweza akaona leo kwako, lakini kama ni twiga ni huyo huyo ataenda kumuona nchi nyngine za jirani. Kwa hiyo wewe usipomtengenezea mazingira rafiki atakukimbia tu. Kwa hiyo wakati tunajipanga, kutamani kuona tunapatajefedha kwenye maeneo haya tuendelee kutengeneza mazingira ya kuimarisha maeneo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilizungumzie suala la uwindaji wa kienyeji. Mheshimiwa Waziri nimefarijika uliposema kwamba wananchi hawa pia tutawarejeshea uwindaji wa kienyeji. Mwananchi ambaye kwa muda wote amekuwa akiwaona wanyama, akishiriki kuwahifadhi, lakini ye ye awe mshangaaji tu anapunguza mori au ile ari ya kuwa mlinzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo tunapozungumzia habari ya uwindaji wa kienyeji itatusaidia sana pia kwenye kuhakikisha kwamba watu hawa wanakuwa ni sehemu ya ulinzi wa maliasili zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na kwa kuheshimu muda, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante; Mheshimiwa Julius Kalanga.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi wake wa kiuungwana na wa kiutu na wa kibinadamu ambao haujawahi kufanyika katika historia ya nchi hii, ya kurejesha baadhi ya maeneo ya maliasili kwa ajili ya wafugaji wa nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Niliwahi kusoma maandiko Fulani, kwamba mwaka 1981 Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimuwa Nyerere, alisema maneno yafuatayo; Kwamba katika kumbukumbu zote amewahi kuona maeneo yakinengwa kwa ajili ya maliasili wanyama, maeneo kwa ajili ya wakulima, lakini hajawahi kuona mahali pametengwa maeneo kwa ajili ya wafugaji. Rais aliyejuja kutengua kauli hiyo ya Hayati Baba wa Taifa ni Mzee na Rais wetu Mzee John Pombe Magufuli kwa kurejesha maeneo makubwa ya wanyama kwa ajili ya wafugaji wa nchi hii. Tunamshukuru sana, na mimi naamini tutamlipa wema kama alivyotutendea wema huo,. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze Wizara kwa sababu kama nao wasingekubaliana na maoni ya Mheshimiwa Rais wangeweza kushauri tofauti, lakini kwa sababu Waziri pamoja na Naibu wake, wote wanatoka katika maeneo ya wafugaji, jambo hili limewagusa na sisi tunaona kuwepo kwenu kwenye Wizara imetusaidia wafugaji wa taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza, Waheshimiwa Wabunge wamewapongeza, kazi nzuri, endeleeni kuchapa kazi. Ni mara ya kwanza na ninyi mnaona Wizara hii watu wanasmama wanapongeza ni kwa sababu kuna mabadiliko makubwa na ninyi mmekuwa wasikivu mmechukua ushauri wa Wabunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nataka niwapongeze katika hili, najua bado tuna tatizo la wafugaji kuingia katika maeneo ya hifadhi, lakini tunajua kabisa wategemezi wetu ambao ni watalii ni wanaotoka nje ya nchi; hawafurahii sana kuona kila siku moshi kwamba wafugaji

wamechomewa maboma. Kwa hiyo mimi nashauri bado hili jambo liendelee kushughulikiwa ndani ya nchi kwa utulivu bila kutumia vyombo vya habari ili kusonekane kwamba kuna uharibifu na kuna uvunjaji wa haki za binadamu kwa sababu inatuathiri sisi kimataifa katika suala la uhifadhi na suala la uwekezaji katika maliasili tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia katika maeneo ya kitaifa naomba nilete maombi yafuatato mezani kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti moja wananchi wetu wenye *WMA ya Randilen* na ambayo unajua inafanya vizuri sana; wanamuomba Mheshimiwa Waziri akawatembelee kwa sababu ya tatizo la *single entry*. Akitoka katika hifadi ya *WMA* aje mpaka barabara ya Makuyuni, halafu aende Tarangire ni takriban km 30. Wao wanaomba kwa sababu kuna hoteli za Treetops kule na imekuwa ikitusaidia mapato; tufungue geti dogo ili wao waweze kuingia pale Tarangire. Wao wamesema watagharamikia gharama zote za kutengeneza lile geti dogo liweze kufanya kazi na tuweze kufanya kazi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla ya kufanya hivyo, ili muweze kufanya tathmini ninaomba Mheshimiwa Waziri au Naibu wako afike akawasikilize wananchi wetu wa *WMA ya Randilen* ili waweze kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaomba kabisa, wako wananchi wetu waliopoteza maisha kwa sababu ya wanyama kama tembo; lakini fidia hii na kifuta jasho vinachelewa sana. Mheshimiwa Waziri naomba upitie faili la wananchi wa Monduli waliopata madhara mwaka 2015, 2016 na 2017; na mwaka huu tunasikitika kwamba tumepoteza tena wananchi wawili, mmoja kutoka Lemoti na mwingine Makuyuni, mwezi wa tatu wameuawa na temba. Mtusaidie basi ili kifuta jasho hicho kitoke kwa wakati ili wananchi wetu waone kwamba uhifadhi huu ni wa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili pia ninaomba, tunayo ahadi ya Mzee wetu Mkurugenzi wa TANAPA Kijazi, na nimemuona hapa na ninaomba anisikie, kwamba aliahidi kutusaidia kukamilisha Kituo cha Afya kilichoko kule Engaruka. Naomba Mzee wangu hili jambo ulitekeleze kwa sababu ni ahadi na mimi nimetangaza kwa wananchi ili tuone uhifadhi ambaao ni ujirani wetu unafanya kazi; kama ambavyo mmekuwa mkitusaidia; mmetujengea mabweni, na hili hamshindwi naomba mlitekeleze na mtusaidie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, Mheshimiwa Waziri, naomba hili pia la nyuki, sisi Monduli maeneo yote mnafahamu, upande wa kwanza tumezungukwa na Tarangire, upande wa pili Manyara, *Lake Manyara* na upande mwingine Ngorongoro, kwa hiyo jimbo letu tumezungukwa na uhifadhi pande zote. Tunaomba mtupe kipaumbele katika ufugaji wa nyuki hasa kwa wananchi ambaao mashamba yao yamezunguka katika eneo hilo ili basi itusaidie kupata chakula, lakini vilevile itusaidie kufukuza tembo ambaao wanaharibu sana mashamba yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho Mheshimiwa Waziri ni kuhusu sheria zetu za maliasili na utalii. Mheshimiwa Waziri unafahamu katika Sheria ya *Corridor*, imekupa mamlaka wewe kuyatoa maeneo ya wafugaji kwa ajili ya kufanya *corridor* na *buffer zone*. Hata hivyo Mheshimiwa Waziri unafahamu ardhi nyingi ni za vijiji, ninaomba kwenye kanuni zenu mtazame jambo hili ili katika kutenga maeneo na kuyatangaza maeneo hayo isibabishwe kuchukua ardhi ya wananchi ambaao pia imekuwa kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna ile Sheria ya Madini, Sheria ya Madini inasema Waziri wa Madini akishatoa leseni, mwenye leseni hiyo anaweza kwenda kuchimba madini mahali popote, na hili pia linaathiri sana mazingira yetu ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazame jambo hilo, ili sheria hizo zisianze kuingiliana, tujue kwamba mwenye mamlaka ya uhifadhi, kama ni Waziri wa Maliasili asimamie

maeneo ya maliasili, na kila dheria iweke *limit*, iwe na *categorization*; sheria hizi zisiingiliane, kama ni Sheria ya Maliasili, inavyotekelawa isiingilie kwenye ardhi ya vijiji, na kama ni Sheria ya Madini inapotekelezwa isiingilie kwenye ardhi nyingine ambayo si ya kwake. Kwamba sheria hizi kwa sababu tunatumia ardhi wote ziwe *specific* na iishie katika mipaka ya sheria nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri, na ninaomba katika hili kabisa, tuoneeni huruma, tunao wafugaji wetu ambao ng'ombe wameingia katika hifadhi za Serikali. Wananchi wale walienda Mahakamani, wameshinda kesi Mahakama za Wilaya, Mahakama za Rufaa, mpaka na Mahakama zote za nchi hii wameshinda. Hata hivyo wameshindwa kurudishiwa hawa ng'ombe, sisi tunasema mtufanyie huruma basi, kama wataalamu hawa hawataki kuhestimu hizo sheria na Mahakama zetu, basi mtuonee huruma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumeenda kwenye vyombo ambavyo tunaamini vinatoa haki, vimetoa haki hiyo lakini bado Serikali imekataa kuwaachia wale ng'ombe. Mheshimiwa Waziri, kwa unyenyekevu kabisa, kiuungwana, kama hatuheshimu hayo maamuzi ya Mahakama tuoneeni huruma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu jambo hili limefika Mahakamani na tumeshinda mtuonee huruma, sisi ni wafugaji. Mtu ukinyang'anywa ng'ombe 200, kwa bei ya kawaida tu ya shilingi laki tano ni shilingi ngapi hizo? Mwananchi yule amekuwa maskini, ametoa gharama ameenda Mahakamani, Mahakama iliona ameonewa na amepewa haki lakini bado ng'ombe wale hawajaachiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu naomba kuunga hoja mkono, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Dkt. Kafumu. (*Makof*)

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya, tunampongeza na tunaomba aendelee kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nichangie mambo matatu tu. Kwanza, ukurasa wa nne wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri inazungumzia dira, dhima na majukumu ya Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namshauri Mheshimiwa Waziri kwamba hii dhima na dira zikaandikwe vizuri kwa sababu ukisoma zinafanana. Dira anasema ni maliasili na malikale zinazohifadhiwa kwa manufaa ya Watanzania kwa ajili ya kukuza uchumi; hiyo ni dira. Dhima na yenye we inasema, uhifadhi endelevu wa maliasili na malikale na kuendeleza utalii kwa manufaa ya taifa. Hivi vitu vinafanana, ni vizuri kuandika dira ambayo inaonyesha tunaenda wapi baada ya miaka kadhaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini, dhima iwe ni tunafanyafanyaje kwenda kwenye hayo mahitaji tunayotaka kuyafikia, kwa namna hii imefanana, naomba nitoe huo ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwamba, Mheshimiwa Rais aliagiza maeneo yote yenye migogoro ya wakulima na wafugaji yafanyiwe kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kweli amesema, iliundwa Kamati ya Mawaziri wanenye na wameenda na wamemaliza kazi lakini kuna maeneo hawajafika. Kule kwetu Manonga Wembele *Game Reserve* Mawaziri hawa hawajafika na wananchi bado wanagombana; nilikuwa naomba nako mfike. Pamoja na kwamba tumeanza kufanya mapatano lakini tunahitaji Waziri aje atoe maelekezo mahsusili ili wananchi waache kugombana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jambo la tatu na la mwisho; ninaiomba sana Serikali na hasa Wizara hii, hebu tujaribu pia

ku-*develop* utalii wa mambo mengine badala ya nature reserve peke yake, badala ya baianuai peke yake. Tanzania tumebarikiwa sana kuwa na masalia ya Watemi na nyumba za Watemi. Ukienda kule Igunga, kuna Mtemi Ng'wanansali wa Igurubi, kuna nyumba yake pale, tunaweza kuitengeneza na watalii wakaja kuona. Ziba pale kuna Mtemi Ntinginya na akina Humbi pale, kuna nyumba yao na makaburi yao, tunaweza kuyafanya; na Mikoa mingi tuna mambo haya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu ukienda Ulaya haya mambo wameya-*develop* sana. Kwa mfano Ubelgiji, mimi nimekaa Belgium miaka kumi, kuna mtoto mmoja historia yake alikojolea bomu wakati wa Vita Kuu ya kwanza, sasa yule mtoto ametengenezwa na akawekwa kwenye kila mji anakojoa, watu wanakuja kuangalia na historia inaelezwa pale. Kwa hiyo ni kivutio kikubwa kweli cha utalii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi na sisi mambo haya tuya-*develop*, yako mengi, kwa mfano, tuna njia ya utumwa sisi, kutoka Bagamoyo mpaka Ujji tungeweza kui-*develop* hiyo njia vizuri na wazungu na wenzetu watalii wangependa sana kuja kuipita hiyo njia kuangalia watumwa walivyokuwa wanachukuliwa na sisi tulivyokuwa tunabebwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sisi tumeng'ang'ania zaidi utalii unaohusu wanyama, mimea, milima nakadhalika, hebu twende na huo upande mwingine itatusaidia sana tutaalika watalii wengi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa na mimi nawashukuru kwa michango yenu, niishukuru Wizara kwa kazi nzuri mnayofanya pamoja na Bodi na mamlaka zake zote, nahairisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12:01 Jioni Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 24 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*